# MPANGILIO WA HADITHI ZA BIBLIA

# MWONGOZO WA VIONGOZI

## Hadithi Arubaini na Mbili (42) na Masomo Yanayoambatanisha kwenye Kitambaa cha Hadithi za Bibilia.

**(inajumuisha ratiba inayowezekana ya hadithi thelathini)**

**ZIMETAYARISHWA NA KUREKEBISHWA NA**
**SERGE KENYA BIBLE STORYING TEAM, KENYA,**

**26 AUGUST, 2026**


ILLUSTRATED BY JIM LEWIS © 2004
DESIGNED BY GREG JACKSON

# YALIYOMO

(* Hadithi zimeshauriwa kwa kosi ya wiki thelathini badala ya wiki arobaini na mbili)


| *PISHA* | *HADITHI* | *UKARASA* |
|---|---|---|
| | **MPANGILIO WA HADITHI ZA BIBILIA (C.B.S) NI NINI?** | **5** |
| **1** | **(*1) UUMBAJI wa MALAIKA** | **7** |
| **2** | **(*2) UUMBAJI wa MBINGU na DUNIA** | **9** |
| **3-A** | **(*3) UUMBAJI wa MWANAMUME na MWANAMKE** | **12** |
| **3-B** | **(*4) MWANAMKE na NYOKA** | **14** |
| 4 | KAINI na Habili | 18 |
| **5** | **(*5) NUHU na GHARIKA** | **21** |
| **6** | **(*6) MWITO wa ABRAMU** | **25** |
| **6-B** | **(*7) KUFUNDISHA JINSI ya KUTENGENEZA MAIGIZA na WIMBO** | **30** |
| **7** | **(*8) ABRAHAMU – KUZALIWA na DHABIHU YA ISAKA** | **31** |
| 8 | ISAKA, JAKOBO, na ESAU | 36 |
| **9** | **(*9) NDOTO ya YAKOBO** | **39** |
| 10 | YAKOBO, LABAN na FAMILIA ya YAKOBO | 41 |
| 11 | YAKOBO ASHINDANA MIELEKA na MUNGU | 43 |
| **12** | **(*10) YUSUFU** | **46** |
| 13 | KUZALIWA na KUTOROKA kwa MUSA | 50 |
| **14** | **(*11) MWITO wa MUSA KATIKA KICHAKA AMBACHO KINACHOMEKA** | **53** |
| 15 | MAPIGO TISA | 56 |
| **16** | **(*12) PASAKA** | **58** |
| **17** | **(*13) KUVUKA BAHARI ya SHAMU** | **62** |
| **18** | **(*14) MLIMA wa SINAI, SHERIA KUMI** | **66** |
| **19** | **(*15) NDAMA wa DHAHABU** | **70** |
| **20** | **(*16) MASKANI / SIKU ya UPATANISHO** | **73** |
| **20-B** | **(*17) KUFUNDISHA JINSI ya KUTENGENEZA HADITHI za BIBLIA kwa KUSEMA** | **78** |
| 21 | *WAPELELEZI KUMI na WAWILI, NYOKA katika JANGWANI* | 81 |
| 22 | WAAMUZI | 85 |
| **23** | **(*18) WAISRAELI WAKATAKA MFALME / SAULI** | **88** |
| **24** | **(*19) MFALME DAUDI** | **92** |
| 25 | ELIYA na MANABII wa BAALI | 95 |
| **26** | **(*20) MANABII WANATABIRI KUJA kwa MWOKOZI ALIYEAHIDIWA na AGANO JIPYA** | **98** |
| **27** | **(*21) TANGAZO na KUZALIWA kwa YESU** | **101** |
| **28-A** | **(*22) HUDUMA ya YOHANA, UBATIZO na KUTAMBULIWA kwa YESU** | **105** |
| 28-B | SHETANI AMJARIBU YESU | 108 |

| | | |
|---|---|---|
| 29 | YESU AKIWAITA WANAFUNZI WAKE | 111 |
| **30** | **(*23) KUPONA kwa MTU ALIYEPOOZA: MAMLAKA KUZISAMEHE DHAMBI** | **115** |
| **31** | **(*24) YESU AONGEA na MWANAMKE MSAMARIA** | **117** |
| 32 | YESU AKAWALISHA WATU ELFU TANO | 121 |
| **33** | **(*25) YESU ALIMPONYA MVULANA MWENYE PEPO MCHAFU** | **123** |
| **34** | **(*26) KUFUFULIWA kwa LAZARO KUTOKA kwa WAFU** | **125** |
| **34-B** | **(*27) KUFUNDISHA JINSI YA KUTENGENEZA MAIGIZA NA WIMBO** | **128** |
| 35 | YESU na KIJANA TAJIRI | 129 |
| 36 | YESU APAKWA MAFUTA na MWANAMKE MWENYE DHAMBI | 133 |
| **37** | **(*28) MEZA ya BWANA ya MWISHO** | **136** |
| **38** | **(*29) GETHSEMANE, KUSHIKWA kwa YESU, na KUPELEKWA kwa PILATO** | **139** |
| **39** | **(*30) KUSULUBISHWA kwa YESU** | **142** |
| **40** | **(*31) UFUFUO wa YESU** | **146** |
| **41** | **(*32) BARABARA ya EMAU** | **149** |
| **42** | **(*33) YESU AKAWATOKEA WANAFUNZI WAKE / KUPAA kwa YESU** | **152** |
| | | |
| | **KIAMBATISHO #1 -** Muhtasari wa CBS: Kufuatilia Ahadi ya Mwokozi | 155 |
| | **KIAMBATISHO #2** – Muundo wa Kuuliza Maswali | 164 |
| | **KIAMBATISHO #3** – Mapendekezo kuhusu Ratiba za CBS | 165 |
| | **KIAMBATISHO # 3-B -** Mfano Rahisi wa Ufundishaji wa Hadithi za CBS | 166 |
| | **KIAMBATISHO #4** – Kioloezo Kilichopangwa ya Mpangilio wa Darasa | 167 |
| | **KIAMBATISHO #5** – Kuunda Maswali ya Mazungumzo kwa Malengo Mengine ya Kufundisha | 169 |
| | **CHART** - QUESTIONS - JEMBE/MIWANI/GUNIA | 171 |
| | **KIAMBATISHO #6** – Kutengeneza Hadithi za Biblia kwa Kusimulia | 172 |
| | **KIAMBATISHO #6-B -** Hatua za Kuunda Hadithi zako atua za Kuunda Hadithi Zako Mwenyewe kwa Mdomo | 173 |
| | **KIAMBATISHO #7** - Shughuli Nyingine Zinazoweza Kuwasaidia Watu Kujifunza au Kukariri Hadithi Za Biblia Katika Makundi | 174 |
| | **KIAMBATISHO #8** - Mada za Mafunzo ya Ziada | 175 |
| | **KIAMBATISHO #9 -** Kutumia Hadithi za Biblia katika Hali za Uinjili wa Tukio Moja Tu | 177 |
| | **KIAMBATISHO #9-B -** Seti Mbili az Maswali Rahisi kwa Uinjili wa Tukio Moja | 182 |

## MPANGILIO WA HADITHI ZA BIBILIA (CBS)

Mpangilio wa hadithi za Bibilia ni mbinu iliyokuweko kwa muda mrefu, ikitumika katika kuboresha kanisa na uongozi ulimwenguni kote.Mfumo wa hadithi za Bibilia uliaanza kukita mizizi kama mbinu na kufundishia munamo mwaka wa elfu moja mia tisa na themanini (1980's) na wamisionari wakafanya kazi katika vitongoji duni vilivyo na makabila tofautitoofauti. Kwa kuwa mpangilio wa hadithi za Bibilia ni mpya unaokusudiwa kuwa mbinu ya uenezajiinjili na kufanya wafuasi wa kristo, ni ya kitambo kama historia ya Biblia.

Hadithi hizi kuanzia uumbaji na kuendelea hadi kanisa la kwanza, imedhihirisha wazi kuwa Mungu mwenyeiz akiendeleza kwa ulimwengu wa dhambi kwa nyakati nyingi zilizopita Mungu ameendelea kufundisha kupitia hadithi kuhusu yeye mwenyewe, asili ya mwanadamu, na jinsi mwanadamu mwenye dhambi anygeweza kurudishwa katika uhusiano na Mungu mwenye huruma.

## MPANGILIO WA HADITHI ZA BIBILIA (C.B.S) NI NINI?

1. **Ni mpangilio**- CBS inafundisha injili katika njia ya kulinganisha ambayo ni ya kudumu kwa uenezaji wa injili na kufanya wanafunzi wa kristo. Mpangilio kupitia hadithi za Bibilia kwa mpangilio maalumu, kuanzia na uumbaji na kuendelea hata mwanzo wa kanisa la kwanza. Kwa kufundisha kimpangilio ninani, mwanadamu ninani na ni kwa jinsi gani mwanadamu mwenye dhambi anaweza kuja mbele za Muungu mtakatifu , Mungu anayetaka uhusiano na wanadamu wa tabaka zote duniani.
2. **Ni Bibilia** –CBS-Mpangilio wa hadithi za Bibilia, sio tu kutumia hadithi za maisha yetu kueleza katika ujumbe wa mahubiri yetu. Pia sio tu kutukia hadithi za Bibilia kwa kuelezea tu, bali inajumulisha kuelezea hadithi ya Bibilia kwa usahihi na kufundisha kanuni muhimu za ukombozi zinazo dhirika katika hadithi hiyo.
3. **Ni hadithi simulizi**- Ni muundo wa kueleza ukweli wa neno la Mungu ( Bibilia) ambao ni wa thamani sana katika mpangilio wa kiafrika, kwa sdababu wafrika ni wasimulizi. Busara nyingi zilizo pitishwa toka kizazi hadi kizazi. Zimezungumziwa kwa njia ya hadithi kufikia jamii kuliko kutumia njia ya vitabu na kuandika. Hadithi husaidia kufichua ukweli uliofichika, kuonyesha maana kwa sababu inahusiasha watu kikamilifu na ni rahisi watu kushika na kusimulia kwa marafiki na familia kuliko kutumia mahubiri ya vipengele vitatu.

## KIPINDI cha KUSIMULIA na KUFUNDISHA HADITHI KINAONEKANAJE?

1. **UTANGULIZI**
   a. Anza kwa kupitia hadithi za awali kuandaa wasikilizaji, kwa hadithi mpya. Anza kwa kutayarisha lengo.
   b. Uliza swali moja au mawili ili kuwafanya wasikilizaji wawe na hamu ya kusikiliza, fahamu , na angazia lengo la hadithi.
      i. Tumia maswali yaliyopendekezwa kuchochea mahojiano kwa ufupi kati ya wahusika kwa makundi ya watu wawili au watatu ama waweze tengeneza maswali yako mwenyewe.
   c. Kama inawezekana, peana wakati wa kusikiza ( jambo unaloweza kuliangalia katika hiyo hadithi) wakati wa kusimulia hadithi.
   d. Thibitisgha kwa Bibilia. (Hakikisha watu wajua hadithi hiyo yotoka kwa Bibilia. Kwa wakati mwingine sisitia kushauri kusoma maandiko yenyewe katika Bibilia .

2. **HADITHI - MJIFUNZE HADITHI PAMOJA**:
   a. Rudia rudia hiyo hadithi mara nyingi iwezekanavyo.
   b. Kuwa na muda wa kutafakari kabla ya marudio mengine ili kudhibiti hamu.
   c. Pitia hiyo hadithi ukiuliza maswali ya mtazamo ilikuangazia undani wa hadithi.

d. Wapange wasikilizaji ama hao wahusika katika makundi wahadithiane hiyo hadiothi kama zoezi la makundi.
e. Mwisho pata mtu mmoja katika kila kundi kusimulia hadithi .
f. Rudia mara kadhaa hadi iwe kila mmoja na kuwez\a kuikariri kwa moyo.

3. **MJADALA kupitia MASWALI: KANUNI ZA MSINGI ZA MAZUNGUMZO - KUWAONGOZA WASIKILIZAJI KUTAMBUA UKWELI KATIKA HADITHI**. (*Angalia appendix pia!*)
    a. Tumia maswali yanayo saidia mwanafunzi kuona undani wa hadithi kumuongoza kuona mtazamo wa kiroho (tafsri).
    b. Hadithi inafundisha nini kuhusu nguvu za Mungu, ufahamu wa Mungu , utakatifu wa Mungu, Neema ya Mungu, na uaminifu wa Mungu?
    c. Hadithi inafundisha nini kuhusu mwanadamu, thamani yake kwa Mungu , asili yake ya dhambi na kutojiweza kujisaidia?
    d. Hadithi inafundiha nini kuhusu wokovu na  ni kwa jinsi gani twawweza kurudi kwa Mungu kupitia njia yake?
    e. Uliza maswali ya kutotumini kuhakikishia wasikilizaji kufikria kusu maisha yao.
    f. Kabiliana na maswali yasiyo sahihi kwa njia ya hekima sana.
    g. Husisha yale majibu ya watu katika maswali yako kuendelea kubuni maswali Zaidi na pia kuweza kufahamu maudhui na mawazo.
    h. Chunga kujibu swali usilo;ijua. Tafuta jawabu na ulizungumzie wakati mwengine .
    i. Pitia kwa muktasari wa hadithi iliyo mbele, au uulize maswali ili kupata tahamaki.
    j. Washauri wahusika au wanafunzi kutengeneza mipango ya kushirikiana kujifunza hadithi wao wenyewe katika familia zao na hata katika huduma.

## HADITHI na MASOMO

### 1. UUMBAJI wa MALAIKA

Kwa muda mrefu kabla ya Mungu kuwaumba watu, Mungu aliwaumba malaika wengi sana ambao waliishi naye mbinguni. Aliwaumba wazuri bila dhambi, na pia walikuwa roho. Malaika walimwabudu Mungu na walikuwa watumishi wake pia.

Malaika mmoja fulani aliyeumbwa na Mungu alikuwa mwerevu na mrembo kuliko malaika wengine wote. Malaika huyo aliitwa Lusifa. Mungu alimpatia Lusifa mamlaka juu ya malaika wengine wote.

Baada ya muda fulani, Lusifa akawa na kiburi sana, akaamua awe muhimu na wa maana kama Mungu. Akataka kuingia mahali pa Mungu. Malaika wengine wengi pia waliamua kuasi dhidi ya Mungu. Lakini Mungu alijua Lusifa na malaika wengine walivyofikiri. Maasi yao yalishindwa kwa maana Mungu anajua kila kitu na ni mwenye nguvu kuliko Lusifa aliyeumbwa na Mungu mwenyewe.

Kwa sababu ya dhambi ya Lusifa na malaika wake, Mungu aliwafukuza kutoka mbinguni walipokuwa wakiishi pamoja naye. Mungu ni mwenye haki na ni mtakatifu kwa hivyo hangeweza kuishi pamoja na walioasi mbele yake. Mungu pia alisema kwamba siku moja atakamilisha adhabu yake kwa malaika waasi na kuwatupa katika Ziwa la Moto.

Mungu alibadilisha jina la Lusifa kuwa Shetani. Jina hilo linamaanisha "Mdanganyifu." Kwa hivyo Shetani na wafuasi wake wakawa maadui wa Mungu. Wao hupinga kazi ya Mungu wakati wote.

Sasa wafuasi wa Shetani ni mapepo waovu. Wao hufuata Shetani kupinga ukweli. Shetani hataki tusikilize Neno la Mungu. Lakini wanaomwamini Mungu hawahitaji kumwogopa Shetani au mapepo yake kwa sababu Mungu ana nguvu juu ya wote.

Maandiko ya Biblia: Nehemia 9:6; Yobu 38:4-7; Zaburi 99:1-3, 103:19-21; Isaya 14:12-15, 45:12; Ezekieli 28:12-15; Nahumu 1:2-3; Luka 10:18; Yohane 8:44, 12:31; Waefeso 2:2, 6:11-12; Wakolosai 1:15-16; 1 Timotheo 3:6; 1 Petro 5:8; 2 Petro 2:4; 1 Yohane 3:8; Yuda 6; Ufunuo 12:7-9, 20:10

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Zungumza wakati katika maisha yako wakati mtu amekudanganya. Je, hili lilikuathirije?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**HADITHI: Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.**

**MASWALI ya KUJADILIANA**

**Je, tunajifunza nini kuhusu MUNGU katika hadithi hii? Mungu alifanana na nini?**

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote kwa jinsi gani?** (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)
    - Mungu aliumba Malaika – viumbe vyote vya kiroho.
    - Malaika wanamtumkia na wako chini ya mamlaka yake.
    - Mungu ni mwenye mamlaka makuu kuliko malaika kwa sababu aliweza kuwaadhibu na kuwafukuza kutoka mbinguni

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu kwa jinsi gani? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali kwa jinsi gani?**
    - Mungu alijua jinsi ya kuumba malaika.
    - Mungu alijua yale Lusifa na wafuasi wake walifikiri na jinsi ya kuwasimamisha.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu kwa jinsi gani? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?)**
    - Mungu aliumba malaika wazuri bila dhambi.
    - Mungu hangeruhusu malaika waasi kukaa pamoja naye.
    - Mungu alimwadhibu Lusifa na malaika waliomfuata kwa sababu ya dhambi zao.
    - Mungu anastahili kupewa sifa na utukufu kutoka kwa malaika wema.
    - Mungu hawezi kuruhusu yeyote kuchukua mahali pake, hawezi shiriki utukufu wake na kiumbe chochote

**<u>Katika hadithi hii tunajifunza nini kuhusu Shetani?</u>**

- Shetani ni mwongo na mdanganyifu huwaongoza wengine katika dhambi na uasi.
- Shetani ni mwenye kiburi na anataka kuwa kama Mungu.
- Shetani anamchukia Mungu na hupingana naye.
- Shetani si mwenye mamlaka kama Mungu na kamwe hawezi kumdanganya au kumshinda.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima):</u>**

- **Ikiwa Mungu ana uwezo juu ya ulimwengu wote wa roho pamoja na malaika wote wazuri na Shetani na mapepo yake, je, ana mamlaka ya aina gani juu ya maisha yetu mwenyewe? Je, hili linapaswa kuathiri vipi jinsi tunavyofikiri, kuamini, kunena, na kutenda?**
    - Je, mtu anawezaje kujua zaidi kuhusu huyu Mungu na kile anachodai kutoka kwake?

- Ikiwa Mungu alijua mawazo na matendo ya Lusifa, anajua nini kukuhusu wewe? Je, hilo linakufanya uhisi vipi?

- Mungu alichukia dhambi na uasi wa Lusifa. Ilimbidi kumwadhibu na kumfukuza kutoka kwa uwepo wake kwa sababu ya utakatifu wake mwenyewe. Kwa hivyo Mungu anafaa achukue hatua gani kuhusu kutotii kwako? Je, hilo linakufanya uhisi vipi?

- Katika hadithi hii tunaona kwamba Shetani na roho wake waovu ni halisi na wanafanya kazi katika ulimwengu wetu. Tunaona kwamba wana nguvu nyingi za kushawishi watu. **Umejifunza nini kutoka kwa hadithi hii ambacho kinaweza kukusaidia kupinga ushawishi wa Shetani maishani mwako?**

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>**

- **Ni njia gani moja ambayo unapaswa kujisalimisha zaidi kwa mamlaka ya Mungu katika maisha yako leo?**

## 2. UUMBAJI wa MBINGU na DUNIA
## Mwanzo 1:1-2:3

*Mwanzo*

Hapo mwanzo wa vitu vyote, Mungu alipoziumba mbingu na dunia, dunia haikuwa na umbo na ilikuwa tupu pia. Giza lilifunika vilindi vya maji. Roho wa Mungu alitulia juu ya maji.

*Siku Sita za Uumbaji*

Mungu akasema, "Iwe nuru," Ikawa nuru. Mungu akatenga nuru na giza. Akaita nuru "mchana," na giza "usiku." Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Jioni ikapita asubuhi ikaja, kwa hivyo siku ya kwanza.

Mungu akasema, "Iwe anga katikati ya maji kuyatenga maji yaliyo juu ya anga kutoka maji yaliyo chini ya anga." Ikawa hivyo. Mungu akaliita hilo anga "mbingu." Jioni ikapita asubuhi ikaja, kwa hivyo siku ya pili.

Mungu akasema, "Maji yaliyo chini ya mbingu yakusanyike mahali pamoja, ili inchi kavu ionekane." Ikawa hivyo. Mungu akaiita ardhi "nchi"; na akayaita makusanyiko ya maji "bahari"; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Mungu akasema, "Nchi ifunikwe kwa miti mizuri yote na kila aina ya mmea wa kijani uliokuwa mzuri kwa chakula." Mungu akaibariki ili ingezidi kuzaana kulingana na aina yao. Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Jioni ikapita asubuhi ikaja, kwa hivyo siku ya tatu.

Mungu akasema, "Mbingu ijazwe kwa mianga yote mbalimbali – mwanga mkubwa utawale mchana, na mwanga mdogo utawale usiku, na nyota zote." Huo mwanga mkubwa ulikuwa jua, na mdogo ulikuwa mwezi. Akaumba nyota. Akasema, "Mianga iwe ishara za siku na misimu na matukio." Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Jioni ikapita asubuhi ikaja, kwa hivyo siku ya nne.

Mungu akasema, "Mbingu ijazwe kwa viumbe vinavyopaa vyote na mabahari yajazwe kwa viumbe vinavyoogelea." Mungu akavibariki ili vingezidi kuzaana kulingana na aina yao. Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Jioni ikapita asubuhi ikaja, kwa hivyo siku ya tano.

Mungu akasema, "Nchi ijazwe kwa wanyama, wanyama wa mwituni, wanyama wa kufuga na wanaotambaa." Mungu akawabariki ili wangezidi kuzaana kulingana na aina yao. Mungu akaona ya kuwa ni vyema.

*Katika Mfano wa Mungu*

Mungu akasema, "Tuumbe mtu katika sura na mfano wetu. Tutamwumba wa kiume na wa kike na tutawapa mamlaka juu ya uumbaji wote." Kwa hivyo Mungu alifanya hivyo. Mungu akawabariki ili wangezidi kuzaana na wajaze dunia. Mungu akawapa kila mmea wa kijani kwa chakula. Na Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na kilikuwa chema sana. Jioni ikapita asubuhi ikaja, kwa hivyo siku ya sita.

*Pumziko la Mungu*

Kwa siku ya saba, Mungu alikuwa amemaliza kazi yake yote ya uumbaji. Kwa hivyo alipumzika. Hii ndiyo sababu Mungu alitenga siku ya saba kwa sababu hii ndiyo siku alipumzika baada ya uumbaji.

## TOLEO FUPI LILILORAHISISHWA

Hapo mwanzo wa vitu vyote, Mungu alipoziumba mbingu na dunia, dunia haikuwa na umbo na ilikuwa tupu pia. Giza lilifunika vilindi vya maji. Roho wa Mungu alitulia juu ya maji.

Mungu akasema, "Iwe nuru," Ikawa nuru. Mungu akatenga nuru na giza. Akaita nuru "Mchana," na giza "Usiku." Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Ilikuwa siku ya kwanza.

Siku ya pili, aliumba anga kwa kugawanya maji yaliyo juu na maji yaliyo chini.

Siku ya tatu, aligawanya bahari na nchi kavu na akaumba mimea na miti yote mizuri kwa chakula.

Siku ya nne, aliumba mianga angani - jua litawale mchana, mwezi utawale usiku, na nyota. Alizifanya kuwa ishara kwa siku, majira na matukio.

Siku ya tano akafanya ndege na samaki.

Siku ya sita, alifanya mambo makubwa mawili. Kwanza aliumba wanyama wote wanaotembea ardhini. Na kila wakati alipoumba kiumbe hai - mmea, ndege, samaki, au mnyama - alikbariki kuwa na uwezo wa kuzaana kulingana na aina yake. Na karibu kila siku alipomaliza kuunba kitu alisema, "Ni nzuri."

Kisha, pia katika siku ya sita, Mungu akasema, "Tuumbe mtu katika sura na mfano wetu." "Tumwumbe wa kiume na wa kike na tuwape mamlaka juu ya uumbaji wote." Kwa hivyo Mungu alifanya hivyo. Mungu akawabariki ili wazidi kuzaana na wajaze dunia. Mungu akawapa kila mmea wa kijani kwa chakula. Na Mungu akaona ya kuwa ni nzuri sana. Hiyo ilikuwa siku ya sita.

Kwa siku ya saba, Mungu alikuwa amemaliza kazi yake yote ya uumbaji. Kwa hivyo alipumzika. Hii ndiyo sababu Mungu alitenga siku ya saba kwa sababu hii ndiyo siku alipumzika baada ya uumbaji.

### MPANGILIO wa SOMO

**<u>UTANGULIZI:</u>** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Mwanadamu na wanyama wana tofauti gani? Kwa nini unafikiri mwanadamu ni maalum?**

**<u>HADITHI:</u>** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**<u>MJADALA baada ya HADITHI:</u>** Ongoza mjadala ukiongozwa na maswali haya:

### MASWALI ya KUJADILIANA

**<u>Tunajifuza nini kuhusu MUNGU?</u>**

- **Je hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye mamlaka yote kwa jinsi gani?**

    - Mungu aliumba kila kitu. (Nuru, mbingu, ardhi, bahari, jua, mwezi, Nyota, mimea, miti, Ndege, Samaki, Wanyama na Mwanadamu).
    - Mungu hana mwanzo, wala hakuumbwa, naye amekuwepo daima.
    - Aliviumba pasipo kutumia kitu. Hakuwa na chochote cha kutumia katika kuumba vitu hivi.
    - Mungu alisema tu, na vitu vyote vikaumbika. Viliumbika kwa uwenzo wa neno lake.
    - Mungu alimwumba Adam kutoka kwa mavumbi na mwanamke kutoka kwa ubavu wa Adam.
    - Aliumba kila kitu kwa hivyo ana mamlaka juu ya kila kitu.
    - Mungu alihifadhi vyote alivyoviumba
- **Hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu na yuko kila pahali?**
    - Mungu alijua jinsi ya kuumba kila kitu na vitu vyote.
    - Mungu alijua jinsi ya kuumba mahali ambapo panafaa kwa mahitaji yote ya mwanadamu.
- **Je hadithi hii inaonyesha kwamba mungu ni mtakatifu? (mkamilifu, mwenye haki, mtoa sheria, anachukia dhambi, na kudai kifo kama malipo ya dhambi?)**
    - Kila kitu ambacho mungu aliumba kilikuwa kikamilifu.
    - Mungu alimwumba Adamu kwa mfano wake, bila dhambi.
- **Je hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (mwenye upendo,mwenye huruma, kwa wenye dhambi? Mkarimu na mwenye kuwasiliana na mwanadamu?)**
    - Mungu akamwumba msaidizi mmoja aliyemfaa Adam.
    - Mungu akawapa Adamu na Eve kila mmea kwa chakula.
    - Mungu alimfanya mwanadamu kama yeye, a awe na uhusiano na Mungu

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- Hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa mungu?
    - Alimwumba mwisho.
    - Akampa msaidizi maalumu.
    - Alimpa mamlaka juu ya chote kilichoumbwa
    - Alimpa chakula na chote alichohitaji.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima):</u>**

- Tunaonaje nguvu za Mungu zikionyeshwa leo? **(Tazama Zaburi 19.)**

- Je, bado tunaona uthibitisho gani katika ulimwengu wa utakatifu wa Mungu? Au kwamba Yeye habadiliki? Au kwamba Yeye bado ni Mungu wa utaratibu? Kwa hiyo ikiwa kweli Mungu ni mtakatifu, hilo linapaswa kutufanya tujisikie na kuitikiaje?

- **Chukua wakati wa kutazama uumbaji kwa ukaribu, uone jinsi ulivyo mzuri na mkubwa, au jinsi ulivyoumbwa kwa undani tata. Je hili linakufanya kujihisi vipi? Au kuhisi vipi kumhusu Mungu?**

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Je, ni kwa njia zipi bado unaona neema ya Mungu au fadhili zake kwa maisha yako leo? Ni baraka gani umepokea kutoka kwa Mungu hivi karibuni?** Je, hii inapasa kuathiri vipi mtazamo wako kwa Mungu? Je, hii inapasa kuathiri vipi mtazamo wako kuhusu jinsi unavyoishi siku baada ya siku?

- Neno la Mungu, yaani Biblia, hutuambia sote kumhusu Mungu na jinsi ya kumjua na kumwishia. **Je, utachukua hatua gani katika maisha yako ili kumjua Yeye zaidi?**

# 3-A. UUMBAJI WA MWANAMUME NA MWANAMKE
## Mwanzo 3

Katika mwanzo wa vitu vyote, Mungu alipoziumba mbingu na dunia, aliumba mwanamume na mwanamke siku ya sita. Hivi ndivyo alivyofanya!

Mungu akamfanya mwanamume kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai. Jina lake lilikuwa Adamu. Mungu pia alipanda bustani maalum iliyoitwa Edeni. Ndani yake alipanda kila aina ya miti mizuri ambayo ilikuwa nzuri kwa chakula. Katikati ya bustani alipanda miti miwili maalum, Mti wa Uzima na Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya.  Basi Mungu akamchukua mwanamume akamweka ndani ya bustani ailime na kuitunza.

Mungu akamwambia, "Ule matunda kutoka kila mti ndani ya bustani, lakini usile matunda kutoka mti uliomo katikati ya bustani uitwao mti wa ujuzi wa mema na mabaya, kwa sababu siku utakayokula hakika utakufa."

Kisha Mungu akasema, "Si vyema huyo mtu awe peke yake. Nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye." Mungu akamletea Adamu viumbe vyote vipite mbele yake.  Adamu akakipa kila kiumbe jina lake. Lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye.

Basi Mungu akamletea Adamu usingizi mzito. Alipokuwa akilala, Mungu akatwaa ubavu wake na akafunika pahali hapo kwa nyama. Na kutoka ubavu Mungu akamwumba mwanamke.  Adamu alipoamka, Mungu akamletea mwanamke. Adamu alipomwona yule mwanamke, akasema, "Hatimaye! Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu. Basi, ataitwa mwanamke kwa maana ametwaliwa katika mwanamume."

Kwa sababu hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye atajiunga na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. Adamu na mkewe walikuwa uchi wote wawili, wala hawakuona haya.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- Fikiria uhusiano fulani katika maisha yako ambao ni muhimu sana kwako. Mwambie jirani yako kuhusu hilo na kwa nini mtu huyu ni wa pekee sana.

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**MASWALI ya KUJADILIANA**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu alimuumba mwanamume kutoka mavumbi ya ardhi.
    - Mungu alimpa uhai kupitia kumpulizia uhai huo.
    - Mungu alimwumba mtu, kwa hivyo ana mamlaka juu yake.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali? Vipi?**
    - Mungu alijua jinsi ya kumuumba mwanamume na mwanamke.
    - Mungu alijua jinsi ya kumwumbia mwanamume msaidizi mkamilifu.
    - Mungu alijua kwamba mwanamume alikuwa na upweke.
- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?) Kwa jinsi gani?**
    - Kila kitu ambacho Mungu alichoumba kilikuwa kikamilifu.
    - Mungu alimuumba Adamu kama yeye mwenyewe, bila dhambi.
    - Mungu alimpa sheria kuhusu mti wa ujuzi wa mema na mabaya, na akaahidi adhabu kwa kutotii.
    - Adhabu ya kutotii ni mauti. Mungu hawezi kustahimili dhambi.
- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?) Kwa jinsi gani?**
    - Mungu alimuumba Yule aliyekuwa mwenzake wa Adamu aliyefaa.
    - Mungu aliwapa Adamu na Hawa kila jani la mti kama chakula isipokuwa moja.
    - Mungu akawapa mahali pazuri pa kuishi
    - Mungu aliongea na Mwanadamu

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>** (kutoka hadithi hii pamoja na Mwanzo 1)

- Mwanzo 1 inatuambia kwamba Mungu:
    - Alimfanya mtu kwa mfano wake.Mwanadamu ni wa pekee sana kwa Mungu. Yaani, mwanadamu ana roho kama Mungu (pamoja na mwili). Ana uwezo wa kumjua, kumpenda, na kumtii Mungu.
    - Alimbariki mwanadamu kwa mwenzi, kwa mamlaka juu ya viumbe vingine vyote, kwa chakula.
- Mungu ana mamlaka juu ya mwanadamu.
- Mwanadamu alibarikiwa kuwa na uwezo wa kuwasiliana na Mungu..
- Alibarikiwa na kazi ya kufanya, yaani kujaza dunia na kutawala juu yake.
- Anapaswa kuishi katika uhusiano na mwenzake, hasa katika ndoa.
- Mwanamume na mwanamke waliumbwa kamilifu, bila dhambi. Walikuwa uchi na hawakuona haya.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Je, unaonaje nguvu na upendo wa Mungu leo kwa jinsi alivyokuumba wewe au mtu unayempenda? Je, hilo linakufanya uhisi vipi kumhusu Mungu na kujihusu wewe mwenyewe?
    - Je, uwezo wake unaweza kukusaidiaje katika maisha yako? Je ,nguvu zake zinawezaje kukuumiza?

- Mungu hajabadilika. Naye bado ni mtakatifu na anachukia dhambi. Pia anajua dhambi zako. Je, haya yanakufanya uhisije? Je, linaathirije maisha yako?

- Nani alianzisha ndoa? Je, hilo litakusaidia vipi kuzielewa ndoa zetu?
    - **Ikiwa ndoa yako imejengwa juu ya msingi wa Neno la Mungu, inaweza kuwa tofauti jinsi gani na ndoa zingine za utamaduni wenu?**
    - Adamu alipompokea mwanamke, alifurahi sana. Wanaume, je, mnathamini nini kuhusu wake zenu? Je, mnawaonyeshaje shukrani na upendo wenu?
    - Wanawake, je, unamthamini na kumheshimu mume wako kama kiongozi na mtunzaji wako?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- Je, Mungu amepeana sheria zozote ambazo anataka uzitii lakini ni vigumu kuzifuata?
- **Unamheshimuje Mungu katika ndoa yako? Unakosa kumuheshimuje Mungu katika ndoa yako?**

## 3-B. MWANAMKE NA NYOKA
## Mwanzo 3

*Mjaribu*

Nyoka alikuwa mwerevu zaidi katika wanyama wote Mungu aliowafanya. Siku moja, mwanamke alikuwa ndani ya bustani. Nyoka alimwendea akasema, "Ati, hivi ndivyo alivyosema Mungu, 'Msiyale matunda ya miti yote ya bustani?'"

Mwanamke akamwambia nyoka, "Hapana. Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula, lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema 'Msiyale wala msiyaguse msije mkafa.'"

Nyoka akasema, "La! Si kweli. Mungu anajua kwamba utakapoyala matunda ya mti huu, utakuwa mwerevu kama yeye."

Mwanamke akauona mti. Akaona kwamba ulipendeza kwa macho na ulifaa kwa chakula. Na ungesaidia kupata hekima. Kwa hivyo, alilichukua tunda na akalila akampa mume wake aliyekuwa naye, naye akala pia. Punde, macho yao yalifumbuka, wakaona ya kuwa walikuwa uchi. Kwa hivyo walikimbilia msituni na wakatwaa majani kufunika miili yao.

*Kujificha*

Wakati huo, walimsikia Mungu akitembea katika bustani. Akamwita mwanamume, "Uko wapi?"

Adamu akasema, "Nilikusikia na nikaogopa, kwa hiyo nikajificha kwa kuwa niko uchi."

Mungu akasema, "Ni nani aliyekuambia kwamba uko uchi? Je, umeyala matunda kutoka mti ambao nilikuagiza usile?"

Adamu akasema, "Huyu mwanamke uliyenipa alinipa tunda nami nikala."

Kisha Mungu akamwambia mwanamke, "Umefanya nini?"

Mwanamke akasema, "Nyoka amenidanganya nami nikala."

*Laana, Rehema, na Utengano*

Basi Mungu akamwambia nyoka, "Kwa sababu ya yale umefanya, umelaaniwa! Utatambaa kwa tumbo lako kwa siku zako zote. Utakula mavumbi ya ardhi. Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino."

Kisha Mungu akamwambia mwanamke, "Kwa sababu ya yale umefanya, umelaaniwa!  Utakuwa na uchungu unapozaa. Tamaa yako itakuwa dhidi ya mumeo, naye atakutawala."

Kisha Mungu akamwambia Adamu, "Kwa sababu umemsikiliza mkeo na hukunisikiliza, wewe pia umelaaniwa na nchi imelaaniwa kwa sababu yako! Utafanya kazi ngumu siku zote za maisha yako ukitoa jasho, na miiba na mimea isiyofaa itakua. Kisha utakufa!  Utarudi mavumbini ambamo ulitwaliwa."

Wakati huo, mwanamume akampa mwanamke jina jipya. Akamwita Hawa, kwa kuwa yeye ndiye alikuwa mama yao wote walio hai.

Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi akawavika.

Kisha Mungu akasema, “Mtu huyo sasa amekuwa kama mmoja wetu kwa kujua mema na mabaya. Sharti asiruhusiwe kuchukua matunda ya mti wa uzima na kula na kuishi milele.” Kwa hivyo Mungu aliwafukuza kutoka bustanini, kisha akamweka malaika na upanga wa moto uliogeuka huko na huko kuilinda njia ya mti wa uzima.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Fikiria wakati ulijaribu kuficha kitu kutoka kwa mtu ambaye alikuwa na uwezo wa kukuadhibu? Hilo lilihisije?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**MASWALI ya KUJADILIANA**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
  - Alikuwa na mamlaka na uwezo wa kuwafukuza Adamu na Hawa kutoka bustanini.
  - Alikuwa na mamlaka ya kuadhibu dhambi kupitia kwa laana na kuwafukuza.
  - Aliweka malaika wake kuzuia mwanadamu kuingia katika Edeni tena.
  - Mungu ana mamlaka kuziunda sheria ambazo mwanadamu anapaswa kuzitii.
  - Mungu alikuwa na mamlaka juu ya shetani.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
  - Mungu alijua kwamba walikuwa wamekula tunda walilokatazwa.
  - Alijua kingechotokea ikiwa wangeweza kula tunda la mti wa uzima.
  - Mwanamume na mkewe hawezi kujificha kutoka Mungu.
  - Alijua kuwa nguo zile za ngozi zingewapa kibali mbele yake na kuficha uchi wao

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
  - Mungu huunda sheria. Kuna sheria za wema na uovu.
  - Mungu huadhibu wale wasiotii. Adhabu ya dhambi ni mauti au kifo.
    - **Je, Mungu alimaanisha nini aliposema, “Kifo” kwa kutotii?**
      - Kutengwa kiroho kutoka kwa Mungu.
      - Kutengwa kimwili na Mungu katika kifo cha mwili. (Alisema, “kisha utakufa na kurudi mavumbini.”
      - Adhabu ya milele katika ziwa la moto.
  - Laana za Mungu juu yao na juu ya ardhi na juu ya nyoka.
    - **Je, bado leo tunaonaje ushahidi wa laana kwa mwanamume na mwanamke?**
      - (Matatizo ya kimahusiano kati ya mume na mke (migogoro, vita, chuki, wivu n.k), uchungu wa kuzaa (magonjwa, uchungu), kazi ngumu na jasho (ukame, njaa, matatizo ya kiuchumi), na kila tatizo lingine lililoingia ulimwengu.)
    - **Ushahidi wa kifo kama Mungu alivyomwahidi Adamu umeingia ulimwengu. Kwa njia gana?**

        - Kwa mara ya kwanza 1) waliona aibu, 2) walikuwa wamejificha, 3) walikuwa wanalaumiana wakajaribu kuzificha dhambi zao. 4) walikuwa wanajaribu kukutana na mahitaji yao wenyewe, kusuluhisha shida zao wenyewe (walipotumia majani kuficha uchi) badala ya kumtegemea Mungu kikamilifu.
        - Laana kwa mwanamume na mwanamke kama shida za uhusiano kati ya mume na mke, na utungu katika kuzaa, na kazi ngumu na jasho na kila shida iliyoingia katika dunia.
        - Walifukuzwa kutoka bustanini.  Na ushirika kati yao na Mungu ulivunjika.
    - Mungu hangeruhusu mwanadamu mwenye dhambi kuwa pamoja naye.
    - Nguo ambazo Adamu na Hawa walitengeneza kuficha uchi wao hazikukubalika kwa Mungu. Hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kujifanya akumbalike na Mungu. Hakuna awezaye kuficha dhambi yake mwenyewe.
    - Nguo za pekee ambazo zilikubalika kwa Mungu ni zile alizotengeneza mwenyewe. Nazo zilitengenezwa kupitia kwa kifo cha mnyama kwa niaba ya mwanadamu mwenye dhambi. Damu ilimwagika ili kutengeneza nguo hizi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema?  (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu kwa neema aliwapatia nguo zilizokubalika kwa wao hata ingawa hawakuzistahili. Alitoa mnyama badala yake afe badala ya Adamu na Hawa.
    - Mungu hakuwaua papo hapo.
    - Kupitia kwa laana kwa nyoka tumeona ahadi ya kwanza ya siri ya mwokozi ambaye atakuja kupitia uzao wa mwanamke ambaye hatimaye atamshinda shetani, Mwongo aliyeleta mauti. Huyu angekuwa Mwokozi ambaye atabatilisha laana ilyoko kwa mwanadamu.
    - Mungu akawapa nafasi ya kutubu.  (Alijua pahali walikuwa kabla ya kuwauliza, lakini alikuwa akiwapa muda wa kutubu na kukubali dhambi yao.)

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu?  (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?).**
    - Mungu alisema kwamba kula tunda kutaleta mauti, na hilo likafanyika. Walitenganishwa na Mungu kiroho.
    - Mungu alitoa ahadi ya Mwokozi ambaye atakuja, uzao wa mwanamke atakayeponda kichwa cha shetani, na ataondoa laana zote zilizofuata wakati mwanadamu alipotenda dhambi.

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu?**
    - Mungu alikuwa na huruma kwake kupitia ngozi ya mnyama, kupitia nafasi zaidi ya kutubu, kupitia kwa mwokozi ambaye atakuja.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi?  Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Mwanadamu alijaribiwa kuwa kama Mungu. Yeye ni mwenye kiburi  na kujiona yeye tu.
    - Mwanadamu alikataa kukubali mamlaka ya Mungu.
    - Mwanadamu aliona aibu na kujificha.
    - Walianza kulaumiana kwa ajili ya dhambi zao.
    - Walianza kujaribu kujiokoa kupitia kukutana na mahitaji yao wenyewe (mavazi ya matawi) badala ya kumtegemea Mungu kama vile walivyofanya hapo <u>awali</u>.
    - Mwanadamu alileta kifo ulimwenguni kupitia kwa dhambi zake. (Kifo cha mnyama)

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Mungu alikataa kukubali nguo zao wenyewe, na lazima atoe njia mwenyewe. Mungu hata aliwavalisha.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- Wokovu huja tu kwa njia ya Mungu. Bidii zao za kufunika shida zao zilishindwa. Lazima Mungu awapatie nguo hata Mungu akawavalisha. Lazima mwanadamu kunyenyekea na kukubali kile ambacho Mungu amepeana.
- Utoaji wa Mungu wa wokovu ni kupitia dhabihu ya damu kupitia kifo cha niaba ya mtu mwingine.
    - Mwanadamu alikukubalika kupitia umwagikaji wa damu. Damu ya mnyama ambaye aliuwawa ilisaidia kuwafanya wakubalike.
        - Hii ilielekeza kwa mwokozi ambaye angekuja na kumwaga damu yake kwa ajili ya mwanadamu.
- Mwanadamu anaweza kutumaini tu kwamba ahadi za Mungu za Mwokozi ni kweli.

**Tunajifunza nini kuhusu Shetani kutoka hadithi hii?**

- Anamchukia Mungu na ni mwongo.
- Anamchukia mwanadamu.
- Ni mwongo Anayejifanya, husema ukweli nusu.
- Humjaribu mwanadamu kujitegemea.
- Huleta mashaka kwa mawazo ya mwanadamu.
- Huleta mitego.
- Humwita Mungu mwongo.
- Hufanya uzuri kuonekana mbaya na kubadili ukweli.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Ingawa tunaona kwamba Mungu anajua kila kitu, bado tunajaribu kuzificha dhambi zetu kutoka kwa Mungu na watu wengine. Tunajifunika majani tukijaribu kuficha aibu na hatia zetu na kutaka kukubaliwa na watu wengine **Je,,kama wakristo tunajaribu KUJIFICHA kutoka kwa Mungu kwa njia zipi?**
- ➢ **Je, huwa unawalaumu wengine kwa dhambi zako?Unajilinganisha na wengine?Unandanya? unatoa visababau na masengenyo?** Je! hadithi hii inaweza kukusaidiaje kutoka mafichon na kukiri dhambi zako kwa Mungu na wenzako?
    - Njia nyingine ya kuuliza swali hilo ni hii: **Je, watu leo bado wanajaribu njia mbalimbali ili wakubaliwe na Mungu na watu wengine?** (Yaani. Je, ni baadhi ya aina gani za “majani ya mtini” ambayo watu hutumia kufunika dhambi zao?) Je, kweli Mungu huwakubali watu wanapojaribu kumpendeza kwa njia zao wenyewe? **Ni njia zipi umekuwa ukijaribu kujifanya ukubalike kwa Mungu peke yako badala ya njia yake?**
- Je, Shetani hutumia njia gani leo kuwadanganya watu?Je vipi katika tamaduni au kijiji chako?
- Je, ni njia gani hasa huwa tunajaribiwa kuchukua nafasi ya Mungu katika eneo fulani la maisha yetu na kujitawala?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- Nikwa njia gani unajaribu kuficha aibu yako kutoka kwa Mungu?Hadithi hii inawezaje kukusaidia kutoka mafichoni
    - Unaonaje kiburi katika maisha yako mwenyewe? Unawezaje kutubu juu yake?
- **Shetani hukudanganya vipi wakati mwingine? Je, ni uongo gani kuhusu Mungu au wewe mwenyewe unaoshawishiwa kuamini? Unajaribiwa vipi kuchukua nafasi ya Mungu katika sehemu fulani za maisha yako? Utatubuje?**

## 4. KAINI NA HABILI
## Mwanzo 4

Baada ya Mungu kuwafukuza Adamu na Hawa kutoka bustanini, Hawa alipata mimba na akamzaa mwana. Wakamwita mvulana huyo Kaini. Baadaye, Hawa alimzaa mwingine aliyeitwa Habili. Kaini alipokua akawa mkulima. Habili naye alipokua akawa mchungaji wa wanyama.

Siku moja wote wawili walimletea Mungu dhabihu. Kaini alileta sadaka kutoka shambani mwake baadhi ya matunda na mboga. Habili naye alileta sehemu nono ya wazaliwa wa kwanza wa kondoo wake. Alizitoa kama dhabihu na damu ilimwagika.

Mungu aliikubali dhabihu ya Habili lakini hakuikubali dhabihu ya Kaini. Kaini alighadhabika sana. Mungu akamwuliza Kaini, "Kwa nini umekasirika? Ukifanya yaliyo mema, je, hutakubalika? Lakini ukifanya maovu, dhambi inakuvizia mlangoni mwako, inakutamani wewe, lakini inakupasa uishinde."

Baadaye Kaini akamwambia kakake Habili, "Twende uwanjani." Walipokuwa wakitembea uwanjani, Kaini alimwua Habili, kisha akaenda zake.

Baada ya mkasa huo, Mungu akamwuliza Kaini, "Kaka yako Habili yuko wapi?" Kaini akasema, "Sijui. Je, mimi ndimi humtunza?" Kisha Mungu akasema, "Damu ya kakako inanililia kutoka ardhini! Umelaaniwa! Nchi haitakutolea mazao. Lazima uondoke pahali hapa na kuzurura huku na huko duniani."

Kaini akasema, "Aaa, jambo hili ni gumu sana kwangu, umenifukuza kutoka duniani. Umenifukuza kutoka uwepo wako, na yeyote atakayeniona ataniua."

Kisha Mungu akaiweka alama kwa Kaini na akasema, "Yeyote atakayemwua Kaini nitamlipiza mara saba."

Kisha Kaini akaondoka akazurura huku na huko. Baadaye Kaini alipata watoto. Walikuwa waovu na hawakumwabudu Mungu.

Nao Adamu na Hawa wakapata mwana mwingine aliyeitwa Sethu mahali pa Habili aliyekufa. Lakini wengi wa familia ya Sethu walimwabudu Mungu.

### MPANGILIO wa SOMO

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kufikiria wakati ambapo ulikuwa na wivu sana na mtu mwingine na wivu wako ukasababisha ufanye jambo baya? Jadili na jirani yako.**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**MASWALI ya KUJADILIANA**

__Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?__

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu ana mamlaka ya kutarajia utiifu wetu kwa sababu alituumba. Mungu alikuwa na mamlaka na uwezo wa kumfukuza Kaini.
    - Alikuwa na mamlaka ya kuamuru dhabihu inayofaa ili kumwendea katika kumwabudu.
    - Alikuwa na nguvu ya kuweka alama kumlinda Kaini.
    - Alikuwa na mamlaka ya kuwapa Adamu na Hawa Sethi pahali pa Habili.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Mungu alijua mawazo maovu ya moyo wa Kaini - hasira na wivu wake.
    - Alijua mawazo mazuri ya moyo wa Habili, na dhabihu inayofaa.
    - Mungu alijua kile Kaini alikuwa amefanya akasema, "Damu ya nduguyo inanililia."

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Mungu aliadhibu dhambi ya Kaini kwa kumfukuza na kulaani ardhi aliyoilima.
    - Mungu anaweza kuendewa tu katika njia anayotaka. Anadai dhabihu inayofaa. Mwanakondoo mzaliwa wa kwanza ambaye damu yake itamwagwa. Anaweza kuendewa tu kwa imani.
    - Mungu aliiheshimu na kuikubali dhabihu ya Habili ambayo ilitolewa kwa imani.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu alimpa Kaini nafasi ya kutubu na alimwuliza ndugu yake alikuwa wapi. Pia alimwonya kwamba dhambi inamvizia mlangoni pake.
    - Mungu alitoa njia kwa mwanadamu kumrudia katika uhusiano naye kupitia kwa dhabihu inayofaa.
    - Mungu anawasiliana na mwanadamu kumwagiza jinsi ya kumwendea katika kumwabudu.
    - Mungu akamwekea Kaini alama ya kumlinda hata iwapo hakuistahili.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.**
    - Mungu alikuwa mwaminifu kwa Adamu na Hawa kwa kuwapa Sethi pahali pa Habili.
    - Alikuwa mwaminifu pia kwa ahadi zake kwa kumtuma mwokozi ambaye atakuwa uzao wa mwanamke atakuja kupita jamaa wa Sethi.
    - Alitimiza ahadi yake ya kumlinda Kaini.

__Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?__

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu?**
    - Mungu alitaka uhusiano nao, akafanya njia ili waweze kumwendea.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Kaini na Habili walizaliwa wapi?
        - Nje ya bustani. Wakazaliwa kama wenye dhambi kwa sababu ya wazazi wao walizaliwa nje ya ushirika na Mungu na mioyo ambayo tayari inapenda kufanya uovu.

        - Wanadamu wote wamezaliwa katika dhambi nje ya bustani, nje ya uhusiano na Mungu.
        - Tazama!  Hata Habili alikuwa mwenye dhambi!  Alipaswa kuja kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu.
    - Kaini alitaka kumwendea Mungu katika njia yake mwenyewe.  Hakuleta dhabihu bora.  Hakuja kwa imani.
    - Kaini akawa mwenye chuki na wivu.  Kaini alikuwa mwuuaji kama Shetani, babake wa kiroho.

- ▪ Je, Mungu anaielezea dhambi kwa Kaini kama nini?
    - Kama mwizi anayekuotea.  Hii inatuambia nini?  Kupigana na dhambi ni vita! Lazima tumtegemee Mungu kutusaidia!

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Ndiyo.  Kaini alipojaribu kumwendea Mungu katika njia yake mwenyewe alikataliwa.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- **Hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu?  (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Habili alimwendea Mungu katika njia ya Mungu, yaani kupitia imani iliyothibitishwa katika dhabihu ya damu. Alikubaliana na Mungu kwamba yeye ni mwenye dhambi. Halafu alikubaliwa.
    - Inawezekana Habili alikuwa ameagizwa na wazazi wake jinsi ya kumwendea Mungu, njia Mungu alikuwa amewambia.
    - Kaini alikuja katika njia yake mwenyewe na hakukubalika.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa?**
    - Habili alikubaliwa na Mungu kwa sababu ya imani yake ambayo ilionyeshwa kwa aina ya dhabihu aliyoileta (yaani dhabihu ya damu, na ya kwanza na bora zaidi) alikuja akiwa amenyenyekea, akikubali dhambi zake na kutojiweza akionyesha imani katika mwokozi ambaye atakuja kwa kuleta dhabihu iliyofaa.  (Wahebrania 11:4, 6)

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- **Ni njia gani mahususi ambayo wakati mwingine tuna ruhusu dhambi kuja na kuingia katika maisha yetu?**
    - Je, unaweza kufikiria wakati, hata sasa, ambapo dhambi imeingia ndani ya moyo wako na ikakutawala kwa muda?
    - Ni njia gani dhambi hugandamiza watu siku hizi?
    - **Tunajifunza nini katika hadithi jinsi ya kukataa mvuto wa dhambi maishani mwetu?**

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je, ni kwa njia gani hasa dhambi hukunyemelea na kuingia katika maisha yako?**
    - ▪ Je unaweza fikiria wakati hivi majuzi dhambi ilingia moyoni mwako na ikakutawala kwa muda?
- **Je, kuna dhambi fulani ya mara kwa mara katika maisha yako ambayo unapambana nayo?** Je, inakudanganya kukutawala vipi ? Imani na toba vinawezaje kukusaidia kuishinda?

## 5. NUHU NA GHARIKA
## Mwanzo 6-9

*Man's Wickedness / God's Plan to Punish*

Baada ya Mungu kumlaani Kaini, Kaini alipata mke nao wakapata watoto. Sethu naye pia alipata mke nao wakazaa watoto. Baada ya vizazi vingi, watu wakawa wengi ulimwenguni. Watu wengine walimpenda Mungu lakini wengi wao waliasi dhidi ya Mungu. Kila mara walikuwa wakipigana.

Mungu akaona kwamba mawazo yote ya moyo wa mwanadamu yalikuwa maovu wakati wote. Mungu alipoona jinsi kazi za mwanadamu zilivyojaa uovu, alisema, "Nitaangamiza kila kitu nilichoumba, mwanadamu na wanyama pia."

*Kazi ya Nuhu*

Lakini Nuhu alipata kibali machoni pa Mungu. Alikuwa mtu mwenye haki aliyetembea na Mungu. Mungu akamwambia Nuhu, "Ninasikitika kwamba niliwahi kumwumba mwanadamu. Nitaangamiza vitu vyote ambavyo vimeumbwa kwa sababu watu wamekuwa waovu, lakini nitafanya agano na wewe. Ni wewe tu, na mke wako, na wanao watatu, na wake wao ambao wataishi.

"Nataka ujenge mashua kubwa inayoitwa safina, kwa sababu nitaleta gharika kubwa itakayoangamiza ulimwengu. Lazima uchukue kila aina ya mnyama na ndege wa kiume na kike. Pia, kwa wanyama ambao wanafaa kwa kutoa dhabihu, lazima uweke wakiume saba na wakike saba. Ulete vyakula pia."

Mungu alimwambia Nuhu jinsi ya kujenga safina hiyo. Naye Nuhu akafanya yote ambayo Bwana alimwamuru afanye. Nuhu alitumia miaka mingi kujenga mashua hiyo. Siku moja Mungu akamwambia Nuhu kwamba yeye na jamaa wake wachukue wanyama wote na ndege waingie katika safina. Kisha Mungu akafunga mlango uliokuwa mmoja tu.

*Mvua na Kusubiri*

Kwa siku arobaini na usiku arobaini maji yaliyo juu yalinyesha chini na maji yaliyo chini yalifunguka yakaja juu ya ardhi. Kila kitu kilifunikwa kwa maji hata milima iliyokuwa mirefu zaidi, na hapakuwa na njia kwa watu kuepuka, kwa hivyo wote walizama wakafa maji. Lakini Nuhu na familia yake na wanyama katika safina walikuwa salama, wakielea juu ya maji.

Baada ya siku arobaini Mungu akamkumbuka Nuhu na akasimamisha maji. Kwa miezi mingi Nuhu alikuwa katika mashua. Baada ya mwaka mmoja mafuriko yakarudi chini, safina ikatua juu ya mlima.

*Baraka ya Mungu*

Kisha Mungu akamwambia Nuhu, "Toka ndani ya safina." Naye Nuhu, na familia yake, na wanyama wakatoka ndani ya safina. Nuhu akajenga madhabahu na akamtolea Mungu dhabihu akimwabudu. Mungu alipendezwa na dhabihu yake. Mungu akasema, "Kamwe sitauangamiza ulimwengu tena kwa gharika. Ninauweka upinde wa mvua

angani kama ishara ya ahadi yangu."  Mungu akambariki Nuhu na wanawe, akawaambia, "Mkaongezeke, mkaijaze nchi."

Mungu akamwambia Nuhu, "Sasa ninawapa wanyama kwa chakula. Bali msile damu ya mnyama, kwa sababu ni uhai wake. Atakayemwaga damu ya mwanadamu, damu yake pia itamwagwa na mwanadamu, maana kwa mfano wake Mungu alimfanya mwanadamu."

Wana wa Nuhu wakapata watoto wengi na wakati ulipoendelea kupita, kukawa na watu wengi ulimwenguni tena.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kufikiria wakati ambapo mtu fulani alikupa maagizo marefu na magumu kuhusu jinsi ya kufanya jambo fulani? Je, maagizo yalikuwa magumu kufuata? Je, ulijaribiwa kukata tamaa?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala ukiongozwa na maswali haya:

**MASWALI ya KUJADILIANA**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu ana mamlaka ya kutarajia utiifu wetu kwa sababu alituumba.  Mungu alikuwa na
    - Uwezo wa kuharibu kila kitu na Kuyadhibiti maji ya gharika.
    - Alikuwa na haki ya kuharibu kwa sababu alikuwa mwumbaji?
    - Alianzisha mvua, maji kutoka chini.
    - Alisimamisha gharika.
    - Akabariki Nuhu na wanawe kuzaana.
    - Alimwambiwa atakapoingia na  atakapoondoka.

- **Hadithi hii inatuonyesha Ujuzi wa Mungu na yupo kila mahali?**
    - Alijua uovu wa mwanadamu hata mawazo yake yote.
    - Alijua jinsi ya kujenga safina [Nuhu hakuwa ameona kitu kama hicho, labda hakuwa ameona bahari.
    - Alijua wanyama waliofaa kutolewa kama dhabihu

- **Hadithi hii inatuonyesha UTAKATIFU wa Mungu? (haki, anachukia dhambi, lazima ahakumu au aadhibu dhambi)**
    - Aliadhibu dhambi. Akawaangamiza watu.
    - Akatoa amri – kuhusiana na umwagikaji wa damu.
    - Amri kamili kuhusu jinsi ya kujenga safina. Nuhu hangeweza kuijenga katika njia nyingine yeyote na ampendeze Mungu?
        - Njia za Mungu ni nzuri kwetu? Ndio hata hapa tunaona ukarimu na neema yake.
    - Mungu akaufunga mlango. Hapakuwa na yeyote ambaye angeweza kuufungua tena. Neema yake ya toba inapatikana kwa muda mfupi tu kwa kila mtu.

- **Hadithi hii inatuonyesha NEEMA ya Mungu? (huruma, anawasiliana na mwanadamu ukarimu na wema).**
    - Alingoja kwa subira kwa miaka mingi nafasi ya kutubu.
    - Aliwasiliana na Nuhu akamwonya.
    - Neema kwa Nuhu, ambaye pia ni mwenye dhambi.
    - Alimwonyesha kikamilifu jinsi ya kuunda safina salama na inayofaa.
    - Akampa Nuhu kila kitu ambacho alikihitaji katika safina na hata baadaye.
    - Akaahidi kwamba kamwe hataharibu dunia tena kwa maji.
    - Akakubali sadaka ya Nuhu.
    - Akaruhusu familia ya Nuhu kuongezeka Akawabariki.

- **Hadithi hii inatuonyesha UAMINIFU wa Mungu? (kutobadilika)**
    - Mungu aliileta mvua kuharibu ulimwengu jinsi alivyoahidi.
    - Upinde wa mvua ni ishara ya ahadi za Mungu kutoharibu ulimwengu tena kwa maji.
    - Hii inatuambia nini kuhusu Mungu? Mungu anatimiza ahadi zake.
    - Alihifadhi uhai wa Nuhu ili atimize hadi ya Mwokozi kupitia kwa uzao wa mwanamke. (Mwanzo 3:15)

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- Wanadamu hawakuwa katika umoja na Mungu kwa sababu ya dhambi ya Adamu, babu yao. Walizaliwa nje ya bustani, mbali na Mungu. Na waliongeza huko dhambi zao na uasi.
- Mwanadamu anapenda njia yake mwenyewe. Mara nyingi hupuuza Mungu na amri zake na kutafuta tamaa zake kwa ubinafsi.
- Mwanadamu ni jeuri dhidi ya mwenzake, hana fadhili, anadhuru, ana ubinafsi.
- Mwanadamu hataki kusikiliza ukweli. Kwa muda wa miaka 120, majirani wa Nuhu waliona kazi yake na pengine waliuliza alichokuwa akifanya, lakini walipuuza maonyo ya kutubu dhambi zao.
- Je Nuhu pia, alikuwa mwenye dhambi? Je alistahili kufa?
    - Ndio Nuhu pia alikuwa mwenye dhambi, Alikuwa wa uzao wa Adam. Kisha baadaye akalewa au ulevi si dhambi? Ndiyo yeye pia alistahili kifo.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Kwa nini Nuhu alikubalika machoni pa Mungu ingawa alikuwa mwenye dhambi?**
    - Kwa sababu alikuwa mwenye haki asiyelaumika kati ya watu wa wakati wake. Alitembea na Mungu. Lakini yeye pia alikuwa mwenye dhambi.
    - Je Nuhu aliishi kulingana na mpango wa Mungu?
        - Ndio aliishi kwa imani

- **Nuhu alijuaje yale ambayo Mungu alimtaka afanye?**
    - Aliisikiliza sauti ya Mungu.
    - Hii imetuambia nini kuhusu Mungu? Mungu anawasiliana na watu.
    - Mungu alimwambia Nuhu afanye nini? Ajenge safina. Atafute kila aina mbili ya kila mnyama na kuwaweka katika safina.
    - Je Nuhu alifanya kile ambacho Mungu alimwamuru? [Ndio].

- **Kwa nini ilimchukua Nuhu imani kubwa kumtii Mungu?**
    - Huenda Nuhu hakuwa amewahi kuona mvua au mashua kubwa. Alikuwa ameishi katikati ya uovu kwa muda mrefu. Angeweza kuvunjwa moyo na uovu wa majirani zake. Ilikuwa kazi ngumu sana na ya gharama kubwa kujenga safina. Huenda watu wengine walimdhihaki kwa kujenga safina..

- **Je, unafikiri ni kwa nini Nuhu alimtii Mungu?** [Alimpenda Mungu. Alikuwa na imani kwamba Mungu angetenda kile ambacho alisema atatenda.

- **Wakati wa gharika kulikuwa na safina moja na mlango mmoja tu. Je, hii inatuonyesha nini muhimu?**
    - Njia moja tu. Mungu huwakubali tu wale wanaomwendea katika njia yake. Kuna njia moja tu ya Mungu kukubali wewe kama mwenye dhambi asiye na tumaini kujiokoa. Weka imani yako katika mwokozi ambaye Mungu ametupatia.
    -
- **Ni nini kilichokuwa muhimu sana katika damu, katika agano la Mungu na Nuhu?**
    - Hangeweza kuila, kwa sababu ilikuwa ya Mungu? Kwa sababu uhai umo katika damu, na ni Mungu mwenyewe na wa pekee anayepeana uhai.
    - Mungu alipotengeneza ngozi kwa Adam na Eve, damu ya mnyama ilimwagika ili waweze kuonyeshwa neema. Nuhu alipotoka kwenye safina alimtolea Mungu dhabihu kama njia ya kumshukuru Mungu kwa kuonyesha neema juu yake.

**<u>MASWALI KWA DARASA NZIMA:</u>**

- **Katika hadithi hii Mungu anahukumu mawazo na nia ya dhambi mioyoni mwetu. Je, ni nia na mawazo gani ya dhambi tunaficha zaidi mioyoni?**

- **Je, ni milango gani isipokuwa Yesu ambayo watu hujaribu kupitia ili kumfurahisha Mungu au kujihisi vizuri maishani mwao?**

- **Nuhu aliombwa kufanya kazi ngumu sana. Ilionekana haiwezekani. Ni mifano gani ya mambo ambayo Mungu angeweza kutaka mwamini afanye kwa imani ambayo yanaonekana kuwa magumu sana?**
    - Mpende mtu ambaye ni vigumu kumpenda, hata kama ni adui.
    - Msamehe mtu aliyekukosea sana.
    - Toa muda au pesa ili kuwasaidia watu wengine.
    - Pitia MLANGO MMOJA unaotuwezesha kuja kwake, yaani kumwamini Yesu.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- Mungu anajua kila wazo lako! Ni dhambi gani umekuwa ukimficha Mungu na unafaa kukiri?

- **Je, uko katika hali gani ambayo ni kama ya Nuhu? Je, Mungu anataka wewe binafsi ufanye jambo gani kwa imani linaloonekana kuwa ngumu?**
    - Je, ni kumpenda mtu ambaye ni vigumu kumpenda? Kumsamehe mtu aliyekukosea? Au kutoa wakati wako au fedha zako kuwasaidia wengine au kumheshimu Mungu? Au kupitia kwa mlango mmoja ambao Mungu alitupatia kumfikia yaani kumwamini Yesu Kristo. Je, hadithi hii inaweza kukusaidiaje kuchukua hatua ya imani?

## 6. MWITO wa ABRAMU—na IMANI KUHESABIWA HAKI
## Mwanzo 12, 13, na 15

*Amri na Ahadi*

Baada ya Mungu kuchanganya lugha kwenye mnara wa Babeli kulikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Abramu. Alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano. Mke wake, Sarai, alikuwa mkongwe pia, nao hawakuwa na watoto. Siku moja, Mungu alimtokea Abramu na akamwambia, "Abramu, ondoka katika nchi yako, waache watu wako na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha. Mimi nitakufanya taifa kubwa, nitafanya jina lako kuu, nitabariki watakaokubariki, na nitalaani watakaokulaani na kupitia kwako mataifa yote duniani yatabarikiwa."

*Kanaani na Misri*

Abramu akamchukua Sarai mkewe pamoja na Lutu mwana wa ndugu yake nao wakasafiri mpaka nchi ya Kanani. Walipofika hapo Mungu akamwambia "Hapa ndipo mahali. Nitawapa uzao wako nchi hii." Wakati huo kulikuwa na njaa kuu katika nchi, naye Abramu akashuka kwenda nchi ya Misri pamoja na familia yake. Huko Misri, Abramu aliwaogopa Wamisri akawadanganya kuhusu mke wake badala ya kumwamini Mungu kumlinda. Lakini hata ingawa alifanya hiyo dhambi, Mungu aliwalinda Abramu na mkewe. Pia alimbariki na mali nyingi sana wakati huo.

*Ugomvi na Lutu*

Abramu na familia yake waliporudi Kanani kutoka Misri, walikuwa na wanyama wengi. Wote wawili, Abramu na Lutu walikuwa matajiri, lakini nchi haikuwatosha kukaa pamoja kwa ajili ya wanyama wao. Ukazuka ugomvi kati ya wachunga mifugo wa Abramu na wale wa Lutu. Abramu akamwambia Lutu, "Tusigombane, sisi ni jamaa moja. Ebu angalia nchi yote. Kama ukielekea kushoto nitakwenda kulia, kama ukielekea kulia, mimi nitakwenda kushoto." Lutu akatazama akaona lile bonde lote akaona linapendeza, lilikuwa na maji tele na nyasi, chakula cha wanyama. Akamwacha Abramu aliyeishi kwenye milima iliyojaa mawe. Lutu alihama akaishi Sodoma, mji uliokuwa na watu waovu.

*Kumwamini Mungu*

Baada ya muda, Bwana alimtokea Abramu na akamwambia, "Usiogope, nimekupa nchi hii yote, mimi ni ngao yako na thawabu yako kubwa sana." Lakini Abramu akasema, "Itakuwa faida gani ukinipa nchi hii yote kama sina hata mtoto atakayekuwa mrithi wangu?"

Naye Mungu akamwambia Abramu, "Utakuwa na mwana kutoka katika mwili wako mwenyewe." Akamleta nje, akasema, "Tazama mbinguni, na uzihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu." Kisha akamwambia, "Ndivyo utakavyokuwa uzao wako." Naye Abramu akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.

Mungu akamwongoza Abramu kutoa dhabihu maalum ambapo Mungu alimtokea akiwa katika usingizi mzito. Akamwambia Abramu wazao wake watakuwa watumwa na watateswa kwa miaka mia nne kwenye nchi ya kigeni lakini Mungu atawaokoa kutoka taifa hilo. Baadaye Mungu alibadilisha jina lake liwe Abrahamu na jina la mkewe liwe Sarah.

**MPANGILIO wa SOMO**

**<u>UTANGULIZI:</u>** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Zungumza kuhusu wakati fulani ambapo mtu fulani alikutolea ahadi kubwa ambayo ulilazimika kuingoja kwa muda mrefu? Je, ahadi hiyo ilitimizwa? Je, hii ilikufanya uhisije?**

**<u>HADITHI:</u>** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**<u>MJADALA baada ya HADITHI:</u>** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**MASWALI ya KUJADILIANA**

**<u>Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Alimlinda na kumbariki Abramu, hata ingawa alikuwa mbali sana na jamaa wake; alimlinda na njaa na hata kutoka kwa Wamisri.
    - Akampa Farao mapigo makuu, akamlinda sarai asinajisiwe
    - Akaanza kuzitimiza ahadi zake akamwongoza katika nchi akamfanya tajiri.
    - Alionyesha mamlaka juu ya Abramu kwa kumwelekeza atakakokwenda. Abramu alikuwa wake kwa hivyo alikuwa na haki ya kumwambia atakachofanya.
    - Akamfanya mfalme wa Misri kumbariki Abramu.
    - Mungu alimchagua Abramu kama chombo chake cha Baraka. Akachagua kumbariki hata ijapo alitenda dhambi katika Misri.
    - Alimwonyesha Abramu mbingu na chote alichokuwa amekiumba.
    - Alimtokea Abramu kwa njia ya mwali wa moto.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Na yupo kila pahali?**
    - Alijua kile ambacho kingemtokea Abramu.
    - Alikuwa na mpango kwa Abramu.
    - Aliweka ahadi za wazi kwa Abramu ya yale angemfanyia katika siku za usoni. Nchi. Taifa kuu. Jina kuu Baraka / laana. Ulimwengu wote kubarikiwa kupitia kwake.
    - Alijua Abrahamu alihitaji kutiwa moyo, na vile angemtia moyo kwa kumuonyesha nyota na kufanya agano naye.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayetoa sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?)**
    - Alipeana amri kwa Abramu kutii alimtarajia atii.
    - Alikuwa anaanza kutenganisha Abramu na jamaa wake kuwa taifa lilitengwa, taifa takatifu ambalo kupitia kwalo Mungu angejionyesha mwenyewe kwa ulimwengu.
    - Alileta laana kwa mfalme wa Misri kwa kuchukua Sara kuwa mke wake, kwa kusudi lake na kutaka kumnajisi. Katika jambo hili Mungu alimlinda Sara kutoka kunajisiwa.

- Dhabihu aliyotoa Abramu. Dhabihu huonyesha utakatifu wa Mungu na dhambi ya binadamu. Binadamu anaweza kuja kwa Mungu kupitia njia ya Mungu pekee.
- Alidhihirisha utakatifu wake/ na haki yake kwa ile dhabihu kwa kutokea kama mwali wa moto.
- Dhabihu—umwagikaji wa damu- unaonyesha umuhimu wa dhabihu takatifu kwa ajili ya dhambi za binadamu.
- Mungu alimtenganisha Abramu na Lutu, utakatifu unamaanisha utenganisho wawema na uovu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na ana wasiliana na wanadamu?)**
  - Abramu alikuwa mwenye dhambi na kwamba hakutenda kila wakati katika imani. Alidanganya Wamisri kuhusu mke wake kwa sababu ya hofu, badala ya kumwamini Mungu. Pia alipokea zawadi katika kujifanya jinsi asivyokuwa.
  - Mungu alitenda mema kutoka kwa maovu, akimbariki Abramu na zawadi kumfanya tajiri na kuanza kumfanya kuwa taifa kuu.
  - Mungu alimchagua Abramu hata ingawa alikuwa mwenye dhambi kuwa atakayebeba na kutimiza agano lake.
  - Alimlinda Abramu alipokuwa mbali na nyumbani kwake.
  - Mungu alimpa nyumbani.
  - Akamfanyia ahadi nyingi za ajabu.
  - Akambariki kwa utajiri.
  - Alikuwa mwenye rehema kwa vizazi vingi, alimbariki Abramu ili akuwe Baraka kwa wengine wengi. Mungu huokoa binadamu na humtumia binadamu kuleta wengine kwa wokovu
  - Alimtokea Abramu na wakazungumza uso kwa uso.
  - Mungu alikuwa mwenye subira hata Abramu alipoonyesha shaka. Alimfunza na kumtia moyo, akamwambia, "usiogope." Alimtuliza
  - Mungu alipokea imani yake, hata ingawa alikuwa mwenye dhambi
  - Mungu alifanya upya ahdi yake kwa Abramu, akafanya agano na Abramu na uzao wake.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.)**
  - Alimfanyia Abramu ahadi kumfanya taifu kuu, na kufanya jina lake kuu, na kubariki na kulinda, na kubariki mataifa yote kupitia kwake.
  - Alimlinda Abramu.
  - Alimwongoza kwa wazi.
  - Hakuruhusu kutoamini kwa Abramu na dhambi katika Misri kuharibu mpango wake wa kumbariki na ulimwengu wote kupitia kwa yeye.
  - Mungu anaendelea kutimiza ahadi yake aliyopeana kwanza katika mwanzo 3:15 kumleta Mkombozi atakayemshinda Shetani. Mkombozi ambaye atakuja kupitia uzao wa mwanamke. Alitimiza ahadi hii hata ingawa Kaini alimwua Habili, hata ingawa kulikuwa na uovu duniani ulioleta mafuriko, hata ijapo kiburi na kujitegemea kwa mwanadamu.
  - Aliahidi kuwarudisha wazao wa Abrahamu kutoka katika utumwa wa miaka mia nne katika nchi ya kigeni.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Tunaweza kujifunza nini kuhusu imani katika hadithi hii?**
  - Hebrews 11:1. *"Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo ya tarajiwayo, ni uhakikisho wa mambo yasiyoonekana."*

- **Je tunaonaje aina hii ya imani ikidhihirishwa katika hadithi hii kumhusu Abramu?**
  - Abramu alitakiwa kuacha vyanzo vyote vya kujitambulisha na kujilinda- familia na nchi yake. Alikuwa amtegemee Mungu kabisa huku akijua vipengele vichache kuhusu siku za usoni. Aliahidiwa tuu Baraka aanapomtii Mungu.

- o Abramu aliendа maramoja, bila kumuuliza Mungu maswali, ingawaje hakujua alikokuwa akienda ama vile angempata mtoto akiwa mzee. Kuwa na mtoto kulikuwa jambo la muhimu ili ile ahadi iweze kutimika.

- **Je, Abramu alisuluhisha ugomvi baina yake na Lutu kwa njia ipi? Jambo hilo laaonyesha imani kwa njia ipi?**
  - o Aliwachilia vitu vizuri vimponyoke, bonde lililopendeza macho, alimtumainia Mungu ambariki. Hakushikilia haki yake.

- **Je, imani inahusiana aje na kutii? Twajifuza nini kwa hadithi hii?**
  - o Imani huja kabla ya kutii. Abrahamu alimwamini Mungu ili aweze kufanya mambo magumu. Imani husababisha kutii. Imani yetu huonekana kwa kutii kwetu. (Gal 5:6)
  - **o Soma: Waebrania 11:8- 12 -** "*Kwa imani Abrahamu, . . .*"

- **Je ,imani ni jambo rahisi?**
  - o La, kuna vizuizi vingi, imani sio rahisi.
- **Je, ni vizuizi vipi Abramu alikumbana navyo?**
  - o Uzee, ukongwewake na kwa mke wake, kutokuwa na mtoto na kuelekea nchi asiyo ifahamu.

- **Je, Mungu anahitaji imani iliyo timilifu ili aweze kutukubali katika neema? Twaonaje jambo hili?**
  - o La, Abramu alikuwa na wasiwasi na alikosa kumtumaini mungu wakati mwingine, kwa mfano, kwa uoga alimdanganya mfalme wa misri.
  - o Pia, hata baada ya imani yake kuhesabiwa haki, alimuuliza Mungu, "ninawezaje kujua?" lakini Mungu alimkubali kwa rehema kwa kuitoa ishara ya kuthibitisha agano lake na Abramu

- **Je, katika familia ya Abramu kunaye yeyote asiye tenda kulingana na imani kwake Mungu? Lutu ANAKOSA kuonyesha imani yake kwa njia ipi? Lutu anafanyaje chaguo lake?**
  - o Anachagua atakapo ishi kwa fikira za kiulimwengu.

- **Je, mbona kutoa dhabihu kulikuwa njia ya maana kwa Abramu kudhihirisha imani yake? Tunajifunza nini kutoka kwa dhabihu ya damu?**
  - o Dhabihu ya dhambi ilimkumbusha Abramu yakuwa alikuwa mwenye dhambi na alihitaji Mwokozi—atakaye kuwa mwana kondoo ambaye damu yake itamwagika mahali pa watenda dhambi ndio aweze kupatana na Mungu Mtakatifu.
  - o Kwetu sisi dhabihu hulenga kwake Yesu Kristo na dhabihu yake msalabani.

**o Je, mungu aliitikia vipi imani ya Abramu—hasa baada ya kumwonyesha nyota na kufanya upya ahadi zake?**
  - ▪ Alimhesabu kama mwenye HAKI
    - ● Warumi 4:3, 22; Wagalatia 3:6, Yakobo 2:23

**o Hii inamanisha nini, kuwa Mungu alimhesabia haki? Hadithi inatuonyesha nini kuhusu maana ya jambo hili?**
  - ▪ Alimkubali kama mtoto wake, alimkubali katika <u>uhusiano</u> ingawaje alikuwa mwenye dhambi. Alimsamehe dhambi yake.
  - ▪ <u>Kabla</u> ya Abramu kujithibitisha kupitia matendo yake ya haki, mungu alimhesabia kama haki kwasababu ya imani yake

<u>**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima):**</u>

- **Je, inaweza kutusaidiaje katika maisha yetu ya kila siku kujua kwamba Mungu ndiye anayetuhesabia haki kuanzia mwanzo hadi mwisho?** Yaani,, inatusaidiaje sisi kama waumini kujua kwamba alituchagua, anatuita, anatupa imani, anatuhesabia haki, anatukubali, anatuongoza, na

anafanya kazi maishani mwetu? **Inawezaje kuanza kubadilisha jinsi mwamini anavyoyachukulia maisha yake kila siku?**

- Inatupa uhuru mkuu na furaha kuhakikishiwa kwamba sisi ni watoto wa Mungu.
- Ninaweza kuwa mkweli kuhusu dhambi zangu, kutubu uwazi na mara kwa mara kwa sababu tayari nimesamehewa. Ninaweza kuwasamehe wengine kwa sababu amenisamehe.
- Niko huru zaidi kumtii Mungu kwa shukrani kwa upendo wake. Ninaishi kwa amani na sihitaji kujilinganisha na wengine. Ninaweza kupigana na kiburi.

- Imani ya Abramu ilimfanya akubaliwe na Mungu na kuhesabiwa mwenye haki. Lakini alithihirisha imani yake kupitia kwa matendo ya utiifui. **Je, ni baadhi ya matendo gani mahususi ya utii ambayo yanaweza kuwa tunda la imani yetu, kutumainia wokovu wa Mungu na utunzaji wake kwetu?**

- Lutu aliongozwa sana na kile alichokiona kwa macho yake. Hakumwamini Mungu ya kutosha kumtunza kama mtoto wake, kwa hivyo hakutafuta mwongozo wa Mungu kabla ya kuhamia Sodoma. **Toa mfano wa jinsi kutoamini kwetu kunaweza kutuongoza katika dhambi?**
  - Kufanya jambo mbaya kwa sababu ya kuogopa kukosolewa na wenzetu.
  - Kuiba ama kudanganya kwa sababu hatuamini Mungu atakimu mahitaji yetu.
  - Kusingizia, kutilia chumvi na kusengenya ndiposa watu watukubali.
  - Kutusi wengine na kuwa na hasira nyingi kwa kuwa hatuamini Mungu anaweza kutushughulikia tunapojaribiwa na kuteswa.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- je, una mfano wa kibinafsi wa hivi majuzi maishani mwako wakati kama Lutu ulifanya makosa au uamuzi mbaya kwa sababu hukumwamini Mungu,wakati huo kwamba umefanyikaa mwenye haki mbele za Mungu na atakutunz? Je. unaweza kutubu hizo dhambi za kutoamini?

- Je, ni kwa jinsi gani Mungu amewahi kukuita utoke nje kwa imani kufanya jambo gumu wakati ulikuwa bado hujaona matokeo ya mwisho wake? **Je, anakuita kwa jambo fulani sasa?** Taja baadhi ya **vikwazo** vinavyofanya iwe vigumu kumwamini Mungu vya kutosha kumtii katika hali hii? Je, hadithi ya Abramu inawezaje kukutia moyo?
- Mungu ametimiza agano lake kwa Ibrahamu kwa kumleta mwokozi. Je, umemwani huyu Mwokozi kwa kumpatia maisha yako?Jje, itakuwa vyema aje ukimwani?

## 6-B. SOMO la CBS - NYIMBO na MICHEZO #1

**<u>NYIMBO za KUSIMULIA HADITHI za BIBILIA</u>:**

Chagua Hadithi ambayo tayari umejifunza katika CBS na uingie katika kikundi cha wanafunzi watano mchukue saa moja kujaribu kuunda na kuandika wimbo unaosimulia moja kwa moja hadithi. Kisha wasilisha wimbo kwa darasa zima.

**<u>MICHEZO wa KUIGIZA wa KUSIMULIA HADITHI za BIBILIA</u>:**

Chagua Hadithi ambayo tayari umejifunza katika CBS na uingie katika kikundi cha wanafunzi 5 hadi 15 (idadi kutegemea hadithi) na uchukue saa moja kuandaa drama. Hakikisha kuwa una majukumu yote yaliyofafanuliwa wazi na kuwa na watu wote wanaohusika. Pawe na mtu mmoja ambaye ni msimulizi wa kusimulia sehemu za hadithi ambazo hazizungumzwi na wahusika wanaowakilishwa. Kisha wasilisha drama kwa darasa zima.

**KANUNI ZA UANDISHI WA NYIMBO:**

- **KUHUSU NYIMBO/MANENO:**
    - Kibiblia - sahihi, kweli
    - Ujumbe Wazi, sana sana wa Injili. Maneno yenye kugusa moyo.
    - Ikumbukwe kwa urahisi
        - Rahisi kutosha kwa wote kukumbuka au kwaya rahisi kwa kudia yenye mistari ya kiongozi wa wimbo kusmilia hadithi
    - Ina madhari wazi (sana sana katika kwaya)
    - Swali zuri: Muulize asiye Mkristo asikilize na kuona JINSI wanavyoelewa maneno ili kuhakikisha unawasiliana vizuri.

- **KUHUSU UWASILISHAJI:**
    - Wimbo wa kuvutia.
    - Inafahamika vya kutosha kwa watu kupenda na kujifunza
    - Rhythm nzuri, mtiririko
    - Furaha, kujihusisha. Kucheza - kukubalika kitamaduni, kumheshimu Bwana
    - Ishara zinalingana na maneno
    - Kuhamasisha, kuchochea hisia. Inatia moyo. Imefanywa kwa kujiamini.
    - Matamshi mazuri
    - Je, sauti ya kuimba inalingana na sauti ya maneno (K.m. Furaha, umakini, huzuni, heshima, furaha, amani)?
    - SI KWA SAUTI SANA. Usiruhusu vyombo ama sauti ya vyombo kuzima maneno!
    - Muhimu zaidi - MANENO na KUABUDU
        - Vyombo ni zana tu

## 7. ABRAHAMU— KUZALIWA na DHABIHU ya ISAKA
## Mwanzo 21:1-7, 22:1-19

*(*Ilani - Kwa wakati huu Mungu alikuwa amebadilisha majina ya Abramu na Sarai kuwa Abrahamu na Sara.)*

Hatimaye, baada ya miaka ishirini na mitano Mungu kumwahidi Abrahamu kumfanya taifa kuu, Sara, katika ukongwe wake, alijifungua mtoto wa kiume kama vile Mungu alikuwa amemwahidi. Wakamuita jina lake Isaka, maanake 'kucheka' kwa sababu Sara alicheka wakati Mungu alipomwambia, atajifungua mtoto. Basi Isaka alikua na akawa kijana.

Baada ya miaka kadhaa, siku moja Mungu alimtokea Abrahamu akamwambia, "Abrahamu, umchukuwe mwanao Isaka, mwana wako wa pekee umpendaye, uende katika nchi ya Moria. Mtoe huko kama sadaka ya kuteketezwa juu ya mlima." Siku iliyofuata asubuhi, Abrahamu alikusanya kuni na kuziweka juu ya punda, kisha akawaita watumishi wawili. Abrahamu akabeba kisu na moto wakaenda na Isaka kuelekea mahali Mungu alikuwa amemwambia.

Abrahamu alipoona mlima Moria kwa umbali, akawaeleza watumishi wake, "Kaeni hapa pamoja na punda. Mimi na kijana tutaenda mlimani kuabudu, kisha tutarudi. Abrahamu akachukua kuni akamtwika Isaka, yeye mwenyewe akachukua moto na kisu. Walipokuwa wakienda pamoja, Isaka akamwuliza Abrahamu, "Moto na kuni zipo. Je, mwanakondoo wa sadaka yuko wapi?" Abrahamu akamjibu, "Mwanangu, Mungu mwenyewe atajipatia mwanakondoo kwa ajili ya hiyo sadaka."

Walipofika mlima Moria, Abrahamu akajenga madhabahu, kisha akaweka kuni juu yake. Akamfunga Isaka mwanawe na akamlaza kwenye madhabahu. Kisha akachukua kisu ili amchinje mwanawe, punde malaika wa Bwana akasema, "Abrahamu! Usimdhuru mwanao! Sasa ninajua kwamba unamcha Mungu kwa sababu, haukunizuia mwanao, mwanao wa pekee."

Abrahamu alipogeuka, akaona kondoo wa kiume amenaswa kwa pembe zake katika kichaka. Abrahamu akamtoa Isaka kwenye madhabahu na kumweka yule kondoo badala yake. Abrahamu akapaita mahala pale, "Yehova-yire." Maanake, "Katika mlima wa Bwana, itapatikana."

Baada ya Abrahamu kumtoa kondoo kama dhabihu, malaika wa Bwana akamwambia, "Nitakubariki na kuzidisha uzao wako kama nyota za angani. Kupitia uzao wako mataifa yote duniani yatabarikiwa."

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kufikiria wakati ambapo mtu fulani amekuomba ufanye jambo ambalo halina maana? Ulifanya nini?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Alimpa Sarai mtoto, akiwa mzee
    - Kupitia mamlaka yake alimwelezea Abramu atakachokifanya, alikuwa na haki ya kutarajia kutii, hata kama ile amri haikuwa ya kawaida. Mungu HAKUMUULIZA Abrahamu, bali ALIMWAMBIA.
    - Alimwamuru Abrahamu asimdhuru mwanawe, na alikuwa na uwezo na mamlaka ya kumsimamisha kabla hajamtoa mwanawe kama dhabihu.
    - Alitoa kondoo atakaye kuwa dhabihu badala ya Isaki

- **Hadithi hii inatuonyesha Ujuzi wa Mungu na yupo kila pahali?**
    - Mungu alikuwemo kumwambia Abrahamu ampeleke mwanawe mlimani, alikuwa kwenye mlima moria akitizama.
    - Alijua atatengeneza njia
    - Alijua vile moyo wa Abrahamu ulivyokuwa.

- **Hadithi hii inatuonyesha UTAKATIFU wa Mungu? (haki, anachukia dhambi, lazima ahakumu au aadhibu dhambi)**
    - Umuhimu wa dhabihu ya damu, ilifanywa kwa njia ya Mungu, inalenga dhambi ya binadamu na utakatifu wa Mungu. Hakuna njia nyingine ya kwenda kwa Mungu
    - Mungu alipeana amri na alitarajia watii
    - Dhabihu ya damu ilikuwa itolewe, badala ya isaki- kondoo dume.
    - Yule kondoo dume alinaswa kwa pembe sio kwenye mguu, kwasababu dhabihu haikupaswa iwe na dosari.
    - Mungu pekee ndiye aliyekuwa mtakatifu na aliyyestahili kutoa dhabihu ingefaa.
    - Abrahamu angemkujia Mungu vile Mungu alikuwa ameagiza.

**Hadithi hii inatuonyesha NEEMA ya Mungu? (huruma, anawasiliana na mwanadamu ukarimu na wema).**

- Alizungumza na Abrahamu.
- Alitoa njia nyingine ya Isaki, anampenda.
- Alitoa njia ya Abrahamu ya kumtii na kutilia maanani ahadi yake.
- Alitoa dhabihu-- ilikuwa njia ya Abrahamu aliyekuwa mwenye dhambi, ili aweze kumwabudu mungu.
- Alimpa Abrahamu baraka, uzao, ushindi dhidi ya maadui, mataifa yote yatabarikiwa kumpitia.

**Hadithi hii inatuonyesha UAMINIFU wa Mungu? (kutobadilika)**

- Alikuwa amemuahidikumfanyia taifa kubwa na kubariki mataifa yote. Aliahidi angetimiza jambo hili kupitia Isaka, na sio kwa kutumia njia zingine gushi (ishmaeli). Mungu alimpatia isaki chote alichohitaji kuishi.
- Mungu alipatia Abrahamu imani ili aweze kumtolea yule kondoo dume. Na akafanya hivyo.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu mwanadamu?**

- Binadamu hawezi kujiokoa, Isaki hakuwa na usaidizi wowote, alikuwa amefungwa, hakuwa na njia ya kujiokoa, Abrahamu alimtii Mungu, na hakuona dhahiri vile Mungu angetimiza ahadi zake
- Binadamu anahitaji mwokozi. Anahitaji dhabibu inayofaa kulipa makosa yake.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi mwanadamu anavyomjia Mungu?**

  - Binadamu lazima aje kwa Mungu kupitia njia ya Mungu pekee. Mungu pekee ndiye anaweza akafanya njia, na atoe dhabihu itakayo faa.
  - Binadamu lazima awe na imani ndio amfurahishe Mungu

- **Je, tunaona imani ya Abrahamu kwa njia ipi?**
  - Kutii kwake, na neno lake kwa watumishi wake yakwamba yeye NA mwana watarudi pamoja. Alijua kuwa Mungu angetoa dhabihu badala ya Isaka ama angemfufua kutoka wafu
  - Imani huonyeshwa kupitia kutii.
  - Abrahamu alikuwa na uhusiano wa karibu na Mungu. Alisikiza na kutii amri zake Mungu. Alitii kwa sababu alimwamini Mungu. Kutii kwake kumetoka kuamini kwake.

- **Je, kwanini kuamini kwa Abrahamu hakukuwa jambo la kawaida? Au, ni vizuizi vipi vilikuwa katika imani ya Abrahamu?**
  - Abrahamu alimpenda Isaki sana, alikuwa mwanawe wa pekee aliyemthamini, mtoto wa miaka yake ya uzee. Kumtoa kama dhabihu hakungekubaalika kwa fikira zake, jambo hilo lilikaa kama linaenda kinyume na amri ya Mungu ya kutotoa uhai wa mtu mwingine. Hakujua ni kwanini Mungu alimwamuru atende jambo hilo. Ama ni kwanini alimwambia akatoe dhabihu bila kondoo. Mungu alikuwa amemwahidi Abrahamu kuwa atamfanya taifa kubwa na abariki mataifa mengine kumpiti Isaki.Mungu alikuwa amesema ile ahadi ingefanikishwa kupitia Isaki, yule ambaye walikuwa wamemsubiri kwa miaka ishirini na mitano. Abrahamu angeweza kujisema, “Ahadi ile ingetimizwa aje kama angalikuwa amekufa?”

- **Je, unafikiri ni kwanini Abrahamu alimtii Mungu?**
  - Alimpenda Mungu. Alikuwa na imani kuwa Mungu angefanya kile alichokuwa amesema.

- **Je, kwanini Mungu aliitisha tohara, baada ya kumhesabia Abrahama haki bure?**
  - Ilikuwa alama au muhuri wa kuonyesha kumilikiwa na Mungu. Kuwa sehemu ya watu watakatifu, taifa lililochaguliwa. Ilikuwa pia alaa ya  kutakaswa na hukumu ya utakaso, ilimtambulisha mtu kama wa familia ya Israeli.

- **Je, kutahiriwa kwa Abrahamu kunaonyeshaje imani yake?**
  - Abrahamu alinyeyekea akatahiriwa, ingawaje alikuwa na umri wa miaka tisini na tisa. Na hakuwa na furaha ya kupata yule mtoto aliyekuwa ameahidiwa.

- **Nini kilikuja kwanza—imani ama kutahiriwa? Mbona jambo hili ni muhimu?**
    - Imani, ni muhimu kwasababu imani ya kweli humuongoza mtu kutii. Wokovu haukuji kwa kutii lakini kwa imani katika ahadi zake Mungu kutii ni tunda la imani

- **Je, kuna hadithi nyingine ambapo mnyama alitolewa kama dhabihu badala ya binadamu? Damu ikamwagika? Jambo hili lilikuwa na umuhimu upi?**
    - Mnyama aliuliwa ili Adamu na Hawa wavikwe nguo.
    - Baada ya gharika MUNGU alifanya wazi kuwa uhai umo kwenye damu. Mnyama alipotolewa kama dhabihu badala ya maisha ya binadamu, uhai kwa uhai.
    - Lazima kungekuwa na dhabihu badala ya binadamu – dhabihu kamilifu, na takatifu.

- **KIELEZO/MFANO nikama picha inayo wakilisha kitu kikubwa kikujacho baadaye. Je, Yule kondoo dume aliye naswa kwa msitu ni KIELEZO/MFANO WA KRISTO kwa njia ipi? Inalenga kwa yesu kristo kwa njia ipi?**
    - Mwana kondoo wa Mungu, anayetoa dhambi za ulimwengu.dhabihu inayostahili na timilifu kulipia binadamu mwenye dhambi. Alikufa mahali pa wengine.
    - Alitoka kwa Mungu kama Yesu ametoka kwa Mungu.
    - Mwana kondoo alinaswa kwa pembe, kwa hivyo, mwili wake na mifupa hayakuwa na dosari, yalikuwa timilifu, dhabihu takatifu.
    - Isaki, kama Yesu, alimtii babake na akakubali kuwa dhabihu kulingana na maopenzi yake.
    - Isaki alibeba kuni atakayo tolewa dhabihu, kama vile Yesu alibeba msalaba aliyosulubiwa.

- **Je, tunajifunza nini kuhusu kuhesabiwa haki kutokana na vile Isaki aliokolewa?**
    - Mwana kondoo alikufa mahali pake na akafanywa huru, yule mwana kondoo lazima angekuwa timilifu, isiyokuwa na dosari.

- **Je ninani aliye peana mwana kondoo? Ni nani anaye hesabu haki?**
- Je, Katika hadithi hii tunawezaje kupatanisha haki ya Mungu na upendo wake? (Abrahamu na Isaki **walikuwa wenye dhambi waliostahili kifo)**
    - Mungu pekee ndiye anayetoa dhabihu timilifu, na itakayoridhisha

- **Ni kwa njia ipi, Isaka akiwa amefungwa pale kwenye madhabahu, anathihirisha vile tulivyokuwa kabla ya kuhesabiwa haki?**
    - Hakuwa na uwezo wa kujiokoa.

- **Waebrania 11:17- 19**: *Kwa imani Abrahamu, alipojaribiwa na Mungu, alimtoa Isaki kuwa dhabihu. Yeye aliyekuwa amezipokea ahadi za Mungu alikuwa tayari kumtoa mwanawe, aliyekuwa mwanawe pekee awe dhabihu. Ingawa Mungu alikuwa amemwambia Abrahamu, "Uzao wako utahesabiwa kwa njia ya Isaki," Abrahamu alihesabu kuwa Mungu angaliweza kumfufua Isaki kutoka kwa wafu na kwa kusema kwa mfano alimpata tena Isaki kutoka kwa wafu.*
    - Hii mistari inatuonyesha nini kuhusu imani?

- **Warumi 4:2- 3, 7- 11**

*"Kwa maana ikiwa Abrahamu alihesabiwa haki kwa matendo, basi, anacho kitu cha kujivunia, lakini si mbele za Mungu. Kwa maana Maandiko yasemaje? "Abrahamu alimwamini Mungu na ikahesabiwa kwake kuwa haki."*

*"Wamebarikiwa wale ambao uovu wao umesamehewa na ambao dhambi zao zimefutwa. Amebarikiwa mtu yule ambaye Mungu hamhesabii dhambi zake." Haki Kabla Ya Tohara . Je, huku kubarikiwa ni kwa wale*

*waliotahiriwa peke yao, au pia na kwa wale wasiotahiriwa? Tunasema, ''Imani ya Abrahamu ilihesabiwa kwake kuwa haki.'' Je, ni lini basi ilipohesabiwa kwake haki? Je, ilikuwa kabla au baada ya kutahiriwa kwake? Haikuwa baada, ila kabla hajatahiriwa. Alipewa ishara ya tohara kuwa muhuri wa haki aliyokuwa nayo kwa imani hata alipokuwa bado hajatahiriwa. Kusudi lilikuwa kumfanya baba wa wote wale waaminio pasipo kutahiriwa na ambao wamehesabiwa haki.*

- **Je, sehemu hii ya Warumi inatueleza nini kuhusu kuhesabiwa haki? Yaanii kufanywa haki na Mungu? Imani inauhusiano upi na kutii?(kutii amri ya Mungu Abrahamu kutahiriwa.)**
    - Kwasababu abrahanu tayari alikuwa amehesabiwa haki kabla ya kutahiriwa, hii inaonyesha kutii ni MATUNDA ya Imani. Tumeokolewa kwa IMANI katika Yesu, sio kwa kiwangi cha kutii.

**MAJUMLISHO—WAZO KUU**

- Imani inayofanya kuhesabiwa haki sio jambo la maramoja, bali ni safari iliyo na milima na mabonde na inahitaji uvumilivu
- Imani huvumilia hata wakati vitu havieleweki.
- Imani ya kweli hujulikana kupitia matunda yake. (kutahiriwa, mlima Moria)
- Binadamu huja kwa Mungu kupitia dhabihu ambayo Mungu hutoa.
- Mungu hueshimu imani.
- Mazao ya imani ni kutii, yaani kutii hutokana na imani.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Ibrahamu angeweza kukataa kumtoa Isaka kuwa dhabihu. Angeweza kudai kwamba haikuwa na maana yoyote! Ni mambo ya aina gani ambayo watu humzuilia Mungu? **Ni mambo gani maishani ambayo ni vikwazo vinavyowazuia watu kumwamini Mungu kikamilifu?** Umejifunza nini kutoka kwa somo la leo ambacho kinaweza kukusaidia kushinda vikwazo hivi na kukuza imani yako?

- Je, ni ahadi gani za Mungu, Ibrahimu aliamini zilizomsaidia kumtii Mungu katika hadithi hii? **Je ni ahadi gani za Mungu kwetu sisi zinaweza kutusaidia kumeamini na kumtii katika hali zetu ngumu?**

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je ni kitu gani,mtu au oja gani inayokuzuia kwa Mungu na kukufanya usijinyenyekeze kwa yale ya haki?** Je, ni vikwazo gani maishani mwako vinavyokuzuia kumwamini Mungu? Hili somo linaweza kukusaidia vipi kushinda hivi vizuizi na kumtumainia Mungu zaidi?

- **Je, kuna kitendo, nia ama mawazo, of utiifu ambayo Mungu anakuitia kufanya ambayo ni magumu kuelewa na haina maana?** Je hii hadithi ya Ibrahimu na Isaka inawezaje kukutia moyo?

## 8. ISAKA, JAKOBO, NA ESAU
## Mwanzo 24-33

*Mke kwa Isaka*

Abrahamu alipokuwa na miaka mia moja na thelithini na saba, mkewe aliaga dunia na Abrahamu akamzika huko Hebroni. Wakati huo, Isaka alikuwa na miaka karibu arobaini na hakuwa ameoa. Kwa hivyo Abrahamu akamtuma mtumishi wake kaskazini Siria kwenda kwa watu wa ukoo wake alikotoka Abrahamu ili kumtafutia Isaka mke kwa sababu Abrahamu hakutaka Isaka kumwoa binti wa Kikanaani.

Mtumishi alipofika huko Siria, alimwomba Mungu kumwonyesha msichana anayefaa. Naye Mungu akamwongoza kwa Rebekah. Rebekah alikuwa binti wa mpwa wa Abrahamu aliyekaa huko Siria. Rebekah na babake walikubali ndoa. Basi Rebeka aliienda Kanaani pamoja na mtumishi wa Abrahamu, na akaolewa na Isaka. Baada ya haya yote, Abrahamu aliaga dunia na Isaka akamzika Hebroni alipozikwa Sara.

*Kuzaliwa kwa Isaka na Wavulana wa Rebeka*

Kwa muda mrefu, Rebeka hakuweza kupata mimba. Kwa hivyo Isaka alimwombea Rebekah. Mwishowe baada ya miaka ishirini, alijifungua mapacha wavulana. Rebeka alipokuwa mjamzito, watoto walishindana tumboni mwake. Mungu akamwambia, "Mataifa mawili yako tumboni mwako. Mkubwa atamtumikia mdogo." Walimwita mzaliwa wa kwanza Esau. Baada ya Esau kuzaliwa, ndugu yake alitoka na mkono wake unamshika Esau kisigino. Kwa hivyo akaitwa Yakobo, maana yake "mdanganyifu."

*Kudharau Haki ya Kuzaliwa*

Kwa sababu ya kuwa mzaliwa wa kwanza, Esau angepata haki ya uzao wa kwanza, (yaani urithi mara mbili), na baraka ya ahadi ya Mungu kuwabariki uzao wa Abrahamu kupitia kwake. Walipokuwa wakikua, Esau akawa mwindaji aliyependa kuwa mwituni. Isaka alimpenda Esau zaidi kwa maana alipenda nyama alizomletea. Lakini Yakobo alikuwa mtulivu aliyekaa hemani. Na alipendelewa sana na mamake.

Siku moja Yakobo alipokuwa akipika mchuzi, Esau alirudi nyumbani kutoka msituni akiwa na njaa kubwa. Akamwambia Yakobo, "Nipe chakula nile." Yakobo akakataa akasema, "Sitakupatia mchuzi usiponiuzia haki ya urithi wako."

Esau akamjibu, "Niko karibu kufa kwa njaa. Haki hii ina faida gani kwa mtu aliyekufa?" Akamwapia kumwuzia Yakobo haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa bakuli moja ya mchuzi. Hivyo Esau akaidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza.

*Kuiba Baraka*

Muda ulipita na Isaka alimwita Esau akasema, "Mimi nimekuwa mkongwe. Sijui nitaishi muda gani zaidi. Nenda uwinde nyama, na uipike jinsi nipendavyo. Ningependa kukupatia baraka yangu kabla nife."

Lakini Rebeka alikuwa akisikiliza, na Esau alipokuwa akiwinda, Rebeka alimsaidia Yakobo kumdanganya baba yake aliyekuwa kipofu akifikiria huyu Yakobo alikuwa Esau akija na nyama nzuri. Kwa hivyo Isaka alimbariki Yakobo na baraka ya Esau aliyekuwa

mzaliwa wa kwanza. Esau alipotambua kuwa Yakobo alimwibia baraka zote mbili, yaani urithi na baraka ya mzaliwa wa kwanza, alighadhabika na akaapa kumwua nduguye. Hivyo Rebekah akamwambia Yakobo, “Nisikilize! Ni bora zaidi ukienda kukaa na ndugu yangu Labani huko Siria mpaka Esau atakapopoa. Nitakwambia utakoweza kurudi salama.”

Pia Rebeka akamwambia Isaka, “Nimechoka na wake wa kigeni wa Esau. Kama Yakobo atamwoa mmoja wao, sina haja ya kuishi.”

Kwa hivyo Isaka akamwambia Yakobo, “Usimwoe msichana Mkanaani. Badala yake, sasa nenda Siria kumchukua binti moja wa mjomba wako Labani.” Kwa hivyo Yakobo akaenda Siria.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kufikiria wakati hivi majuzi ambapo ulifanya uamuzi bila kufikiria kabisa kile ambacho Mungu angetaka? Ilikuaje?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Alimpatia Isaka mke.
    - Alimwongoza mtumishi wa Isaka kwa Rebekah baada ya kuomba.
    - Alimfanya Yakobo kupata haki ya mzaliwa wa kwanza.
    - Amemlinda Yakobo kupitia mateso mengi.
- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Mungu alijua kwamba Isaka alihitaji mke kutoka familia yake.
    - Mungu alijua na kumwambia Rebeka kilichokuwa kikiendelea katika tumbo.
    - Mungu alijua Isau mzaliwa wa kwanza atakuwa asiye na imani.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba Mungu ni mtakatifu?**
    - Anakataa kupatisha ahadi yake kupitia mtu asiye mwaminifu aliyewaoa wanawake wa kigeni.
    - Mungu hakumruhusu Yakobo kumwoa mwanamke wa kikanani ambaye angemwelekeza kuabudu sanamu. Alitaka taifa lililotenga kutoka kwa uovu.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba Mungu ni mwenye neema?**
    - Alimlinda Yokobo kwa miaka mingi, na hata kutoka kwa ghadhabu ya kaka wake.
    - Alimpa Rebeka watoto baada ya miaka ishirini bila watoto.
    - Aliendelea kutimiza ahadi yake kumleta mwokozi kupitia kwa uzao wa mwanamke na uzao wa Abrahamu.
    - Alichagua kubariki na kufanya kazi yake kupitia kwa Yakobo hata ingawa alikuwa mwenye dhambi.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.)**
    - Mungu alitabiri kwamba mtoto wa kwanza angetumikia mtoto mdogo. Na ilianza katika hadithi hii.

  - Mungu aliendelea kutimiza ahadi yake kuyabariki mataifa yote kupitia uzao wa Abrahamu, hata ingawa Esau, mtu ambaye angeirithi ahadi, alikuwa asiye na imani. Alimlinda Jakobo.
  - Mungu aliendelea kutimiza ahadi ya kumleta Mwokozi kuyabariki mataifa yote.
  - Mungu alimpatia Yakobo tena ahadi ambazo aliwapatia Abrahamu na Isaka.

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu.**
  - Ndiyo. Mungu alimtunza Yakobo na neema na aliendelea kutimiza ahadi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
  - Isau alijali tumbo lake tu. Hakujali vitu vya kiroho au ahadi za Mungu.
  - Hata kama Yakobo alizitaka ahadi za Mungu, bado alikuwa mwenye dhambi. Tunaona dhambi zake kwa sababu ya uongo na wizi wake. Hata Mama yake Rebeka alimdanganya bwana wake kupata ahadi kwa Yakobo.
  - Hata Isaka alikuwa mwenye dhambi kwa maana alihukumu mioyo ya wana wake vibaya kwa sababu alimpenda Isau zaidi ya Yakobo licha ya upendo wake wa vitu vya dunia kuliko vya kiroho.
  - Hata Rebekah alikuwa mwenye dhambi pia. Alisikia ahadi ya Mungu, lakini akahisi kwamba angeielekeza kufanyika jinsi yeye mwenyewe alivyotaka.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
  - Ni Mungu tu pekee ambaye angeweza kumlinda na kumhifadhi Yakobo kupitia katika majaribu yake yote, na kuweza kumbariki katika wakati huo.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- Hadithi hii inaonyesha vipi kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wake.)
- Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.
  - Mtoto ambaye alikuwa na imani katika Mungu na ahadi zake alibarikiwa, hata ingawa alifanya dhambi kwa kujaribu kuichukua baraka hiyo mwenyewe.
  - Mungu hakumbariki au kumjibu mtu kama Isau asiye na imani.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- **Je, ni vipi siku hizi watu wako kama Esau wanajali sana tumbo zao kuliko ahadi za Mungu?**
- Wakati mwingine Yakobo alidanganyana kulazimisha mambo yaende kwa njia zake. Alikuwa anajaribu kuendesha mipango ya Mungu. Je, tunatendaje kama Yakobo kwa njia hii?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je, unakuaje kama Esau wakati mwingine?** I.e. Ni kwa njia gani hususa unatawaliwa sana na hamu yako ya kula au matamanio yako ya kibinafsi?

- Wewe, kama Yakobo, umejaribu jinsi gani nyakati fulani kudhibiti hali fulani badala ya kumtumaini Mungu? Je, ni njia gani bora zaidi ya kukabiliana na hali hii inayoonyesha kwamba unamwamini Mungu?

# 9. NDOTO ya YAKOBO
# Mwanza 28:10-22

Wakati nduguye Yakobo, Esau, alipotambua kwamba alikuwa amedanganywa kutoka kwa haki yake ya mzaliwa wa kwanza na baraka yake na Yakobo, alikasirika na akaapa kumuua kaka yake. Kwa hiyo, kwa kusihiwa na wazazi wake, Yakobo alikimbilia Siria ili aende kwa Labani, ndugu ya mama yake. Akiwa njiani kuelekea kaskazini, Yakobo alilala mahali fulani usiku. Huko, baada ya kuchukua jiwe na kulitumia kama mto kumsaidia kulala, aliota ndoto ya wazi. Katika ndoto yake aliona ngazi kutoka duniani hadi mbinguni, na malaika wa Bwana walikuwa wakipanda na kushuka juu yake. Juu ya ngazi hiyo Bwana alisimama, ambaye alisema, "Mimi ni Bwana, Mungu wa Abrahamu na Mungu wa Isaka. Nitakupa wewe na uzao wako nchi hii ambayo unalala juu yake. Uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, nawe utaenea mashariki na magharibi, kaskazini na kusini, na kupitia wewe mataifa yote ya dunia yatabarikiwa. Mimi nipo pamoja nawe na nitakulinda popote uendapo, nami nitakurudisha katika nchi hii."

Yakobo alipoamka katika usingizi wake, aliogopa na kuwaza, "Hakika Bwana yupo mahali hapa, wala mimi sikujua. Mahali hapa panastaajabisha sana! Ni nyumba ya Mungu na lango la mbinguni!" Kwa hiyo akalichukua lile jiwe alilokuwa ameliweka chini ya kichwa chake na kulisimamisha kama nguzo na kumimina mafuta juu yake, na kupaita mahali hapo Betheli. Yakobo akaweka nadhiri, akisema, "Ikiwa Mungu atakuwa pamoja nami, na kunilinda katika safari hii, na kunirudisha nyumbani kwa baba yangu kwa amani,… ndipo BWANA atakuwa Mungu wangu, na jiwe hili litakuwa nyumba ya Mungu, na katika yote utakayonipa nitakupa wewe sehemu ya kumi." Kwa hiyo Mungu alirudia kwa Yakobo ahadi zilezile alizowapa Abrahamu na Isaka kabla yake. Kisha akampeleka mpaka nyumbani kwa mjomba wake huko Siria.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Zungumza na jirani yako kuhusu wakati fulani katika maisha yako ambapo Mungu alikutia moyo ulipokuwa katikati ya jambo fulani gumu sana, wakati ambapo uliogopa ni nini kingetokea baadaye?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Alimchagua Yakobo kupata haki ya mzaliwa wa kwanza, pamoja na ahadi za Abrahamu.
    - Alimlinda Yakobo kupitia mateso mengi.
    - Alimtokea Yakobo kupitia kwa ndoto.

    - Alisema, "Mimi ndimi Bwana, Mungu wa Abrahamu na Isaaka."
    - Aliweza kutimiza ahadi zake, ahadi za nchi, za watoto, na za Baraka, hata kama Jakobo hukuwa na kitu chochote.
    - Aliweze kurudisha Yakobo kwa nchi ya agano.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Alijua na akamwambia Yakobo katika ndoto baraka zote ambazo angezipokea.
    - Alijua kwamba mataifa yote yangebarikiwa kupitia Yakobo.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba Mungu ni mtakatifu?**
    - Inaonyesha utakatifu wake kupitia hadithi zake kamilifu kuu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi  kwamba Mungu ni mwenye neema?**
    - Aliendelea kutimiza ahadi yake kumleta mwokozi kupitia kwa uzao wa mwanamke na uzao wa Abrahamu.
    - Aliwasiliana na Yakobo katika ndoto.
    - Alichagua kubariki Yakobo na kufanya kazi yake kupitia kwake hata ingawa alikuwa mwenye dhambi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba Mungu ni mwaminifu?  (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.**
    - Mungu aliendelea kutimiza ahadi ya kumleta Mwokozi kuyabariki mataifa yote.
    - Mungu alimpatia Yakobo tena ahadi ambazo aliwapatia Abrahamu na Isaka.
    - Mungu alimwahidi kumlinda, na kumrudisha nchi ya Kanaani, na uzao wengi, na kuyabariki mataifa yote kupitia kwake. Mungu alitimiza ahadi zote.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu MWANADAMU?</u>**
- Yakobo alikuwa hoi kujijali. Alipaswa kutegemea neema ya Mungu pekee kwa baraka.
- Yakobo na uzao wake walipendwa sana na Mungu.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

    - Wokovu hutoka kwa Bwana tu. Yeye ndiye tumaini letu pekee. Ni lazima tumtumaini Yeye na ahadi zake, katika Mwokozi ambaye amemtuma. Ni lazima tumsikilize Mungu.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Yakobo alikuwa pekee yake katika hali ngumu bila mtu wa kumjali. Mungu aliponena naye katika ndoto, alitambua sauti yake na akasikiliza ahadi zake na akatiwa moyo kuendelea mbele. **Je, ni ahadi gani Mungu ametupa leo** tunapomfuata hata kuenda kwa maeneo hatujawai fika wala kujua?
- Je, ni kwa njia gani tutajua zaidi kuhusu ahadi za Mungu kwetu?
- Je, hii hadithi inatusaidia vipi kuamini  kwamba Mungu anaweza kutenda mema kutoka na hali yoyote ngumu tunayopitia.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>**  (chagua moja au mbili)

- **Je,ni ahadi gani za Mungu unahitaji kuamini kukusaidia leo? Unapitia hali gani leo maishani mwako, unahitaji kumwamini Mungu zaidi?**
- Je, wewe binafsi utajitolea kufanya nini katika wiki ijayo ili kujua na kuamini katika ahadi za Mungu zaidi?

## 10. YAKOBO, LABANI, na FAMILIA ya YAKOBO
## Mwanzo 29:15-35

Baada ya ndoto yake kuhusu ngazi, Yakobo akaenda zake mpaka nchi ya mjomba wake Labani. Baada ya Yakobo kukaa kwa Labani mwezi mzima, Labani akamwambia, "Hata kama wewe ni jamaa yangu, haifai unifanyie kazi bila ujira. Niambie, mshahara wako utakuwa nini."

Labani alikuwa na binti wawili, binti mkubwa aliitwa Lea na binti mdogo aliitwa Raheli. Lea alikuwa na macho dhaifu, lakini Raheli alikuwa na umbo la kupendeza na mzuri wa sura. Yakobo akampenda Raheli, akamwambia Labani, "Nitakutumikia kwa miaka saba kwa ajili ya kumpata Raheli binti yako mdogo."

Labani akasema, "Ni bora zaidi nikupe Raheli kuliko kumpa mtu mwingine yeyote. Kaa pamoja nami hapa." Kwa hiyo Yakobo akatumika miaka saba ili kumpata Raheli, lakini ilionekana kwake kama siku chache tu, kwa sababu ya upendo wake kwa Raheli.

Ndipo Yakobo akamwambia Labani, "Nipe mke wangu. Muda wangu umekamilika, nami nataka kulala na yeye."

Basi Labani akaalika watu wote wa mahali pale na akafanya karamu. Lakini ilipofika jioni, akamchukua Lea binti yake akampa Yakobo, naye Yakobo akalala naye. Kesho yake asubuhi, Yakobo akagundua kuwa amepewa Lea! Basi Yakobo akamwambia Labani, "Ni jambo gani hili ulilonitendea? Nilikutumikia kwa ajili ya Raheli, Sivyo? Kwa nini umenidanganya?"

Labani akajibu, "Sio desturi yetu kumwoza binti mdogo kabla ya kumwoza binti mkubwa. Maliza juma la arusi ya binti huyu, kisha pia nitakupa huyu binti mdogo, kwa kutumika miaka mingine saba."

Naye Yakobo akafanya hivyo. Akamaliza juma na Lea, kisha Labani akampa Raheli binti yake kuwa mke wake. . . . Pia Yakobo akalala na Raheli, naye akampenda Raheli zaidi kuliko Lea. Yakobo akamtumikia Labani kwa miaka mingine saba.

Kulikuwa na wivu kati ya Lea na Raheli. Lea alikuwa na wivu kwa sababu Raheli alipendwa zaidi na bwana wao. Raheli naye alikuwa na wivu kwa sababu Lea alikuwa na wavulana wengi kabla ya Raheli apate hata mmoja. Mwishowe Raheli alizaa Yusufu na Benyamini. Baada ya kupita muda, Mungu alimbariki Yakobo na wavulana kumi na wawili. Pia, licha ya Labani kujaribu kumdanganya tena na tena, Mungu alimbariki na utajiri.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, watu hufanya mambo ya aina gani wanapotaka kitu zaidi ya inavyopaswa?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
  - Alimtunza vyema yakobo na akampeleka nyumbani kwa mjombake Labani.
  - Alimpatia wake na watoto.
  - Alimfanya Yakobo awe tajiri ingawaje Labani alijaribu kumdanganya..
- **Je, Hadithi hii inatuonyesha vipi UTAKATIFU wa Mungu? (haki, anachukia dhambi, lazima ahakumu au aadhibu dhambi)**
  - Mdanganyifu alidanganywa. Dhambi hufuatwa na matokeo Fulani.
- **Je, Hadithi hii inatuonyesha vipi NEEMA ya Mungu? (rehema, anawasiliana na mwanadamu ukarimu na wema).**
  - Alimbariki Yakobo ingawaje alikuwa mdanganyifu
  - Alimlinda kutokana na madanganyo ya mjombake, na akamfanyia utajiri.
  - Alimpa wana wengi.
  - Alimyenyekesha Yakobo, kwa kubalisha adanganywe pia.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba Mungu ni Mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema)**
  - Aliendelea kumbariki Yakobo, alimfanya mkubwa na kupanua familia yake, hii ikiwa sehemmu ya ahadi Mungu aliyo mfanyia Abrahamu, Isaki, na Yakobu
  - Aliendelea kulinda familia ya Yakobo iliyo linda ahadi ya Mwokozi atakaye kuja kwa laini ya mwanamke.
  - Alimpa Lea, mke ambaye yakobo hakumpenda sana, wana wa kiume wengi akiwemu Judah, aliyekuwa babu wa zamani wa Yesu

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- Labani alikuwa mtu mbinafsi, mwenye dhambi aliye mtumia Yakobo.
- Yakobo mdanganyifu, alionja tunda la udanganyifu. Dhambi huwa na matokeo kwa binadamu.
- Yakobo hangeweza kujifanya tajiri au taifa kuu.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Hii hadithi inatusaidia vipi tutanapokumbana na anayetutesa?
- Yakobo alikuwa mdanganyifu na baadaye akadanganywa mwenyewe. Je, unajua mtu ambaye dhambi zake zilimrudia mwenyewe kumwuma? Je, haya yanatufunza nini kuhusu matokeo ya dhambi? Je hili linathibishaje kwamba tunahitaji mwokozi?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):**

- **Je, dhambi yako imewahi kugeuka na kukuumiza vipi?** Kwa maneno mengine, je, wewe binafsi umewahi kuona mtu akikutenda dhambi kwa njia sawa na wewe umemkosea mtu mwingine? Kupitia porojo? Kusengenya? Wivu? Kuiba? Uongo? Hilo lilihisije? Je, hii hadithi inakutia moyo vipi?

## 11. YAKOBO ASHINDANA MWELEKA na MUNGU
## Mwanzo 32 & 33

Baada ya Yakobo kukaa miaka mingi na Laban, alibarikiwa na makundi mengi ya wanyama wa kuchunga, na watoto wengi na watumishi wengi. Aliamua kurudi Kanaani lakini bado aliogopa kakake Esau aliyemwibia baraka yake ya Baba.

Walipokaribia nchi ya Kanani, Yakobo alizituma zawadi nyingi za wanyama kujaribu kupata fadhili kwa kakake. Wajumbe wake walirudi wakamwambia, "Esau anakuja na wanaume mia nne." Yakobo aliogopa sana, kwa hivyo aliomba, "Ee Mungu wa baba yangu Abrahamu, Mungu wa baba yangu Isaka, Eee BWANA, ambaye uliniambia, 'Rudi katika nchi yako na jamaa yako, nami nitakufanya ustawi,' mimi sistahili fadhili na uaminifu wako wote ulionitendea mimi mtumishi wako. Nakuomba, uniokoe na mkono wa ndugu yangu Esau. Ninaamini ahadi yako kufanya uzao wangu kuwa mwingi na kuwa hauwezi kuhesabika!'

Walipofika Mto wa Yordani, Yakobo aliwavusha wake zake na watoto wake ng'ambo ya mto, naye akarudi upande mwingine. Yakobo alikuwa peke yake. Baadaye usiku, mtu mmoja alishindana naye mweleka hadi mapambazuko. Yule mtu alipoona hashindwi akagusa nyonga ya Yakobo hivyo nyonga yake ikateguka huku akishindana na mwanaume huyo. Akasema, "Niache niende, maana kunapambazuka." Lakini Yakobo akajibu, "Sitakuacha uende usiponibariki."

Ndipo yule mtu akasema, "Jina lako halitakuwa tena Yakobo, bali Israeli, kwa sababu umeshindana na Mungu na watu pia nawe umeshinda."

Yakobo akasema, "Nimemwona Mungu uso kwa uso, na hata hivyo maisha yangu yameokoka."

Malaika alipoondoka, Yakobo alimwona Esau akija na jeshi. Alimwendea akainamisha kichwa chake kwa unyenyekevu. Esau akampokea kwa huruma na msamaha akashangaa jinsi Mungu alivyombariki Yakobo na watoto na wanyama. Yakobo akampatia Esau zawadi nyingi kama kondoo, mbuzi, ng'ombe, na ngamia akisema, "Kuuona uso wako ni kama kuuona uso wa Mungu, kwa kuwa umenipokea kwa neema kubwa. Tafadhali ukubali zawadi zilizoletwa kwako kwa kuwa Mungu amenineemisha na vyote nilivyohitaji." Badaye, Yakobo na Esau waliishi kama majirani kwa miaka mingi.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Zungumza na jirani yako kuhusu wakati ambapo ulikuwa unakabiliwa na hali ambayo haikuwa na uhakika na ulijihisi kuwa na woga na kutokuwa na uwezo? Ulifanya nini?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu alimbariki Yakobo na watoto na wanyama.
    - Alibadilisha moyo wa Yakobo kuongeza imani yake.
    - Mungu alimtokea Yakobo kama mwanamume. Alimlazimisha kuwa kiwete.
    - Alimlinda Yakobo.
    - Alibadilisha moyo wa Esau kwa Yakobo.
    - Alimsaidia Yakobo kurudi kuishi katika Kanaan

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali? Vipi?**
    - Mungu alimwambia Yakobo kwamba angemrudisha nchi ya ahadi.
    - Mungu alijua Yakobo alikuwa wapi na akakutanana naye kama mtu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi? Vipi?**
    - Yakobo alishangaa kuona kwamba bado yuko hai licha ya kuona uso wa Mungu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?) vipi?**
    - Yakobo aliomba akitambua kwamba matendo yote ya upendo wa kudumu na uaminifu Mungu alimwonyesha.
    - Mungu alimlinda Yakobo na kumrudisha hata ingawa hakustahili.
    - Alibadilisha moyo wa Yakobo azione dhambi zake, halafu akanyenyeshwa nazo, na kumtegemea Mungu kumsaidia.
    - Mungu aliumiza nyonga ya Yakobo kumkumbusha kwamba kutoka wakati huo hangezitegemea nguvu zake ila Mungu tu.
    - Mungu alimruhusu Yakobo kumwona na kuishi licha ya dhambi zake.
    - Mungu alibadilisha moyo wa Esau ili alimsamehe kaka wake.
    - Yakobo alipoona uso wa Mungu na kuishi, aliweza kuuona uso wa Esau aliouogopa na kuona msamaha na upendo. Ni picha ya neema ya Mungu kwa wateule kupitia Kristo Mwokozi wetu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
    - Mungu alitimiza ndoto ya Yakobo kwa kumrudisha Kanaan, kumlinda, na kumbariki.
    - Alimwokoa aliyeteuliwa wa ahadi ya Abrahamu, atakayekuwa uzao ambamo Kristo Mwokozi aliyeahidiwa atkuja siku moja.

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- Yakobo alitambua kwamba alistahili ghadhabu ya Esau, kwamba alikuwa amemkosea.
- Yakobo aliona jinsi alivyokuwa bila uwezo, na jinsi alivyohitaji Mungu.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- Mungu anajibu kwa unyenyekevu na kumtegemea. Yakobo alitambua neema ya Mungu katika maisha yake na aliyenyekeshwa mbele ya Mungu.
- Yakobo alionyesha imani yake katika Mungu alipomwendea mbele ya Esau. Hakukataa dhambi zake kwa Esau lakini alikuja kwa unyenyekevu.
- Mungu alianza kuhusiana na mwanadamu anakutana naye, akafanya ndani ya maisha yake kubadilisha moyo wake, kama alivyofanya akigusa nyonga yake alipoongea naye.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- **Yakobo alidhoofishwa na Mungu Kwa kugusa nyonga yake. Ni njia gani hasa Mungu anaweza gusa nyonga ya mtu?** Au mungu anaweza kutumia kutudhoofisha ili tumtegemee zaidi kwa imani?

- Yakobo alijua alimkosea Esau kwa hivyo alisimama mbele zake kwa unyenyekevu. Je ni hatari vipi kwetu tukichukua hii njia ya unyenyekevu mbele ya mtu ambaye tumemwumiza? Hii hadithi ina tuhimizaje?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Je,Mungu alikugusa vipi nyonga yako? Unahisi dhaifu kwa njia zipi?** Je, Mungu anaweza kuwa anafanya kazi katika maisha yako ili kuongeza imani yako kwake?

- **Ni watu gani katika maisha yako ambao umewakosea?** Unahitaji kuomba msamaha kutoka kwa nani? Je, injili inawezaje kukusaidia kuwa tayari kukiri dhambi yako na kutafuta msamaha kutoka kwao na pia kwa Mungu?

## 12. YUSUFU
## Mwanzo 37, 39-50

*Kupendwa na Baba yake, Kuchukiwa na Ndugu zake*

Yakobo aliporudi nchi ya Kanaani alikuwa na wana kumi na wawili. Mzaliwa wa kumi na mmoja, yaani mzaliwa wa kwanza wa Raheli, aliitwa Yusufu. Yakobo alimpenda Yusufu zaidi ya wana wengine. Hasa alimpatia Yusufu koti ya rangi nyingi tofauti maridadi. Wana wengine walipoona kwamba Yakobo alimpenda Yusufu zaidi yao, walimchukia Yusufu. Na pia Yusufu alipowaambia ndoto zake zilizodokeza kwamba siku moja watamsujudia, walizidi kumchukia na kumwonea wivu.

Siku moja, Yusufu alikwenda mahali ambapo ndugu zake walikuwa wakichunga kondoo na mbuzi. Mwanzoni ndugu walipanga kumuua, lakini wakaishia kumuuza kwa wafanyabiashara fulani walipokuwa wakienda Misri. Baadaye walichinja mbuzi na kuifunika kanzu hiyo na damu, kisha wakaipeleka nyumbani kwa Yakobo, ambaye aliomboleza kifo cha Yusufu, akifikiri kwamba mnyama-mwitu amemuua mwana wake.

*Watumwa huko Misri*

Wakati huo, wafanya biashara walimpeleka Yusufu Misri, wakamuuzia mtu mkuu aliyeitwa Potifa kama mtumwa. Hata ingawa Yusufu alimtumikia Potifa vizuri na alimletea baraka katika nyumba yake, mke wa Potifa alimsingizia kwamba alitaka kumbaka. Kwa hivyo Yusufu alifungwa gerezani.

Alipokuwa gerezani, mfalme wa Misiri, aliyeitwa Farao, aliota ndoto asiyoielewa. Mfanyakazi wa Farao aliyekuwa amefungwa gerezani pamoja na Yusufu alikumbuka kwamba Yusufu aliweza kutafsiri ndoto. Kwa hivyo Farao alimwita Yusufu. Kwa usaidizi wa Mungu, Yusufu alitafsiri maana ya ndoto. Kungekuwa na miaka saba ya mavuno tele na miaka saba ya njaa kuu. Farao alifurahi sana kwamba Yusufu aliweza kumwambia maana ya ndoto. Kwa hivyo alimfanya mtawala juu ya Misiri. Yusufu alikuwa chini ya Farao tu. Punde, Yusufu alianza kuweka nafaka katika maghala ili kujiandaa kwa njaa. Baada ya miaka saba ya kushiba, kulikuwa na njaa kuu ndani ya Misiri.

*Kuungana Tena na Ndugu Zake*

Wakati huo, pia kulikuwa na njaa nchi ya Kanaani walipoishi Yakobo na wanake. Lakini, kwa sababu ya mpango wa Yusufu, bado kulikuwa na nafaka Misiri. Yakobo aliposkia kwamba kulikuwa na nafaka Misri, aliwatuma wanake kumi ili kuenda kuleta chakula. Ndugu za Yusufu walipofika Misri, Yusufu aliwatambua, lakini wao hawakumtambua Yusufu. Wao walikuja wakiinama mbele ya Yusufu kwa sababu alikuwa mkubwa wa Misri. Baada ya muda kwa Yusufu kuwajaribu ndugu zake kwa siri kwa njia kadhaa, aliona kwamba walijuta sana kwa kumuuza utumwani. Kisha Yusufu akajidhihirisha kwao kwa machozi. Akasema, "Mimi ni Yusufu, yule mliyemuuza Misri; msiwe na huzuni, wala msijikasirikie nafsi zenu, kwa kuniuza hapa. Kutakuwa na miaka

saba ya njaa. Lakini Mungu alinituma niwatangulie ili kuhifadhi jamaa yangu na kuokoa maisha yenu kwa wokovu mkuu. Kwa hiyo, si ninyi mlionileta huku, bali Mungu ndiye aliyeniweka kuwa bwana wa nyumba ya Farao na mtawala wa Misri yote." Baada ya hayo, Yusufu akawatuma watu wamlete baba yake Yakobo, na jamaa wake wote. Yakobo aliishi huko Misri miaka kumi na saba kabla ya kufa kwake na akarudishwa Kanaani kuzikwa.

Baada ya Yakobo kufa, ndugu za Yusufu waliogopa kwamba Yusufu angewaadhibu kwa sababu ya yale waliyomtendea, hivyo walimwomba tena awasamehe. Lakini Yusufu akawaambia, "Msiogope! Je, mimi ni badala ya Mungu? Mlikusudia kunidhuru, lakini Mungu alikusudia kuwa mema ili kutimiza yale yanayofanyika sasa, kuokoa maisha ya watu wengi. Msiogope, nitawapa riziki ninyi na watoto wenu." Naye akawatuliza na kusema nao kwa upole.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Ni lini umekuwa na wakati mgumu kuwasamehe watu waliokukosea? Kwa nini tuwasamehe wengine?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Je, tunajifunza nini kuhusu MUNGU katika hadithi hii? Mungu alifanana na nini?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu alimlinda Yusufu – kutoka kwa nduguze waliotaka kumwua, kutoka kisimani ambamo angezama, kutoka kwa kutenda uzinzi, kutoka kwa uovu katika gerezani.
    - Mungu aliongoza mioyo ya ndugu wa Yusufu, kle ambacho mwanadamu alikusudia kwa uovu Mugnu alikusudia mema na aliyafanya kulingana na mpango wake.
    - Mungu aliongoza mawazo ya kaka wa Yusufu, akawafanya kufikiri wazo jingine badala ya kumwua.
    - Mungu aliwaokoa Waisraeli kutoka kwa njaa kwa kuwapa pahali pa usalama katika Misri.
    - Mungu alikuwa na uwezo kutimiza ndoto ambazo alimpa Yusufu.
    - Mungu aliruhusu vitu vibaya kumfanyikia Yusufu naye akaleta uzuri kutoka kwa vitu hivyo. Alikuwa enzini akiongoza.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali? Vipi?**
    - Mungu alijua mipango ya ndugu za Yusufu na akabadili mawazo yao.
    - Mungu alijua kwamba Yusufu atakuwa na uwezo juu ya babake na nduguze, na akamwosha hivyo katika ndoto.

- Mungu alijua kwamba njaa na kiangazi vingeua familia ya Yakobo kwa hivyo alipaswa kuwafanyia njia ya kuepuka.
- Mungu alimpa Yusufu uwezo wa kutafsiri ndoto.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?)**
  - Si lengo kuu la hadithi, lakini tunaona utakatifu wake kwa kulinda taifa la Israeli ili kwamba wangeweza kuwa taifa maalum.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na ana wasiliana na wanadamu?)**
  - Kwa familia ya Yakobo – Mungu aliwaokoa kutoka kwa kiangazi.
  - Kwa kaka zake Yusufu – Mungu alimsaidia Yusufu kuwa na huruma kwao.
  - Kwa Yusufu – Mungu alimlinda kutoka kwa hatari katika njia nyingi.
  - Kwetu sisi wote – Mungu aliwaokoa Waisraeli kutoka kwa njaa na kwa hivyo aliendelea kutimiza ahadi yake ya kutuma Mwokozi kupitia kwao, kupitia kwa uzao wa mwanamke, na kupitia katika uzao wa Ibrahim.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.)**
  - Alikuwa mwaminifu kutimiza ahadi kwa Abrahamu kubariki mataifa yote ya ulimwengu kupitia kwake. Hakuruhusu familia yake kufa na kumalizika.
  - Alifanya ndoto za Yusufu kutimia na hata kutafsiri kwa ndoto za Farao kuweza kutimia.

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu.**
  - Alitimiza ahadi yake kwa Abrahamu kwa kuhinda na kuhifadhi familia yake.
  - Alimtunza Yusufu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
  - Nduguze Yusufu walimtendea dhambi kwa kumwonea wivu.
  - Mke wa Potifa alimtendea Yusufu dhambi.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi jujiokoa mwenyewe?**
  - Yusufu hakuwa na uwezo wa kujiokoa mwenyewe – kutoka kwa nduguze na jela.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyeshaje kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa?**
  - Yusufu alimtumainia Mungu kwa maisha yake tena na tena. Alionyesha imani yake kwa kuwa mtiifu. Kwa mfano alijizuia kutoka kwa jaribu la uzinzi, akijiweka hatarini ili aitii sheria ya Mungu. Pia alimtumainia Mungu kuhukumu nduguze na hakujaribu kulipiza kisasi kwao kwa kumfanya mtumwa.

- **Je, tunajifunza jambo lingine lolote kuhusu jinsi imani inavyopaswa kuonekana katika maisha yetu, hasa mtu anapotutendea dhambi?**
  - Hakuwa na kinyongo dhidi ya ndugu zake. Alijua kwamba hakuwa katika nafasi ya Mungu kuhukumu.
  - Alitambua kwamba Mungu ana udhibiti, na ana kusudi kuu la kuwaokoa watu

- Aliwapenda maadui zake. Alizungumza na kuwatendea wema.
  - Alijua kwamba angeweza kuwaonyesha ndugu huruma kwa sababu ya rehema ambayo Mungu alikuwa amemwonyesha.
- **Ni njia zipi tunazojaribu kujiweka mahali pa Mungu?**
  - Kwa kujaribu kuwa mamlaka yetu wenyewe ya kimaadili, tukijiamulia wenyewe yaliyo mema na mabaya.
  - Kwa kuwatafuta watu wengine ili kukidhi mahitaji yetu ya ndani kabisa.
  - Kupitia wasiwasi mkubwa (kutilia shaka kama Mungu ana nia njema kwako).
  - Kupitia kushikilia kinyongo (Lazima tukumbuke kwamba kisasi ni cha Mungu. Tusiposamehe, sisi wenyewe tunakuwa waovu.)
    - "Njia ya haraka zaidi ya kuwa kama Shetani ni kujaribu kuwa Mungu."
    - "Njia ya haraka zaidi ya kuwa kama Mungu ni kukataa kuwa Mungu."

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- **Yusufu alikataa kujiweka mahali pa Mungu.** Je ni baadhi ya njia gani unajaribu kujiweka mahali pa Mungu badala ya kusamehe kwa kweli?

- **Yusufu aliweza kuchukua mtazamo wa Mungu.** Unawezaje kuangalia nyuma katika nyakati ngumu maishani mwako na kuona kwamba Mungu ndiye anayetawala na amefanyia kazi baadhi ya magumu yako kwa manufaa ya wazi?

- Kwanini ni vigumu sana kuchukua mtazamo wa Mungu na kumwamini kwa kutazama mbele badala ya kuitika kwa hasira na machungu wakati unapoumizwa?

- Je, ni dhambi gani Mungu ametusamehe? Je, kukumbuka haya yatatusaidiaje kusamehe?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Shiriki wakati mtu alikuumiza na ukataka kuchukua nafasi ya Mungu?**

- **Je, ni changamoto gani katika maisha yako sasa ambapo ni vigumu kuamini** kwamba Mungu anafanya kazi? Labda mambo hayaonekani kuwa sawa au yana maana? Je, ni kwa jinsi gani kuwa na mtazamo wa Mungu (yaani, kuamini kwamba Mungu anadhibiti na kufanyia kazi mambo kwa wema) kunaweza kukusaidia kukabiliana na changamoto hizi?

- **Je, umepitia maumivu ya muda mrefu na yenye uchungu yaliyosababishwa na mtu mwingine?** Je Mungu amekuwaje wa rehema kwako? Je, rehema yake itakusadiaje kusamehe? Imani yenye kina zaidi katika enzi kuu ya Mungu na upendo wake kwako kunaweza kukusaidia kwa jinsi gani kuacha machungu na kusamehe?

## 13. KUZALIWA na KUTOROKA kwa MUSA
## Kutoka 1-2

Yusufu aliaga dunia na akazikwa huko Misri. Na familia ya Yakobo wakawa watu wengi. Waliitwa watu wa Israeli au Waebrania. Basi kukawa na mfalme mpya katika Misri asiyemjua Yusufu. Alipoona kwamba watu wa Israeli walikuwa wengi sana, aliogopa, akawafanya watumwa. Aliogopa kwamba wangewashambulia Wamisri na kuwashinda, hivyo hata akaamuru kwamba kila mtoto wa kiume aliyezaliwa katika Israeli auawe anapozaliwa. Lakini wakunga Waisraeli walimheshimu Mungu na hawakufanya walivyoambiwa na Farao. Bali Mungu aliwalinda kutoka na Farao. Basi Waisraeli wakaendelea kuongezeka.

Palikuwa na familia ya Israeli kutoka ukoo wa Lawi nao wakawa na mtoto wa kiume aliyekuwa mrembo. Walimficha kwa muda wa miezi mitatu, lakini hatimaye wakamweka katika kikapu kilichofunikwa kwa lami na kukiacha kikielea mtoni. Dada mkubwa wa mtoto huyo aliitwa Miriamu. Alikaa kwenye karibu na kikapu akitazama ni kitu kipi kingemfanyikia mtoto huyo.

Basi binti wa mfalme wa Misri alikuja kwenye mto Nile pamoja na marafiki wake, akamwona mtoto akamchukua awe mwana wake. Akamwita jina lake Musa kwa maana alimtoa kwenye maji. Miriamu akamjia binti wa mfalme na kumwuliza, "Je ungependa nikutafutie mwanamke Mwebrania kukunyonyeshea mtoto huyu?"

Binti wa mfalme akasema, "Ndiyo, nitafutie mwanamke nami nitamlipa kumnyonyesha mtoto huyu." Ikawa hivyo. Mtoto huyu alipokuwa mkubwa, Mama yake alimpelekea binti wa mfalme naye akawa mwana wake. Basi Musa akakulia katika jumba la mfalme wa Misri.

Wakati Musa alipokuwa mtu mzima, siku moja alitoka kati ya watu wake Waisraeli. Hapo aliona Mmisri akimpiga Mwisraeli. Aliangalia pande zote asione mtu yeyote, kisha akamwua Mmisri huyo na kuuficha mwili wake. Lakini jambo hili lilijulikana naye Musa akatorokea jangwani.

Lakini Mungu aliyaona mateso ya watu wake Waisraeli, akakumbuka agano lake na Abrahamu, Isaka, na Yakobo.

### MPANGILIO wa SOMO

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kutaja wakati ambapo ulikuwa hoi kutatua tatizo fulani kisha Mungu akakusaidia?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

<u>**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**</u>

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Ulinzi wa Musa kutoka kwa mfalme mwuuaji.
    - Mungu alikuwa na mpango kwa watu wake kukomboa watu kutoka utumwani na alikuwa anaanza mpango huo.
    - Alichagua kutoka familia ya Lawi.
    - Mungu alimwongoza binti wa Farao kuenda kuoga katika mto Nile wakati ule mtoto musa alikuwa hapo. Ulikuwa mpango wake kumwokoa katika njia hii.
    - Hata ingawa binti wa Farao alijua kwamba mtoto huyo alikuwa Mwaisraeli, Mungu alimlinda Musa ili huyu msichana kumlea badala ya kumwua.
    - Alimlinda kutokana na kuzama, mbu na wanyama wa mwituni.
    - Mungu alimweka Musa katika jumba la Farao ambapo ingemsaidia baadaye katika kukumbana na Farao.
    - Aliwapa wazazi wa Musa hekima ya kumficha kwa miezi mitatu.
    - Alitayarisha maisha ya mwanzo ya Musa, kupata elimu nzuri, na bado alimruhusu kulelewa na mama yake katika miaka ya kwanza kabisa ili aweze kuwa bado ni Mwisraeli.
    - Mungu alimtuma Musa jangwani kwa matayarisho zaidi.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Alijua kwamba njia ya kuwakomboa watu wake ni kupitia kwa Musa, na alijua jinsi ya kumwokoa.
    - Alijua mipango ya binti wa Farao ya kuenda kuoga.
    - Alijua kwamba mtoto Musa alikuwa maalum na alihitaji utunzi na pia elimu nzuri.
    - Mungu alijua kwamba Musa alihitaji wakati katika jangwa kumtayarisha ili amtumikie.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?)**
    - Alimtenga Musa na Wamisri wasiomjua Mungu katika wakati uliofaa.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na ana wasiliana na wanadamu?)**
    - Hata ingawa binti wa Farao alijua kwamba mtoto alikuwa Mwisraeli, Mungu alimwongoza kumlea badala ya kumwua.
    - Mungu alimlinda mtoto huyo kwa miezi mitatu kabla ya kuwekwa mtoni.
    - Alimwua Mmisri lakini Mungu kwa neema yake alimlinda licha ya yeye kuwa mwenye dhambi.
    - Ulinzi
    - Alisaidia jamaa ya Musa.
    - Mungu bado anafanya mpango wa kuwaokoa watu wake.
    - Alifanya Israeli kuwa taifa kuu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.)**
    - Mungu bado anaendelea kutimiza ahadi yake ya kuwakomboa watu wake kutoka Misri. Hapo awali aliahidi Abrahamu na Yakobo kuwakomboa watu kutoka utumwani baada ya miaka mia nne.
    - Alikuwa mwaminifu kuilinda Israeli hata ingawa mfalme alitoa agizo la uovu.
    - Alikuwa ameahidi Abrahamu kwamba atawafanya uzao wake kuwa wengi na alitimiza ahadi hiyo hata ingawa walikuwa utumwani.

<u>**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**</u>

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu?**
    - Mungu aliwalinda Musa na Waisraeli hata ingawa waliteswa sana.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Wamisri walikuwa waovu kwa Waisraeli, waliwatesa, wakijaribu kuwana watoto wao.
    - Musa aliua, akajaribu kiuficha kitendo hicho.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Jamaa ya Musa walijaribu kumwokoa, lakini mwishowe walishindwa Mungu alihitaji kupeana njia ya kufanya hivyo.
    - Musa alijaribu kusaidia watu wake, lakini alishindwa, juhudi zake hazikufaulu.
    - Watu waliokuwa utumwani hawangejisaidia wenyewe.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- Ni katika mikono ya Mungu tu kwa sababu mwanadamu hawezi kujiokoa, anaweza kufuata mpango wa Mungu pekee.
- Mama alimtumainia Mungu kufanya mpenzi yake kwa mwanawe.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Ni mambo gani hutufanya kuwa watumwa siku hizi? Je, hii hadithi inaweza kukusaidia vipi?

- Wakunga wa Kihibrania walikosa kuti amri za mfalme. Je, kuna wakati wowote unaofaa wa kuvunja sheria au kutotii amri ya kiongozi?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):**

- **Ni changamoto gani hasa unayo katika maisha yako ambapo unahitaji msaada wa Mungu? Je, unajihisije kutegwa kama mtumwa Misri? Je, hadithi hii inaweza kukusaidiaje?** Inaweza kukusaidiaje kujua kwamba Mungu anajua na anajali kuhusui kila kitu, hata hiyo hali uliyo nayo sasa?

## 14. MWITO wa MUSA KATIKA KICHAKA AMBACHO KILICHOMEKA
## Kutoka 3-4

Musa alikuwa na umri wa miaka arobaini alipokimbia kutoka Misri. Aliishi jangwani kwa miaka arobaini zaidi na akamwoa Sipora, binti Yethro, aliyekuwa kuhani wa Midiani.

Siku moja, Musa alikuwa akichunga kondoo za baba mkwe wake karibu na Mlima Sinai, na malaika wa BWANA akamtokea katika miali ya moto kutoka ndani ya kichaka. Musa akaona kwamba hata ingawa kile kichaka kilikuwa kinawaka moto, hakikuteketea. Kwa hiyo akakaribia kuona maono haya ya ajabu, na Bwana akamwita kutoka ndani ya kile kichaka, "Musa! Musa!"

Musa akajibu, "Mimi hapa."

Mungu akasema, "Usikaribie zaidi. Vua viatu vyako, maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Nimeona mateso ya watu wangu huko utumwani Misri. Sasa ninapanga kuwaokoa na kuwarudisha katika nchi ya Wakanaani, nchi tele inayotiririka maziwa na asali. Basi sasa nenda, nakutuma kwa Farao ili kuwatoa watu wangu Waisraeli kutoka Misri."

Ndipo Musa akaficha uso wake, kwa sababu aliogopa kumwangalia Mungu. Naye akaanza kubishana na Mungu akisema, "Mimi ni nani hata niende kwa Farao na kuwatoa Waisraeli kutoka Misri? Je, Waisraeli wasiponiamini? Na je, wakiuliza ni nani aliyenituma? Jina lake ni nani?"

Mungu akasema, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Hivi ndivyo utakavyowaambia Waisraeli: ' MIMI NIKO amenituma kwenu.'" Pia Mungu akamwambi Musa, "Nitakuwa pamoja nanyi. Na hii itakuwa ishara kwako kwamba Ndimi Mimi niliyekutuma: Utakapowatoa watu kutoka Misri, mtaniabudu kwenye mlima huu."

Mungu akampa Musa ishara nyingine mbili ili kuwaonyesha watu ili waweze kuamini kile alichokisema. Akasema, "Itupe chini fimbo yako." Musa alifanya hivyo, na ikawa nyoka! Ndipo Mungu akasema, "Sasa mshike kwa mkia." Musa alipoiokota, ikawa fimbo tena. Kisha Mungu akamwambia aweke mkono wake ndani ya vazi lake. Alipoutoa, ulikuwa umefunikwa na ukoma, lakini alipourudisha tena ukapona. Kisha Mungu akasema, "Utawaonyesha Waisraeli ishara hizi ili wapate kuamini kwamba Bwana, Mungu wa baba zao, amekutokea."

Mungu pia aliahidi kumtuma Haruni ndugu ya Musa pamoja naye. Kwa hiyo Musa akakubali na kurudi Misri.

### MPANGILIO wa SOMO

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kufikiria wakati ambapo ulihisi kulemewa na ukuu na utakatifu wa Mungu? Hilo lilikufanya uhisije?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu alikuwa na uwezo kuonekana kama mwale wa moto, lakini alikuwa na uwezo kutoteketeza kichaka. Mungu hutawala uumbaji wake wote.
    - Mungu alikuwa na uwezo kumwonyesha Musa ishara kubwa kama kugeuza fimbo kuwa nyoka na kufanya mkono kupooza.
    - Mungu alikuwa na mamlaka juu ya Musa na Waisraeli. Musa alipaswa kutii.
    - Jina la Mungu, "Mimi niko ambaye niko," linatuambia kwamba Mungu hakuhitaji mtu yeyote. Yupo kwa nguvu yake mwenyewe na amekuwepo tangu kabla ya mwanzo. Yuko juu ya yote.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Mungu alijua hali ya watu wake katika Misri.
    - Alijua kwamba Musa alikuwa kiongozi aliyefaa. Alikuwa amejua kabla ya wakati huo na alikuwa amemtayarisha kwa kazi hii kwa kumwokoa alipokuwa mchanga. Pia alimtayarisha kwa kulazimisha kulelewa katika jumba la mfalme wa Misri na kukimbilia jangwani.
    - Mungu alijua alivyopanga kufanya kuwaokoa Waisraeli.
    - Alijua kwamba Waisraeli wangerudi Mlima wa Sinai kumwabudu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Mungu mwonekania Musa kama mwale wa moto.
    - Akasema, "Usikaribie. Toa viatu vyako kwa maana hapa ni pahali patakatifu." Pangepaswa kuwa utengano kati ya Mungu na mwenye dhambi Musa.
    - Jina lake, "Mimi niko ambaye niko" linatuambia kwamba Mungu yuko juu na anajitenga kutoka kwa wenye dhambi . Mungu ni mtakatifu zaidi!

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu aliyaona mateso ya watu wake na alipanga kuwaokoa na kuwaongoza kwa nchi aliyowaahidi.
    - Mungu aliongea na Musa.
    - Mungu aliomtokea Musa lakini hakumwadhibu hata ingawa ni mwenye dhambi.
    - Mungu alimtumia mwenye dhambi kama Musa kutimiza mapenzi yake.
    - Mungu alipanga kuwaokoa Waisraeli ili angetimiza ahadi yake kuyabariki mataifa yote kupitia kwao. Hangewaruhusu kuangamizwa katika Misri. Alikuwa na mpango kukomboa watu wake wote katika historia.
    - Alimlinda Musa kwa nyoka aliyemchukua.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
    - Mungu alitimiza mpango wake kuwaokoa watu wake.
    - Alisema wangerudi kuabudu kwa Mlima wa Sinai.
    - Aliahidi kuwa na Musa
    - Alikuwa mtulivu sana na Musa aliyekuwa na mashaka mengi. Angemwangamiza kwa kutoamini kwake. Mungu ni mvumilivu na watu wanaong'ang'ana kuamini.

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu.**
    - Mungu aliwajali watu wake wateule na alipanga kuwaokoa.
    - Alipanga kuwaokoa wanadamu kupitia uzao wa mwanamke atakayekuja kupitia taifa la Israeli. Mungu alitaka kurudisha uhusiano na watu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Kwa sababu Musa alikuwa mwenye dhambi, alipaswa kutoa viatu vyake na kusimama mbali na kichaka. Mwenye dhambi hawezi kumkaribia Mungu mtakatifu isipokuwa Mungu anafanya njia.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Waisraeli hawangeweza kujiokoa.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- **Hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Waisraeli wangeokolewa tu kwa mpango na mapenzi ya Mungu.
    - Musa alipaswa kumwendea Mungu kama Mungu alivyomwamuru.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.**
    - Musa alijua kwamba yeye alikuwa mwenye dhambi aliyesimama katika uwepo wa Mungu mtakatifu.
    - Mungu alihitaji Musa kuamini ili angetii mwito mgumu wa Mungu kwa maisha yake.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Musa alibadilishwa wakati alikutana na Mungu uso kwa uso katika utakatifu wake. Je, mtu anawezaje leo kupata ufahamu mkuu wa utakatifu kamili wa Mungu? Kwa kutazama uumbaji? Kufikiria kuhusu sheria za Mungu?
- Unaweza kustaajabu kwa sababu ya **utakatifu wa Mungu** au kunyenyekewa na **hali yako ya dhambi** ukilinganisha na matakwa matakatifu ya Mungu. J**e, hii inawezaje kukusaidia katika uhusiano wako na Mungu?**
    - Inaonyesha jinsi unahitaji mwokozi na inakuvuta kwake kupitia toba.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- Je, wewe binafsi unawezaje kuzingatia utakatifu wa Mungu na hali yako ya dhambi kwa ukamilifu zaidi? Mungu angeweza kukuonyesha nini? Unapaswa kuitika vipi?

- **Je, unapitia wakati wa mateso au kuhisi kama uko katika jangwa la kiroho?** Je, Mungu anaweza kuwa anakutayarisha kwa nini?

- **Je, unaamini kwamba Mungu anakuita kufanya jambo gani ambalo linaweza kuwa gumu au changamoto?** Je, ingekuwaje kwako kumwamini Mungu katika eneo hili?

# 15. MAPIGO TISA
## Kutoka 7-11

Baada ya Musa na ndugu yake Haruni kukutana na wazee wa Israeli, walimwendea Farao wakasema, "Mungu wa Israeli asema, "Uruhusu watu wangu kuenda, ili wapate kuniabudu jangwani."

Farao akasema, "Bwana ni nani, hata niisikize sauti yake? Mimi simjui Bwana wala sitawapa Waisraeli ruhusa waende zao. Kwa nini mnawachukua watu kutoka kazi yao? Nendeni sasa!" Farao alikasirika kwa hivyo alisababisha kazi ya Waisraeli iwe ngumu zaidi. Waisraeli wakamlilia Musa.

Musa akamwomba Mungu na Mungu akasema, "Nenda waambie Waisraeli, 'Nimekisikia kilio chenu na nitawaokoa kutoka kwa Misri na nitawafanya watu wangu na nitawaleta katika nchi ambayo nimewaahidi Abrahamu, Isaka, na Yakobo."

Basi Musa na Haruni walimrudia Farao na mashindano kati ya mfalme wa Misri na Mungu wa Israeli yakaanza. Kwanza, Haruni alimwonyesha ishara ya fimbo iliyobadilika na kuwa nyoka. Lakini Farao hakuamini akakataa kuwaruhusu Waisraeli kuenda. Kisha mapigo yakaanza. Musa alinyoosha mkono wake juu ya maji ya Misri na mito na maziwa na maji yote yalibadilika kuwa damu hata maji yaliokuwemo ndani ya mitungi. Samaki wote katika Mto wa Nile walikufa na mto ulinuka vibaya na watu, hawakuweza kunywa maji yake. Hata hivyo, Mungu akaufanya moyo wa Farao kuwa mgumu na akakataa kuwaruhusu waende.

Kwa hivyo, Mungu alilituma pigo la vyura kwa nchi yote na Farao akamwita Musa, "Mwombe Bwana kuwaondoa vyura hawa na nitawaruhusu waende." Musa akafanya hivyo lakini Farao akabadilisha mawazo yake.

Kisha Haruni alinyoosha fimbo yake na kupiga mavumbi yote ya Misri yakabadilika kuwa pigo la chawa. Waganga hawakuweza kuiga pigo hilo kama walivyofanya kwa mapigo mengine na wakasema, "Hiki ndicho kidole cha Mungu!" Lakini Farao akakataa tena kusikiliza.

Basi Mungu aliyatuma mapigo mengine sita kwa Wamisri ila hayakuwaguza Waisraeli hata kidogo. (Yalikuwa mapigo kama mainzi, magonjwa ya mifugo, majipu, mvua ya mawe, nzige, na giza nzito.) Kila pigo lilipokuja, Farao alisema "Ndiyo, waende." Lakini baada ya pigo kuondolewa alikuwa akikataa waende.

Kwa hivyo Mungu akamwambia Musa, "Nimefanya moyo wa Farao kuwa mgumu ili kuwaadhibu Wamisri kwa miungu yao. Ninafanya ishara hizi ili mtawaambia watoto wenu na wajukuu wenu hata mjue kwamba mimi ndimi Bwana! Nitalileta pigo lingine moja kwa Misri, halafu Farao atawafukuza kabisa."

### MPANGILIO wa SOMO

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- Ni nini kinachofanya mioyo yetu kuwa migumu kwa Mungu? Jinsi gani dhambi ndogo inaweza kutuongoza kwa kubwa zaidi?

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu alikuwa enzini, alikusudia kuonyesha utukufu wake kwa Wamisri na Waisraeli alijua kwamba Farao angepinga. Mungu hashikwi na wasiwasi anajuia kila kitu ambacho kinafanyika.
    - Mungu aliongoza moyo mgumu wa Farao. Akamfanya mbumu hata zaidi.
    - Alikuwa na haki ya kufanya alichotaka kufanya na Farao na Wamisri.
- **Je, hadithi hii inaonyeshaje vipi kuwa Mungu ANAJUA yote? (Yupo kila Pahali)**
    - Je, hadithi hii inaonyesha vipi Utakatifu wa Mungu? (Haki, anachukia dhambi, lazima kuhukumu na kuadhibu dhambi kwa kifo.)
    - Mungu alichukia kuabudu sanamu kwa Wamisri. Aliadhibu ugumu wa moyo wa Farao.
    - Dhambi ilileta kifo katika Misri hata pia mapigo hayo mengine.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kuwa Mungu ni mwenye Neema? (Huruma, Anawasiliana na mwanadamu, Ukarimu, Wema)**
    - Aliwaokoa Waisraeli hata ijapo walikuwa wenye dhambi.
    - Aliwasiliana na Waisraeli kupitia kwa Musa.
    - Aliwapa Wamisri nafasi nyingi kubadilika.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kuwa mungu ni Mwaaminifu? (Habadiliki)**
    - Mungu anatimiza ahadi yake ya kuleta mwokozi kwa ulimwengu kupitia kwa Waisraeli.
    - Anatimiza ahadi yake kwa Abrahamu ya kuwaondoa wazao wake kutoka utumwani baada ya miaka mia nne, na kuwatoa utumwani wakiwa na mali nyingi mno.
    - Anatimiza ahadi yake kwa Musa ya kumtumia kukomboa watu wake.
    - Anatimiza ahadi yake ya kuadhibu wasiokuwa nyuma ya damu.

**Tunaweza kujifunza nini kuhusu MWANADAMU kutoka kwa hadithi hii?**

- Mwanadamu ni mwenye dhambi. Msumbufu. Moyo mgumu wa Farao. Ibada ya Wamisri ya miungu mingine.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Mungu aliwaadhibu Wamisri kwasababu ya kuabudu miungu wa uwongo**. Je, baadhi ya miungu wa uwongo wanaoabudiwa katika jamii zetu leo ni gani?** Kuabudu hawa miungu wa uwongo haimaanishi kuwainamia tuu. **Je, ni njia gani myingine tunaabudu au kuwategemea hawa miungu wa uwongo?**

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je, ni sanamu moja gani au mungu wa uwongo yupi katika maisha yako leo amabaye wewe humtegemea badala ya Mungu?** Je, sanamu hii inakuzuiaje kumwamini Mungu au kukua katika Kristo?

- Mungu aliwalinda Waisraeli kutokana na mapigo yaliyowaumiza Wamisri. **Je, ni katika eneo gani la maisha yako ambapo Mungu anakuomba wewe binafsi umtegemee kwa subira zaidi?**

## 16. PASAKA
## Kutoka 12

*Ugumu wa Moyo wa Farao / Pigo Moja la Mwisho*

Baada ya mapigo tisa ya kwanza, Mungu alimwambia Musa, “Nimefanya moyo wa Farao kuwa mgumu kuwaadhibu WaMisri kwa miungu yao. Ninafanya ishara hizi ili mtawambia watoto wenu na wajukuu wenu hata mjue kwamba mimi ndimi Bwana! Nitalileta pigo lingine moja kwa Misri halafu Farao atawafukuza kabisa.

*Maelekezo ya Mungu*

Haya ndio yalikuwa maelekezo ya Mungu kwa Waisraeli.

Mnisikilize kwa makini.

1) “Lazima kila familia (au familia mbili pamoja kama ni familia ndogo) kuchukua mwana kondoo au mbuzi moja wa mwaka mmoja wa kiume asiye na waa achinjwe jioni giza linapoingia.

2) “Chovya mti unaitwa hisopo katika damu na mpake pande zote mbili za mlango wa nyumba na juu ya mlango, katika ile nyumba ambamo mtamla mwana kondoo. Kisha kaeni ndani ya nyumba na ishara ya damu mpaka asubuhi.

3) “Mwichome nyama na kuila yote. Msiyaache mabaki hata msivunje mifupa. Mle na mboga chungu na mkate bila chachu. Mle haraka mkivaa mavazi ya safari.”

“Usiku ule nitapita katikati ya Misri na kuwauwa kila mzaliwa wa kwanza kuwaadhibu Wamisri kwa kuwaabudu miungu ya uongo. Lakini damu itakuwa ishara kwenu. Nitakapoiona damu juu ya mlango nitapita juu yenu.

“Ni lazima msherehekee sherehe hii kila mwaka. Watoto wenu watakapowaulizeni, ‘Maana ya sherehe ni nini?’ Waambieni, ‘Kwa siku hiyo, Bwana alituleta kutoka utumwa katika Misri.’”

*Kutoa Mwanakondoo / Ukombozi*

Basi, watu walitoa dhabihu ya wanyama na damu ikamwagwa kisha wakaiweka kwenye milango. Usiku wa manane Mungu alipita kwenye Misri, akawaua kila mzaliwa wa kwanza – kutoka jumba la ufalme la Farao, mpaka mfungwa gerezani na wazaliwa wa kwanza wa wanyama pia. Lakini Mungu alipoiona damu ya dhabihu ya mwana kondoo kamilifu kwenye milango ya Waisraeli, alipita juu yao. Kulikuwa kimya kule Waisraeli walikuwa, hata mbwa hawakubweka. Lakini mahali Wamisri walipoishi, kulikuwa na kilio kikuu katika usiku.

Usiku, bado kukiwa na giza Farao aliwaita Musa na Haruni akasema, “Chukueni kila kitu mlicho nacho mwondoke!” Na majirani wao wa Wamisri walisema, “Ndiyo

nendeni au tutakufa!" Nao wakawapa Waisraeli vitu vyao vya thamani kama dhahabu, fedha na kadhalika, kama vile Mungu alivyowaambia Musa, hata Abrahamu zamani.

Siku hiyo Mungu aliwakomboa watu wake kutoka nchi ya Misri. Walikuwa karibu wanaume laki sita na wanawake, watoto na mifugo yao.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Zungumza kuhusu wakati ambapo ulilazimika kujificha ili kujikinga na hatari. Ulijisikiaje?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
  - Mungu alikuwa enzini, alikusudia kuonyesha utukufu wake kwa Wamisri na Waisraeli alijua kwamba Farao angepinga. Mungu hashikwi na wasiwasi anajuia kila kitu ambacho kinafanyika.
  - Mungu aliongoza moyo mgumu wa Farao. Akamfanya mbumu hata zaidi.
  - Alikuwa na haki ya kufanya alichotaka kufanya na Farao na Wamisri.

- **Je, ni vipi hadithi hii inaonyesha kuwa Mungu ANAJUA yote? (Yupo kila Pahali)**
  - Alijua moyo wa Farao, na kile angefanya, na jinsi Mungu angetukuka katika mambo hayo yote.
  - Alijua kile kingefanyika na kwamba Waisraeli wangeyakumbuka na kusherehekea kupitia kwa Pasaka.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi Utakatifu wa Mungu? (Haki, anachukia dhambi, lazima kuhukumu na kuadhibu dhambi kwa kifo.)**
  - Mungu alichukia kuabudu sanamu kwa Wamisri. Aliadhibu ugumu wa moyo wa Farao.
  - Dhambi ilileta kifo katika Misri hata pia mapigo hayo mengine.
  - Njia ya pekee ya wokovu ilikuwa kupitia kwa dhabihu ambayo itachukua mahali pa dhambi. Damu ya mwanakondoo.
  - Mwanakondoo alipaswa kuwa kamilifu bila waa. (Je, hii inakukumbusha kuhusu hadithi myingine hapo awali?
  - Ni nini kilipaswa kufanyika kwa mwanakondoo? Alipaswa kufa. Damu yake ilipaswa kumwagika. Inaonyesha kwamba dhambi huleta kifo katika ulimwengu.
  - Walipaswa kufanya kila kitu kikamilifu walivyoagizwa. Wasivunye mifupa yake.
  - Njia ya pekee kwa wokovu ni njia ya Mungu.
  - Hata Waisraeli, kwa sababu walikuwa wenye dhambi, wangekufa ikiwa wangebaki nje, na siyo nyuma ya damu ya mwanakondoo.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi Neema ya Mungu? (Huruma, Anawasiliana na mwanadamu, Ukarimu, Wema)**
  - Aliwaokoa Waisraeli hata ijapokuwa walikuwa wenye dhambi.
  - Aliwaokoa waliomwamini kwa kukaa nyuma ya damu ya mwanakondoo.
  - Aliwasiliana na Waisraeli kupitia kwa Musa.
  - Aliwapa Wamisri nafasi nyingi kubadilika.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi Uaminifu wa Mungu (Habadiliki)**
    - Mungu anatimiza ahadi yake ya kuleta mwokozi kwa ulimwengu kupitia kwa Waisraeli.
    - Anatimiza ahadi yake kwa Abrahamu ya kuwaondoa wazao wake kutoka utumwani baada ya miaka mia nne, na kuwatoa utumwani wakiwa na mali nyingi mno.
    - Anatimiza ahadi yake kwa Musa ya kumtumia kukomboa watu wake.
    - Anatimiza ahadi yake ya kuwaokoa watu wliojificha nyuma ya damu.
    - Anatimiza ahadi yake ya kuadhibu wasiokuwa nyuma ya damu.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- Mwanadamu ni mwenye dhambi. Msumbufu. Moyo mgumu wa Farao. Ibada ya Wamisri ya miungu mingine.
- Mwanadamu hawezi kujiokoa. Waisraeli hawangeweza kuwaokoa wana wao wa kwanza kutoka kwa malaika wa kifo.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- Ni lazima mwanadamu amjie Mungu katika njia ya Mungu tu. Kamilifu. Hawezi kufanya njia yake mwenyewe. Ni Mungu tu anaweza kufanya njia, na anaweza kuitoa dhabihu inayofaa.
- Ni nini kingefanyika ikiwa jamaa wa Waisraeli hawangeweka damu kwenye mlango? Au hawangebaki katika nyumba?
- Lazima mwanadamu awe na imani ili kumpendeza Mungu.
- Tunaonaje imani ya Waisraeli?
    - Imani inaonyeshwa katika utiifu.
- Je hadithi hii inaonyeshaje binadamu lazima awe na imani ili aweze kumpendeza Mungu?
- Iliwabidi wamwamini Mungu na wabaki kwenye nyumba.
- Je, ni pahali gani pengine kwenye hadithi zilizopita ambapo temeona kwamba damu ya mnyama iliokoa maisha ya mtu? Tunamwitaje mnyama huyo?
    - Katika hadithi ya Adamu na Hawa Mungu alipowafanyia mavazi kutoka kwa ngozi za wanyama, na katika agano pamoja na Nuhu inatufunza kwamba uzima umo katika damu na kubadishwa kwa mwanadondoo kuchukua pahali pa Isaka juu yam lima Moria.
    - Tunamwita mnyama huyo dhabihu iliyochukua nafasi hiyo." Mnyama anamwaga damu au kupoteza maisha yake kwa niaba ya mtu aliyehusika.
- Je ni kwa jinsi ipi mwanakondoo ni MFANO au PICHA wa Kristo? Katika njia nyingine, ni vipi inaelekeza kwa Kristo?
    - Mwanakondoo wa Mungu anayezichukua dhambi za ulmwengu. Yeye tu ndiye anayefaa kuchukua nafasi kwa niaba ya mwanadamu mwenye dhambi.
    - Kama damu ya kondoo ilileta kifuniko kwa dhambi za Waisraeli, hivi ndivyo damu ya Yesu inaleta kifuniko kwa dhambi zetu. Mungu alipotuona, badala ya kuona dhambi zetu, yeye huona haki ya Yesu. Kwa hivyo sisi tunaamini haki ya Yesu, naye Mungu akaihesabu imani yetu kama haki.
    - 2 Wakorintho 5:21 – Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye!
- Kwa mfano: Kubadilisha vifuniko vya vitabu viwili. Kitabu moja kina matendo yote yangu. Kingine kina matendo yote ya Yesu. Lakini nikiweka imani yangu kwa Yesu, ni kama Yesu angechukua matendo yangu na angenipatia matendo yake, yaani haki yake.
- Mara nyingi sisi hujaribu kujenga haki yetu kupitia matendo mazuri yetu, yaani kujiamini badala ya kumwamini Yesu pekee. Kama tunahisi kama hatuna muhimu, tunaweza kujaribu kupata sifa mzuri mbele ya watu badala ya kuamini sifa ya Kristo ambayo tuko nayo kwa sababu sisi ni watoto wa Mungu. Kama tunamwamini Yesu, Mungu hazioni dhambi zetu. Anaiona damu ya Yesu, au haki yake.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Damu ya mwana kondoo iliyopakwa kwa miimo ya mlango ilifunika dhambi za Waisraeli, ili waokolewe kutoka kwa malaika wa kifo. **Mara nyingi hata sisi Wakristo hujitengenezea haki yetu wenyewe kujaribu kuficha dhambi zetu nyuma ya matendo mema**. Je ni njia gani sisi hutumia kujaribu kujificha? Je hii hadithi inatufunza nini kuhusu kuishi maisha yetu ya kila siku?
    - Sisi hujaribu kuficha dhambi zetu na makosa yetu kwa kutii mafunzo ya kanisa, kujitolea, au kuona tuko bora kuliko watu wengine.
    - Kwanza tunastahili kukubali wokovu ambao Mungu anapeana kwa **kujificha nyuma ya damu ya mwana-kondoo mkamilifu**. Yesu ndiye mwana kondoo wetu mkamilifu.
    - Wakati wote tunapotenda dhambi maishani mwetu tunafaa kumkimbilia yeye kwa toba tukiamini kwamba damu yake bado inatufunika na kutufanya wenye haki mbele za Mungu.

- **Tafakari kuhusu Meza ya Bwana.** Inaangazia kile Kristo alikutendea jinsi tu pasaka ilivyowakumbusha Waisrael vile Mungu alivyowakomboa kutoka Misri. Je, Meza ya Bwana inawezaje kuimarisha imani yako? Inawezaje kukumbusha kuhusu Yesu Kristo? Je, kuna njia tunaweza fanya ili Meza ya Bwana iwe na maana zaidi katika makanisa yetu?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Je, wewe binafsi wakati mwingine hujaribuje kuunda haki yako mwenyewe ili kujifanya ujisikie vizuri?** Chukua muda sasa kuungama dhambi hii kwa Mungu na kaka au dada mwingine katika Kristo na ufanye upya imani yako katika Kristo pekee.

- Waisraeli, ingawa walikuwa wenye dhambi waliokolewa kutoka kwa malaika wa kifo **kwa kujificha kwa damu ya mwana kondoo**. Yesu ni mwana kondoo wetu mkamilifu. Je, unaficha maisha yako ya dhambi katika damu ya Mwanakondoo wa Mungu? Je uko tayari kutubu dhambi zako na kumwamini Yesu pekee kama mwokozi wako?. Je, unajua mtu gani ambaye anahitaji kusikia huu ujumbe wa Habari njema? Taja mtu huyo na mumuombee kama kikundi.

## 17. KUVUKA BAHARI YA SHAMU
## Kutoka 13:17-14:31

*Kutembea Jangwani / Kunaswa!*

Baada ya Mungu kuwakomboa wana wa Israeli kutoka Misri, badala ya kwenda njia iliyo karibu sana na Kanaani, aliwaongoza kupitia jangwani mpaka Bahari ya Shamu. Wakati wa mchana, Mungu aliwaongoza kwa nguzo ya wingu na usiku katika nguzo ya moto ili kuwapa mwanga wa kuona.

Lakini Farao aliposikia kwamba waliondoka, alibadilisha mawazo yake tena. "Tumefanya nini? Tumewaachilia watumwa wetu!" Kwa hivyo Farao alilichukua jeshi lake na magari ya farasi wake na wakawafuata Waisraeli. Wakawafikia katika Bahari ya Shamu. Waisraeli walitegwa baina ya jeshi na bahari. Hawakuweza kutoroka.

Watu walipowaona Wamisri, waliwaogopa sana. Wakamwuliza Musa, "Musa, kwa nini umetuleta hapa jangwani kufa? Je! hili silo tulilokuambia huko Misri: 'Utuache ili tuwatumikie Wamisri'? Kwa maana ingekuwa heri kwetu kuwatumikia Wamisri kuliko kufa jangwani."

*Msimame Imara! / Gawanya Bahari na Kuvuka!*

Musa akawajibu watu, "Msiogope. Simameni imara! Nanyi mtaona ukombozi ambao BWANA atawaletea leo. Wamisri mnaowaona leo, hamtawaona tena. BWANA atawapigania ninyi; mnahitaji tu kutulia." BWANA akanena na Musa, na kumwambia, "Mbona unanililia? Waambie watu wasonge mbele! Inua fimbo yako juu ya bahari, ili kuyagawanya maji, ili watu wavuke kwenye nchi kavu. Nami nitaifanya mioyo ya Wamisri kuwa migumu, nao watakufuata, nami nitajipatia utukufu kwao; nao Wamisri watajua ya kuwa mimi ndimi BWANA." Wakati huo Bwana akasogea nyuma yao katika nguzo ya wingu ili kuwalinda na jeshi la Wamisri. Usiku kucha lile wingu lilileta giza kwa Wamisri na mwanga kwa Waisraeli. Kwa hivyo Musa alinyoosha fimbo yake na Mungu akafanya bahari irudi nyuma kwa nguvu za upepo mkali. Maji yaligawanyika na Waisraeli wakavuka kupitia ndani ya bahari kama kupitia juu ya nchi kavu, kukiwa na ukuta wa maji kulia na kushoto. Farasi na magari yote ya Farao yaliwafuata ndani ya bahari.

*Ukombozi*

Usiku ulipokaribia kwisha, Mungu aliangalia jeshi la Misri na akalifanya kuchanganyikiwa. Akafanya magari yao yapoteze magurudumu yao, na kuwa vigumu kuyaendesha. Wamisri wakasema, "Tuwaache Waisraeli peke yao. Bwana anawapigania dhidi yetu."

Basi Mungu akamwambia Musa, "Nyoosha mkono wako juu ya bahari, ili maji yarudi juu ya Wamisri." Kisha bahari ikarudi pamoja na kuwaangamiza Wamisri wote. Hakuna hata mmoja ambaye alitoroka.

Siku hiyo, Mungu aliwaokoa Waisraeli dhidi ya Wamisri. Kesho yake alfajiri wakawaona Wamisri wakiwa wamekufa ufukoni mwa bahari. Walipoona uwezo mkuu

wa Mungu, walimcha Mungu, na wakamtumaini. Na pia, wakamtumaini mtumishi wake Musa.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **When have you been trapped needing a way of escape? How did you escape?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu aliumba na kuelekeza nguzo ya wingu na mto.
    - Mungu alitawala upepo na mawimbi na kugawanya bahari.
    - Mungu alitawala umbaji wake wa asili wote.
    - Akawalinda dhidi ya Wamisri.
    - Akawafanya Wamisri kuwafuata Waisraeli ndani ya bahari ili kwa kuwaangamiza angepata utukufu kwake mwenyewe na Wamisri wangejua kwamba "Mimi ndiye Bwana."
    - Aliwachanganyisha Wamisri.
    - Akafanya magari yao ya farasi kuharibika magurudumu.
    - Wamisri wakasema, "Bwana anawapigania." Waliona kwamba yeye ndiye Bwana.
    - Mungu aliwafanya Waisraeli kumwogopa, kumweshimu na kumtumaini na kumtumaini mtumishi wake Musa.
    - Mungu alikusudia kuongoza Waisraeli katika pahali ambapo hawangejiokoa.
    - Mungu aliwaokoa watu wake wateule hata ingawa walikuwa wenye dhambi.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Mungu alijua kile kingewatokea Wamisri na kujua wangewafuata Waisraeli.
    - Alijua Wamisri wangeangamizwa na wangejua kwamba yeye ndiye Bwana.
    - Alijua kwamba atawaokoa Waisraeli.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Nguzo ya wingu ilitenganisha Waisraeli na Wamisri wasioamini Mungu.
    - Aliadhibu Wamisri kwa kuabudu sanamu na dhambi zao dhidi ya Waisraeli.
    - Aliwakemea kwa mashaka na kuwahimiza wasonge mbele.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Aliwaokoa Waisraeli katika hali wasingaliweza kujisiadia.
    - Waisraeli walikuwa wenye dhambi hata walikuwa na shaka na Mungu. Hata hivyo, Mungu akawaokoa.
    - Alitimiza ahadi yake kuleta Mwokozi kupitia Waisraeli kwa ulimwengu wote. (Mwanza 3, ahadi kwa Abrahamu, n.k.)

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni Mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.)**
    - Mungu alikuwa amemwambia Abrahamu kwamba atambariki, atampa nchi ya Kanani, atamfanya taifa kuu, kuwalaani wote ambao watamlaani. Mataifa yote yatabarikiwa kupitia kwake. Kwahivyo Mungu alikuwa anatimiza haya yote.
    - Mungu alikuwa amemwambia Abrahamu kwamba wazao wake watakuwa watumwa katika nchi ya kigeni kwa miaka mia nne. Kisha wataletwa Kanani. Mungu alifanya jambo hili.
    - Mungu alisema Wamisri wangewafuata Waisraeli katika bahari. Wakafanya hivyo.
    - Wamisri walisema, "Bwana anawapigania." Waliona kwamba yeye ndiye Bwana.
    - Alitimiza ahadi yake kuleta Mwokozi wa dunia yote kupitia Waisraeli.

<u>**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**</u>

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Moyo mgumu wa Farao.
    - Wamisri walijaa chuki.
    - Wamisri waliabudu sanamu.
    - Waisraeli walikuwa wananung'unika wakiwa na mashaka hata ingawa walikuwa wameona maajabu ya Mungu katika kuwaokoa.
    - Walikuwa wamepiga kelele, "Utuache ili tuwatumikie Wamisri!" Haya ni maombi ya waasi kwa Mungu. "Tuache peke yetu ili tuendeshe maisha yetu wenyewe!"

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Walinaswa! Bahari mbele, milima kando, Wamisri nyuma. Kama sisi tumenaswa katika dhambi.
    - Walikuwa na hali ya kutojiweza.

- **Je, hadithi hii inaonyeshaje kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu?**
    - Mungu alionyesha uangalifu wa pekee kwa watu wake. Alikuwa na kusudi kwao.

<u>**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**</u>

- **Je, hadithi hii inaonyeshaje kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Wokovu unaweza kupeanwa na Mungu tu.
    - "Tulia na kuona wokovu wa Mungu."
    - Je, inamaanisha nini kusema "tulia" katika hadithi hii?
    - Ni kuwa na tumaini, kutojaribu mwenyewe na kutolia na kutonung'unika. Tulia ndani ya moyo na mwili na akili.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa. Yaani, inafundisha nini kuhusu imani inaweza kuonekana katika maisha yetu?**
    - "Ruhusuni Mungu kuwapigania!"
    - "Tulia na kuona wokovu wa Mungu." Mungu aliwaita wawe na imani.
    - Mwishowe, walimtumaini na kumwogopa Mungu.
    - Je, kumwogopa inamaanisha nini?
    - **Je, nyinyi wawili mnawezaje "kutulia" NA "kusonga" kwa wakati mmoja? Je, hilo linatuambia nini kuhusu imani?**
    - Walimtumaini mtumishi wa Mungu, wakiamini mpango wa Mungu na njia yake kupata Wokovu kupitia Musa.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- **Je, watu siku hizi hutaka vipi kutenda kama Waisraeli katika hadithi hii?** Ni changamoto gani zinazofanya iwe rahisi kwa watu kusahau baraka za Mungu na kuanza kulalamika na kutilia shaka utunzaji wake?

- **Inaweza kumaanisha nini kwa mtu ambaye ana wasiwasi "kutulia" na "kusimama imara," akimngoja Mungu?** Je, wanawezaje kuwa na tabia ya kutulia wakiendelea kusonga mbele ?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):**

- **Je, una changamoto gani (au wingu jeusi) katika maisha yako ambapo unajitahidi kupata jibu au kulia na kulalamika juu yake?** Je, hii inaweza kuwa fursa ya kumwamini Mungu? Je, ingekuwaje kwako "kutulia" na "kusimama imara", ukingoja kuona ni ukombozi gani ambao Mungu anao kwako?

## 18. MLIMA wa SINAI, SHERIA KUMI
## Kutoka 19, 20, 24, 33, 34

*Ahadi za Mungu kwa Watu Wake wa Agano*

Miezi miwili baada ya Waisraeli kutoka Misri, walitua mbele ya Mlima wa Sinai. Musa alipanda mlimani kukutana na Mungu. Mungu akasema, "Waambie watoto wa Israeli, 'Mmeona jinsi niliwaokoa kutoka Misri. Mkinitii kikamilifu na kutimiza ahadi yangu, ndipo kutoka kwa mataifa yote, mtakuwa urithi wangu wa thamani. Mtakuwa ufalme wa makuhani na taifa takatifu"

Musa alipowaambia watu, wakasema, Tutafanya kila kitu Bwana alichosema."

*Utakaso na Nguvu*

Ndipo Mungu akasema, "Musa, nitakujia katika wingu ili watu wote wataniskia nikiongea nawe na watakuamini. Waambie watu kujitakasa kwa siku mbili nami nitakuja siku ya tatu. Usiruhusu mtu yeyote au mnyama kuuguza mlima. Wakifanya hivyo watakufa kwa maana hapa ni pahali patakatifu." Watu walimtii Mungu na siku ya tatu wingu zito likafunika mlima. Kulikuwa na radi na umeme na kelele kuu kama sauti ya tarumbeta. Moshi ulichemka kutoka kwa mlima kama unaotoka katika tanuru na mlima wote ukatetemeka. Waisraeli wote walitetemeka kwa hofu kuu.

*Amri Kumi*

Baadaye Musa akapanda juu mlimani na Mungu akampa amri kumi:

1) Amri ya kwanza, Mimi ni Bwana Mungu wako niliyekutoa Misri katika nchi ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi.
2) Amri ya pili, Usijifanyie sanamu yeyote. Usiziinamie au kuziabudu. Mimi ndimi Mungu wa wivu, na nitakuadhibu na watoto wako ukifanya hivyo.
3) Amri ya tatu, Usitumie jina langu bure.
4) Amri ya nne, Ikumbukeni Sabato na kuitakasa kwa kupumzika siku hiyo.
5) Amri ya tano, Waheshimu baba na mama yako.
6) Amri ya sita, Usiue.
7) Amri ya saba, Usizini.
8) Amri ya nane, Usiibe.
9) Amri ya tisa, Usiseme uongo.
10) na Amri ya kumi, Usitamani mali ya jirani wako, sio mke wake, watumishi wake, mifugo yake, na kitu kingine chochote chake.

Pia Mungu, aliwapa sheria nyingine nyingi ambazo zilitungwa hasa ili kuwasaidia Waisraeli wafanye kazi kama taifa chini ya Mungu.

*Majibu ya Wananchi*

Baada ya hayo yote, watu walikuwa wakitetemeka kwa hofu. Musa akawaambia, "Msiogope. Mungu amekuja kuwajaribu, ili hofu yake iwe pamoja nanyi ili kuwaepusha na dhambi anapowaongoza katika nchi ya ahadi. Mtakapofika huko, msifanye agano na

Wakanaani au miungu yao, wala kuishi pamoja nao, kwa sababu watawafanya mtende dhambi dhidi yangu."

Asubuhi iliyofuata Musa alijenga madhabahu chini ya mlima na kutoa dhabihu kwa Mungu ili damu ikamwagike. Kisha Musa na msaidizi wake, Yoshua, wakapanda tena mlimani na Mungu akampa Musa nakala zingine mbili za agano kati yake na Israeli, zilizoandikwa katika mawe. Wingu liliufunika mlima na kila watu walipotazama juu, waliona utukufu wa Mungu uking'aa kama moto juu yao.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Ni nini kusudi ya sheria kwa ujumla?**
- **Ni nini kusudi au thamani ya sheria ya Mungu?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
  - Mungu alikuja ndani ya wingu juu yao.
  - Mlima ulitetemeka ulitoa moshi, umeme, radi, sauti kuu. Zilionyesha nguvu ya Mungu juu ya umbaji wake.
  - Waisraeli walitetemeka katika hofu.
  - Mungu aliwazuia watu kuguza mlima.
  - Watu alimtii Mungu kwa sababu ya hofu kuu.
  - Mungu alipeana sheria. Akawa Mwumbaji wao na aliwamiliki. Alikuwa Bwano wa agano.
  - Mungu hakuwa akiwaomba utii. Bali alidai kwa sababu yeye alitawala kabisa.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
  - Mungu alikumbuka ahadi zake kwao na matendo yake kwa niaba yao.
  - Mungu ana hekima kuhusu jinsi ya watu kuhusiana na Mungu na watu wengine katika amri kumi.
  - Mungu anajua moyo wa mwanadamu na pahali gani ambapo anafanya dhambi sana.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
  - Kutakaswa kwa watu. Walipaswa kujitakasa kusimama mbele ya Mungu.
  - Mungu alisema, "Msiguse mlima. Mkifanya hivyo mtakufa." Watu wametengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi yao. Waliweza kumgusa Mungu mwenyewe bila usaidizi. Naye Mungu hataki kugusa mwenye dhambi.
  - Uwepo wa Mungu. Mungu alikuwa na watu kwa njia maalum.
  - Mlima ulifunikwa kwa uwingu zito ishara ya uwepo wa Mungu katika njia maalum. Hangejionyesha wazi wazi. Alijiificha katika wingu.
  - Uwepo wa kuogofya wa Mungu kupitia kwa radi na umeme na kutetemeka kwa ardhi.
  - Jibu la watu. Waliogopa sana hata kusikia sauti ya Bwana. Waliogopa kifo. Walihisi walitaka mpatanishi.

- Kupeana kwa sheria kunaonyesha kwamba kuna uzuri na kuna ubaya. Kwamba kuna dhambi na kuna haki.
- Sheria ilipeanwa kusaidia Waisraeli kutotenda dhambi na kufuata mfano mtakatifu na mapenzi ya Bwana.
- Amri ya Mungu ya kutochanganyika na Wakanani, kuwa na agano nao au kuishi na wao au kugeukia miungu yao. Kuna hitaji la kujitenga kutoka wenye dhambi, kuwa taifa takatifu na kutopotoshwa na wasio amini.
- Mungu aliwapa sheria zilizokuwa takatifu, akijua kwamba hawangezitimiza kikamilifu.
- Dhabihu yoyote katika agano la kale ilituambia kanuni fulani, yaani 1) Mungu ni mtakatifu, 2) Sisi ni wenye dhambi, 3) Sisi hatuwezi kujiokoa, 4) Lasima tuwe na mpatanishi au dhabihu ya damu kwa niaba yetu ili tuokolewe. (Bila kumwaga damu, hakuna msamaha wa dhambi.)
- Punde baada ya kupeana sheria, tunaona dhabihu kwa sababu hawakuweza kutii sheria hizo vizuri. Walihitaji dhabihu kwa niaba yao.
- Mungu alikusudia Israeli kuwa taifa takatifu.
- Wingu lilifunika mlima na wakaona utukufu wa Mungu uking'ara juu yao.
- Katika amri ya kwanza, yaani "Usiwe na miungu mingine," Mungu hawezi kushiriki utukufu wake au kuabudiwa kwake.
- Amri ya pili, Mungu ni mwenye wivu, aliyejitenga, mtakatifu. Hawezi kuchanganywa na vitu vingine.
- Msiweke kitu chochote mbele ya Mungu. Anastahili kuabudiwa peke yake.
- Jina lake ni takatifu, lisitumike katika njia isiyo na heshima.
- Amri ya kuikumbuka Sabato na kuitakasa, kupumzika, na kuacha kujaribu kufanya vitu wenyewe.
- Sabato inamaanisha kupumzika kutoka kujaribu kurekebisha shida zako mwenyewe bila Mungu na kutukumbusha kwamba tunamtegemea Mungu na kuwakumbusha Waisraeli kuweka tumaini lao katika Mwokozi atakayekuja.
- Anatutaka tuhusiane na wengine katika njia takatifu katika amri ya tano hadi kumi,
- Heshima.
- Thamani ya uhai wa watu.
- Usafi wa uhusiano kati kati ya wanaume na wanawake.
- Ukweli
- Kutosheka.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
  - Mungu aliwaonya watu kutougusa mlima wasije wakafa. Hii ni neema yake.
  - Mungu alikuja kuongea na Musa. Ni neema kwa Mungu kuongea nasi.
  - Dhabihu inatuonyesha kwamba Mungu alipeana njia ya kuwendea kupitia dhabihu ya damu.
  - Israeli watakuwa miliki ya thamani, na ufalme wa makuhani, ambao wangewasaidia watu wengine kuhusiana na Mungu.
  - Mungu alijua kwamba Waisraeli hawangetii sheria, bali aliwapa ili iwasaidie kuona dhambi zao na hitaji lao kwa Mwokozi kwa maana hawangejiokoa kupitia kutimiza sheria.
  - Sheria ni neema kwa sababu inatuonyesha dhambi zetu ili tutageukia Mwokozi.
  - Sheria ni mwalimu anatuelekeza kwa Kristo. (Warumi 3:19)
  - Hata kama wenye dhambi, Mungu aliwapatia ahadi ya kuwarudisha Kanani.
  - Anatuonyesha jinsi ya kufuata Mungu na jinsi ya kutii.
  - Tukifuata sheria yake nzuri, basi tutabarikiwa. Baraka inapatikana katika utii wa sheria unaoletwa na imani.
  - Mungu alijionyesha mwenyewe lakini si katika njia ya kuangamiza.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
  - Aliwakumbusha, "Mimi ndimi Bwana aliyewaokoa kutoka Misri."
  - Aliwapatia ahadi ya kuwa miliki ya thamani.
  - Mkitii, nitawabariki.
  - Msipotii nitawalaani.

    - Aliwaahidi kuwarudisha Kanani kama alivyomwahidi Abrahamu.

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- **Je, hadithi hii vipi, inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu.**
    - Katika yote Mungu anatenda kwa neema.
- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Wanadamu wanapaswa kujitakasa ili kusimama mbele ya Mungu.
    - Wanadamu walihitaji maelezo ya sheria kuhusiana na Mungu na wao wenyewe.
    - Wanadamu hawangegusa mlima kwa maana ya dhambi zao, hata baada ya kujitakasa kwa siku tatu.
    - Kuwa na dhabihu ya damu, na kunyunyuzia kwa damu na kuwa na mpatanishi kunaonyesha utakatifu wa Mungu.
    - Sheria haiwezi kuondoa dhambi katika mioyo yetu.
- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Walijihisi kwamba hawawezi kujisaidia. Wakamlilia Musa kuongea na Mungu kwa niaba yao.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- Hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)
- Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.
    - Mwanadamu anaweza tu kumjia Mungu kwa njia ya dhabihu.
    - Lazima mwanadamu kukubali dhambi zake na kutoweza kwake kujiokoa.
    - Lazima kutumaini katika Mwokozi ambaye angekuja aliye wakilishwa kwa ishara ya dhabihu ya mnyama.
    - Lazima mwanadamu kuonyesha imani yake kupitia katika utii wa sheria.
    -

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Je, siku hizi watu huvunja vipi sheria za Mungu? Na Wakristo je? Tunatendaje usherati na kuua katika mioyo yetu? Tunashuhudiaje uwongo kwa maneno yetu au kimya chetu? Ni vipi tunakosa kutii wazazi wetu? Sisi hutamani vitu gani?
- Ni katika hali gani tunaweza kuona undani wa utakatifu wa Mungu ambao ni wa ajabu na wa kuogofya? Je, inafaa kutufanya kuhisi vipi kuhusu dhambi zetu? Je tunapaswa tuitike vipi kwa Mungu katika hali kama hiyo?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Fikiri kuhusu hali uliyopitia ambapo uliona utakakatifu wa Mungu wa ajabu na wa kuogofya?** Je uko na hatia gani ya kutengeneza sanamu katika kwa kitu chochote au mtu katika maisha yako? Hii hadithi imekufunza nini kuhusu jinsi Mungu anavyo tazama hii ibad ya sanamu maishani mwako?
- **Je, umevunja vipi amri kumi hivi majuzi?** (Ndio umefanya!) Je, **umeuaje moyoni mwako?** Kwa mfano: 1) Je, unaweza kufikiria uhusiano maalum sasa ambapo unang'ang'ana na kumchukia mtu? Utambuzi huu unapaswa kukufundisha nini? Unapaswa kuitikia vipi? 2) **Umezini vipi moyoni mwako?** 3) Ni njia gani zingine umezivunja amri ambazo hukuwahi kuzifikiria hapo awali kwa sababu dhambi zilikuwa sanasana moyoni mwako? (Kusema Uongo? Kutamani? Kutoheshimu wazazi wako?) Je, kutambua jinsi dhambi zako zilivyo ndani kunaweza kukusaidia kusonga karibu na Mungu?

## 19. NDAMA wa DHAHABU
## Kutoka 32

Musa alipoenda juu mlimani kuongea na Mungu, Mungu alifanya mbao mbili za mawe na kwa kidole chake akaandika Amri Kumi kwenye mbao hizo. Musa akakaa mlimani kwa siku arobaini.

Watu walipoona kwamba Musa alikawia kushuka mlimani, walikusanyana wakamwendea Haruni wakamwambia, "Haya! Katufanyizie miungu itakayokwenda mbele yetu, kwa maana Musa huyo aliyetutoa katika nchi ya Misri, hatujui yaliyompata. Watu wote wakazivunja pete za dhahabu zilizo katika masikio yao, wakamletea Haruni. Akazichukua na akafanyiza sanamu katika mfano wa ndama. Kisha wakasema, "Hiyo ndiyo miungu yako Waisraeli, iliyowatoa katika nchi ya Misri." Kisha wakaanza kuimba na kucheza na kuiabudu sanamu ya ndama wa dhahabu.

Kileleni mwa mlima, Mungu alikuwa amemaliza kuandika Amri Kumi na akamwambia Musa, "Watu wameshaniasi. Niache ili niwaangamize!" Lakini Musa alimwomba Mungu kukumbuka agano lake na Abrahamu, Isaka, na Yakobo na kutowaangamiza watu wake.

Basi Musa akashuka mlimani. Alipoona watu wakiimba, kucheza, na kuuabudu sanamu ya ndama wa dhahabu, alighadhabika. Akatupa zile mbao za mawe za amri chini nazo zikavunjika vipande vipande. Kisha Musa akatoa sauti kuu akasema, "Kama yeyote anamwabudu Mungu wa kweli, aje kwangu!" Kabila la Lawi tu, ndiyo walimjia. Musa akawaambia, "Kila mtu atwae upanga wake na kuwaua wale wote ambao wanaabudu ndama wa dhahabu." Watu wengi wakafa na Waisraeli wengine, wakatubu dhambi zao.

Kwa sababu Musa alikuwa ameshavunja zile mbao za mawe za Amri Kumi, alirudi mlimani kwa Mungu. Naye Mungu akatengeneza nyingine. Hizo zilikuwa mbao ambazo Musa aliziweka kwenye sanduku la agano.

Baada ya siku nyingi kwenye Mlima wa Sinai, Mungu aliwaongoza kuelekea katika nchi ya ahadi.

### MPANGILIO wa SOMO

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kukumbuka wakati fulani katika maisha yako ulipokuwa ukingojea jambo jema lakini ukakosa subira na ukafanya uamuzi mbaya?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
  - Mungu ana mamlaka kuwapatia Musa na watu maagizo.
  - Mungu aliweza kuandika kwa mawe.
  - Mungu alikuwa na uwezo kumtunza Musa mlimani kwa siku arobaini.
  - Alikuwa na mamlaka kuadhibu dhambi.

- **Je, ni vipi hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
  - Mungu alikuwako na Musa, lakini, kwa wakati huo, alikuwa na watu chini ya mlima na akajua kwamba waliasi dhidi yake.
  - Alijua kwamba walihitaji sheria za kuwaongoza na kuwaonyesha dhambi zao.
  - Pia alijua kwamba Musa alivunja mbao za mawe.

- **Je, ni vipi hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
  - Punde, Mungu aliwahukumu watu kwa kugeuka dhidi yake.
  - Mungu alikasirishwa kwa dhambi za watu.
  - Watu walikufa. Hata Mungu aliwaagizo waaminifu wake kuwauwa wengine wasiyo waminifu yaani walioabudu sanamu.
  - Badhi ya watu walitubu.
  - Mungu aliwapatia sheria. Kuna mambo ambayo ni sawa na mambo yasiyo sawa. Mungu tu ndiye anayeamua.
  - Mungu aliwatuza waliosimama kwa utakatifu wake, yaani waliojitenga na uasi. Mungu alikuwa pamoja nao.

- **Je, ni vipi hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
  - Mungu hakuwagusa Walawi na Musa, hata ingawa walikuwa wenye dhambi pia.
  - Mungu alikumbuka agano lake na Abrahamu na Isaka na Yakobo kutoangamiza watu wake. Kwa hivyo hakuwaamgamiza.
  - Alikuwa na huruma na watu wote waliotubu.
  - Alionyesha Haruni huruma.
  - Aliongea na Musa.
  - Aliwapatia nakala nyingine ya amri kumi.

- **Je, ni vipi hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
  - Mungu alikumbuka agano lake na Abrahamu, Isaka, na Yakobo kuwafanya kuwa taifa kuu, kwa hivyo hakuwangamiza kabisa.
  - Alikuwa mwaminifu kwa watu wakati wote ambao wangeweka imani yao katika Mwokozi aliahidi kubariki ulimwengu wote kupitia kwa Israeli.

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- **Je, ni vipi hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Watu walisahau haraka sana yale yote Mungu alikuwa amewafanyia wakasahau amri zake ambazo alikuwa amewapa. Walisahau utakatifu wake.
    - Walitaka Mungu yeyote. Walikubali kitu chochote kisicho na thamani kama Mungu.
    - Walikosa kutii na kueshimu Mungu kwa kusema "Huyu ndiye Mungu wetu aliyetutoa Misri."
    - Wakavunja amri ya kwanza.
    - Wakavunja amri ya pili kuhusu sanamu.
    - Wakavunja amri ya tatu. Walitumia jina la Bwana vibaya kwa kuita ndama Mungu.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- **Hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Walijaribu kumjia Mungu kwa kutumia sanamu badala ya kungojea mtumishi wa Mungu au mpango wa Mungu.
    - Wakajaribu kuunda miungu yao wenyewe, haikufaulu.
    - Walawi wakatenda kulingana na imani na Mungu aliwaheshimu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.**
    - Walawi walitenda katika imani.
    - Watu wengine walitubu na Mungu akawasamehe.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- **Je, kuna hali gani katika maisha yako ambapo ni vigumu sana kumngoja Mungu kwa subira?** Je, unajaribiwa vipi kugeukia njia nyingine au kuchukua njia za mkato?

- Waisraeli walitaka kitu ambacho wangeweza kuona kwa macho ili kuabudu. Kwetu sanamu ni kitu chochote maishani mwetu isipokuwa Mungu ambacho tunategemea. Kama kuna fursa au cheo au uhusiano maishani mwetu ambao unatishiwa ama kupoteza na kupoteza huko kunakukasirisha sana hadi unapoteza tumaini inawezeka umefanyika sanamu kwako.
    - Kwa kuzingatia hili, **ni baadhi ya mambo gani ambayo mara nyingi tunageuza kuwa sanamu?**

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je, kuna hali gani katika maisha yako ambapo ni vigumu sana kumngoja Mungu kwa subira?** Je, unajaribiwa vipi kugeukia njia nyingine au kuchukua njia za mkato? Hii hadithi itakusaidia vipi kumtumaini zaidi Bwana na kungoja jibu lake kwa subira?

- **Je, nini ambacho wakati mwingine unajaribiwa kukitumaini badala ya Mungu?** Je ni kitu gani maishani mwako wakati mwingine wewe hukigeuza kuwa sanamu? Unaweza kutubu vipi kuhusu hiyo sanamu?

## 20. MASKANI / SIKU ya UPATANISHO
## Kutoka 25-29, 34-40; Mambo Ya Walawi 1-10, 16, 17

*Maelezo ya Maskani*

Baada ya wana Waisraeli kutubu kwa kumwabudu ndama wa dhahabu, ilikuwa wakati wa kujenga maskani, yaani pahali pa Mungu kuishi nao. Watu walizileta sadaka za vitu vyote vya thamani ambavyo mafundi hodari wangeweza kutumia kwa kujenga. Ilichukua mwaka mzima kumaliza kujenga maskani kama vile Mungu alivyomwambia Musa.

Maskani ilipokwisha kujengwa, ilikuwa kama hema kubwa iliyogawanywa kwa pazia nzito. Katika chumba cha mbele ya pazia, yaani pahali patakatifu, mlikuwa na vitu vitatu:

- Kwanza, mlikuwa na kinara cha dhahabu safi chenye taa saba,
- Pili mlikuwa na meza ya dhahabu yenye mikate kumi na miwili isiyotiwa chachu, mmoja kwa kila kabila la Israeli,
- Tatu mlikuwa na madhabahu ndogo ya dhahabu kuchomea uvumba mbele ya Mungu mchana na usiku.

Katika chumba nyuma ya pazia, yaani pahali patakatifu zaidi, mlikuwa na sanduku la mbao ambalo Mungu alimwambia Musa atengeneze. Sanduku hilo lilifunikwa kwa dhababu. Ndani yake mlikuwa na nakala mbili za mawe za agano, yaani amri kumi. Juu ya sanduku hilo kulikuwa na mifano miwili ya makerubi waliyotazamana. Mabawa yao yalinyooka juu. Naye Mungu alionyesha uwepo wake kwa watu wake katika nuru kuu iliyokuwa juu ya sanduku chini ya mabawa ya makerubi.

Mbele nje ya hema, palikuwa na madhabahu kubwa ya kumtolea Mungu dhabihu. Pia palikuwa na karai ya maji ili makuhani wangeweza kunawa mikono na miguu kabla ya kutoa dhabihu.

Kila kitu kilikuwa maridadi na kitakatifu. Mungu akasema kwamba yeyote isopokuwa makuhani akigusa vitu vitakatifu, atakufa. Kwa hivyo kulikuwa na ukuta wa chandarua uliozunguka hema kwenye milingoti ya mbao.

Kisha Mungu akamwambia Musa amweke wakfu ndugu yake Haruni awe Kuhani Mkuu, na wana wa Haruni wawe makuhani chini yake. Pia wazao wengine wa Lawi walikuwa wasaidizi wa makuhani kufanya kazi mbalimbali kama kubeba vitu vya maskani watu walipokuwa wakisafiri.

*Kutoa Dhabihu*

Kila asubuhi na kila jioni, makuhani walimuua mwana kondoo asiye na waa, kisha wakamchoma juu ya madhabahu. Pia, waliingia chumba cha kwanza cha hema, yaani pahali patakatifu, ili kuchoma uvumba na kuwasha taa mbele ya Mungu.

Mtu alipovunja sheria za Mungu alileta mwana kondoo au mbuzi kama dhabihu ya dhambi. Kuhani alimchinja mnyama huyo na kumwaga damu yake juu ya madhabahu. Hii ndiyo sababu Mungu alisema, "Usile nyama pamoja na damu. Uhai wa mwili u katika hiyo damu, nami nimewapa ninyi hiyo damu juu ya madhabahu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu."

Kulikuwa na aina kadhaa za dhabihu, zilizofaa kumtolea Mungu - ng'ombe, kondoo, mbuzi, au njiwa. Na kila mmoja alipaswa kuwa mkamilifu asiye na dosari na asiwe mgonjwa, mzee, au mlemavu. Dhabihu mbadala hazikukubalika na Mungu na haziondoi dhambi. Njia pekee ya kuondoa dhambi za watu ilikuwa jinsi Mungu alivyowaagiza.

*Siku ya Upatanisho*

Mara moja kila mwaka, katika Siku ya Upatanisho, kulikuwa na dhabihu maalum. Kwanza, Kuhani Mkuu aliwachagua mbuzi wawili, mmoja wa kuchinja na mwingine wa kumfukuza. Baadaye, Kuhani Mkuu alimtoa fahali na aliingia nyuma ya pazia katika Pahali Patakatifu Zaidi, katika uwepo wa Mungu. Kwanza alinyunyizia damu ya fahali juu ya madhabahu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe.

Akarudi nje amchinje mmoja wa mbuzi akaingia tena nyuma ya pazia na kunyunyizia damu ya mbuzi huyo juu ya kifuniko cha sanduku. Hii ilikuwa ya kupatanisha kwa dhambi za watu wa Israeli. Mwishowe, alimleta yule mbuzi aliye hai na kuweka mikono yake juu ya kichwa chake na kuungama dhambi zote za Waisraeli. Alikuwa anaweka dhambi zao juu ya kichwa chake. Baadaye, mtu fulani alimpeleka mbuzi huyo jangwani mbali sana na kambi, ili asiweze kurudi kamwe. Mbuzi huyo alikuwa akizibeba juu yake dhambi za watu.

*Kutotii:*

Licha ya yote, watu bado hawakumtii Mungu, hata wana wawili wa Haruni ambao walikuwa makuhani. Wao walijaribu kuchoma uvumba kwa njia yao wenyewe badala ya njia ya Mungu. Kwa hiyo Mungu akatuma moto kutoka mbinguni na kuwateketeza hapo hapo ndani ya hema. Kwa sababu hawakumheshimu Mungu na utakatifu wake, baba yao Haruni hakuruhusiwa kuwaomboleza.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unafikiri unawezaje kupata uzoefu kamili zaidi wa Mungu kuwa PAMOJA nawe?**

**HADITHI**: Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
    - Mungu alikuwa na mamlaka kuagiza Waisraeli kujenga maskani.
    - Alikuwa na mamlaka kuwapatia maagizo kamili.
    - Mungu alitawala kabisa jinsi ya kujenga maskani na jinsi ya kutoa dhabihu.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Mungu alijua kwamba watu walihitaji kukutana naye.
    - Alijua alikuwa akishughulika na wenye dhambi na alijua ni aina gani ya pahali palipofaa kwa wenye dhambi kukutana naye.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Dhabihu zote zinatuonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi na hawaezi kumwendea bila kutoa dhabihu inayofaa.
    - Mungu alitaka dhabihu takatifu kamili – yaani dhabihu isiyo na waa.
    - Mungu aliwaangamiza wana wa Haruni kwa sababu ya kutoheshimu utakatifu wake kwa kuchoma uvumba.
    - Maskani iligawanywa na pazia nzito.
    - Tunaona utakatifu wa Mungu katika kila kitu ambacho kilitenganisha vitu vitakatifu na visivyovitakatifu. Ua ulizuia Waisraeli kuingia katika maeneo ya vitu vitakatifu. Nyua za maskani zilizuia wote isipokuwa makuhani kuingia. Pazia nzito ndani ya maskani ilizuia yeyote isipokuwa Kuhani Mkuu kuingia Pahali Patakatifu Sana. Naye angeingia pahali hapo mara moja tu kwa mwaka. Watu hawakuweza kumwendea Mungu moja kwa moja. Walihitaji kupitia kuhani, yaani mpatanishi, kwa dhabihu ya damu.
    - Kuhani mkuu alipaswa kuleta dhabihu kwa dhambi zake kwanza, kisha dhabihu kwa dhambi za watu.
    - Katika dhabihu iliyofaa, damu ilipaswa kumwagika. Damu ilikuwa ya thamani kwa sababu uhai ulikuwa katika damu. Kila mara damu iliwakumbusha kwamba uhai ulipaswa kutolewa ili uhai wa binadamu uokolewe. Uhai ulikuwa kwa niaba ya uhai mwingine. Uhai kwa uhai.
    - Kila kitu kilifaa kufanywa katika njia Mungu alivyoagiza bila kushusha viwango.
    - Utakatifu na ukamilifu wa maskani na mtindo wa dhabihu ulionyesha dhambi ya mwanadamu mbele ya Mungu.
    - Dhambi za watu ziliwekwa kwa mnyama aliyetolewa kama dhabihu. Pia ziliwekwa kwa mbuzi ambaye alifukuzwa jangwani.
    - Mbuzi huyo alitenganishwa na watu wa Mungu. Ilikuwa picha ya dhambi zao kutolewa kutoka kwao.

- Ni aina fulani tu ya wanyama ambao walikubalika kama dhabihu yaani wanyama waliokuwa wakamilifu na wenye afya.
    - Makuhani walipaswa kutiwa wakfu kufanya kazi hii takatifu kwa sababu wao pia walikuwa wenye dhambi.
    - Watu wengine wa kabila ya Lawi walitiwa wakfu pia kwa kazi ya maskani.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu alionyesha neema yake kupitia UWEPO wake kwa watu wake.
    - Mungu alikuwa anajenga pahali ambapo angekutana na wenye dhambi katika njia maalum. Mungu alipaswa kuwafukuza Adam na hawa kutoka uwepo wake.
    - Mungu alionyesha uwepo wake katika nuru iliyongaa katikati ya mbawa za malaika.
    - Katika maskani, tunaona ghadhabu ya Mungu au utakatifu wake ukikutana na neema na upendo wake. Mungu alifanya pahali kamili ili utakatifu wake ungebaki na pia neema yake ingeonekana.
    - Kwa kuwa nao, Mungu alikuwa anawafunza jinsi ya kuishi pamoja kama jamii takatifu yenye umaridadi, mpangilio, utakatifu, na utakaso.
    - Mungu alionyesha huruma kwa kuruhusu Haruni na wenye dhambi wengine kumtumikia kama wapatanishi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.)**
    - Mungu bado aliwatenga watu kwake mwenyewe ambao kupitia kwao atamleta Mwokozi aliyeahidiwa.
    - Maskani ilikuwa ishara ilioelekeza kwa Kristo, yaani Mwokozi aliyeahidiwa.
    - Yesu alitakiwa kuwa dhabihu kamili , kama vile kila kitu kwenye maskani ilikuwa kamili na takatifu
    - Maskani ilielekeza kwa Yerusalemi Mpya kwa siku zijazo kwa waminifu kuishi na Mungu.
    - Mungu alikuwa akitumia matukio ya historia kufunza kuhusu mpango wake wa Wokovu.
    - Mungu alikuwa akifunza kuhusu dhabiu na akiielekeza kwa Kristo.
    - Je, unaweza kuunganisha hadithi hii vipi na hadithi za hapo awali.
    - Kumbuka hadithi za Mwanamke na Nyoka, Kaini na Habili, Abrahamu na Isaka, Pasaka, na kathalika.

<u>**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**</u>

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu.**
    - Mungu alifanya mambo makuu ili wenye dhambi wamrudie.
    - Mungu alitoa mtindo wa dhabihu ulioelekeza kwa Mwokozi.
    - Mungu alitaka kukutana na mwanadamu. Kwa hivyo alifanya pahali kukutana nasi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Kila mara damu inapomwagwa kama dhabihu, inafunza kwamba dhambi ya mwanadamu ilileta mauti ulimwenguni na kwamba dhambi inaweza kulipiwa tu kwa mauti kwa mauti.
    - Hata kuhani mkuu alikuwa mwenye dhambi na alipaswa kutowa dhabihu.
    - Wana wa Haruni waliasi dhidi ya Mungu kwa kutofuata maagizo yake.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Ni Mungu tu anayeweza kufanya njia kwa mwanadamu kukutana naye. Ni lazima tufuate njia ya Mungu ya Wokovu.
    - Hata kuhani alipaswa kufuata njia ya Mungu.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Mwanadamu anamwendea Mungu katika njia ya Mungu tu.
    - Mwanadamu anamwendea Mungu kupitia dhabihu ya damu, kwa niaba ya dhambi zake.
    - Dhabihu lazima iwe kamilifu na takatifu
    - Ni lazima mwanadamu kumwamini Mungu na Kufuata njia yake.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.**
    - Kwa kuleta dhabihu, Mwanadamu anakubali dhambi zake mwenyewe, na kuweka tumaini lake katika mwokozi ambaye atakuja.
    - Bado tunaokoka kwa kukubali dhambi zetu na kumwamini Mwokozi

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Mara nyingi hatumwendei Mungu kwa sababu hatujisikii kustahili vya kutosha. Je, ni mambo gani ambayo hufanya tujihisi hatustahili?

- Hatuwezi kamwe kujifanya watakatifu kiasi cha kustahili uwepo wa Mungu. Je, kuamini ukweli huu kunaweza kukusaidiaje kumjia Mungu kwa njia gani? Hema ya Bwana inatuonyesha kwamba tumaini letu pekee la kuja kwa Mungu ni kupitia dhabihu ya dhambi kamilifu iliyotolewa kwa niaba yetu. Ni Mungu pekee anayeweza kutoa dhabihu hii na alifanya kupitia kwa Yesu Kristo. Kuamini haya yanaweza kutusaidia vipi kumkaribia na Mungu tu kwa huru kwa imani na toba?

- Mungu alikuwa pamoja na watu wake kila siku kupitia hema. Sasa yuko nasi kila siku kwa njia ya Kristo. Anataka kuhusika katika maisha yetu ya kila siku - akitoa mwongozo, chakula, ushirika na kila kitu. Huu ukweli unaweza kuathiri maisha yako kwa njia gani?
    - Kuzalisha shukrani. Kujenga imani yako kukabiliana na hali ngumu maishani. Kusaidia kutubu na kuishi maisha matakatifu? Kusaidia kukaribia watu wengine.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- Mungu angali anakaa pamoja na watu wake na anataka kuwa karibu nawe. **Ni kwa njia ipi umekuwa ukimzuia kukaribia maisha yako?** Unawezaje kutubu na kumsongea Mungu anapokusongea?

- Je, kuamini uwepo wa Bwana katika maisha yako kupitia Kristo kunawezaje kukusaidia katika changamoto mahususi unayopitia kwa sasa?

## 20-B. SOMO la CBS - KUTENGENEZA HADITHI

**KUFUNDISHA JINSI YA KUTENGENEZA HADITHI ZA BIBLIA kwa KUSEMA**

- **Shughuli:** Mfanye kila mtu afungue au kushiriki Biblia na jirani yake na **kusoma na kurudia**mojawapo ya hadithi hizi kamili. (Mwanzo 27) Yusufu (Mwanzo 37,39-50) Mwanamke Msamaria (Yohana 4).
  - Uliza maswali haya kwa kikundi:
    - **Je! hadithi katika Biblia iko na tofauti gani na hadithi zetu ambayo tumetunga za CBS?** Je, tumefanya mabadiliko gani?
    - **Kwa nini hatuwezi kutumia tu hadithi hii kama ilivyoandikwa? Kwa nini tulihitaji kufanya mabadiliko fulani?**
      - § ( *wakati mwingine ni ndefu sana, maelezo mengi kwa kumbukumbu)*
    - **Je, tunahitaji kufanya nini ili kuifanya iwe ya manufaa zaidi kwa kufundisha kwa njia ya kusimulia hadithi za Biblia?**
      - § *Lazima uiweke KIBIBLIA!!! USIBADILI ukweli wowote!*
      - § *Ifanye tu iwe FUPI, kutosha kukariri na kuwaambia wengine kwa urahisi*
    - **Je, tunapaswa kufupishaje hadithi?** Ni vitu gani tunapaswa kuondoa au tusiondoe? (angalia jinsi tulivyofupisha baadhi ya hadithi zilizotajwa hapo juu.)
    - **Hadithi inapaswa kuwa ya muda gani tunapoisimulia?**
      - **Dakika mbili hadi tano** . Fupi ni bora zaidi! Ikiwa ni ndefu sana, labda ni bora kutengeneza hadithi mbili fupi badala ya moja.

Kwa muhtasari:

- **SIFA ZA HADITHI YA BIBLIA ILIYOUNDWA VIZURI -** Hadithi ya Biblia ambayo imeundwa vyema ili kusimuliwa ni:
- **Kweli kwa Maandiko!**
  - § Sema tu kile kilicho katika Biblia. Usiongeze vitu ambavyo havipo. Kwa watu wengine hii itakuwa aina yao kuu ya Maandiko. Ni muhimu kuwa ni sahihi na kweli.
  - § Daima hakikisha kwamba watu wanaelewa kwamba hadithi zako ulizotunga si Maandiko yenyewe, lakini kwamba zimechukuliwa **kutoka kwa** Biblia. Ni muhimu nyakati mbalimbali watu wasome masimulizi ya Biblia. Biblia lazima iwe mamlaka yetu ya mwisho.
- **Wazi na Inaeleweka** .
  - § Jaribu hadithi na watu wengine ili kuelewa
  - § **Zingatia mambo muhimu** . Kumbuka malengo yako ya kufundisha wakati wa kuunda hadithi. (yaani kwa madhumuni tofauti yatasisitiza sehemu za hadithi)
- **Kukumbukwa / Kuweza Kujifunza** .

- § Yaani lazima iwe **FUPI** vya kutosha ili wengine wajifunze hadithi kwa moyo kwa urahisi.
  - § **Acha maelezo ambayo si muhimu** kuwasilisha maana kuu ya hadithi kwa wakati huu.
  - § Ondoa majina ya watu na mahali (**ambaya yamerueliwa mara nyingi** ).
  - § Ondoa **marudio mengi** ili kusaidia kukariri kwa urahisi zaidi.
  - § Hakikisha hadithi inatiririka kiasili kama inavyofanya katika Biblia.

- Tambua **manukuu muhimu** na uyakariri neno kwa neno.
  - § Kwa mfano. "Nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, kati ya uzao wako na uzao wake. Yeye atakuponda kichwa, na wewe utauma kisigino chake."

**MAWAZO MENGINE kuhusu KUTUNGA HADITHI ZA BIBLIA kwa KUSEMA:**

- **Aina za hadithi za Biblia zilizotungwa** (pamoja na mifano kutoka katika kijitabu hiki):
  - · **Neno kwa neno** - Mifano: Mwanamke Mwenye Dhambi Anaosha Miguu ya Yesu, Kumponya Mtu Aliyepooza.
  - · **Imeundwa** - kwa uhariri mdogo au ufupishaji - Mifano: Nuhu, Pasaka, Mwanamke Msamaria
  - · **Imekusanywa** - kutoka kwa vifungu vingi vya Biblia - Mifano: Uumbaji wa Malaika, Kusulubiwa, Ufufuo

- **Uelewa:** Hakikisha una kuelewa kwa kutosha kwa hadithi wewe mwenyewe kabla ya kuitunga ili kusimuliwa.
  - · Wahusika ni akina nani? Nini kilitokea kabla ya tukio hili? Mpango ni nini? Hadithi inafundisha au inasisitiza nini? Jaribu kufikiria kwa nini hadithi hii ilisimuliwa.
    - § Tazama hadithi na wahusika ndani yake.
  - · Funga macho yako na uone hadithi unaposikiliza wahusika wakizungumza.
  - · Zingatia vidokezo vinavyotambulisha wahusika. (Kut. Esau alikuwa na nywele)
    - § Jihadharini na mambo, ambayo yanaweza kuudhi, au kuvuta tahadhari au kuchanganya.
    - § Zingatia ni wapi hadithi inaanzia na inaishia. Tambua sehemu zinazo ondoa umakini kutoka kwa hadithi.
    - § Eleza mambo yasiyo ya kawaida au yasiyo julikana katika hadithi kabla ya kuanza hadithi.

- **Kazi ya nyumbani:** Tengeneza hadithi ya wiki ijayo (hakikisha mwanzoni mwa darasa)
    - Unaweza kukaa na Biblia, kalamu, na karatasi ili kutengeneza hadithi AU…
    - Unaweza kutumia njia mbadala ya mdomo ili kuandika hadithi. (Tazama Kiambatisho 6B)

**HADITHI ZINAZOWEZEKANA ZA KUTUNGA DARASA/KAZI YA NYUMBANI:**

| | |
|---|---|
| **Mwanzo 19:1-29** | **Sodoma na Gomora** |
| Mwanzo **20** :1-18 | Abrahamu na Abimeleki |
| Mwanzo **24** :1-66* | **Isaka & Rebeka** |
| Mwanzo 30:25-31:55 | Yakobo anakuwa Tajiri na kumuacha Labani |
| Mwanzo **34** :1-31 | **Dina na Washekemu** |
| Mwanzo **38** :1-29 | **Yuda na Tamari** |
| Kutoka **16** :1-36 | Manna na Kware |
| Kutoka **18** :1-27 | **Yethro Anamtembelea Musa** |
| Yoshua **2** :1-24 | Rahabu na Wapelelezi |
| Yoshua **3** & **4** | Kuvuka Yordani |
| Yoshua 5:13-6:27 | **Yeriko** |
| Yoshua **7** :1-26 | **Dhambi ya Akani** |
| Yoshua **9** :1-27 | **Udanganyifu wa Wagibeoni** |
| Waamuzi 3:12-30 | **Ehud** |
| Waamuzi **4** :1-23 | **Debora** |
| Waamuzi **7** :1-25 | **Gideoni Awashinda Wamidiani** |
| 1 Samweli **1** :1-28 | **Hana & Samweli** |
| Mt 13:1-23 | **Mfano wa Mpanzi** |
| Mt 13:24-43 | **Mfano wa Magugu** |
| Yohana 4:1-42 | **Mwanamke Msamaria** |
| Yohana 9:1-49 | **Yesu Anaponya Kipofu** |
| Matendo 2:14-41 | **Mahubiri ya Petro** |
| Matendo 4:1-22 | **Petro na Yohana mbele ya Baraza** |
| Matendo 5:17-42 | **Mitume Wafungwa na Kuachiliwa** |
| Matendo 6:8-7:60 | **Stephen** |
| Matendo 10:1-11:18 | **Petro na Kornelio, Injili kwa Mataifa** |

## 21. WAPELELEZI KUMI na WAWILI na NYOKA JANGWANI

Hesabu 13:1 – 14:12; 21:1-9

*Wapelelezi Kumi na Wawili Wanaichunguza Kanaani:*

Baada ya Bwana kutoa maagizo kwa Musa katika Mlima Sinai, watu walielekea Kanani kwa sababu hii ndiyo ilikuwa ahadi ambayo Mungu alimpa Abrahamu, Isaka, na Yakobo. Musa akatuma wapelelezi kumi na wawili walioenda katika nchi yote ya Kanaani kwa siku arobaini. Kusudi lao ilikuwa kupata habari ili Waisraeli wapange jinsi ya kuivamia.

Hata hivyo, wapelelezi waliporudi, wote walikubali ya kwamba ilikuwa nchi nzuri na ilikuwa ikitiririka maziwa na asali ya nyuki, lakini kumi kati yao walikuwa na ujumbe mbaya wakisema kwamba, watu wa miji huko walikuwa hodari sana na kwamba Waisraeli hawangewashinda. Lakini wapelelezi wawili, Yoshua na Kalebu, walijaribu kuwashawishi kuingia, wakiwakumbusha yale yote Mungu alikuwa amewafanyia kuwaokoa kutoka Misri, na huyo huyo Mungu angewasaidia kuwashinda adui zao. Lakini watu waliasi wasiingie.

Kwa hivyo, Mungu alileta hukumu juu yao akitangaza kwamba hakuna yeyote aliyekuwa na miaka ishirini au zaidi kwa wakati huo, ambaye angeingia nchi ya ahadi, na kwamba Waisraeli wangezunguka jangwani kwa miaka arobaini, mwaka mmoja kwa kila siku ambayo wapelelezi walikuwa katika nchi ya Kanaani, mpaka kizazi chote kife na kwisha.

*Miaka Arobaini Jangwani / Kutokuamini kwa Israeli:*

Hivyo basi, Waisraeli walizurura jangwani. Musa aliwaongoza na Mungu aliwaletea chakula na maji katika njia ya ajabu. Lakini watu walikuwa wanalalamika mara kwa mara.

Wakati mmoja, walipokuwa wakizurura watu walimnung'unikia Mungu na Musa, wakisema, "Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani? Hakuna mkate wala maji, na tunachukia sana hii mana ambayo Mungu alitupatia!"

Mungu alikasarika. Bwana akatuma nyoka za moto kati yao, wakawauma, na watu wengi wakafa. Watu wakamwendea Musa, wakasema, "Tumefanya dhambi kwa sababu tumemnung'unikia Mungu, na wewe; utuombee kwa BWANA, ili atuondolee nyoka hawa. Basi Musa akawaombea watu.

Bwana akamwambia Musa, "Jifanyie nyoka wa shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu atakayeumwa, aitazamapo ataishi." Musa akafanya nyoka wa shaba, na kumweka juu ya mti. Baadaye, wakati mtu yeyote alipoumwa na nyoka, akimtazama yule nyoka wa shaba aliishi.

Lakini mwenendo kama huu ulikuwa kawaida kwa kizazi hicho cha Waisraeli. Basi walizurura jangwani kwa miaka arobaini kama Mungu alivyosema.

*Kuingia katika Nchi ya Ahadi:*

Mwishowe, baada ya miaka arobaini katika jangwa, Mungu aliwaleta Waisraeli mpakani wa nchi ya ahadi. Akawaambia Waisraeli hivi,

1) Moja, msiabudu miungu mingine au kuiinamia sanamu kamwe!
2) Pili, msiwe na kiburi. Mungu hawapi nchi hii kwa sababu ya wema wenu. Ndiyo nyinyi ni watu wa shingo ngumu. Ninawatumia nyinyi kuwaadhibu mataifa kwa sababu ya maovu yao.
3) Tatu, Mungu anawapatia nchi hii kwa sababu anawapenda na anatimiza ahadi ambayo aliwafanyia Abrahamu, Isaka, na baba wenu Israeli. Na aliweka agano hilo kwa Mlima Sinai kuwafanya kuwa mali yake ya thamani na taifa takatifu.
4) Nne, iwapo, kama mkitimiza sehemu yenu ya agano kwa kumtii Mungu, atawapenda na atawabariki zaidi ya watu wengine.
5) Tano, mkiabudu miungu mingine, hasira ya Mungu itawachoma na itawaondoa katika nchi hii. Bali mtakapotubu na kumtafuta Bwana na kumtii, atawahurumia na kukumbuka ahadi yake.

Baadaye, Musa alipanda Mlima Nebo kuiangalia Kanani. Akafa hapo na kuzikwa na Mungu mwenyewe. Mungu alikuwa amechagua Yoshua kuwa kiongozi wa watu wake. Basi Yoshua aliwaongoza Waisraeli kuvuka Mto wa Yordani na kuanza kuwafukuza Wakaanani na kuchukua Nchi ya Ahadi.

**<u>MPANGILIO wa SOMO</u>**

**<u>UTANGULIZI:</u>** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Ni mambo gani maishani huwa unayalalamikia au kunung'unika?**

**<u>HADITHI:</u>** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**<u>MJADALA baada ya HADITHI:</u>** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**<u>Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
    - Mungu alikuwa amewapangia kuenda Kanaani. Alikuwa amewaahidi nchi hii.
    - Mungu hakuogopa miji iliyolindwa.
    - Mungu alikuwa na mamlaka kuwatuma kurudi jangwani. Waisraeli hawangekataa.
    - Mungu alimpa Musa maagizo katika Mlima wa Sinai.
    - Aliwapa chakula na maji.
    - Alikuwa na uwezo kuadhibu kunung'unika kwao na kuwatuma nyoka kuwauma.
    - Mtu yeyote hangeweza kuepuka.
    - Mungu alikuwa na nguvu kuwaponya watu ambao waliumwa na nyoka. Mungu ana mamlaka juu ya uumbaji. Aliwaumba nyoka, kwa hivyo alikuwa na mamlaka juu yao.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Mungu alijua mawazo yote ya watu hawa walionung'unika.
    - Mungu alijua ujumbe wapelelezi wangetoa, na ungejaribu imani ya Waisraeli.
    - Mungu alijua kwamba angewasaidia kuwashinda maadui wao.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Kwa sababu ya manung'uniko yao, Mungu aliwahukumu. Hangewaruhusu watu wazima kando na Kalebu na Yoshua kuingia katika nchi ya ahadi. Badala yake, watazunguka jangwani hadi kizazi hicho kilipokufa na kumalizika kabisa.
    - Kila wakati Mungu huadhibu dhambi. Aliwaadhibu waliolalamika kwa kuumwa na nyoka. Watu wengi walikufa.
    - Lazima Mungu kuadhibu dhambi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu alitoa nyoka ya shaba ili yeyote ambaye angeiangalia angeokoka.
    - Mungu alitoa chakula na maji.
    - Mungu aliwaongoza jangwani.
    - Aliwalinda kutoka kwa makabila mengine walipozunguka jangwani.
    - Mungu alikuwa mvumilivu kwa sababu aliwavumilia badala ya kuwaangamiza.
    - Mungu aliwasikiliza akasikia kilio chao baada ya wao kuumwa na nyoka.
    - Aliwaongozea nchi ya ahadi tena baada ya miaka arobaine.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
    - Mungu alisema kwamba kizazi hicho kitakufa jangwani na ikawa hivyo.

- Mungu alitimiza ahadi yake ya nchi kwa Abrahamu, Isaka, na Yakobo.
    - Alisema kwamba ikiwa watu wangeiangalia nyoka ya shaba wangeishi. Ikawa hivyo.
    - Hata ingawa Mungu alikiadhibu kizazi hicho, aliendelea kuwalinda Waisraeli ambao kupitia kwao angebariki dunia.
    - Mungu alikuwa amesema angewaletea kizazi kipya nchi ya ahadi. Alifanya hivyo.

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Waisraeli walilalamika tena na tena, hata baada ya Mungu alikuwa amewafanyia mambo mengi.
    - Walikataa kuziamini ahadi zake.
    - Hawakuwa na imani.
    - Walisikiliza, mashaka na hofu.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Mwanadamu hawezi kuepuka adhabu ambayo Mungu alitoa.
    - Hawangeweza kujiokoa wenyewe kutoka nyoka.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Waliweza kuokoka tu kwa kumwangalia nyoka ya shaba, yaani kwa kufuata njia ambayo Mungu aliwatolea.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa?**
    - Kwa kumwangalia nyoka ya shaba, walikuwa wanatubu dhambi zao na kugeuka kwa imani katika njia ambayo Mungu aliwapa ili waokoke.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Waisraeli walisikiza habari mbaya ya wapelelezi kumi badala ya habari ya imani kwa Mungu kutoka kwa Joshua na Kalebu. Ni katika hali gani tunasukumwa kupita kiasi na watu wengi hivi kwamba inatupofusha tusiione njia ya imani?

- Ni katika matukio gani ambayo hutufanya kuanza kunung'unika na kulalamika maishani mwetu? Hadithi hii itatusaidiaje kukumbana na hali kama hizo?

- Je Mungu anapotuadhibu maishani, tunafaa kupokea adhabu vipi kulingana na hadithi hii?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Je, wakati huu, unapitia hali gani ambayo ni rahisi kunung'unika badala ya kumwamini Mungu?** Je, unaogopa nini katika hii hali? Je, hadithi hii itakusaidia vipi kukabliana na hofu yako? Unaweza kukiri kwa Mungu hofu yako na kutoamini kwako?

- **Fikiria eneo fulani la maisha yako ambalo unashindwa kumtii Mungu?** Je, kushindwa kwako kumtii Mungu kunaonyesha vipi ukosefu wa imani katika maisha yako?

## 22. WAAMUZI
## Yoshua 7-28; Waamuzi; 1 Samweli 1-4

Waisraeli walipokuwa wakishinda Wakanani, makabila kumi na mawili wake walichukua sehemu ya nchi. Ilikuwa kazi yao kuwaondoa Wakanani walioishi hapo ili wasije kuchanganyika nao na kuabudu sanamu zao.

Baada ya kifo cha Yoshua, makabila kumi na mawili walijitawala. Lakini walipojisikia kwamba wamestarehe na kunawiri katika nchi mpya, walisahau alivyowaambia Mungu kufanya. Kila mtu akafanya yaliyokuwa mema machoni pake.

Basi malaika wa Bwana akawaambia watu, "Nilipowatoa Misri nilisema, 'Msiwaruhusu Wakanani kuishi pamoja nanyi.' Lakini mmevunja ahadi hii kati yetu. Mmeruhusu Wakanani kuishi nanyi na hamkuvunja madhabahu yao na kuchoma sanamu zao. Kwa hivyo sitawaondoa tena kutoka nchi yenu. Watakuwa miiba ubavuni mwenu na miungu yao itakuwa mitego yenu."

Na hivyo ndivyo ilifanyika. Kizazi kipya kilimsahau Mungu. Wakaanza kuabudu miungu ya Wakanani na kufanya mambo maovu sana. Maadui wao waliwavamia, na kila wakati Waisraeli walipoenda kupigana, Mungu alikuwa dhidi yao nao walishindwa.

Walipokuwa watumwa tena, walimkumbuka Mungu, kisha wakamlilia awaokoe. Ndipo Mungu aliinua kiongozi aliyewaokoa kutoka kwa maadui. Kila kiongozi aliitwa mwamuzi.

Lakini baada ya muda wangemsahau Mungu tena, na mtindo huu ungeanza tena. <u>Mara kumi na nne</u> katika miaka mia tatu hamsini, Waisraeli waliasi dhidi ya Mungu na kuziabudu sanamu za Wakanani. Kila mara, Mungu aliwaadhibu kama alivyosema alipowapatia Amri Kumi katika Mlima wa Sinai. Lakini kila mara Waisraeli walitubu dhambi zao na wakaanza kutii tena na Mungu aliwasamehe na akawabariki tena na mwamuzi kuwaokoa. Huu unaitwa wakati wa Waamuzi. Gidioni, Debora, na Samsoni walikuwa baathi ya waamuzi. Mwamuzi wa mwisho kuwaokoa wana wa Israeli alikuwa mtu aliyeitwa Samweli. Samweli alipokuwa mvulana, Mungu alizungumza naye, na kumwambia mambo ambayo yangetokea wakati ujao. Alipokuwa akikua, Mungu alikuwa pamoja naye, na yote aliyosema yalitimia. Hivyo watu wote walijua kwamba Samweli alikuwa nabii wa Mungu.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kufikiria njia ambayo dhambi moja inaweza kusababisha dhambi nyingine ili mambo yawe mabaya zaidi na zaidi?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
    - Waisraeli waliwashinda maadui wao Mungu alipokuwa pamoja nao. Lakini walishindwa, Mungu alipowaacha.ilikuwa tu kwa uwezo wake Mungu ndipo wangeshinda
    - Kila mara Mungu alikuwa na uwezo wa kuwaokoa kutoka kwa maadui wao

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Mungu alijua halisi ni nani aliyetenda dhambi na kile alichotenda
    - Mungu kila wakati alijua
    - Waisraeli walipofanya dhambi dhidi yake.
    - Pia alijua walipotubu na alijua jinsi ya kuwaokoa.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Mungu alipeana amri na alitarajia utii.
    - Waisraeli walipoasi dhidi ya Mungu, Mungu aligeuka dhidi yao ili kulinda utukufu wake.
    - Mara baada ya nyingine Waisraeli waligeuka dhidi ya Mungu na naye aliwaadhibu

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Alionyesha neema tena na tena kila walipotubu dhambi zao. Akawapatia mwamuzi kuwaongoza na kuwaokoa.
    - Mungu aliendelea kuwalinda watu hawa wa ahadi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?**
    - Mungu aliahidi wapa nchi ya ahadi na alifanya hivyo hata wakati ambao walikosa kutii.
    - Mungu aliendelea kuwalinda watu wa ahadi ambao kupitia kwao angemtuma Mwokozi ambaye aliahidiwa zamani

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Waisraeli walijaribiwa tena na tena kugeukia sanamu na kutoka kwa Mungu

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi, kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**

    - Waisraeli hawangeshinda hata mji  mdogo wa Ai bila usaidizi wa Mungu
    - Tena na tena Waisraeli walishindwa na maadui wao na hanwangeweza kujiokoa.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu?  (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Waisraeli wangeweza tu kushinda maadui wao ikiwa wangefuata amri za Mungu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa?**
    - Kila mara Waisraeli walipotubu dhambi zao na kumwamini Mungu tena, aliwaokoa.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Je, ni kwa njia gani tunaona watu wakipitia kwa sababu ya matokeo au matunda ya dhambi zao hapa duniani?

- Njia moja ya watu" kutenda yaliyo mema machoni mwao wenyewe"  ni kutotilia maanani dhambi zao wenyewe.  Je, ni katika njia gani watu hupuuza dhambi zao ama kuziona kama sio muhimu? Peana mifano.

- Je, ni kwanini dhambi zetu "ndogo" ni za muhimu? Je huonyesha nini kuhusu mioyo yetu? Je, ni kwa nini hizi dhambi ni hatari hata kama haizimuumizi mtu mwingine?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>**  (chagua moja au mbili)

- **Je, unaweza taja dhambi katika maisha yako ambayo unaiona kama sio muhimu sana?**  Je, dhanbi hii inaonyesha nini kuhusu moyo wako?  Je, ni hatari gani iliyoko kwako na wengine kama dhambi hii haitashughulikiwa?

- Ni kwa njia gani hivi majuzi umekuwa ukitenda yaliyo mema machoni mwako badala ya kutazama mambo kupitia kwa macho ya Mungu?  Yaani  ni dhambi gani unapambana nayo kwa sasa maishani? Je, ni ukosefu wa uaminifu, wizi, wivu au masengenyo? Je, dhambi hii imeharibuje uhusiano wako na Mungu? Na Wakristo wengine? Je, kuna tumaini gani kwako ikiwa utakiri dhambi yako na kutubu?

## 23. WAISRAELI WAKATAKA MFALME / SAULI
## 1 Samweli 8-10, 13:2-15, 15:1-23, 16:1-13, 2 Samweli 5:1-12

Samweli alipokuwa mkongwe, Waisraeli walimwambia, "Tunataka mfalme kama mataifa mengine."

Samweli hakufurahia lakini Mungu akasema, "Waisraeli wananikataa kama Mfalme. Tangu nilipowaondoa Misri, waliasi dhidi yangu na kuiabudu miungu mingine. Kwa hivyo wape wanachotaka. Lakini kwanza, uwaonye watakavyotawaliwa na wafalme."

Samweli alijaribu kubadilisha mawazo yao na akasema, "Mfalme atalazimisha wana wenu kupigana katika jeshi lake. Na atachukua mashamba yenu mazuri na mifugo yenu iliyo bora. Nanyi mtakuwa watumwa wake."

Lakini Waisraeli hawakumsikiza Samweli wakasema, "La! Tunataka mfalme kama mataifa mengine, yaani mfalme anayeweza kutuongoza katika vita."

Basi Mungu alimwongoza Samweli kwenye kijana aliyeitwa Sauli. Samueli alimtia mafuta kumweka wakfu akisema, "Bwana anakutia mafuta wewe kama mfalme wa watu wake wa Israeli."

Kisha Samweli akamleta Sauli mbele ya watu, nao wakashangilia wakisema "Mfalme aishi muda mrefu."

Sauli aliwasaidia Waisraeli kushinda maadui wao, lakini alianza kujitegemea badala ya kufuata Mungu. Siku moja, badala ya kumgojea kuhani wa Mungu Samueli amtolee Mungu dhabihu kabla ya vita, aliwaogopa maadui na akamtolea Mungu dhabihu yeye mwenyewe hata ingawa yeye hakuwa kuhani. Mungu akakasirika sana.

Wakati mwingine Mungu akaongea kupitia kwa Samweli na kumwambia avamie Waameleki kulipiza kisasi kwa sababu Waameliki walikuwa wakiwaavamia Waisraeli waliporudi kutoka Misri. Waameleki waliabudu sanamu. Mungu akasema, "Mharibu kila kitu hata mifugo." Lakini Sauli hakumwua mfalme wao au wanyama wazuri. Pia Sauli alijisimamishia sanamu ya ukumbusho.

Baada ya vita, Samueli akamwendea Sauli. Naye Sauli akamwambia, "Bwana akubariki! Nilifanya kile Mungu aliniambia wakati huu.".

Samweli akasema, "Ni kweli? Maana yake nini basi hiki kilio cha kondoo masikioni mwangu na huu mlio wa ng'ombe ninaousikia?"

Sauli akamjibu, “Majeshi waliweka wanyama walio bora zaidi kwa kutoa kama dhabihu kwa Bwana Mungu wako.  Lakini tuliharibu kila kitu kingine chochote!  Tulimtii Mungu!”

“Nyamaza!” aliamuru Samweli. “Je, unafikiri Bwana anapenda dhabihu zaidi ya utiifu? Kutii ni bora kuliko sadaka. Uasi na kiburi ni mbaya kama ibada ya sanamu. Kwa kuwa umelikataa neno la BWANA, yeye amekukataa wewe kuwa mfalme." Samweli akageuka ili aondoke, lakini Sauli akalishika vazi lake, nalo likararua jirani."

Hatimaye Sauli akasema, “Sawa, nimefanya dhambi. Nilikiuka agizo la Mungu. Niliogopa watu na hivyo nikakubali. Sasa nakuomba, unisamehe dhambi yangu, urudi pamoja nami, ukaniheshimu mbele ya wazee wa watu wangu, na mbele ya Israeli; urudi pamoja nami, ili nipate kumwabudu BWANA.”  Hivyo Samweli akarudi, naye Sauli akamwabudu Bwana, lakini Samweli akamwua mfalme wa Waameleki mbele ya Bwana. Kisha akaenda na hakumwona Sauli tena akamwombolezea.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je! umewahi kumwambia mtu, "Samahani," lakini haukumaanisha hivyo? Kwa nini ulisema samahani?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
  - Alikuwa na uwezo wa kujionyesha mwenyewe kwa waisraeli kupitia kwa mtumishi wake Samueli. Akikuwa naye kwamba kila kitu alichosema kilitimia ilithibitika kwa watu kwamba Samueli alikuwa Nabii wa Mungu.
  - Mungu alikuwa na uwezo wa kuwapa Israeli mfalme na hata kuchagua Saulo na kumwamuru afanye nini.
  - Alikuwa na uwezo wa kumkataa Saulo kama Mfalme.
  - Mungu alimpa Samueli Roho wa nguvu na alimlinda alipoenda kumkemea Mfalme Saulo.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
  - Samueli alipokuwa mchanga, Mungu alimwambia kile kitakachotendeka siku za usoni. Mungu anajua kila kitu.
  - Mungu alijua na  kuwambia waisraeli kile ambacho mfalme angewafanyia.
  - Alijua Saulo atakuwa Mfalme wa aina gani.
  - Mungu alijua kwamba Saulo hakumtii, alipokataa kuwaua wameleki wote na wanyama wao.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Mungu alikataa dhabihu iliyotolewa na mfalme Sauli kwa sababu hakuwa kuhani. Hakuwa aliyechaguliwa na Mungu kwenye ofisi {cheo} hiki. Hakumtumaini Mungu ya kutosha kumngojea
    - Mungu pia alimkataa.
    - Utakatifu wa Mungu unahitaji utiifu kikamilifu bila kuuliza maswali au kutoa visababu.
    - Sauli alikufa mbali na mungu kwa sababu hakutii.
    - Kwa sababu ya ukweli kwamba dhabihu ilihitajika kabla ya vita inaonyesha utakatifu wa Mungu.
    - Israeli ilikuwa inaadhibiwa kwa kukataa kujitenga na wakanani wasiomwabudu mungu kama wafilisti. Mungu alitaka taifa takatifu, taifa lililojitenga na uovu.
    - Ni dhabihu ya aina gani ambayo Mungu alitaka. Alitaka dhabihu ambayo ilitoka kwa moyo uliojitolea kwa Mungu. Moyo uliomwamini Mungu. Dhabihu haikuwa njia ya kumtolea Mungu hongo. Ili asiadhibu dhambi. Haikuwa tu kufanya matendo bure. Ilipaswa kuwa kwa imani, na ingefanywa tu katika njia ya Mungu.
    - Mungu alimwaadhibu Sauli kwa kujitukuza mwenyewe badala ya kumtukuza Mungu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu aliwapa Nabii wa kuongea na wao.
    - Aliwapa njia ya dhabibu ili kuweza kukutana nao.
    - Mungu aliwasikiliza watu wake na aliwajibu.
    - Alikuwa mvumilivu sana na Sauli. Hakumwua punde hata ijapo alikuwa amemkataa kama mfalme. Bado alikuwa na nafasi ya kutubu na kuokoka.
    - Alimpa maisha marefu.
    - Mungu alikuwa mwenye neema kwa waisraeli kuweza kuwapa mfalme mwingine aliyemcha mungu zaidi.
    - Mungu aliwaonya kuhusu shida ambazo zingeletwa na mfalme.
    - Hata ijapo Israeli ilimkataa Mungu kama mfalme, Hakuwaacha bali alikaa nao.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
    - Bado alikuwa mwaminifu kwa Israeli, watu waliochaguliwa ambao kutoka kwao, angeleta mwokozi.
    - Mungu alimwaadhibu Sauli kwa kutoa dhabihu, kwa kuwa ilikuwa kazi iliyopewa makuhani pekee.
    - Mungu alipomkataa Sauli, Ndipo alipokataliwa kabisa.
    - Mungu ameahidi kuleta mwokozi kupitia kwa taifa hili.Anawalinda hata katika mkono wa mfalme mwovu.
    - Mungu alikuwa amemwambia Abrahamu kwamba atawalaani watakaomlaani. Mungu alikuwa anawaadhibu waameleki kwa kuwavamia waisraeli walipotoka Misri kuingia katika nchi ya ahadi miaka ya hapo awali.
    - Mungu anawakumbusha jinsi alivyowatoa Misri. Anawakumbusha uaminifu wake.
    - Mungu alikuwa ameahidi kuwalinda Israeli, na alikuwa anasaidia katika kushinda maadui wao.

<u>**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**</u>

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Waisraeli walikataa muumba wao awe mfalme wao. Badala yake, walidai kwamba wanamtaka mfalme wa kibinadamu. Hawakuwa wakimtumaini mungu.
    - Sauli alifanya vitu katika njia yake mwenyewe badala ya njia ya mungu hata ilipokuwa wazi kabisa. Alikataa kumaliza kuwaua wameleki na mifugo yao kama vile mungu alimwambia wazi kabisa kufanya.

    - Sauli alikuwa na sababa nyingi kutotii – aliwalaumu maaskari na watu, alijaribu kujifanya kama mtakatifu kuleta wanyama kwa dhabihu, etc. Alijali sifa yake kuliku Mungu.
    - Sauli alikuwa anatoa dhabihu yake mwenyewe. Badala ya kumtumaini mungu kumpa moja.
    - Sauli alijenga mnara wake mwenyewe akijifikiria mwenyewe kuhusu sifa yake mwenyewe na si ya Mungu.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Ndiyo, waisraeli walimtegemea Mungu kuwasaidia katika vita.
    - Sauli hangefanya kitu chochote kuhusu kukataliwa kwake.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Lazima mwanadamu kumtumaini Mungu vya kutosha kumtii. Anapaswa kumtumaini Mungu hata asipoelewa au inapoonekana vigumu{Kama kumngojea Samueli kufika}.
    - Mwanadamu anapaswa kumjia Mungu katika njia ambayo Mungu amempa. Mungu alisema kwamba ni makuhani pekee wangeweza kutoa dhabihu.
    - Mungu anajali zaidi kuhusu moyo kuliko utiifu wa juu juu. "Kutii ni bora kuliko dhabihu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.**
    - Tunaona kwamba Sauli hakumwendea mungu kwa Imani, lakini kwa dhambi yake mwenyewe. Hakuonyesha toba ya kweli na alikataliwa.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Waisraeli walitaka mfalme kama mataifa mengine. **Je, Wakristo katika jumuiya wanaathiriwa vipi kwa kutaka kufanana na utamaduni unaowazunguka?**

- Sauli alitafuta vijisababu kadhaa kujaribu kuonyesha dhambi zake kuwa ni nzuri. Alidai kuwa mtiifu kamili hata wakati ulikuwa utiifu usiokamilika. Aliwalaumu askari na watu wengine. Alidai kuwa alikuwa na wazo bora zaidi (kuliko amri ya Mungu) jinsi ya kutumia hao ng'ombe wanono! Akasema tunaweza kuwatumia kama dhabihu!
    - **Je, ni jinsi gani sisi Wakristo hupeana vijisabau kwa ajili ya dhambi zetu badala ya kuzikiri na kutubu kwa kweli?**

- Je, mtu akitenda dhambi na ajaribiwe kumlaumu mtu mwengine, anastahili kufanya nini badala ya kulaumu?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Je ni kwa njia gani ambayo wewe huathiriwa vibaya na utamaduni wako?** Toba ya kweli itakuwa vipi kwako katika hali hii?

- **Je, ni changamoto gani unayokumbana nayo kwa sasa** (kama Sauli akimsubiri Samweli ili atoe dhabihu) **ambapo unajaribiwa kuchukua njia ya mkato au kufanya maafikiano kuhusiana na Mungu?** Hali ambayo unakosa subira unapomngoeja Mungu?

- **Je, unaweza fikiria kuhusu hali ambayo unatoa visingizio vibaya vya kutotii?** Je, hii hadithi itakusaidia vipi kutubu na kutii?

## 24. MFALME DAUDI
## 1 & 2 Samweli, Hasa 1 Samweli 16, 17 na 2 Samweli 6, 7, 11, 12

Baada ya Mungu kumkataa Sauli kama mfalme, alimwongoza Samweli kumtembelea mtu aliyeitwa Yese katika mji wa Bethlehemu, ili kutafuta mfalme aliyechaguliwa. Samweli alifikiri Mungu angemchagua mmoja wa wana wakubwa wa Yese, lakini Mungu alisema, "Hapana. Mwanadamu anaangalia nje ya mtu lakini Mungu anaangalia moyo." Kwa hivyo alimchagua mwana mdogo zaidi aliyeitwa Daudi. Samweli akamtia mafuta. Na Roho wa Mungu akawa naye tangu siku hiyo.

Mfano mmoja wa usaidizi wa Roho wa Mungu kwa Daudi, ulifanyika wakati Daudi bado alipokuwa mvulana. Alienda kuwatembelea ndugu zake katika jeshi la Israeli lilipopigana na jeshi la Wafilisti. Daudi alipofika kambi ya jeshi aliona kwamba Goliathi alikuwa akiwadhihaki Waisraeli na Mungu wao, kwa sababu wote waliogopa kupigana naye. Daudi aliona kile kinafanyika na akakasirika akasema atapigana naye. Hata ingawa alikuwa mtu mdogo ambaye hakujua kutumia silaha za vita, Daudi alijua kwamba Mungu atamsaidia kama alivyomsaidia alipokuwa mchungaji alipowalinda kondoo wake kutokana na wanyama kama simba. Basi Daudi alipopambana na Goliathi, alimwua na kombeo na jiwe na akawapatia Waisraeli ushindi.

Sauli aliendelea kuwa mfalme kwa miaka mingine kumi na mitano. Alimweka Daudi kuwa msimamizi wa baadhi ya askari wake, lakini Sauli angeskia wanawake wakiimba, "Sauli ameua maelfu, lakini Daudi ameua makumi ya maelfu!" Kwa sababu ya wivu wake, mara nyingi sana Sauli alikuwa akijaribu kumwua Daudi. Bali Daudi kamwe hakujaribu kumwumiza Sauli, naye Mungu alimlinda Daudi. Baada ya Sauli na wanawe kufa katika vita, viongozi wa watu walimtia Daudi mafuta ili awe Mfalme wa Israeli kama Samweli alivyofanya miaka mingi iliyopita. Daudi alikuwa na miaka thelathini alipokuwa Mfalme na akatawala kwa miaka arobaini.

Daudi alikuwa mpiganaji mkuu, naye alimtumaini Mungu sana. Ila, alifanya dhambi nyingine kubwa sana katika maisha yake, lakini alitubu na akasamehewa na Mungu. Daudi alipokuwa amewashinda adui zake wote, alileta sanduku la agano katika Yerusalemu, mji mkuu wake. Daudi alitaka kujenga nyumba kuu, hekalu, kwa Mungu. Lakini Mungu, akatuma ujumbe kwake kupitia kwa nabii Nathani akasema, "Hutajenga nyumba yangu kwa sababu umemwaga damu nyingi, lakini kijana wako ataijenga. **Ninakuahidi kwamba utakuwa na mwana kukaa katika kiti chako cha enzi milele na ufalme wako utakaa milele**." Naye Daudi alimsifu Mungu kwa ajili ya ahadi zake.

Hata ingawa Daudi alikuwa mwenye dhambi aliyehitaji neema ya Mungu, alikuwa mtu aliyependeza moyo wa Bwana. Mungu alimtumia kuziandika nyimbo nyingi za kumwabudu katika neno lake.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Fikiria wakati ulimwona mtu kwa mara ya kwanza na kufanya uamuzi fulani katika akili yako juu yake lakini baadaye ukagundua kuwa umekosea. Unafikiri ni kwa nini ulikuja na maoni yasiyofaa?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
  - Mungu alimkataa Sauli na kumchagua Daudi kama mfalme.
  - Mungu alimsaidia kijana Daudi kushinda Goliathi.
  - Mungu aliwasaidia waisraeli kuwashinda maadui wao.
  - Mungu alimlinda Daudi kutoka kwa mfalme Sauli.
  - Mungu alimfanya Daudi kuwa mpiganaji hodari.
  - Mungu alimwezesha Daudi kuleta sanduku la agano katika Yerusalemu.
- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
  - Mungu alijua moyo wa Daudi alichamgua kutoka kati ya kaka zake wakubwa wenye nguvu zaidi.
  - Mungu alijua kuhusu dhambi ya Daudi.
  - Mungu alijua kwamba mwana wa Daudi angejenga hekalu.
  - Mungu alijua kwamba Daudi angekuwa na mwana kwenye kiti cha enzi kila wakati.
- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
  - Mungu aliadhibu familia ya Sauli kwa kuwaua.
  - Mungu alikuwa akihifadhi jina lake alipomsaidia Daudi kumwua Goliathi.
  - Mungu hakumruhusu Daudi kujenga hekalu kwa sababu alikuwa amemwaga damu nyingi.
  - Hata ijapo kuwa Mungu alimsamehe Daudi kwa uzinzi wake, bado kulikuwa na matokeo kwa dhambi zake. Mtoto wao na Bethsheba alikufa, na baadaye kulikuwa na shida za kifamilia.
- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
  - Mungu alimlinda Daudi kutoka kwa wanyama wa mwituni kama mvulana, kutoka kwa Goliathi na hata kutoka kwa Sauli.
  - Mungu alikuwa mwenye neema kumpa Sauli wakati zaidi hata baada ya kukataliwa kama mfalme.
  - Mungu alimpa Daudi ushindi katika vita.
  - Mungu alimsamehe Daudi kwa uzinzi wake.
  - Mungu alimtuma Nabii Nathani na akampa nafasi ya kutubu.
  - Mungu alimtumia Daudi ingawa alikuwa mwenye dhambi.
  - Mungu aliahidi kwamba mwana wa Daudi atakuwa mfalme kila wakati.
  - Mungu aliruhusi sanduku la agano ambalo liliashiria uwepo wake kwao kurudi.Israeli, hata ingawa walikuwa wamelipoteza kwa ajili ya dhambi zao.
  - Mungu alipoahidi mwana atakuwa kwenye kiti cha enzi kila mara alikuwa akielekea kwenye mwokozi atakayekuja ambaye alikuwa ameahidiwa kutoka wakati wa kuanguka kwa mwanadamu katika bustani ya edeni. Huyu mwokozi ambaye angekuwa mfalme, atakuja kupitia uzao wa Daudi. Hii ilionyesha neema ya mungu kwa Daudi, Israeli, na mataifa yote duniani.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?).**
  - Mungu alimwahidi Daudi kwamba mwanawe angejenga hekalu.
  - Mungu alimwahidi Daudi kwamba mwanawe atakuwa kwenye kiti cha enzi.
  - Mungu alikuwa angali mwaminifu kwa Israeli kuleta mwokozi aliyeahidiwa Zamani katika bustani ya Edeni na tena kwa Abrahamu. Hapa anaahidi kuleta mwokozi huyo, mfalme, kupitia uzao wa Daudi.
  - Mungu aliahidi kwamba Daudi atakuwa mfalme,miaka kumi na mitano kabla ya kutimia lakini alitimiza ahadi yake na kumlinda Daudi kutoka kwa hatari ya Goliathi na Sauli.

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
  - Daudi, aliyekuwa mtu aliyependeza moyo wa Mungu, na aliyeandika zaburi za kumwabudu Mungu na aliyetumikia Mungu, aliweza kufanya dhambi kuu kama kutamani, na kuzini, na kuua kwa kudhamiria na hata kutamani.
  - Wafilisti, maadui wa Mungu, walikuwa waovu, wasiomcha mungu na waabuduo sanamu.
- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
  - Waisraeli hawangeweza kujiokoa kutoka kwa wafilisti, lakini mungu alimleta Daudi kuwakomboa.
  - Daudi hangeweza kumshinda Goliathi lakini mungu alimsaidia.
  - Daudi alikuwa na hali ngumu na Bathisheba, alipatikana lakini mungu akamsamehe.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa?
  - Daudi alitembea kwa imani, akimtumainia mwokozi kumsamehe na kumsaidia.
  - Daudi alipotubu mungu alimsamehe.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Mfalme Daudi alikuwa mfano au picha ya Mfalme mkuu Yesu ambaye angekuja kuwa Mwokozi wetu!
  - Je,tunawezaje kupeleka ujumbe huu wa Mfalme Yesu kwa watu wa jumuiya zetu ambao wanahitaji Mfalme wa kweli?
  - Je, ni kwa njia gani sisi kama kanisa tunaweza kunyenyekea zaidi kwa utawala wa Kristo?

- Je, wakati mwingine **tunahisi kana kwamba Mungu hawezi kututumia kwa sababu tuko wadhaifu sana au wadogo au tumetenda dhambi sana?** Mungu anataka kukufunza nini katika hadithi hii?

- **Tazama Zaburi 32:1-2** uone jinsi kutotubu dhambi kunavyotuathiri. Ikiwa Mungu anajua mambo yote, inatuathiri vipi tunapogundua ya kwamba kuna dhambi ambazo tunamficha Mungu na watu wengine?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Je? Ni matatizo gani katika maisha yako ambayo unahisi kwamba huwezi kuyashinda kwa sababu yanakaa kama jitu?** Je, ni jinsi gani kumwamini Yesu, ambaye ni Mwokozi Mungu amepeana, itakusaidia kukabiliana na matatizo haya?
- Je, ni dhambi gani ambayo hujaungama unahitaji ili kumjulisha Mungu na marafiki wenye upendo?
- Je, ni sehemu gani ya maisha yako ambayo unahitaji kutiisha kwa utawala wa Kristo kwa imani?

## 25. ELIYA NA MANABII WA BAALI
## 1 Wafalme 18

Eliya alikuwa nabii mkuu ambaye Mungu alimtuma kwa ufalme wa kaskazini wa Israeli katika siku za mfalme mwovu, aliyekuwa akiabudu sanamu, jina lake, Ahabu. Kwa sababu ya dhambi ya Israeli, Eliya alitabiri ukame, na Mungu akasimamisha mvua yote kwa miaka mitatu. Wakati huo Eliya alijificha mbele ya Ahabu. Mwishoni mwa miaka mitatu bila mvua, Eliya alijitokeza tena na kujionyesha kwa Mfalme Ahabu.

Ahabu akamwona Eliya akasema, Je ni wewe ewe mtaabishaji wa Israeli? Eliya akajibu, sio mimi niliyewataabisha Israeli, bali ni wewe na nyumba ya baba yako kwa kuwa mumeziacha amri za Bwana, na kuabudu sanamu Baali. Kisha Eliya akasema, "Wakusanyeni Israeli wote kwenye Mlima Karmeli, nasi tutaona ni nani aliye Mungu wa kweli, Yehova au Baali.

Katika siku iliyochaguliwa, Mfalme Ahabu alikuwa huko na manabii mia nne na hamsini wa Baali. Na Israeli wote wakakusanyika katika Mlima Karmeli. Eliya alisimama peke yake kwa ajili ya Bwana. Eliya akawaambia watu, "Acha nitoe dhabihu bila moto. Hebu manabii mia nne wa Baali pia watoe dhabihu bila moto. Mungu atakayejibu kwa moto ndiye Mungu wa kweli." Watu wote wakasema, "Ndiyo! Huo ni mpango mzuri!"

Basi, asabuhi iliyofuata, manabii mia nne wa Baali waliomba, "O Baali! Utusikie! Uutume moto!" Walilia mpaka adhuhuri na hakukuwa na chochote kilichofanyika. Saa sita, Eliya aliwadhihaki akasema, "Pengine Baali analala! Au labda alisafiri. Pazeni sauti!" Basi manabii wa Baali walianza kuruka na kucheza ngoma na kupiga kelele hata kujikata wenyewe kwa visu mpaka damu ikamwagika. "O Baali! Tusikie! Tuma moto!" Oh Baali!, Tuskie! Tuma moto! Lakini, jioni ilipofika, bado hakukuwa na chochote kilichofanyika.

Kisha Eliya akasema, "Tosha! Sasa ni wakati wangu!" Eliya akajenga madhabahu kwa Bwana kwa kutumia mawe kumi na mawili. Akamchinja fahali na kumweka juu ya madhabahu. Kisha akachimba mtaro kuzunguka madhabahu na akawafanya wanaume kuchukua mitungi kumi na miwili ya maji na kumwagilia dhabihu hadi yakamwagika na kujaza mtaro. Basi Eliya akaomba akisema, "Ee, Mungu. Jionyeshe wewe ndiwe Mungu nami ni mtumishi wako." Punde si punde, moto ukashuka kutoka mbinguni na ukachoma dhabihu kabisa pamoja na kuni na hata mawe na maji.

Kisha watu wote wakashangilia, "Bwana ni Mungu!" "Bwana ni Mungu!" Kisha Eliya akasema, "Wachukue manabii wa Baali na kuwaua. Baada ya jambo hili, Mungu alileta mvua tena.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Sanamu ni nini?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu alifanya mvua kukosa kwa miaka mitatu. Ana mamlaka juu ya uumbaji wake.
    - Mungu alimlinda Eliya kutoka kwa Ahabu.
    - Mungu aliteketeza dhabihu, pamoja na mawe na maji, punde si punde.
    - Mungu alionyesha uwezo wake kwa kujibu maombi ya mtu mmoja wa imani dhidi ya watu 400 ambao walikuwa wakiomba sanamu iliyokufa.
    - Mungu alikuwa na mamlaka ya kudai utakatifu kutoka kwa watu wake.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali?**
    - Mungu alijua kwamba kutakuwa na kiangazi kikuu na kitaisha baada ya miaka mitatu.
    - Mungu alijua kitakachofanyika kwa dhabihu na manabii wa baali.
    - Tofauti sana na Mungu wa uongo, baali, Mungu wa kweli halali au kuenda popote ili kwamba asiweze kuona au kujua kila kitu ambacho kinafanyika katika maisha ya watu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Mungu aliadhibu Ahabu na Israeli kwa kuleta kiangazi kwa sababu ya kupotoka na kuabudu sanamu.
    - Mungu alionyesha utakatifu wake kwa kuteketeza dhabihu yote.
    - Aliadhibu manabii wa baali kwa kuagiza wauwawe.
    - Alikataa kujibu maombi ya waliopotoka na kuabudu sanamu.
    - Utakatifu wa mungu unaonekana katika hitaji la dhabihu ya kuondoa dhambi ili mwanadamu aweze kuja mbele za Mungu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu aliongea na Eliya na kupitia kwake kwa watu na mfalme.
    - Mungu aliwapa waisraeli nafasi ya kutubu kwa kuabudu baali.
    - Mungu alionyesha uwezo wake kwa watu kwa kuwasaidia ili wamrudie.
    - Mungu alimlinda Eliya hata ingawa yeye mwenyewe alikuwa mwenye dhambi.
    - Mungu alijibu ombi la imani la Eliya.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?).**
    - Eliya alitabiri kiangazi kama mungu alivyomwambia na ikafanyika.
    - Mungu alikuwa mwaminifu kumlinda Nabii wake.
    - Alikuwa mwaminifu pia kujionyesha mtakatifu kwa taifa la Israeli.

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
  - Kwa wazi mungu amekuwa akitumia kiangazi kuadhibu Israeli kwa kupotoka kwao na kuabudu sanamu.
  - Manabii wa baali walikufa kwa sababu ya kupotoka kwao.
  - Ahabu alijaribu kumlaumu Eliya kwa sababu ya kiangazi badala ya kuabudu kwake kwa sanamu hasa yeye kama kiongozi.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
  - Waisraeli hawangejiokoa kutoka kwa kiangazi. Ni Mungu tu, katika wakati wake angeleta mvua.
  - Eliya hangeweza mwenyewe kujilida kutoka kwa Ahabu.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- **Hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
  - Mungu alichukia ibada ya sanamu. Watu kamwe hawangemjia mungu katika njia hiyo. Wangemjia tu katika njia yake. Kutubu dhambi na kuweka imani ndani ya mwokozi atakayekuja.
  - Eliya alifanya alivyoamriwa na mungu,na akawasilisha mungu kwa watu kama vile mungu alivyotaka.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.**
  - Katika hadithi hii ukosefu wa Imani na toba wa Ahabu ulileta mateso mengi miongoni mwa wayahudi.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Je, ni mambo gani katika maisha yetu yanayoweza kuonekana kama miaka mitatu ya kiangazi?

- Ikiwa Mungu bado ana nguvu leo na anatawala juu ya uumbaji wake mwenyewe, hiyo inasema nini kuhusu jinsi anavyokujali nyakati za ugumu?

- Ahabu na manabii wa Baali waiweka tumaini lao kwa miungu wa uwongo. Je, nini tunajaribiwa kuweka tumaini letu badala ya kumtumaini Mungu?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je, kuna ukame gani katika maisha yako?** Ni mapambano gani ya muda mrefu unayojaribu kuvumilia? Je! hadithi hii inawezaje kukutia moyo? Omba Bwana akusaidie na akupe nguvu.

- Ni nguvu gani moyoni mwako zinashindana na Mungu kwa utawala wa maisha yako? Unaamini nini badala ya Mungu kukuokoa?

## 26. MANABII WANATABIRI KUJA KWA MWOKOZI ALIYEAHIDIWA NA AGANO JIPYA

Manabii walionya watu wa Mungu kuhusu hukumu kwa dhambi zao, lakini pia waliwaambia kuhusu huruma na msamaha wa Mungu kwa watu waliotubu na kumwamini. Waliwakumbusha kuhusu Mwokozi ambaye Mungu aliyekuwa amehidi zamani. Walisema, "Kuna Mmoja ambaye anakuja kuwaokoa kutoka kwenye dhambi zenu."

Nabii Isaya alisema kwa Wayahudi, "Bwana mwenyewe atakupa ishara: bikira atamzaa mwana. Atamwita Immanueli, maana yake 'Mungu pamoja nasi.' Ataitwa Mfalme wa Amani. Enzi yake haitakuwa na mwisho kamwe." Pia alitabiri kuhusu Mwokozi huyu kama mtumishi, kwamba atateseka na kudharauliwa, ambaye ataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini manabii walitabiri kwamba Mwokozi atafufuka. Na pia walitabiri vitu vinginevyo ambavyo vitamfanyikia Mwokozi. Kwa mfano, Mikono na miguu kudungika, kuuzwa kwa shilingi thelathini, kusalitiwa na rafiki, kuhesabiwa pamoja na wenye dhambi, n.k.

Manabii waliongea kuhusu Agano Jipya ambalo lingetimilia katika Mwokozi aliyeahidiwa. Mungu alisema kupitia nabii Yeremia, "Watu wangu walivunja agano langu lakini nitafanya agano jipya nao. Nitawatoa katika utumwa. Nitaweka sheria yangu katika akili zao na kuiandika kwa mioyo yao. Nitakuwa Mungu wao na watakuwa watu wangu."

Mungu alimwambia nabii Ezekieli pia kitu kama hicho akisema, "Nitawapatia moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu. Nitaondoa kutoka kwenu moyo wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama . Nitaweka Roho wangu ndani yenu na kuwafanya kufuata maagizo yangu na kuwa waangalifu kutii amri zangu.

Baada ya watu wa Mungu kurudi Yerusalemu kutoka utumwani Babiloni, na baada ya kujenga Yerusalemu na hekalu, Mungu alisimama kuongea kupitia manabii kwa miaka mia nne. Lakini katika wakati huo wa mateso, bado Wayahudi wengine walikumbuka ahadi za Mungu kuwaletea Mwokozi.

**Baadhi ya Unabii wa Agano la Kale**
**kuhusu Mwokozi Ambaye Angekuja**

| Ushairi wa Ahadi | Unabii | Ushairi wa Kutimiza |
|---|---|---|
| Isaya 9:7 | Atarithi kiti cha enzi cha daudi | Mathayo 1:1 |
| Mika 5:2 | Pahali pa kuzaliwa kwake | Mathayo 2:1 |
| Danieli 9:25 | Mzaliwa atakapozaliwa | Luka 2:1-2 |
| Isaya 7:14 | Nani atakayemzaa | Mathayo 1:18 |
| Yeremiah 31:15 | Watoto wengi watauwawa | Mathayo 2:16 |

| | | |
|---|---|---|
| Hosea 11:1 | Kutoroka kwake hadi Misri | Mathayo 2:14 |
| Isaya 9:1-2 | Kazi yake katika Galilaya | Mathayo 4:12-16 |
| Zaburi 110:4 | Yeye ni kuhani kama Melkizedeki | Waebrania 6:20 |
| Isaya 53:3 | Atakataliwa na Waisraeli | Yohana 1:11 |
| Isaya 11:2 | Baadhi ya tabia zake | Luka 2:52 |
| Zakaria 9:9 | Anakuja katika Yerusalemu | Mathayo 21:1-11 |
| Zaburi 41:9 | Alisalitiwa na rafiki | Marko 14:10 |
| Zakaria 11:12-13 | Vipande thelathini vya fedha vililipwa | Mathayo 26:15 |
| Zaburi 27:12 | Mashahidi wa uwongo walimshtaki | Mathayo 26:59-62 |
| Isaya 53:7 | Alinyamaza aliposhtakiwa | Mathayo 26:62-63 |
| Isaya 50:6 | Alipigwa na kutemewa mate | Marko 14:65 |
| Zaburi 69:4 | Alichukiwa bila sababu | Yohana 15:23-25 |
| Isaya 53:4-5 | Aliumia kwa ajili ya wengine | Mathayo 8:16-17 |
| Isaya 53:12 | Alisulubishwa kati ya wenye dhambi | Mathayo 27:38 |
| Zaburi 22:16 & Zakaria 12:10 | Mikono yake na miguu ilidungwa | Yohana 20:25-27 & Yohana 19:37 |
| Zaburi 22:6-8 | Alithihakiwa na kutukanwa | Mathayo 27:39-44 |
| Zaburi 69:21 | Alipewa siki kunywa | Yohana 19:29 |
| Isaya 53:12 | Anawaombea maadui wake | Luka 24:34 |
| Zaburi 22:18 | Walilichezea kamari vazi lake | Marko 15:24 |
| Zaburi 16:10 | Anafufuka kutoka kwenye wafu | Luka 24:1-8 |
| Zaburi 68:18 | Anapaa Mbinguni | Luka 24:50-51 |
| Mwanzo 12:3 | Kupitia kwake makuja Baraka aliyoahidiwa Abrahamu | Wagalatia 3:14-29 |

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, kuna kitu ambacho unatamani sana katika maisha yako ambacho umekingoja kwa muda mrefu na bado unakisubiria? Mwambie jirani yako kuhusu hilo.**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana.**

- **Je, kazi ya manabii ilikuwa ipi?**
    - Kuonya dhidi ya hukumu. Kuelezea kuhusu huruma ya Mungu.
    - Kuwakumbusha kuhusu Mwokozi atakayekuja na vile atakavyokuwa, na kile atakachokifanya?

- **Je tunaona waaminifu wa Mungu vipi katika hadithi hii? Au. Ni ahadi zipi muhimu kutoka kwa manabii kuhusu Mwokozi?**
    - Kutoka kwa Isaya:
        - Atazaliwa na Bikira.

        - Ataitwa Emanueli, mungu pamoja nasi.
        - Mfalme wa amani, atakayeleta amani.
        - Ufalme wake hautakuwa na kikomo.
        - Atakuwa kama kondoo kafara..
        - Ata teseka bila kulipisha kisasi .
        - Atakufa ili kulipia dhambi zetu.
    - Kutoka kwa manabii wengine:
        - Atafufuliwa.
        - Atatoka bethlehemu.
        - Mikono a miguu yake yata tobolewa.
        - Atasalitiwa kwa peni thalathini za fedha.
        - Atasalitiwa na rafiki yake.
        - Atasulubiwa kati ya wenye dhambi.
        - Vazi lake litapigiwa kura.
    - Je, kutoka Ezekieli na Yeremia Agano Jipya ni nini? Linaonyeshaje uaminifu wa Mungu?
        - Atabadilisha mioyo na fikra zao, lengo lake likiwa maisha ya ndani.
        - Atakuwa mungu wao, nao watakuwa watu wake.
        - Atawapatia Moyo mpya wa nyama abadilishe ule wa jiwe.
        - Atawaptia Roho Mtakatifu ili kuwasaidia kufuata sheria.

- **Baadhi ya wayahudi walimsubiri kwa hamu Mwokozi aliye kwa ameahidiwa! (kwa mfano Simioni na Anna) Je, ahadi hizi zingewasaidiaje wana wa Israeli kutengeneza imani yao?**

- **Ukifikiria mbele na utizame again jipya, je, ahadi hizi zilitimizwa kivipi?**

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Mungu ni mdumisha ahadi. Mungu alitoa ahadi nyingine nyingi katika Maandiko kwa wale wanaomtumaini.
    - Ni zipi baadhi ya ahadi hizo? Tengeneza orodha ya ahadi hizi.

- Tutaona katika hadithi za Agano Jipya kwamba Mungu alitimiza unabii huu wote. Hilo linakusaidiaje jinsi unavyoitazama Biblia, hasa kuhusu kuaminika kwayo? Ikiwa Neno la Mungu linaaminika, hilo linapasa kuathiri maisha yako vipi?

- Wale Wayahudi waliomtumaini Mungu kwa kweli walikuwa wakingoja kwa kutazamia na kwa subira siku ambayo Mwokozi angekuja. Iliwapa matumaini. Je, tunaweza kupata wapi tumaini la maisha haya na yajayo?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Je, ni ahadi gani ya Mungu ambayo hasa ni ngumu kwako kuamini leo?** Je, ni wapi kuna ugumu wa kuwa na tumaini? Je, unahitaji kutubu kwa sababu ya kutoamini? Hii hadithi itakuhimiza moyo vipi siku ya leo?

- Mungu alitumia watu au manabii kunena neno lake kwa watu waliokuwa uhamishoni? Unawezaje kutumiwa na Mungu kunena ukweli Wake kwa wengine? **Je,ni nani utaenda kuambia huu ujumbe wa Mungu wiki hii?**

## 27. TANGAZO NA KUZALIWA KWA YESU
## Luka 1:5 - 2:20

Kwa zaidi ya miaka mia nne Mungu hakuongea na Wayahudi kupitia manabii. Kulikuwa kimya kabisa. Pia, Wayahudi walitawaliwa na ufalme wa Rumi. Basi siku moja, Mungu aliongea tena! Alimtuma malaika aliyeitwa Gabrieli kuongea na Zakaria, mmoja wa makuhani hekaluni. Akamwambia kwamba mke wake Elisabeti angemzaa mwana ambaye angetangaza kuja kwa Mwokozi aliyeahidiwa. Zakaria hakuamini kwa sababu yeye na mke wake walikuwa wakongwe na hawakuwa na mtoto. Mungu akamfanya Zakaria kuwa bubu hadi baada ya kuzaliwa kwa mwanawe.. Lakini Mungu alifanya alivyosema. Elisabeti alimzaa mtoto aliyeitwa Yohana. Yeye ndiye alikuwa Mhubiri jangwani kutangaza kuja kwa Mwokozi.

Miezi sita baada ya Malaika Gabrieli kuongea na Zakaria, Mungu alimtuma malaika wake Gabrieli katika mji wa Nazareti, katika nyumba ya bikira aliyeitwa Mariamu. Mariamu alikuwa ameahidiwa ndoa na mwanamume aliyeitwa Yusufu aliyekuwa wa jamaa ya Daudi."

Malaika Gabrieli alimwambia Mariamu, "Salamu kwako, uliyebarikiwa na Mungu. Mariamu alichanganyikiwa na kuogopa. Gabrieli akamwambia, "Mungu amekubariki kwa maana utamzaa mwana. Utamwita Yesu. Atakuwa mkuu, naye ataitwa Mwana wa Aliye Mkuu Zaidi. Mungu atampa kiti cha enzi cha babake Daudi naye atatawala juu ya Israeli na Yuda milele.

Yusufu, mchumba wa Mariamu alikuwa mtu wa haki. Alipotambua kwamba Mariamu alikuwa na mimba, hakutaka kumtia aibu mbele ya watu, kwa hivyo alipanga kuvunja ile posa na kumpa talaka katika njia ya siri. Alipokuwa akififikiria kuhusu jambo hilo, malaika wa Bwana alimjia katika ndoto. "Yusufu, mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Mariamu awe mke wako. Mimba aliyo nayo ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu wa Mungu. Atajifungua Mwana nawe utamwita Yesu maana yake "Bwana anaokoa," kwa sababu atawaokoa watu wake kutoka kwa dhambi zao. Yusufu alipoamka kutoka kwa ndoto yake, alimchukua Mariamu kama mkewe akampeleka nyumbani lakini hakulala naye hadi alipojifungua.

Miezi sita baada ya Elisabeti kujifungua, Mariamu alikuwa tayari kujifungua pia. Wakati huo, mfalme wa Urumi alitoa amri kwamba kila mtu anapaswa kurudi katika mji wa jamaa yao, ili kuhesabiwa kwa lengo la ushuru. Yusufu alitoka katika nyumba ya Daudi. Kwa hivyo alirudi Bethlehemu ya Yuda ili kuhesabiwa pamoja na Mariamu, mkewe aliyemposa, aliyetarajia mtoto.

Watu wengi walikuwa wanasafiri ili wahesabiwe kwa hivyo hawakupata pahali pa kukaa katika Bethlehemu. Kwa hivyo walipata pahali pa wanyama. Walipokuwa hapo,

Mariamu alijifungua mtoto wa kiume akamfunga katika nguo za kitoto na kumlaza katika hori ya kulisha ng'ombe.

Karibu na hapo, kulikuwa na wachungaji wakichunga wanyama wao usiku. Punde, malaika akawatokea, na utukufu wa Bwana ukawaangazia, nao wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akawaambia, "Msiogope. Nawaletea habari njema yenye furaha kuu kwa watu wote. Katika mji wa Daudi, Mwokozi amezaliwa kwenu ambaye ni Kristo Bwana. Hii itakuwa ishara kwenu kumtambua. Mtapata mtoto amefungwa katika nguo za kitoto na amelazwa katika hori ya kulisha ng'ombe." Halafu, jeshi la malaika likatokea na kuimba, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia."

Malaika walipotoweka, wachungaji waliambiana, "Twendeni Bethlehemu na tuone jambo hili ambalo Bwana alilotujulisha." Kwa hivyo walienda kwa haraka wakampata Yusufu, Mariamu, na mtoto aliyelala katika hori.

Baada ya kuona Yesu, wachungaji walirudi wakimtukuza na kumsifu Mungu kwa mambo yote walikuwa wameyasikia na kuyaona na wakaeneza neno hilo kila pahali kuhusu walichoona na kusikia. Na kila mtu aliyesikia habari hii alistaajabu.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Ni wakati gani umejiweka katika nafasi isiyo ya maana, ya chini ili kuwasaidia wengine katika maisha yako?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu alitumia amri ya Kaisare kumpeleka Mariamu Bethlemu, pahali ambapo nabii alikuwa amesema Mwokozi angezaliwa Mungu aliguza ulimwengu mzima kwa sababu ya mwanamke mmoja mjamzito.
    - Mungu alimsaidia Maria kujifungua Mwana wake hata katika zizi chafu.
    - Mungu aliwatuma maliaka kutangaza kuzaliwa kwa Mwokozi.
    - Mungu alipeana zizi na ori ili kumlinda na kumtunza motto mchanga Yesu.
    - Alituma malaika kutangaza kuzaliwa kwa Mwokozi na akachagua kwanza kutangaza habari njema kwa wachungaji maskini.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu?**
    - Mungu alijua wakati na pahali Mwokozi angezaliwa. Alijua watu ambao angetumia kumleta Mwokozi.
    - Mungu alijua mioyo ya wachungaji na kwamba wangeeneza habari.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Utukufu wa Mungu na utakatifu wake ulionekana katika malaika.
    - Wachungaji walihofu sana kwa sababu walikabiliana na ukuu na utakatifu wa Mungu.
    - Kwa sababu Mungu ni mtakatifu na mwanadamu ni mwenye dhambi, tulihitaji Mwokozi.
    - Yesu alizaliwa na bikira. Baba yake alikuwa Mungu katika Roho Mtakatifu, siyo mwanamume. Kwa hivyo hakuzaliwa katika dhambi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu alikuja "kuwa nasi." Alikuja katika ulimwengu wetu mchafu, wenye dhambi na ulioharibika.
    - Mungu aliwafikia watu kupitia kwa watu wa chini sana katika jamii – wachungaji, seremala, mscihana maskini.
    - Alizaliwa katika hori, alizaliwa kumpenda mtu wa kawaida.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?).**
    - Mungu alitimiza ahadi yake ya kumleta Mwokozi.
    - Mungu alisema Mwokozi angezaliwa katika Bethlemu.
    - Alisema angezaliwa na bikira.
    - Mungu alisema kwamba Mwokozi angezaliwa kupitia uzao wa Daudi.

<u>**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**</u>

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu?**
    - Mwanadamu alipendwa na Mungu. Mungu alimtuma mwana wake wa pekee kutusaidia.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Ndiyo, kwa sababu alihitaji Mwokozi.
    - Wachungaji waliogopa kwa utuukufu wa Mungu na hali yao ya dhambi ya kuwa karibu na utukufu wa Mungu.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?**
    - Mwanadamu hangejifanyia njia yake mwenyewe. Ni Mungu tu angeweza kumtuma Mwokozi.

<u>**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**</u>

- **Hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Wokovu hutoka kwa Mungu tu. Mwokozi ambaye Mungu alitupatia ni njia pekee ya kuokoka.

<u>**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**</u>

- Soma Wafilipi 2:5-8. Yesu ni Mwana wa Mungu. Alijishusha kutoka kwa nafasi yake ya usawa na Mungu ili aweze kuingia katika ulimwengu wetu kwa njia ya unyenyekevu ili ashiriki nasi katika udhaifu wetu wote. Tuna udhaifu, sehemu chafu zilizofichikia mioyoni na maishani mwetu. Je, tunawezaje kumruhusu vipi Yesu kikamilifu katika sehemu hizo?

- Yesu alizaliwa katikati ya watu wa chini sana na mahali pa chini sana, alizaliwa katika udhaifu. Je hili linawezaje kuwa himizo kwetu katika maisha yetu ya kila siku?

- "Msiogope! Kwa maana nawaletea habari njema ya ya furaha kuu kwa watu wote. . . Mwokozi amezaliwa kwenu. . ." Ni jinsi gani tunafaa kupokea habari hizi kuu?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- Fikiria wakati mmoja ulipohisi ya kwamba Mungu hakuelewi au hakujali kwa sababu wewe sio wa maana. Hadithi hii inaweza kukuhimiza vipi?
- **Yesu anataka ukubali kwamba unahitaji msaada wake! Unawezaje kumruhusu Mwokozi kuja katika sehemu duni, chafu katika moyo wako au maishani mwako? Hiyo ingeonekanaje?** Je, umeitikiaje kwa Mwokozi huyu ambaye Mungu alituma? Ikiwa bado hujatubu dhambi zako na kuweka tumaini lako kwa Kristo, ni nini kinachokuzuia kufanya hivyo leo?
- "Usiogope!. . . Mwokozi amezaliwa kwenu . . !" Je, unaipokeaje binafsi habari hii njema leo?

# 28-A. YOHANA MBATIZAJI ATAYARISHA NJIA; UBATIZO WA YESU
## Yohana 1:19-31, Mathayo 3

Hii ni hadithi ya ushuhuda wa Yohana kuhusu Kristo. Yohana alipokua akawa mwanamume, alijionyesha kwa waIsraeli jangwani. Basi Yohana alivaa mavazi yaliotengenezwa kwa singa na ngozi ya ngamia. Chakula chake kilikuwa ni nzige na asali ya mwitu. Alikuja akihubiri, "Tubuni! Kwa maana ufalme wa Mungu umekaribia!" Na wale waliotungama dhambi zao walibatizwa katika mto wa Yordani.

Na sasa watu wengi walikuwa wakimwendea kutoka Yerusalemu na Uyahudi ili kumsikia akiongea na pia kubatizwa. Lakini Makuhani wakuu na walimu wa sheria, yaani viongozi wa Israeli, walibaki katika Yerusalemu na kuwatuma wajumbe wao kwa Yohana. Wajumbe hao waliuliza, "Je, wewe ndiwe Kristo?" Yohana alisema, "Mimi siye." Wakauliza, "Je, wewe ni Eliya?" Yohana alisema, "La." "Wakauliza, basi wewe ni nani?" Yohana alisema, "Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, 'Tayarisheni njia ya Bwana.' Kuna yule ajaye baada yangu, ambaye ni mkuu kuliko mimi, kwa sababu alikuweko kabla yangu."

Wakati huo, Yesu pia akaja ili naye abatizwe na Yohana. Alipotoka ndani ya maji, Roho Mtakatifu akashuka kama hua na kutulia juu yake. Nazo mbingu zikafunguka na sauti ikatoka juu mbinguni, ikisema, "Huyu ndiye mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye."

Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu akitembea katikati ya makutano na akasema, "Tazameni! Mwana kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu! Huyu ndiye nilikuwa nikiwaambieni niliposema, "Kuna mmoja ajaye baada yangu, ambaye ni mkuu kuniliko mimi kwa sababu alikuweko kabla yangu!"

**<u>MPANGILIO wa SOMO</u>**

**<u>UTANGULIZI:</u>** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, ni mambo gani katika moyo wako na maisha ambayo unatafuta zaidi? Je, ni maeneo gani ya jangwa katika maisha yako?**

**<u>HADITHI:</u>** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**<u>MJADALA baada ya HADITHI:</u>** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**<u>Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Roho Mtakatifu aliwavuta watu kuenda jangwani kumsikiliza Yohana Mbatizaji.
    - Yohana anasema kwamba Yule ajaje angekuwa mkuu kuliko yeye mwenyewel

    - Mungu anafungua mbingu na kumtuma Roho  Mtakatifu kama njiwa.
    - Mungu alimtangaza Yesu kuwa Mwana wake. Kuwa wa uungu alimtangaza pia kuwa anayependezwa naye. Ni Mungu pekee ambaye ana uwezo wa kutangaza kile ambacho ni kizuri.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu?**
    - Mungu alijua na kupanga jinsi Yohana angetangaza kuja kwa Yesu.
    - Mungu alijua na kutangaza kwamba Yesu alikuwa nani.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu?  (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
    - Mungu alimtenga Yohana Mbatizaji kwa kazi maalum takatifu ya kuandaa njia kwa ajili ya Yesu.
    - Yohana aliwauliza watu kuzitubu dhambi zao, kama kusafishwa kiroho kupitia kwa ubatizo.
    - Yesu alikuwa mkuu kuliko Yohana. Kwa sababu Yohana alikuwa mwenye dhambi, na Yesu alikuwa Mungu Mtakatifu, Yohana hakustahili kuvishika viatu vyake.
    - Mungu alimtangaza Yesu kuwa Mtakatifu kwa kuzifungua mbingu na kumtuma Roho Mtakatifu kama njiwa, na kutangaza kwamba Yesu alikuwa “Mwanawe mpendwa, ambaye alipendezwa naye.”
    - Yohana alisema, “Tazama Mwana Kondoo wa Mungu ambaye anazichukua dhambi za ulimwengu alikuwa anaunganisha Yesu na dhabihu za kondoo za Agano la kale – hasa kondoo wa pasaka. Kondoo huyo alipaswa kuwa bila waa, awe kamilifu na damu yake ingefunika dhambi za watu kuwalinda kutoka kwa ghadhabu takatifu ya Mungu.
    - Kwa maana Yesu ni Mwana wa Mungu, tabia zote za Mungu zinapatikana kwa Yesu pia.
    - Yesu alikuwa mwenye haki. Kwa hivyo alisimama na watu wenye haki hata ingawa yeye mwenyewe hakuwa na dhambi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema?  (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Mungu aliongea na watu kupitia kwa Yohana.
    - Mungu alimtunza Yohana jangwani.
    - Yohana alipohubiri, Mungu alibadilisha mioyo ya watu na kuwaongoza kutubu dhambi zao na kubatizwa.
    - Mungu aliwapa watu muda wa kuisikia injili na kutubu.
    - Yesu, Mwana wa Mungu, alijinyenyekesha akaja ulimwenguni kama mtu na kuishi pamoja nasi. Alikuwa “Mungu pamoja nasi.”
    - Yesu alikuwa “Mwana kondoo wa Mungu aliyekuja kuzichukua dhambi za ulimwengu.” Hii inatukumbusha neema ya Mungu kwa Waisraeli wakati wa pasaka, na hata mtindo wote wa kutoa dhabihu wa agano la kale ambapo watu walimleta kondoo kamilifu kama sadaka kwa niaba ya dhambi zao. Yesu angekuwa Mwanakondoo wa mwisho, dhabihu ya mwisho.
    - **Je, ni hadithi gani unazoweza kukumbuka ambazo tumezifanya katika Agano la Kale zinazozungumza kuhusu mwana-kondoo aondoaye dhambi?
    - Yesu alijitambulisha na mwanadamu mwenye dhambi kwa kubatizwa, ingawa hakuwa na dhambi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu?  (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?).**
    - Mungu aliahidi kupitia kwa Isaya mamia ya miaka kabla ya Yesu kuja kwamba angekuja mmoja ambaye angekuwa “sauti iliayo nyikani, itayarisheni njia ya Bwana.” Yohana Mbatizaji alitimiza ahadi hiyo.
    - Mungu alisema kupitia kwa Yohana kwamba angekuja mmoja ambaye angekuwa mkuu kuliko yeye.  Huyo alikuwa Yesu.
    - Yesu alikuwa timizo la mwisho la mwana kondoo katika agano la kale – mwana kondoo wa Pasaka, mwana kondoo ambaye Habili alimtoa kama dhabihu, mnyama ambaye aliuwawa kupata nguo kwa Adamu na Hawa baada ya kutenda dhambi, na kila aina nyingine ya dhabihu wa kondoo angekuwa dhabihu kwa niaba ya adhabu ya kifo.

    - Mungu aliahidi katika Bustani ya Edeni alipomlaani nyoka kwamba siku moja Uzao wa Mwanamke ungemshinda Shetani milele Yesu alizaliwa na Mwanamke alikuwa uzao huo. Alikuwa Mwokozi aliyeahidiwa.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi yake?**
    - Yohana alikuwa akiwaita wenye dhambi kutubu ili kujitayarisha kwa kuja kwa ufalme wa Mungu.

- **Hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu? (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Njia ya pekee ya kusamehewa dhambi ingekuwa kupitia kwa Yesu, Mwana Kondoo wa Mungu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.**
    - Yohana aliwatayarisha watu kumpokea Yesu kwa kuwaambia watubu. Na walikuwa wakibatizwa, kama kielelezo cha kusafishwa kiroho ambako Mungu alikuwa akifanya katika mioyo yao.
    - Yonana alisema, "Tazameni, Mwana Kondoo wa Mungu ambaye anazichukua dhambi za ulimwengu! Alikuwa akiwahimiza watu kuweka imani yao ndani ya Yesu.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Watu wakaenda nyikani wakimtafuta Yohana. Ni mamboya aina gani watu huenda kutafuta au kutamani? Je, ni maeneo gani tupu na jangwa maishani mwa watu?

- Wakati watu walipoisikia Yesu akiitwa "Mwana Kondoo wa Mungu", wangefikiria kuhusu dhabihu za agano la kale kama pasaka na kondoo dume ambaye Ibrahimu alimchukua kutoka kwa kichaka.Pia wangekumbuka kuhusu mtumishi aliyeteswa katika Isaya 53. Wangefikiria kuhusu dhabihu iliyokufa kwa niaba yao kulipa dhambi zao. Je, ni dhambi aina gani katika maishani ya watu leo ambazo Kristo alilipa kwa kifo chake.

- Waisraeli walikuwa wamesubiri kwa muda wa maelfu ya miaka kutimilika kwa ahadi ya Mwokozi aliyeahidiwa. Je ni katika hali gani ambapo unaangaika kumngoja Mungu, unahisi amechukua muda mrefu sana .

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- Watu walienda nyikani kumtafuta Yohana. Je, ni **mambo gani** moyoni mwako ambayo wewe **huenda kule nje kuyatafuta?** Je ni sehemu gani ambazo ni tupu maishani mwako? Yesu anaweza kukujaza vipi hiyo sehemu.

- Yesu ni Mwanakondoo wa Mungu, ambaye amekuja kuchukua dhambi za ulimwengu, pamoja na dhambi zako. Je, ni dhambi fulani gani unahitaji kuleta kwake leo ili usamehewe na kutakaswa?

- Je, wakati mwingine unahangaikaje kumngoja Mungu, kuamini kwamba Mungu anaweza kutimiza kile ambacho amekuahidi? **Ni ahadi gani za Mungu unahitaji zaidi kuamini na zidhihirike kwako?** (Utunzaji wake kwako, msamaha wake kwako, kusikiliza kwa maombi yako, kipawa chake cha Roho mtakatifu au kurudi kwake, nini?)

## 28-B. SHETANI AMJARIBU YESU

**Mathayo 4:1-11, Luka 4:1-13**

Baada ya Yohana kumbatiza Yesu, Roho Mtakatifu, alimwongoza Yesu hadi kwenye jangwa lililoko kati ya Yerusalemu na Yeriko. Alikaa hapo na kufunga kwa siku arobaini na usiku arobaini, shetani alipomjaribu. Hakula chochote na baada ya siku hizo alihisi njaa.

Kisha Shetani akamwambia Yesu, "Ikiwa wewe kwa hakika ni Mwana wa Mungu, aliyepakwa mafuta, thibitisha. Yaamuru mawe haya yabadilike na yawe mikate."

Lakini Yesu akamwambia Shetani, "Maandiko yanasema, 'Mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno linalotoka katika kinywa cha Mungu.'"

Kisha Shetani akamchukua akampeleka Yerusalemu akamsimamisha pahali parefu zaidi pa hekalu, pahali ambapo urefu wake ulikuwa mita mia moja arobaini kufika chini katika bonde la Kidroni. "Ikiwa wewe ndiwe Mwana wa Mungu, Mpakwa mafuta, ebu ruka! Maandiko yanasema, "Mungu ataagiza malaika wake nao watakulinda. Yanasema pia, 'Watakushika kwa mikono yao hata kwamba hutaweza kujikwaa hata mguu wako juu ya jiwe.'"

Lakini Yesu akamjibu, "Maandiko pia yanasema, 'Usimjaribu Bwana Mungu wako.'"

Punde si punde, Shetani akamchukua Yesu tena akampeleka juu ya  mlima na kumwonyesha falme zote za dunia na fahari zake. "Nitakupa mamlaka juu ya falme hizi zote na sifa zake. Zimepewa mimi, nami naweza kumpa yeyote nitakaye. Zote zitakuwa zako. Kile ambacho unapaswa kufanya ni kuinama na kuniabudu mimi."

Ndipo Yesu alijibu kwa mara ya mwisho, "Nenda zako Shetani! Maandiko yanasema, 'Usiabudu mwingine ila Bwana Mungu wako tu.'"

Shetani alipomaliza kumjaribu wakati huo, alimwacha Yesu pekee kwa muda nao malaika wakaja na kumhudumia katika maisha yake. Shetani alimjaribu Yesu kwa kila aina ya dhambi ambayo wanadamu wamewahi kufanya au kufikiri kufanya. Lakini Yesu alilipinga kila jaribu la Shetani kila mara alipomjaribu.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Ni njia gani ambayo umewahi kuhisi majaribu ya Shetani kwa nguvu nyakati fulani maishani mwako?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu YESU?**

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Yesu alikuwa MTU kwa hakika?**
    - Alijaribiwa kwa kweli kama watu wengine.
    - Alihisi njaa.
    - Alihitaji kuomba nakumtegemea Mungu. Alihitaji Roho Mtakatifu kmfariji.
    - Shetani alijaribu kumjaribu katika njia sawa anafanya wanadamu, yaani kupitia tama za mwili, na kiburi, na hata vyeo kati ya watu.

- **Je, kwa nini ilikuwa muhimu kwa Yesu kuwa mwanadamu kamili?**
    - Yesu alipitia majaribu magumu nay a uchungu kufanya dhambi kama wanadamu wengine wote.
    - Yesu anaweza kutusikilia huruma kwa yale tunapitia.
    - Yesu alitegemea utunzi mkuu wa Mungu kumlinda na kumhudumia na malaika.
    - Yesu alikuwa uzao wa Mwanamke, kama vile Mungu aliahidi katika Bustani ya Edeni. Alizaliwa kama mtu.
    - Uzao wa Mwanamke ulipaswa kumshinda shetani. Angebadilisha laana ambalo lilitokea katika bustani kwa kushinda mauti. Hapa katika hadithi hii Yesu anaanza kumshinda Shetani.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba kwa kweli Yesu alikuwa Mungu mwenyewe?**
- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote kama Mungu?**
    - Yesu alikuwa na mamlaka kumkemea na kumpinga Shetani, na kumfukuza.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Yesu anajua kila kitu?**
    - Yesu alimjua Shetani na mipingo yake.
    - Yesu aliyajua maandiko na jinsi ya kutumia neno la Mungu kumpinga Shetani na uwongo wake kwa ukweli.
    - Alionyesha hekima kamili ya Mungu katika njia ambazo alimjibu Shetani.
    - Alimwelewa Shetani na utupu wa uwongo wake.
    - Alijua kwamba ni Mungu tu ambaye alipaswa kuabudiwa.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Yesu ni mtakatifu?**
    - Esu alikuwa mtakatifu. Hakutenda dhambi, hata ingawa alijaribiwa katika njia kuu.
    - Yesu alitumia neno la Bwana katika njia ya takatifu nay a kweli akisema, "Imeandikwa . . ."

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Yesu ni mwenye neema?**
    - Yesu alibakia Mwanakondoo mtakatifu asiye na waa, ambaye agekuwa dhabihu kwa dhambi za ulimwengu.
    - Yesu, kwa neema, alijinyenyekesha, akawa mwanadamu, ili atumikie na kuokoa wanadamu.l
    - Yesu alijitambulisha nasi kama wanadmu kupitia mateso ya kibinadamu na majaribu.

- **Je, hadithi hii inatufundisha nini kuhusu Shetani?**
    - Shetani ni mwongo!

    - Shetani hutumia hata vitu vizuri, kama maandiko, ili kuwadanganya watu wanafuate.
    - Shetani hutumia maandiko, lakini hubadilisha maana akigeuza ukweli kuwa uwongo.
    - Shetani alimjaribu Yesu katika njia sawa na vile aliwajaribu Adamu na Hawa katika Zbustani. Alimjaribu Yesu katika njaa, na katika kiburi cha kiroho, na  hatat katika nafasi yake kama Mwana wa Mungu. Alimjaribu ili aweze kujitawala pekee na kukataa Babake.
    - Shetani anajua sehemu zetu dhaifu. Anajua jinsi ya kutujaribu.
    - Shetani ana ujasiri wa kukumbana na yeyote hata Yesu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu (Mungu) ni mwaminifu?**
    - Yesu ndiye Uzao uliohidiwa Mungu alipolaani nyoka, yaani Shetani, katika Edeni.
    - Yesu alimshinda Shetani kama vile Mungu aliahidi atafanya.
    - Yesu alikuwa Mwaminifu kutumia maandiko. Agano la kale lilikuwa Biblia ya Yesu.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu MWANADAMU na jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa? Kwa njia gani?**
    - Tunaweza kumtumaini Yesu na kumwamini pia. Alijaribiwa lakini hakutenda dhambi.
    - Yesu ni Mungu na anastahili imani na tumaini letu.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Je, ni njia gani ambayo shetani mara nyingi hutumia kuwajaribu watu katika utamaduni wenu na jamii yenu?

- Je, shetani huwajaribuje waumini? Yeye hutujaribu kwa njia gani zinazofanana na jinsi alivyomjaribu Yesu?  Je, hadithi hii inawezaje kutusaidia kusimama dhidi yake tunapojaribiwa?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>**

- **Shetani ametumia njia gani hivi karibuni kujaribu kukudanganya na kuathiri maisha yako?** Je, kuna eneo la udhaifu fulani maishani mwako ambapo shetani hupenda kushambulia?
    - Je, wakati mwingine wewe hujiamini sana kumshinda shetani kwa nguvu zako za kimwili? **Kuzingatia Neno la Mungu kunaweza kukusaidiaje kumtumaini Mungu kikamililfu zaidi badala ya kujitumaini mwenyewe?**

## 29. YESU AKIWAITA WANAFUNZI WAKE

**LUKA 5:1-11, 27-31,6:12-15**

Siku moja yesu akiwa amesimama kando ya ziwa la Galilaya pamoja na watu walio kuwa wamemzunguka wakisikiliza neno la Mungu, aliangalia ufuoni mwa ziwa na aliona mashua mbili, zikiwa zimeachwa na wavuvi wa samaki, wenyewe wakiosha nyavu zao. Yesu aliingia ndani ya chombo kimoja, kilicho kuwa ni cha Simoni na kumsihi akipeleke kwenye maji kiasi. Ndipo Yesu aliketi katika chombo na kuanza kufundisha huo umati wa watu akiwa ndani ya chombo.

Alipomaliza kuongea, alimwambia Simoni , " Peleka chombo kwenye maji mengi na ushushe nyavu zako," Simoni alijibu, " Bwana mkubwa , tumefanya kazi ngumu usiku kucha na hatukupata chochote.Lakini kwa sababu wewe wa sema nitazishusha nyavu. Basi walipofanya hivyo walipata Samaki wengi mno nyavu zao zikaanza kukatika wakawapungia mkono washirika wao waliokuwa katika chombo kingine, ili waje kuwasaidia. Wakaja wakajaza vyombo vyote viwili hata vikataka kuzama.

Simoni Petero alipoyaona haya alianguka magotini mwa Yesu akisema," Ondoka kwangu kwa kuwa mimi ni mwenye dhambi," kwa maana alishikwa na mshangao yeye na wote waliokuwa pamoja naye , Yakobo, Yohana wana wa Zebedayo kwa sababu ya wingi wa Samaki waliowapata. Yesu akamwambia Simoni, usiogope kuanzia sasa utakua ukivua watu. Wakaviegesha vyombo vyao ufuoni wakaviacha na wakamfuta Yesu.

Baada ya hayo akatoka akaona mtoza ushuru jina lake Mathayo au Lawi, akiwa ameketi forodhani akamwambia, " nifuate." Mathayo, akaamka akaacha vyote akaondoka akamfuata Yesu. Mathayo, akamfanyia karamu nyumbani kwake na kundi kubwa la watu , watoza ushuru na wengine walikuwa wakila chakula pamoja nao. Lakini wale mafarisayo pamoja na waandishi na walimu wa sheria walianza kulalamika/ Kunung'unika kwa wanafunzi wake; kwa nini kula na kunywa pamoja na watoza ushuru wenye dhambi? Yesu akawajibu, sio wale wenye afya wanaohitaji daktari bali wale wagonjwa. Sikuja kuwaita watakatifu bali kuwaita wenye dhambi wa tubu.

Ndipo siku moja Yesu akaenda mlimani kuomba na aliomba Mungu usiku kucha. Asubuhi ilipofika aliwaita wanafunzi na akachagua wale kumi na wawili, ambao aliwaita mitume. Walikuwa ni Simoni aliye mwita Petero, nduguye Andreya, Yakobo, Yohana, Mathayo, na wengineo akiwemo Yudasi Iskariote ambaye baadaye alimsaliti.

### MPANGILIO wa SOMO

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Kama ungekuwa Yesu kuchagua watu ambao wangekuwa wanafunzi wako, je ungechagua watu wa aina gani?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu YESU? Ni kwa jinsi gani Yesu ni Mungu?**

- **Je hadithi hii inonyesha vipi kuwa Yesu ana nguvu zote? (Ananamlaka , ni mtawala , mwwenye enzi yote) Kivipi?**
    - Yesu aliennda kwa Simoni na Lawi alianzisha.
    - Mamlaka juu ya uumbaji. Alisababisha Samaki kuingia kwa nyavu.
    - Mamlaka ya kumwambia Simoni kutupa nyavu tena.
    - Nguvu ya kutukia uumbaji kuwaita wanafunzi kwake , na kuachana na kazi zao za awali.
    - Simoni Petero alianza kuwa Yesu ni Mungu akashikwa na mshangao, akakumbuka hiyo kuwa Yesu ni Bwana na akamwita hivyo.
    - Mamlaka ya kumwita Lawi, na kumfuata bila ya kuuliza maswali.
    - Nguvu zote na mamlaka yote kama alivyo Mungu.

- **Je hadithi hii inmaonyesha vipi kuwa Yesu anajua kila kitu?**
    - Alijua kuivuta mioyo ya Petero, Yakobo na Yohana kumfuata yeye.
    - Alijua kwamba watashika samaki wengi
    - Alijua mipango yao ya baadaye kuwa watakuwa wavuvi wa watu.
    - Alijua moyo wa Law
    - Alijua yote kwa hiyo alikuwa Mungu.
    - 
- **Je, hadithi hii inayaonyesha vipi kuwa Yesu ni mtakatifu? (mwenye haki, mpeana amri, anaye chukia dhambi, anaye hukumu watenda dhambi,anayehukumu dhambi kwa kifo/mauti.**
    - Petero alishikwa na uoga kwa kutambua utakatifu wa Yesu na kujiona kuwa mwenye dhambi, alipoona nguvu za Yesu akihisi kuwa hasitahili kuwa mbele za Yesu..
    - Hata samaki walimuheshimu.
    - Mtakatifu Zaidi ya mafarisayo, Zaidi ya utiifu wa inje , kutawala au kuonyesha mbele za watu. Yesu alihusika sana kwa kubadilisha mioyo na kufanya watu kuwa watakatifu wa kweli.

- **Je hadithi hii inonyesha vipi kuwwa Yesu au Mungu ni wa neema ? (upendo,mwenye huruma kwa wenye dhambi, mpole, aongeaye na wenye dhambi.**
    - Yesu aliwafikia Simoni na Lawi akawahubiria kwanza.
    - Akawafanya kushika Samaki wengi kwa upendo na ukarimu.
    - Alichagua kujionyesha/kujiwasilisha kwa mwanadamu mwenye dhambi- Simoni, na wengine.
    - Alichagua watu wenye dhambi, watu kutoka nje ya kijiji, watu wa daraja la chini kupitia hao kufanya kazi kubwa.
    - Alimpa moyo Simoni-Akimwambia ," usiogope"
    - Mungu alimuita Simoni petero kuvua watu Mungu ni mwenye huruma kuwafikiia wanadamu. Petero akiwa chombo.
    - Anamwita mwanadamu mwenye sifa mbaya-Mtoza ushuru-kumfuata na kumtumikia.
    - Lawi ajawa na furaha hata baada ya kuacha kazi mzuri ya mshahara mkubwa, moyo wake ulibadiishwa na Mungu kwa neema, ndipo akaandaa karamu.
    - Kwa sababu moyo wa Lawi ulikuwa umebadilika, alitaka marafiki zake wamjue Yesu.
    - Kula, kutangamana, na wenye dhambi na wale waliokuwa na sifa mbaya ,kuwafikia wale waliokuwa wamekataliwa na jamii.
    - Alikuwa daktari kwa wale waliokuwa wagongwa wa dhambi, kwa wao watambuao.
    - Yesu aliwavutia wale wasio kubalika kwa kanisa.
    - Yesu aliwa na karamu , kwa wale walio mwendea kwa unyenyekevu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kuwa (Yesu) Mungu ni mwaminifu? (Asiye badilika, anayeweka agano lake, anafanya analosema).**
    - o Aliendelea kushuhulikia mpango wake wa kuinua wanafunzi. Alikuwa na mpango.
    - o Aliwambia itakuwafaidi kwenu mkitupa nyavu zenu tena , na akawawezesha kupata samaki wengi.
    - o Alikuja kwa wenye dhambi, na ni mwaminifu kuwa na wenye dhambi, kuingia katika ulimwengu wao.

- **Je hadithi hii inaonyesha vipi kuwa Yesu alikuwa mwanadamu?**
    - o Alitumia mashua/boti kuvuka bahari.
    - o Alitumia maji na chakula.
    - o Alihitaji usaidizi wa baba na ushauri, akiomba.

**<u>Twajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- **Ni kwa jinsi gani hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani mbele za Mungu?**
    - o Alitaka kumtumia Petero na marafiki zake kwa utukufu wake na huduma yake , ingawaje walikuwa wenye dhambi na wanyonge.
    - o Hujali wagonjwa wa moyo, wale walioachwa na kudharauliwa na ulimwengu .Aliwaza kukaa nao.

- **Ni kwa jinsi gani hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi, anastahili adhabu/ hukumu kwa dhambi zake?**
    - o Simoni alikuwa na shaka kwa Yesu, ingawaje alimpenda
    - o Simoni alihutubu," Mimi ni mwenye dhambi," sistahili kuwa mbele za utakatifu wako."
    - o Yesu aliwashuhulikia wale walio jitambua kuwa ni wenye dhambi na kuhitaji msaada ( Petero, mtoza ushuru, wenye dhambi).
    - o Dhambi, mioyo ya hukumu ya mafarisayo.
    - o Mafarisayo- Kuchukia wengine.

- **Ni kwa jinsi gani hadithi hii inaonyeha kuwa mwanadamu anamuhitaji Mungu na hawezi kujisaidia, kujiokoa mwenyewe?**
    - o Petero-hakuweza kujisaidia mbele za Yesu
    - o Mtoza ushuru, na wenye dhambi.
    - o Daktari-Ni vizuri kwa wote waungamao huhitaji msaada wale wagonjwa.
    - o Hawashuhulikii wale wasio ungama/kukubali kuwa ni wagonjwa wenye "afya". Hakuja kwa hao.
    - o Kama mwanadamu , Yesu alimtumainia Mungu kwa muongozo na uamuzi kama kuchagua wanafunzi.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- **Je hadithi hii inaonyesha vipi mwanadamu ni lazima awe na Imani na toba ili aweze kumpelendeza Mungu na kuweza kuokolewa?**
    - o Yesu alipanga kuijenga Imani ya wanafunzi. Aliwaonyesha haja yao ya kutubu na kuweka tumaini kwake.
    - o Wale walio mkaribia Yesu katika Imani na toba walimpata neema yake.
    - o Wale wasio mwamini Yesu na kukataa kuona dhambi zao, wanahukumiwa na Yesu.
    - o Hata Yesu alimtegemea Baba yake aliye mbinguni katika mombi kwa kumsaidia kuchagua wale mitume kumi na wawili alitaka huo uhusiano.
    - o Simoni, yakobo, Yohana , na Lawi, waliacha kila kitu, na kumfuata Yesu, yawezekana Lawi aliacha kazi nzuri sana . Hii ndiyo aina ya tegemeo/ tumaini ambalo Yesu anatuitia.
    - o Tunaona ya kwamba Lawi hakuweza kusaidia kualika marafiki zake kumjua Yesu !! Hili ni tunda la ishara ya kubadilika kwa maisha yake.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Yesu alisema ni wagonjwa tu wanahitaji daktari. Mafarisayo hawakuamini kwamba wao ni wangonjwa au wenye dhambi. Je, tumekuwa tukishindwa vipi kuona dhambi na udhaifu wetu? Je, hili linatuzuiaje kumtegemea Yesu?

- Yesu alichangamoto imani ya wanafunzi kwa kuwaambia warushe nyavu hata kama walikuwa wamejaribu usiku kucha bila kupata samaki. **Je, ni katika njia gani Yesu anaweza kutuuliza" kurusha nyavu zetu"?**

- Kwa kuwaita wanafunzi Yesu alikuwa akianza kujenga kanisa lake.  Je, tunaweza kujifunza nini kutoka kwa hadithi hii kuhusu kujenga kanisa mahali ambapo tupo?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- Je, wakati mwingine unafikiri wewe ni mwenye dhambi sana au si wa maana sana hata Mungu asiweze kukujali? Kwa nini? Je! hadithi hii inakuhimiza vipi? **Mungu anawezaje kukutumia hata wewe?**

- **Je, Mungu anaweza kuwa anakuitaje "kushusha nyavu" zako?** Kwa maneno mengine, Mungu anawezaje kukuita kuchukua hatua ya imani ili kumtumikia? Je, una hisi kwamba Mungu anakuita kwa tendo fulani au mtazamo fulani? Hiyo inaweza kuwa nini?

- Simoni Petro na Lawi waliwacha yote wamfuate Yesu. **Je, Mungu anaweza kuwa anakuuliza kuwacha nini ili umfuate kwa ukaribu zaidi?**

## 30. KUPONA KWA MTU ALIYEPOOZA: MAMLAKA KUZISAMEHE DHAMBI
## Marko 2:1-12

Siku moja Yesu alikuja Kapernaumu na akaingia katika nyumba moja. Aliketi na kuanza kufunza, na umati ulijaza nyumba na hata nje ya nyumba. Watu walikuwa wakiangalia kwenye madirisha na milango. Kila mtu alimsikiliza Yesu akifunza.

Basi, kulikuwa na mtu aliyepooza huko Kapernaumu. Alikuwa na marafiki wanne. Hawa walimpeleka kwa Yesu, lakini hawakuweza kumfikia Yesu kwa maana watu walikuwa wengi sana. Walijaribu njia yoyote bila kufaulu. Mwishowe, walipanda juu ya nyumba. Kisha wakatoboa shimo kwenye paa. Wakafunga godoro la mgonjwa kwa kamba, na wakamshusha mtu huyo mbele ya Yesu. Yesu alipoona imani yao alimwambia mtu aliyepooza, "Mwanangu, dhambi zako zimesamehewa."

Hapo palikuwa na walimu wa sheria wakimsikiliza Yesu. Waliposikia maneno haya waliwaza mioyoni mwao, "Anawezaje kusema hivyo! Ni Mungu tu anaweza kusamehe dhambi! Anakufuru!"

Lakini Yesu akafahamu rohoni mwake kile walivyofikiri. Akawaambia, "Ni lipi gumu - mimi kusema, 'Dhambi zako zimesamehewa' au kusema, 'Inuka! Chukua kitanda chako uende!?' Sasa nataka mjue kwamba Mwana wa Adamu ana mamlaka duniani ili kuzisamehe dhambi." Ndipo Yesu akamwambia mtu aliyepooza, "Simama ujitwike godoro lako uende nyumbani mwako."

Naye akafanya hivyo! Mara akasimama akajitwika godoro lake akatoka mbele yao wote. Wakastaajabu wakamtukuza Mungu wakisema, "Namna hii hatujapata kuiona kamwe!"

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je! ni baadhi ya njia gani umeenda nje ya njia yako kusaidia rafiki? Au labda kwa njia ambayo rafiki amejitahidi kukusaidia?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu YESU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu (au YESU) ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mamlaka juu ya dhambi na uovu. Mamlaka ya kuponya mwili.
    - Mamlaka ya kusamehe dhambi.
    - Mwuujiza wa mwili unasaidia kuanza mamlaka ya kiroho.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu (au Yesu) anajua kila kitu kwa njia gani?**
    - Yesu alijua mawazo ya mioyo ya walimu.
    - Yesu alijua mioyo ya mlemavu na marafiki wake. Aliona imani yao naye akawatendea.
    - Alijua jinsi ya kuonyesha mamlaka yake ya kusamehe dhambi – kwa kuponya mwili.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu (au Yesu) ni mtakatifu vipi? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?)**
    - Yesu hapendezwi na mashaka.
    - Ukosefu wa imani ya walimu uliwahukumu.
    - Mungu ni mkamilifu. Yesu hakujali tu kuhusu mwili bali hasa kuhusu roho ya mtu huyu. Alitaka kumwokoa mtu aliyepotea katika dhambi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu (au Yesu) ni mwenye neema vipi? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
    - Alimsamehe mtu mwenye dhambi dhambi zake.
    - Aliponya mwili wa mtu.
    - Alionyesha mashaka ya dhambi ya walimu, akiwapa nafasi ya kutubu na kuamini.
    - Alikuwa mvumilivu na makutano hata wanaume ambao waliingilia mkutano wake.
    - Alijidhihirisha kwa watu hao na hata kwetu sisi.
    - Kwamba Yesu, Mwana wa Mungu angeketi na wenye dhambi na kwa subira kuwafunza ni neema ya ajabu.
    - "Ni Mungu tu anayeweza kusamehe dhambi," basi akijionyesha kwamba (dhibitisha) yeye ni Mungu.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu (au Yesu) ni mwaminifu vipi? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?). )**
    - Alisema kwamba atamponya mlemavu na kasha alifanya hivyo.

**<u>Tunajifunza nini katika hadithi hii kuhusu MWANADAMU?</u>**
**(k.m. Ni muhimu kwa Mungu; ni mwenye dhambi; haiwezi kujiokoa.)**

- Yesu anapenda mwanadamu, na anataka kumhurumia.
- Shida kuu ya mwanadamu ni dhambi zake, ambayo inamtenganisha na Mungu.
- Kama vile Yule mlemavu hangeweza kumwendea Yesu mwenyewe, watu wote hawawezi kujiokoa wenyewe kutoka kwa adhabu ya dhambi.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**
(k.m. Anaweza kumwendea Mungu kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu mwenyewe. Lazima aje kwa imani na tubu aokoke.)

- Yesu huwatendea wote wanaomtumaini. Hutendea imani.
- Badala ya kukasirika na watu ambao walibomoa paa, Yesu aliwashukuru kwa imani yao.
- Tunda la imani ni matendo. Marafiki hao wanne walijitolea kwa kumleta rafiki wao kwa Yesu.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Unawezaje kutumia hadithi hii katika uinjilisti wa kibinafsi? Je, inawezaje kusaidia kushirikisha Injili na maisha ya rafiki yako aliyepotea?
- Mtu aliyepooza ilimbidi "kuishi imani yake" Je, ni katika njia gani yunaweza kuitwa kuchukua hatua dhabiti za imani maishani mwetu?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Umeonaje ulemavu wako na unyonge wako mwenyewe wa kujiokoa hivi majuzi?** Ni katika eneo gani maishani mwako**?** Je, umekuwa na wakati mgumu katika maisha yako kumtumaini Mungu hivi majuzi? Unawezaje kujitupa kwa imani miguuni pa Yesu kupata msaada?

- Mwanamume huyu alihitaji kuonyesha imani yake ili kupata uponyaji kamili. Je una changamoto maishani inayohitaji imani? Je, inaweza onekana vipi maishani mwako ukitoka nje kufanya imani yako kuonyesha matendo katika maisha ya halisi?

## 31. YESU AONGEA NA MWANAMKE MSAMARIA
## Yohana 4:1-45

Baada ya pasaka Yesu na wanafunzi wake walirudi Galilaya. Mara hii walitumia njia fupi ambayo ilienda moja kwa moja kaskazini kutoka Yerusalemu kupitia nchi ya vilima iliyoitwa Samaria. Wayahudi waliwachukia Wasamaria. Wasamaria walitokana na wana wa Waisraeli walipooana na Waashuri wakati Ashuri ilipovamia na kushinda ufalme wa kaskazini miaka 750 iliyotangulia. Kwa hivyo Wasamaria walikuwa watu wachafu wasiokuwa na tumaini na mtu yeyote ambaye alihusiana nao alikuwa akihesabiwa mchafu pia.

Walipokuwa katika nchi ya Samaria, Yesu na wanafunzi wake walifika kwenye kisima ambacho babu yao, Yakobo alikuwa amechimba. Ilikuwa karibu na adhuhuri naye Yesu alikuwa amechoka. Kwa hivyo aliketi kwenye kisima wakati wanafunzi wake walipoenda mjini kununua chakula.

Wakati huo, mwanamke Msamaria fulani alikuja kuteka maji, Yesu akamwambia, “Nipe maji ninywe.”

Alistaajabu, Wewe ni mwanamume Myahudi nami ni mwanamke Msamaria. Je, umawezaje kuniuliza nikupe maji?” (Kwa maana Wayahudi hawakuchangamana na Wasamaria.)

Yesu akasema, “Ungalijua karama ya Mungu naye akuulizaye umpe maji, ungemwuliza naye angekupa maji ya uzima.”

Akajibu, “Bwana, huna kitu cha kutekea na kisima ni kirefu. Utapata wapi haya maji ya uzima?”

Yesu akamwelezea, “Mtu anapokunywa maji kutoka kwa kisima hiki, yeye hupata kiu tena. Lakini yeyote anayekunywa maji ninayompa, hataona kiu tena. Maji nitakayompa yatakuwa chemichemi ya maji yakibubujika uzima wa milele kwake.”

“Bwana, nipe maji haya ili nisione kiu tena na kuja hapa katika kisima hiki kuteka maji.”

Yesu akamwambia, “Nenda umwite mumeo, na uje hapa.”

“Sina mume,” mwanamke huyo alimjibu Yesu.

“Hapo umesema ukweli.” Yesu akasema. “Umekuwa na waume watano na hata yule unayeishi naye si mumeo.”

“Bwana, naona kwamba wewe u nabii.  Babu zetu waliabudu katika mlima huu lakini ninyi Wayahudi mnasema kwamba Yerusalemu ndipo pahali ambapo watu wanapaswa kuabudu.”

Yesu akamwambia, “Wakati unakuja ambao hamtaabudu hapa au pale. Saa yaja, nayo ipo, ambapo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na kweli, kwa maana Baba anawatafuta watu kama hao wamwabudu, Nao wamwabuduo lazima wamwabudu katika roho na kweli.”

“Naam, najua kwamba Masihi anakuja,” mwanamke huyo akamwambia, “Na atakapokuja, atatueleza kila kitu.”

Kisha Yesu akamwambia kwa wazi, “Mimi ndiye.”

Mwanamke huyo akauacha mtungi wake kisimani akarudi mjini na kuambia kila mtu. Njooni mwone yule aliyeniambia kila kitu ambacho nimefanya. Je, aweza kuwa ndiye Masihi?” Kwa hivyo walirudi kisimani naye kumwona Yesu.

Wengi wao wakamwamini Yesu kwa sababu ya yale mwanamke huyo aliyoyashuhudia, nao wakamsihi asiondoke kwa hivyo Yesu alikaa siku mbili zaidi, akiwafunza watu, na hata wengi zaidi wakamwamini.

Kisha wakamwambia huyo mwanamke, “Sasa tunaamini wala si kwa sababu ya yale uliyotuambia, lakini tumesikia sisi wenyewe na tumejua kwamba mtu huyu kwa kweli ndiye Mwokozi wa ulimwengu.”

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Ask one of these pre-story questions to the whole group or discuss in pairs.
- **Je, wewe na kanisa lako mnahusiana vipi na wale ambao wamekataliwa na jamii?**
- **Mahali ni wapi na ni mazingira gani ambayo unaweza kupata unaweza kumwabudu Mungu vyema zaidi?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Tunajifunza nini kuhusu YESU?  Tunaona kwamba Yesu ni Mungu kwa njia gani?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba YESU ni mwenye uwezo wote vipi? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
    - Alivuka vizuizi vya utamaduni bila hofu ya kudhihakiwa na wayahudi.
    - Alikuwa na mamlaka ya kupeana maji ya uzima bure kwa mwanamke msamaria bila kubagua.
    - Yesu alimwamuru mwanamke huyu kuenda na kumwita mume wake.
    - Yesu alikuwa na mamlaka ya kubadili mioyo. Watu ambao walimwona walibadilika. Waliamini.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi kwamba Yesu au Mungu anajua kila kitu?**

- Yesu alijua kila kitu ambacho mwanamke huyu alikuwa amefanya. Aliujua moyo wake.
- Yesu alijua hitaji la mwanamke huyu alihitaji maji ya kawaida lakini maji ya kiroho zaidi.
- Yesu alijua wakati halisi ambao kuabudu halisi kungefanyika. Alijua ibada halisi itakuwa ya aina gani?
- Yesu alijua njia bora zaidi ya kumfikia mwanamke huyu mwenye hitaji kumwongoza kwa toba na imani. Aliyajua mahitaji yake halisi na hali yake.
- Alijua jinsi ya kuepuka ubishi wake na kuufikia moyo wake. Alijua jinsi ya kuongea naye katika upendo na ukweli.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Yesu au Mungu ni mtakatifu kwa njia gani? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?**
  - Alimwuuliza kuhusu dhambi yake ya uzinzi.
  - Alitamani ibada ya kweli, sio tu kufuata mila za Kiyahudi au Kisamaria.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Yesu au Mungu ni mwenye neema kwa njia gani? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
  - Yesu aliongea na mwanamke huyu kwa neema, heshima na upole.
  - Aliongea na mwanamke ambaye alikuwa Msamaria na mwenye sifa ya dhambi.
  - Alimpenda na aliongea naye katika njia ambayo ingemwongoza bora zaidi kwa toba na imani.
  - Alimpa mwanamke huyu maji ya uzima ambayo yangemwongoza kwa uzima wa milele. (Isaya 12:3,Zaburi 42:18, Yeremia 2:13)
  - Alijidhihirisha kwa mwanamke huyu kwamba yeye ndiye Masihi.
  - Alikaa na watu hawa siku mbili zaidi, akihubiri na kuwapa uzima wa milele Wasamaria ambao walikuwa maadui wa Wayahudi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu kwa njia gani? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?).**
  - Yesu alimfuatilia mwanamke huyu na alikuwa mwaminifu kumfuata mpaka alipoona dhambi yake na neema ya Yesu.
  - Mungu alimwahidi Abrahamu kwamba mataifa yote yangebarikiwa kupitia uzao wake. Pia, kupitia manabii, aliahidi kwamba Mwokozi angekuja kwa ajili ya Mataifa na vilevile kwa Wayahudi. Hapa Yesu alimwokoa mwanamke huyu Msamaria pamoja na majirani zake.
  - Yesu alikuwa mwaminifu kujidhihirisha kwa watu kwamba alikuwa Masihi aliyeahidiwa.

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni wa thamani kwa Mungu kwa njia gani?**
  - Yesu alimpenda mwanamke huyu. Alitumia nafasi hii kupumzika na hata kuweza kuongea naye.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi vipi? Anayestahili adhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zake?**
  - Mwanamke huyu alikuja kisimani adhuhuri kuwaepuka watu wengine. Alikuwa na sifa ya kuwa mwenye dhambi.
  - Mwanamke huyu alikuwa ametalikiwa mara nyingi na alikuwa katika wakati huo anaishi dhambini na mwanamume mwingine.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba mwanadamu anahitaji Mungu na kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe vipi?**
  - Mwanamke huyu hakujua chochote kuhusu uzima wa milele au jinsi ya kupata maji ya uzima. Maji ambayo alipata yangeweza tu kudumu kwa muda mfupi, kisha angeona kiu tena.
  - Alionyesha hitaji lake halisi la kiroho alipomwamini Yesu na kukimbia kuenda kuwaambia majirani wake.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

- **Hadithi hii inaonyesha kwamba mwanadamu anaweza tu kwenda kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu?  (Yaani, kulingana na mapenzi na mpango wa Mungu.)**
    - Mtu haokolewi kwa sababu ya pahali anapoabudia, bali kwa njia ya Mungu ambayo ni roho na kweli, yaani, ukweli wa Yesu unapoingia katika mioyo yao kwa imani.
    - Alibadilika.  Hakuogopa tena kuwa na watu wa kijiji.  Alitaka kuwaambia wengine kuhusu wokovu wake mkuu. Katika njia nyingine, alipokunywa kwa imani kutoka katika maji ya uzima ya Yesu, kijito cha ukweli na uzima kilitiririka hata kwa majirani wake.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba lazima mwanadamu awe na imani na toba ili kumpendeza Mungu na kuokolewa.**
    - Mwanamke huyu alikubali jinsi Yesu alimwuuliza kuhusu dhambi zake na akaamini kwamba alikuwa Masihi.
    - Baada ya watu wa kijiji kukaa na Yesu, wao pia waliamini.
    - Watu huokoka, si kwa sababu desturi zao, bali kwa sababu ya mioyo yao kubadilishwa na ukweli.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Je, umewahi jihisi kukataliwa na watu wengine? Je, unajiona kuwa mwenye dhambi sana hata Mungu asiweze kukuokoa? Baada ya kusikia hadithi hii, unafikiri Yesu angekuambia nini unapojihisi hivyo?

- Yesu aliwafikia waliokataliwa. Je, kanisa lako mnahusiana vipi na wale ambao wamekataliwa na jamii? (Waathiriwa wa VVU/UKIMWI, walevi, watu wanaovuta sigara au wenye lugha chafu, n.k.) Je, Mungu angependa vipi makanisa yetu kubadilisha jinsi tunavyowatendea maskini au waliokataliwa katika jumuiya zetu?
- Je, wewe na kanisa lako mnawatazama wanawake kama Yesu anavyowatazama? Je, unawathamini kama dada katika Bwana na washirika katika Injili? Je, ni nini kingeonekana tofauti katika maisha yako au maisha ya kanisa lako ikiwa ungewatendea kama Yesu alivyofanya?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):**  (chagua moja au mbili)

- Yesu alijua mambo yote huyu mwanamke aliwai tenda. Mungu bado anajua kila kitu, pamoja na moyo wako na dhambi zako zilizofichwa. Unahitaji kukiri nini kwake leo?

- Je ni nani aliyekataliwa au mtu wa kabila tofauti na lako au mtu wa nchi tofauti ambaye Mungu anakuita kumfikia na injili wiki hii?

## 32. YESU AWALISHA WATU ELFU TANO
## Marko 6:30-44

Siku moja Yesu alikuwa na wanafunzi wake, ikawa kwamba, hawakupata wakati wa kula. Yesu akawaambia nifuateni huku katika sehemu tulivu, ili mpate kupumzika. Kwa hivyo walienda wakaingia kwenye chombo wakavuka ng'ambo ya pili ili kupata mahali bila watu.

Basi watu walitambua mapema kule walikokuwa wakienda na wakatangulia kwa miguu na wakafika mapema mbele yao. Yesu aliposhuka katika chombo aliona umati mkubwa na akawahurumia sana, kwa sababu walikua kama kondoo waliokosa mchungaji hivyo alianza kuwafundisha, aliwafundisha, mambo mengi.

Muda uliendelea kusonga jioni ikaingia, hivyo wanafunzi wake walimjia Yesu na kumwambia, "Hapa ni nyikani na tayari jioni inakaribia watume hawa watu waende vijijini kujitafutia chakula wenyewe." Lakini Yesu akawajibu, "Wapatieni ninyi kitu wale." Wakajibu, "Ile itatumia mshahara wa mtu wa miezi minane! Je, tutumie gharama hii yote kwa mikate tu?" Yesu akawauliza, "Mna mikate mingapi? Walipojua wakasema, "Mikate mitano na samaki wawili." "Leteni hapa." Yesu akawaelekeza wawaketishe watu kwa makundi. Akachukua ile mikate mitano na samaki wawili na akaiangalia mbinguni akashukuru Mungu na kuwapatia wanafunzi wake wawagawanyie pia, akagawanya wale samaki wawili kwao wote . Wote wakala na kutosheka na wanafunzi wakajaza vikapu kumi na viwili vya mabaki. Idadi ya watu wanaume waliokula walikuwa elfu tano.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unaweza kukumbuka wakati ambapo Mungu alikuandalia kimuujiza? Umeonaje utoaji wa Mungu katika maisha yako?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha nini kuhusu UWEZO wa Yesu? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**

- **Katika hadithi hii tunaonaje nguvu za Yesu?**
    - Aliteka watu kwa nguvu ya maneno yake.walikua naye kwa siku nzima wakimsikiliza.
    - Aliamuru watu wapewe chakula
    - Aliongeza mikate na samaki
    - Alipeana chakula zaidi ya vile watu walihitaji.
    - Ana nguvu juu ya ulimwengu asili

- **Katika hadithi hii tunaonaje Yesu anaufahamu wote**
    - Alijua atawalisha watu wote na kuikabili Imani ya wanafunzi wake
    - Alijua hali halisi ya watu ,moyo,na mwili,upweke wa kuitaji mchungaji mwema

- **Katika hadithi hii tunaonaje  kuwa Yesu ana neema.**
  - Kwa kupatiana chakula kea wingi kutosheleza watu wote
  - Alionyesha nguvu zake kwa wote kwa kuwasaidia kutokuamini kwao.
  - Alikuwa na huruma kwa watu, ingawaje yeye na wanafunzi wake walikuwa wamechoka aliwaangalia, akaweka mahitaji yao kama yake.
  - Aliwafundisha, akawapa neno la Mungu.
  - Alikabili Imani ya wanafunzi wake.
  - Alitumia kichache kile wanafunzi walikuwa nacho kilisha umati wote

- **Katika hadithi hii, tunaonaje kuwa Yesu ni mwaminifu ?**
  - Mungu aliahidi katika bustani ya Edeni mwokozi atakaye vunja laana iliyo letwa na shetani. Sehemu ya laana hiyo ilikuwa ni kule kung'ang'ana kupata kujishibisha (Mwanadamu atakula kwa jasho) Yesu ndiye mvunja laana. Alionyesha nguvu kwa kuwalisha na kuwoatia watu wake.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

  - Kumtegemea Yesu tu peke yake kwa kupeana chakula cha kutoshekeza.
  - Wanafunzi hawakuweza kusaidia kusuluhisha tatizo. Walichokuwa nacho kilikuwa hakiwatoshi/ hakiwatoshelezi wote.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Dunia yote ililaaniwa kwa sababu ya dhambi ya mwanadamu dhidi ya Mungu katika bustani la Edeni. Kutokana na hatua hiyo mwanadamu angetatizika kujilisha mwenyewe na familia yake. (Mwanzo 3) Yesu ndiye Mwokozi ambaye anabadilisha sehemu hii ya laana! Ana uwezo wa kupeana.  Je, ni maeneo gani ya mahitaji ni muhimu sana katika maisha ambayo tunafaa kumtumaini Mungu leo kutushughulikia?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- Fikiria maeneo fulani katika maisha yako ambapo **unang'ang'ana kupata kile unachohitaji kulisha au kuvisha au kuelimisha au kutunza familia yako.** Je! hadithi hii inaweza kukusaidia vipi kukabiliana na mapambano yako leo? Je, ni hitaji gani linaloonekana kuwa lisilowezekana ambalo Yesu anakuuliza umtumaini?

- Yesu alitumia samaki wadogo na mikate aliyopewa kuwalisha watu wake. **Je, una kitu gani kidogo cha kumtolea Mungu ili akitumie kwa ajili ya ufalme wake? Unawezaje kukiacha?** Je, Mungu anaweza kukusaidia vipi ikiwa utachukua hatua hii ya imani?

## 33. YESU AKIMPONYA MVULANA ALIYEPAGAWA NA PEPO MCHAFU
## Marko 9:14-29

Siku moja Yesu alirudi kutoka safari na Petero, Yakobo, na Yohana. Walipowafikia wale wanafunzi wengine, wakawakuta wamezungukwa na umati mkubwa wa watu na baadhi ya walimu wa sheria wakibishana nao. Mara wale watu walipomwona Yesu, wakastaajabu sana, wakamkimbililia, ili kumsalimu.

Akawauliza wanafunzi wake, "Mnabishana nao kuhusu nini?" Mtu mmoja miongoni mwa ule umati wa watu akajibu, "Mwalimu, nilimleta kwako mwanangu ambaye ana pepo mchafu ambaye anamfanya asiweze kuongea. Kila mara huyo pepo mchafu ampagaapo mwanangu, humwangusha chini na kumfanya atokwe povu mdomoni na kusaga meno, kisha mwili wake hukauka. Niliwaomba wanafunzi wako wamtoe huyo pepo mchafu, lakini hawakuweza."

Naye akawajibu, "Enyi kizazi kisicho na imani, nitakaa nanyi hadi lini? Nitawavumilia hadi lini? Mleteni kwangu." Wakamletea huyo kijana wake. Na yule pepo alipomwona, mara akamtia mvulana kifafa, kama baba yake alivyosema. Naye Yesu akamwuliza baba yake, Je, amekuwa katika hali hii tangu lini?" Naye akasema, "Tangu utotoni. Na mara nyingi amemtupa motoni na majini, ili kumwangamiza. Lakini kama unaweza kufanya jambo lolote, utuhurumie na utusaidie." Naye Yesu akamwambia, "Kama unaweza? Yote yanawezekana kwa mtu aaminiye." Mara babaye yule mtoto akapaza sauti, akasema, Naamini; nisaidie kutokuamini kwangu!"

Yesu alipoona kwamba umati wa watu unakusanyika pamoja mbio, akamkemea yule pepo mchafu, akimwambia, "Wewe pepo bubu na kiziwi, nakuamuru umtoke wala usimwingie tena!"

Yule pepo mchafu akiisha kupiga kelele, akamtia kifafa kwa nguvu na, akamtoka, akamwacha yule mvulana akiwa kama maiti, hivyo watu wengi wakasema, "Amekufa." Lakini Yesu akamshika mkono akamwinua, naye akasimama.

Baada ya Yesu kuingia ndani ya nyumba, wanafunzi wake wakamwuliza wakiwa peke yao. "Mbona sisi hatukuweza kumtoa huyo pepo mchafu?"

Yesu akawajibu, "Hali hii haiwezi kutoka isipokuwa kwa kuomba."

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, ni imani kiasi gani inahitajika ili Mungu atusaidie katika shida zetu?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha nini kuhusu UWEZO wa Yesu? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
- **Je hadithi hii inaonyesha vipi kuhusu uwezo wa Yesu? ( ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote ?) Kivipi?**
    - o Alikuwa na nguvu juu ya mapepo. Aliamuru yatoke inje.
    - o Alifanya kwa nguvu za Neno lake.
    - o Mapepo sharti yamtii Yesu. Yuko na mamlaka
    - o Aliwakemea wanafunzi wake kwa sababu ya uhaba wa Imani.
- **Je tunaona vipi kuwa Yesu anaufahamu wote katika hadithi hii.**
    - o Yesu alijua moyo wa yule baba, kung'ang'ana kwake kuamini, ingawaje alitamani kuamini.
    - o Yesu alimtambua ni aina gani ya Roho chafu iliyokuwa ndani ya yule kijana, na jinsi ya kumponya huyo mvulana
- **Ni kwa jinsi gani tunaona Yesu ana Neema katika hadithi hii?**
    - o Alimponya yule mvulana, kwa kuifikia Imani haba ya Bba.
    - o Aliwasiliana na wanafunzi, aliwasaidia kufahamu Imani na maombi.

- **Ni kwa jinsi gani tunaona Yesu ni mwaminifu katika hadithi hii?**
    - o Yesu ni Mwokozi aliyeahidiwa ambaye angemshinda Shetani na mapepo yake. Yesu alionyesha nguvu zake juu ya mapepo katika hadithi hii.
    - o Wakati wote Yesu anaweza kujibu imani ya watu wake, hata kama imani ilikuwa dhaifu. Alijibu maombi ya baba hata kama aliungama mashaka yake.
    - o Yesu hupona wagonjwa.
    - o Yesu ni Mwokozi aliyeahidiwa ambaye angebadilishi athari ya Shetani na mapepo yake.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- o Uokovu unatoka kwa imani tu. Kila kitu kinawezekana kwa wanaoamini.
- o Mwanadamu anang'ang'ana kuamini. Lakini katika neema yake Mungu anaweza kujibu maombi ya mwanadamu hata kama anaungama dhaifu ya imani yao. Kama mwanadamu anaweza kulia kwa usaidi wa Mungu kama huyo baba, Mungu anaweza kujibu. Mungu anahesabu imani kama yake kama haki.
- o Baba ya mvulana hakuwa na uwezo hata kidogo. Hata wanafunzi wa Yesu. Mungu (Yesu) tu aliweza kumsaidia.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- **"Bwana, ninaamini. Nisaidie kutokuamini kwangu!"** Je, Yesu anaahidi kujibu vipi hata kwa imani ndogo zaidi? Hali gani tunakabilia nazo ambazo ni vigumu sana kwetu kumwamini Mungu? Je, hadithi hii inatuhimiza vipi? Hadithi hii inaweza kutusaidia vipi katika maisha yetu ya maombi?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **"Bwana ninaamini. Nisaidie kutoamini kwangu" Je, hivi majuzi umekua vipi kama huyo baba**, unataka kuamini lakini unang'ang'ana katika imani yako? Je, hadithi hii inakuhimiza vipi?

- Yesu anakuita uje kwake. Sio lazima kuelewa kila kitu juu yake. Unahitaji kuacha kujitengenezea njia yako mwenyewe na kutumainia maisha yako kwake Mungu. Kumtumaini Mungu namna hii kunawezaje kukupatia uzima hata sasa? **Je, ni uamuzi gani wa imani unahitaji kufanya leo?**

## 34. KUFUFULIWA KWA LAZARO KUTOKA KWA WAFU
## Yohana 11:1-44

Kulikuwa na mwanamume aliyeitwa Lazaro aliyekuwa rafiki wa karibu wa Yesu. Alikuwa na dada wawili walioitwa Mariamu na Martha. Siku moja, Lazaro alikuwa mgonjwa sana na dada zake walimtumia Yesu ujumbe. "Bwana, umpendaye ni mgonjwa sana." Yesu alipoupokea ujumbe aliwaambia wanafunzi wake, "Ugonjwa huu hautaleta kifo lakini utukufu kwa Mungu."

Yesu alimpenda Lazaro na dada zake wawili, alikaa siku mbili zaidi pahali hapo kabla ya kusafiri na wanafunzi wake nyumbani kwa Lazaro. Aliwaambia wanafunzi wake, "Lazaro amekufa, na kwa ajili yenu nina furaha kwa sababu sikuwepo, ili muweze kuamini. Lakini ebu twende kwao." Alipofika, Lazaro alikuwa amekufa siku nne zilizopita . Alipokaribia nyumbani kwao alipata watu wengi wakilia na kuomboleza Lazaro. Martha akamjia Yesu na kusema, "Bwana, ungekuwa hapa tu, kaka wangu hangekufa. Lakini ninajua kwamba, yoyote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa."

Yesu akamwambia, "Lazaro atafufuka".

Martha akasema, "Ndiyo ninajua kwamba, atafufuka tena siku ya mwisho".

Lakini Yesu akamwambia, "Mimi ndimi ufufuo na uzima. Yeyote anayeniamini ataishi hata ikiwa atakufa. "Je, unayaamini haya?"

Martha akasema, "Ndiyo ninaamini, wewe ndiye Kristo, Mwana wa Mungu." Kisha Martha akakimbia kwake Mariamu na kumwambia kwamba, "Yesu yuko hapa."

Mariamu alipokuja kwake Yesu, alisema, "ikiwa ungekuwa hapa, kaka wangu hangekufa."

Kisha Yesu alikuja kwenye kaburi la Lazaro, na akalia. Yesu akasema, "Liondoeni jiwe kutoka kwa kaburi."

Martha akasema, "Lakini amekufa zapita siku nne sasa, kutakuwa na harufu mbaya sana!"

Kisha Yesu akasema, ikiwa utaamini utaona utukufu wa Mungu." Walipoliondoa jiwe, Yesu aliomba, "Baba, asante sana kwa sababu umenisikia ili watu hawa waweze kuamini kwamba umenituma." Kisha akaamuru, "Lazaro, toka nje!" Naye Lazaro akatoka kwenye kaburi. Yesu akasema, "Ziondoeni sanda na mmwache aende." Watu wengi walimwamini siku hiyo.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, unakumbuka wakati ulipoomba kwa bidii kwa ajili ya jambo fulani na ikabidi usubiri kwa muda mrefu jibu la Mungu? Au labda bado unasubiri?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha nini kuhusu UWEZO wa Yesu? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
  - Alimfufua Lazaro.
  - Vipi? – kwa neno lake (inatukumbusha uwezo wa Mugnu katika uumbaji)
  - Kwa nini? – kuonyesha utukufu wake mwenyewe (Alikuwa na kusudi, alikuwa mamlakani)
  - Inaonyesha kwamba yeye ndiye huongoza uzima na kifo.
  - Mamlaka kwake Yesu.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Yesu au Mungu anajua kila kitu vipi?**
  - Alijua kile ambacho kingetokea – aliwaambia wanafunzi kila kitu kabla ya wakati.
  - Alijua kwamba Lazaro alikuwa amekufa.
  - Alijua kusudi la kifo chake – ili kwamba wanafunzi wangeamini, na kwamba watu wangeona utukufu wa Mungu, na wangejua kwamba Mungu alikuwa amemtuma.
  - Alijua kile mioyo ya watu hata wanafunzi wake, ilihitaji.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Yesu au Mungu ni mwenye neema vipi? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?)**
  - Aliwapenda Maria, Martha, na Lazaro, kwa hiyo alingoja kwa sababu alikuwa na kusudi kubwa zaidi akilini. Pia aliwapenda watu ambao wangeambiwa au wangesoma hadithi hii baadaye
  - Fadhili – alilia machozi ya uchungu.
  - Huruma – wote, pamoja na Lazaro walikuwa wenye dhambi, hawakustahili huruma.
  - Alipenda kwa kuonyesha.
  - "Mimi ndimi ufufuo na uzima." Alikuwa mwenye kupeana uzima.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu vipi? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.)**
  - Kifo cha Lazaro hakikumalizikia katika kifo, kama vile Yesu alikuwa amesema.
  - Yesu alitaka kwamba Mungu aweze kutukuzwa. Yeye ndiye aliye mamlakani.
  - Kusudi lake lilitimizwa.
  - Yesu ndiye Mwokozi aliyeahidiwa! Alikuwa na nguvu za kuvunja laana ya mwenye dhambi! (Gen 3:15) Alionyesha mamlaka yake juu ya kifo na Shetani.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?**

  - Maria na Matha walionyesha imani kwa kumwita Yesu.
  - Maria aliamini kwamba Yesu angeweza kusimamisha kifo. Kwa hivyo walikuwa na kiasi cha imani na shaka pia. Yesu hutendea hata imani ndogo zaidi.
  - Mungu alijitukuza ili watu wangeamini.

- o Yesu mwenyewe ndiye ufufuo na uzima!!!! Hakuna njia nying'ine kupata uzima au kuokoka!!!
- o Neno la Kigiriki kwa Furaha ni *chairo*. Inamaanisha kufurahi na kushangilia. Yesu alifurahishwa na uhakika wa kwamba hakuwepo ili kutimiza uhitaji wa Lazaro. Kukawia kwa Yesu kutimiza uhitaji wa Lazaro hakukuwa na maana kwa mawazo ya wanadamu. Lakini Yesu alikuwa na kusudi kuu zaidi - kuonyesha nguvu zake mwenyewe na kusaidia kukuza imani yao.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Je, Yesu alihitaji **imani kamilifu** kutoka kwa Maria na Martha ili kutenda? Yesu anajibuje wakati imani yako imechanganyika na mashaka na kukata tamaa?

- Je, ni baadhi ya njia zipi ambazo watu huitika wakati jibu la Mungu kwa maombi yao ni "Hapana" au "Ngoja"? Hadithi hii inatufunza vipi jinsi ya mwitikio ulio bora?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je, ni sehemu gani za mahitaji katika maisha yako ambazo unapambana nazo huku ukififikiri kwamba Yesu amechelewa kutimiza?** Labda utasubiri siku nne kama Lazaro au miaka arobaini kama Waisraeli walipokuwa jangwani. Je, unaweza kumtumainia Kristo kwa kumsubiri? Je, Mungu anaweza kuwa anajaribu kukufundisha nini?

- Je, una wasiwasi kuhusu kitakachotokea ukifa, unajiuliza utaenda wapi? Je, unaweza kuwa na uhakika? Unaweka wapi tumaini lako? Unaamini nini kukusaidia kukabiliana na kifo?

## 34-B: SOMO la CBS: NYIMBO na MICHEZO #2

**NYIMBO za KUSIMULIA HADITHI za BIBILIA:**

Chagua Hadithi ambayo tayari umejifunza katika CBS na uingie katika kikundi cha wanafunzi watano mchukue saa moja kujaribu kuunda na kuandika wimbo unaosimulia moja kwa moja hadithi. Kisha wasilisha wimbo kwa darasa zima.

**MICHEZO ya KUIGIZA wa KUSIMULIA HADITHI za BIBILIA:**

Chagua Hadithi ambayo tayari umejifunza katika CBS na uingie katika kikundi cha wanafunzi 5 hadi 15 (idadi kutegemea hadithi) na uchukue saa moja kduandaa drama. Hakikisha kuwa una majukumu yote yaliyofafanuliwa wazi na kuwa na watu wote wanaohusika. Pawe na mtu mmoja ambaye ni msimulizi wa kusimulia sehemu za hadithi ambazo hazizungumzwi na wahusika wanaowakilishwa. Kisha wasilisha drama kwa darasa zima.

**KANUNI ZA UANDISHI WA NYIMBO:**

- **KUHUSU NYIMBO/MANENO:**
  - Kibiblia - sahihi, kweli
  - Ujumbe Wazi, sana sana wa Injili. Maneno yenye kugusa moyo.
  - Ikumbukwe kwa urahisi
    - Rahisi kutosha kwa wote kukumbuka au kwaya rahisi kwa kudia yenye mistari ya kiongozi wa wimbo kusmilia hadithi
  - Ina madhari wazi (sana sana katika kwaya)
  - Swali zuri: Muulize asiye Mkristo asikilize na kuona JINSI wanavyoelewa maneno ili kuhakikisha unawasiliana vizuri.

- **KUHUSU UWASILISHAJI:**
  - Wimbo wa kuvutia.
  - Inafahamika vya kutosha kwa watu kupenda na kujifunza
  - Rhythm nzuri, mtiririko
  - Furaha, kujihusisha. Kucheza - kukubalika kitamaduni, kumheshimu Bwana
  - Ishara zinalingana na maneno
  - Kuhamasisha, kuchochea hisia. Inatia moyo. Imefanywa kwa kujiamini.
  - Matamshi mazuri
  - Je, sauti ya kuimba inalingana na sauti ya maneno (K.m. Furaha, umakini, huzuni, heshima, furaha, amani)?
  - SI KWA SAUTI SANA. Usiruhusu vyombo ama sauti ya vyombo kuzima maneno!
  - Muhimu zaidi - MANENO na KUABUDU
    - Vyombo ni zana tu

## 35. YESU NA KIJANA TAJIRI
## Matayo 19:16-26 (& Luka 18:18-30, Marko 10:17-27)

Siku moja mtawala kijana alimjia Yesu, akampigia magoti na kumuuliza, "Mwalimu Mwema, nifanye jambo gani jema ili nipate uzima wa milele?"

Yesu akamjibu, “Mbona unaniita mimi mwema? Hakuna aliye mwema ila Mmoja tu, ndiye Mungu: Lakini ukitaka kuingia uzimani, zitii amri.”

Yule mtu akamwuliza, “Amri zipi?”

Yesu akamjibu, “Usiue, usizini, usiibe, usishuhudie uongo, waheshimu baba yako na mama yako na umpende jirani yako kama nafsi yako.”

Yule kijana akasema, “Hizi zote nimezishika. Je, bado nimepungukiwa na nini?”

Yesu akamwambia, “Kama ukitaka kuwa mkamilifu, nenda, kauze vitu vyote ulivyo navyo na hizo fedha uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo, unifuate.”

Yule kijana aliposikia hayo, akaenda zake kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake, “Amin, amin nawaambia, itakuwa vigumu kwa mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mbinguni. Tena nawaambia, ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu.”

Wanafunzi wake waliposikia haya, walishangaa sana na kuuliza, “Ni nani basi awezaye kuokoka?”

Lakini Yesu akawatazama, akawaambia, “Kwa mwanadamu jambo hili haliwezekani, lakini kwa Mungu mambo yote yanawezekana.”

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Habari yako tajiri? Kwa maneno mengine, ni maeneo gani ya baraka au uwezo au karama au karama ulizonazo katika maisha yako?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

- **Huyu kijana alikuwaje? Tunajua nini kuhusu maisha yake? Tabia zake? Sifa yake?**
    - o Tajiri, kijani, kiongozi. Alifikiri kwamba alikuwa amefuata sheria zote. Hata wanafunzi wa Yesu walifikiri hivyo kwa sababu walishangaa waliposikia mawazo ya Yesu juu yake. Alikuwa na sifa nzuri.
    - o Sifa yake alitegemea nini?
        - ▪ Kutii, kuwa na heshima, kuwa kiongozi, kubarikiwa na mali.

- **Kijana alimwuliza Yesu nini?**
    - o "Nifanye jambo gani jema ili nipate uzima wa milele?"
    - o Hili suali linatuonyesha nini juu ya mawazo yake kuhusu njia ya kupata uzima wa milele?
        - ▪ Lazima utii kustahili maisha ya milele.

- **Kijana alimwitaYesu nani? Kwa nini?**
    - o Mwalimu mwema! Labda alitaka kumrairai.
    - o Hii inatuonyesha nini juu ya mawazo yake kuhusu jaribio lake kupata maisha ya milele?
        - ▪ Lazima ustahili wokovu kupitia kufanya au kutii mambo yanayofaa. Lazima uwe na sifa nzuri kwa watu wengine.

- **Yesu alimjibu vipi?**
    - o Tii sheria!
    - o Je, unafikiri kwamba Yesu alitarajia kijana azifuate sheria zote bila kukosa kustahili maisha ya milele? Angeweza kupata maisha ya milele kupitia utiifu? Kama sivyo, kwa nini Yesu aliweza kumjibu hivyo?
        - ▪ Hapana. Yesu alijua moyo wake na fikira zake. Alitaka kumwonyesha kwamba hawezi kutegemea matendo yake kupata wokovu. Ni kama Yesu alitaka kusema, "Sawa! Ukitaka kumpendeza Mungu kwa njia hii, lazima utii sheria kikamilifu! Bila kukosa hata kidogo! Lakini hii njia haiwezekani!

- **Yesu aliposema, "Tii sheria," kijana alisema nini?**
    - o Sheria gani?
    - o Hii inatuonyesha nini kuhusu fikira zake?
        - ▪ Aliamini sana! Alikuwa na hakika kwamba anaweza kufanya kila kitu Yesu atakapomwamuru. Alikuwa na kiburi sana. Alifikiri, "Mimi naweza kutii amri kabisa!" (Lakini alijidanganya!)

- **Yesu alimwambia nini alipouliza, "Sheria gani"?**
    - o Alitaja baadhi ya sheria za Mungu.
- **Je, ni sheria gani sisi tunaweza kujaribu kutii ili tuhisi "sisi ni wenye haki"?**
    - o
- **Kijana alijibu vipi?**
        - ▪ Basi, nimeshashika hizi zote! Niongeze nini kingine?
    - o Alihisi vipi aliposikia Yesu kutaja sheria fulani? Alifurahi sana kwa sababu alifikiri kwamba amefaulu! Alitarajia sheria zingine aweze kutimiza. Hii ingeweza kuongeza kiburi chake!

- **Kwa hivyo alifikiri nini kuhusu kutii sheria za Mungu?**
    - o Alifikiri kwamba utiifu wa sheria ya Mungu unawezekana!
    - o Hii inonyesha nini juu ya fikira zake kuhusu utakatifu wa Mungu?
        - ▪ Ilionyesha kwamba hakuheshimu sana utakatifu wa Mungu. Alifikiri kwamba yeye mwenye anaweza kufikia utakatifu wa Mungu maishani mwake.
        - ▪ Je, kwa njia gani kijani aliweza kujidanganya kwamba ana uwezo wa kutii sheria za Mungu kumpendeza?
            - Pengine kwa kujilinganisha na wengine.

- **Yesu alimjibu vipi?  Alihisi vipi kwake?**
    - Alimpenda sana na akamhurumia.
  - Kwa hivyo, alimsisitiza kuuza vitu vyake kumwumiza au kumsaidia?
  - Yesu alisema nini?
    - "Kama ukitaka kuwa mkamilifu, nenda, kauze vitu vyote ulivyo navyo na hizo fedha uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo, unifuate."
  - Yesu aliposema, "Kama ukitaka kuwa mkamilifu," ilimaanisha nini? Haya maneno yanamwonyesha kijana nini kuhusu kupata maisha ya milele kupitia kutii sheria?
    - Ukitaka kutii sheria kupata wokovu, lazima ufanye bila kukosa. Ukikosa sheria hata kidogo, utakosa wokovu!

- **Yesu alimwamuru "uuza zote."  Baada ya hii, kijana alihisi vipi? Kwa nini?**
  - Alikuwa na huzuni mwingi.  Akamwacha Yesu akaenda zake kwa sababu ya mali nyingi.
  - **Hii inatuonyesha nini juu ya kijana?**
    - Mali yake ilikuwa ya muhimu sana kwake kuliko maisha ya milele, kuliko uhusiano na Mungu. Aliitegemea kwa maisha yake – kukula, kumpatia sifa, kumpatia maisha ya anasa.
  - Inatuonyesha nini kuhusu maisha ya milele au azizi za mbingu?
    - Hakuamini sana. Maisha katika mbingu siyo muhimu kwake kama maisha hapa duniani. Hakuamini kwamba hakuna kitu muhimu kuliko uhusiano na Mungu.  Uhusiano huu ni maisha!
    - Ni UHUSIANO na Yesu!  Katika uhusiano huu ni mali nyingi ya dhamani! Tunahitaji uhusiano huu pekee!  Unapatikana saa hii.

- **Baada ya kijana kuenda zake, Yesu aliwaambia wanafunzi nini?**
  - Itakuwa vigumu kwa mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mbinguni. Tena, ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu
  - Waliposikia haya wanafunzi  walisema nini?
    - Kama mtu mtiivu tajiri kama huyu hawezi kuokoka, ni nani basi awezaye kuokoka?
  - Kwa nini walishangaa sana?
    - Kwa maana walifikiria kama kijana au kama dunia, kwamba lazima ustahili au ufanyie kazi kila kitu ambacho unapata.  Walifikiri kwamba Mungu alimbariki kwa sababu ya haki yake. Walifikiri kwamba alistahili baraka zake!

- **Yesu aliwajibu vipi?**
    - Kwa mwanadamu haiwezekani.  Kwa Mungu kila kitu kinawezekana!
  - Yesu alimaanisha nini alivyosema hivyo? Alikuwa anasema nini kuhusu njia ya kujiokoa kupitia kutii amri kama kijani na wanafunzi walitaka kutegemea? Je, njia hi inafanyika?
    - Yesu aliwaonyesha kwamba njia hii haifanyiki!  Haina maana. Mungu tu anaweza kutimiza sheria!  Yaani, Yesu alikuwa mwanadamu mmoja pekee ambaye aliweza kufuata sheria kamili. Mungu peke yake anaweza kutupatia wokovu.  Haiwezekani kwa wanadamu. Kuna njia moja tu kwa mwanadamu kupata wokovu au kupata maisha tele - yaani ikiwa Mungu mwenyewe aliweza kuwa mwanadamu na kutii sheria kamili kwa niaba ya wanadamu.Yesu alifanya hivyo! Lazima mwanadamu kuweka amani yake katika huyo aliyeweza kutimiza amri. Hii ndiyo njia ya kupata maisha tele au maisha ya milele!

- **Kwa hivyo katika hadithi hii kuna njia mbili ya kujaribu kupata maisha. Hizi ni gani? Ni njia ngani moja iliyofanya?**
  - 1) kujitegemea – kupitia sheria, 2) kumtegenea Mungu na njia yake ya kutubu na kumwamini Yesu.
- **Je, mali ya kijana ilikuwa inamsaidia au kumwumiza? Ilikuwa inamwumiza vipi?**
  - Ilimwumiza kwa maana ilimzuia kuwa na uhusiano na Yesu.

- **Je, Mungu anachukia mali? Je, Mungu anaweza kuhakikisha kila mtu kuuza mali yake yote na kuwa mtajiri kabla ya kuweza kufuata Mungu vizuri? Kwa nini unafikiri Yesu alimwambia kijana kuuza yote? Unafikiri Yesu alitambua nini ndani ya moyo wa kijana?**
    - o Aliona kwamba kijana alikuwa anaweka tumaini yake yote katika mali yake – kama ilivyomsaidia na mahitaji yake na sifa yake na haki yake mbele ya watu.
- **Yesu alipotaja "mtu tajiri," inamaanisha nini? Je, inamaanisha mali ya dunia peke yake?**
    - o Hapana. Anaongea kuhusu mali ya kila aina, baraka zozote, uwezo wowote, bidii yoyote, vitu vyovyote ambavyo mtu anaweza kuvzitegemea kuliko Mungu kuhesabiwa kama mwenye haki mbele ya Mungu.
- **Taja mifano ya "mali" tunaweza kuona katika maisha yetu?**
    - o Shamba, ng'ombe, elimu, sifa, tabia nzuri, nafasi ya juu katika kanisa au katika jamii, afya, uwezo, talanta, ufanisi, ujuzi, n.k.
- **Je, mali kama hii inaweza kutuletea shida katika maisha yetu, ata kwa Wakristo?**
    - o Ndiyo! Tunaweza kuzitegemea kubarikiwa na Mungu, kuhifadhi sifa zetu. Lakini tukijaribu hii, zinaweza kuzuia uhusiano na Mungu. Yesu anataka tumtegemee kila wakati. Hataki tuitegemea mali yetu. Anataka tuitumie mali yetu kumpatia utukufu. Lakini hatuwezi kuitegemea kujiokoka.
- **Kwa nini hatuwezi kujiokoa kupitia kutii sheria?**
    - o Kwa sababu kiwango cha Mungu hakifikiwi. Lazima tuwe bila waa, bila kosa. (SOMA Matayo 5:20,21,22,27,28,43,44) Hakuna mtu anaweza kutimiza kiwango hiki.
    - o Yesu alisema,"Haiwezekani."
- **Wanafunzi hawakuwa na tumaini ya kuokoka! Lakini Yesu aliwapatia tumaini gani?**
    - o "Kwa Mungu, mambo yote yanawezekana." Huruma ya Mungu ni ya kushangaza!

- **Kwa jumla:** Mungu anataka kutuambia sisi sote, "Utajiri wako, au mali yako inazuia uhusiano na mimi!" Lazima uuze yote! Azizi za mbingu zinabaraka kuliko mali ya dunia. Halafu, nifuate. Kaa nami. Pokea nguvu zangu. Pumzika ndani yangu."

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- **Je, mara nyingi tunadanganywaje na jitihada zetu wenyewe za kuwa wema?**
    - o Kwa kujitahidi sana kushika sheria zote za Biblia au kanisa (au shule, au utamaduni) hivi kwamba unafikiri kwamba umefaulu au kufikiri kwamba umeshika sheria kikamilifu**.**
    - o **Lakini ukweli ni upi kuhusu utunzaji wako wa sheria?** Je, umewahi kutamani au kuchukia au kusengenya au kuwa na kiburi? Bila shaka umefanya hivyo! Je, daima wewe humwombea adui yako? N.k. Je, ni nini hasa ambacho Mungu anadai? Anadai kutii kikamilifu!

- Yesu anaambia kila mmoja wetu**, "Uza vyote!"** Unafikiri anamaanisha nini anapokuambia "Uza vyote?"

- **Mungu anahisije hasa kukuhusu?** (Kumbuka jinsi Yesu alivyohisi kuhusu kijana huyo alipoona jinsi alivyodanganywa kwa kujifanya mwenye haki na pia na utajiri wake mwenyewe). Je, unaweza KUFANYA chochote ili kumfanya akupende zaidi? HAPANA! Je, hii inakufanya uhisije? Je, inakufanya utake kufanya nini? Unawezaje kuitikia sasa kwa upendo wake mkuu kwako?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je, ni utajiri gani wa duniani ambao unao maishani mwako?** Ni mali?Uwezo? Elimu? Afya? Sifa ama cheo kanisani au kwa jumuiya? Mafanikio au matendo mema? Je umeyaruhusu vipi haya mambo kukudanganya, yaani **kukutosheleza hadi humtazamii Yesu** kupata msamaha na msaadakutoka kwake? **Je, itakaa vipi kwako kuuza jambo hili?**

- Je kuna matendo mema maishani mwako ambayo unahitaji kutubu? **Yaani, je, kuna wakati hivi majuzi matendo yako mema yalikufanya uwe na dhambi ya kiburi?** Unawezaje kutubu dhambi hii?

## 36. YESU APAKWA MAFUTA NA MWANAMKE MWENYE DHAMBI
## Luka 7:36-50

Basi Farisayo mmoja aliyeitwa Simoni alimwalika Yesu nyumbani kwake kwa chakula. Hivyo Yesu akaenda nyumbani mwa yule Farisayo na kukaa katika nafasi yake mezani. Naye mwanamke mmoja kwenye ule mji, ambaye alikuwa mwenye dhambi, alipojua kwamba Yesu alikuwa akila chakula nyumbani kwa yule Farisayo, akaleta chupa ya marimari yenye manukato. Yule mwanamke akiwa amesimama nyuma ya miguu ya Yesu alilia. Akailowanisha miguu yake kwa machozi yake, kisha akaifuta kwa nywele zake akaibusu na kuimiminia manukato.

Yule Farisayo aliyemwalika Yesu alipoona yanayotendeka, akawaza moyoni mwake, “Kama huyu mtu angekuwa nabii, angejua kwamba ni nani anayemgusa na kwamba yeye ni mwanamke wa namna gani na ya kuwa huyu mwanamke ni mwenye dhambi.”

Yesu akanena akamwambia, “Simoni, nina jambo la kukuambia.” Simoni akajibu, “Mwalimu sema.”

“Palikuwa na mtu mmoja aliyewakopesha watu wawili fedha: Mmoja alidaiwa dinari mia tano na mwingine dinari hamsini. Wote wawili walipokuwa hawawezi kulipa, aliyafuta madeni yao wote wawili. Sasa ni yupi kati yao atakayempenda yule aliyewasamehe zaidi?”

Simoni akajibu, “Nadhani ni yule aliyesamehewa deni kubwa zaidi.” Naye Yesu akamwambia, “Umehukumu kwa sahihi.”

Kisha akamgeukia yule mwanamke akamwambia Simoni, “Je, unamwona mwanamke huyu? Niliingia nyumbani mwako, hukunipa maji ya kunawa miguu yangu, lakini huyu ameninawisha miguu kwa machozi yake na kunifuta kwa nywele zake. Hukunisalimu kwa busu, lakini huyu mwanamke hajaacha kuibusu miguu yangu tangu nilipoingia. Hukunipaka mafuta kichwani mwangu, lakini yeye ameipaka miguu yangu manukato. Kwa hivyo, nakuambia, dhambi zake zilizokuwa nyingi zimesamehewa, kwa hivyo ameonyesha upendo mwingi. Lakini yule aliyesamehewa kidogo, hupenda kidogo.”

Kisha akamwambia yule mwanamke, “Dhambi zako zimesamehewa.” Lakini wale waliokuwa wameketi pamoja naye chakulani wakaanza kusemezana wao kwa wao, “Huyu ni nani ambaye hata anasamehe dhambi?”

Yesu akamwambia yule mwanamke, “Imani yako imekuokoa, nenda kwa amani.”

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Umewahi kumjua mtu ambaye alihisi aibu sana juu ya jambo fulani, hata akaepuka watu wengine? Au kulikwepa kanisa? Ikiwa unajisikia huru, zungumza kuhusu hili na jirani yako.**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

Tunajifunza nini kuhusu YESU? Na kwamba Yesu ni Mungu mwenyewe?

- **Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu nguvu ya Yesu?**
    - Alikuwa na nguvu kusamehe na kuwaokoa wenye dhambi wabaya. Alikuwa na uwezo wa kubadilisha maisha ya mwanamke ili hakuwa na aibu kuingia nyumba ya Farisayo.

- **Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu hekima ama ujuzi ya Yesu?**
    - Alijua Simoni alivyofikiri na alivyomhukumu Yesu.
    - Alijua moyo wa mwanamke na dhambi zake.

- **Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu neema ya Yesu?**
    - Alimkaribisha mwanamke alipokuja kupitia imani.
    - Alimkaribisha Farisayo katika maisha yake kwa kuenda nyumba yake na kualika kuamini hata kama baado hatuwezi kuona toba yake.
    - Aliahidi kwamba yule aliyesamehewa nyingi ataweza kuwapenda wenye dhambi wengine sana.

- **Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu uaminifu ya Yesu?**
    - Mwokozi aliyeahidiwa angesamehe dhambi na kuivunjua laana ya dhambi. Alifanya hivyo na huyo mwanamke.

Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu MWANADAMU?

**Kuna watu wawili muhimu katika hadithi hii pamoja na Yesu. Katika hawa wawili nani ni mwenye dhambi?**

- Wote wawawili!!! Dhambi ya mwanamke ilikuwa maisha mabaya, labda uasherati. Dhamba ya Farisayo ilikuwa kiburi, majivuno, na kuhukumu wengine.

**Ni nani aliyesamehewa? Ni nani asiyesamehewa?**

- Mwanamke alisamehewa. Farisayo hakusamehewa.

**Tofauti ni nini katikati ya watu hawa wawili kwa njia zao kukabiliwa na dhambi zao?**

- Mwanamke alizijua na kuziungamisha dhambi zake. Alijua kwamba alihitaji Mwokozi. Alikufuraha kupata Mwokozi. Lakini Farisayo hakukubali dhambi zake. Kwa hivyo hakuweza kupokea Mwokozi.
- Kwa sababu mwanamke alihisi upendo na rehema ya Mwokozi, aliweza kuonyesha upendo wake wazi wazi. Hakuogopa watu wengine au mawazo yao. Alimpenda Mwokozi! Kwa hivyo angeweza kuwapenda watu wengine pia, labda kuwaambia wengine kuhusu mahali alipopata usaidizi, yaani kuhusu Mwokozi.
- Farisayo alikuwa na kiburi nyingi. Alihukumu wengine. Alikuwa na chuki. Hakutambua dhambi zake au hatari yake kiroho.

        - Kwa hivyo hakuweza kuwapenda wengine. Aliwachuki wengine. Alijipenda mwenyewe peke yake.
        - Kuamini dhidi ya kutoamini – injili ya Yesu.
            - Kusamehewa (mwanamke) dhidi ya kutosamehewa (Farisayo)
            - Kuwapenda wengine (mwanamke) dhidi ya kutowapenda wengine (Farisayo)

    **Yesu alisema, "Dhambi zake zilizokuwa nyingi zimesamehewa, kwa sababu ameonyesha upendo mwingi. Lakini yule aliyesamehewa kidogo, hupenda kidogo." Je, hii inamaanisha nini? Je, mwanamke alistahili kusamehewa kwa sababu ya upendo wake?**

        - Hapana! Yesu alisema, "Imani yako imekuokoa." Si upendo wako.
        - Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba UPENDO ni shuhuda ama hakikisho ya msamaha wake na uokovu wake.

- **UFUPISHO**

    Mtu ambaye amesamehewa na kuamini na kuishi ndani ya msamaha hupenda Mungu na mwanadamu!
    Injili ni nini? Injili ni kama maskini ama fukara awezaye kuwaongozea maskini wengine kwa chakula.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Je, ni watu wa aina gani ambao huwa tunapata ugumu sana wa kuwapenda? Je, ni nani ambaye sisi humwukumu kwa ukali sana?

- Je, ukitambua kwamba wewe ni mwenye dhambi mkubwa na jinsi unvyoahitaji Mwokozi wakati wote, jambo hili linawezaje kubadilisha mawazo yako kuhusu jirani yako ama adui wako? Kwa njia gani?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>**

- **Ni nani ambaye huwezi kumpenda?** Je, ni nani unayehukumu kwa ukali? Ni nani unaonea wivu? Ni nani huwezi kusamehe? Je, inawezekana kwamba shida ni kwamba wewe hujawahi kusikia msamaha wa Yesu katika maisha yako? **Je, kupokea msamaha wa Yesu kikamilifu zaidi kunaweza kukusaidia vipi kumpenda huyu mtu?**

## 37. MEZA YA BWANA YA MWISHO
## Luka 22:1-22; Matthayo 26:26-30; 1 Wakorintho 11:23-25

Wakuu wa makuhani na walimu wa sheria walikuwa wakitafuta njia ya kumwua Yesu. Shetani akaingia ndani ya Yuda Iskariote mmoja wa wanafunzi kumi na wawili wa Yesu ili amsaliti. Kwa hivyo Yuda alikwenda kwa viongozi wa Wayahudi na kukubaliana nao kumtoa Yesu kwao kwa kulipwa fedha fulani.

Wakati huo ulikuwa wa sherehe za pasaka naye Yesu alikuwa amewatuma wanafunzi wake kuandaa sherehe hiyo. Akasema, "Nimetaka sana kula chakula cha pasaka nanyi kabla ya kuteseka. Sitakula tena mpaka wakati wake kamili utakapotimizwa katika Ufalme wa Mungu. Lakini mmoja wenu hapa atanisaliti. Mwana wa Adamu atakufa jinsi Mungu alivyoamua lakini ole wake mtu anayemsaliti!"

Wanafunzi wakafadhaika, wakaanza kumwuliza, "Je! Bwana, ni nani?" "Ni mmoja wa wale kumi na wawili, ambaye anachovya mkate katika sahani pamoja nami."

Baada ya kula chakula cha pasaka, Yesu alichukua mkate, akashukuru, akaumega akawapa wanafunzi akisema, "Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka." Katika njia hiyo, Yesu akakichukua kikombe akasema, "Hili ndilo agano langu jipya katika damu yangu ambayo itamwagika kwa ajili ya msamaha wa dhambi."

Baada ya kushiriki katika mkate na kikombe na baada ya Yuda kutoka nje, Yesu akasema "Ninyi nyote mtanitoroka. Lakini baada ya kufufuka, nitakutana nanyi katika Galilaya." Nao wanafunzi wakahuzunika sana. Baada ya chakula cha pasaka kuisha waliimba zaburi. Kisha wakaondoka mji wa Yerusalemu kuenda kwenye bustani katika Mlima wa Mizeutuni pamoja.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Meza ya Bwana ina maana gani kwako? Unafikiri kwa nini tunafanya hivyo kanisani?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu / Yesu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
    - Mungu alikuwa na mamlaka juu ya kuteseka kwa Yesu kwa ajili ya dhambi zetu.
    - Mungu katika ukuu wake huruhusu Shetani kuwafanya watu kufanya vitu vibaya, lakini yeye hufanya mambo haya kulingana na mpango wake. Kama Yuda na usaliti wake.

- Mamlaka ya kuwaamuru wanafunzi wake.
- Hadi wakati ule nitakula nanyi katika ufalme wa Mungu – atafufuliwa tena.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha vipi kwamba Mungu anajua kila kitu?**
    - Alijua kwamba atateseka.
    - Alijua atafufuka.
    - Alijua Yuda angemsaliti. Alijua yale Shetani alikuwa amefanya.
    - Alijua kwamba wanafunzi wake wangetoroka.
    - Alijua kwamba msamaha wa dhambi ungekuja tu kupitia kuteseka kwake mwenyewe.
    - Alijua kwamba angekutana na wanafunzi baada ya kufufuka.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba Mungu ni mtakatifu?**
    - Ghadhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi ingelipiwa tu kwa kifo cha Yesu. Yesu alipaswa kuteseka.
    - Atateseka, yule ambaye atamsaliti Mwana wa Adamu. Ni lazima dhambi kuadhibiwa.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi  kwamba Mungu ni mwenye neema?**
    - Yesu angepeana mwili wake kuvunjwa na damu yake kumwagika ili kuleta njia ya msamaha wa dhambi.
    - Alipeana mkate na mvinyo kuwafunza wanafunzi kuhusu kifo chake na kutusaidia kukumbuka dhabihu yake kwetu mpaka atakaporudi.
    - Kama vile Yesu alivyo mkate wa uzima, ndivyo mesa ya Bwana inavyotupa chakula cha kiroho kutusaidia kukumbuka Yesu.  Ni chakula kwa wenye dhambi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi kwamba Mungu ni mwaminifu?  (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema.**
    - Meza ya Bwana inatukumbusha pasaka na ahadi ya Mungu ya Mwokozi. Yesu angekuwa Mwanakondoo mwaminifu wa Mungu ikielekezwa kwake na pasaka na kila aina ya dhabihu takatifu. Alikuwa mwanakondoo anayeteseka aliyetabiriwa na Isaya.
    - Mvinyo – unatosha kwa mada ya damu katika kila pahali katika maandiko.
    - Yesu aliongea kuhusu agano jipya akiwakumbusha mafunzo ya nabii Yeremia.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- Yuda alishindwa na majaribu. Inaonyesha dhambi ya mwanadamu. Hata baada ya miaka mitatu katika uwepo wa Yesu, Yuda hakuamini kwa halisi.  Moyo wake ungekubali kuelekezwa na Shetani.
- Yesu alitabiri kwamba wanafunzi wangemtoroka. Wote walikuwa dhaifu na wasiojisaidia wenyewe. Hakuna yule aliyekuwa na nguvu kusimama na Yesu katika mateso yake.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**

- Mwanadamu anaweza kusamehewa tu kwa sababu Yesu alitoa mwili na damu yake mwenyewe kama dhabihu.
- Mtu anamjia Mungu kupitia kwa imani katika dhabihu ya Kristo. Meza ya Bwana inatusaidia kukumbuka na kuweka imani yetu dhabiti.  Mwanadamu hawezi kufanya imani yake mwenyewe. Hata imani ni kipawa cha Mungu.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Yesu aliwaambia wanafunzi wake, “ Ninyi nyote mtaniacha, lakini baada ya kufufuka nitakutana nanyi Galilya.”  Haya maneno yanatufunza nini kuhusu Mungu nasi? Yanaweza kutufunza nini tunapokosa?
    - Yesu anajua kwamba tutatenda dhambi na kumsaliti nyakati fulani. Hata hivyo, ana mikono yake juu yetu na hatatuacha kamwe. Kwa hiyo, bado atatuongoza kwenye toba na ataendelea kufanya

kazi nasi na kuwa pamoja nasi - yote kwa sababu alikufa na kufufuka tena. Hatachoka nasi lakini ataendelea kufanya kazi njema aliyoianza ndani yetu.

- Yesu alisulubishwa ili tuweze kuwasiliana na Mungu. Tunawezaje kutafuta kuwa na ushirika na Mungu?
    - Kupitia kwa neno, maombi, kuabudu, na meza ya Bwana, n.k.
- Yesu aliahadi kwamba kutakuwa na siku tutashiriki naye mbinguni. Je, unawezaje kuwa uhakikisho kwamba utakuwa huko pamoja naye? Ikiwa una uhakika, haya yatabadilishaje jinsi unavyoishi maisha yako kila siku?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- Ni katika suala gani maishani mwako siku hizi ambapo wakati mwingine hujaribiwa kumkimbia Mungu au kujitegemea zaidi kuliko Yeye?

- Maneno ya Yesu, “Nikishafufuka, nitakutana nanyi Galilaya,” yanawezaje kukutia moyo katika toleo hili?

## 38. GETHSEMANE, KUSHIKWA KWA YESU, NA KUPELEKWA KWA PILATO
## Matthayo 26:36-50; Yohanna 18:12-19:16

Baada ya Yesu na wanafunzi wake kumaliza kula Pasaka, aliwaleta nje ya mji kwenye Mlima wa Mizeutuni katika bustani iitwayo Gethsemane. Akawaambia "Kesheni mkiomba ili msiingie majaribuni." Akachukua Petero, Yakobo, na Yohana akaenda nao hatua chache, akasema, "Roho yangu ina huzuni kiasi cha kufa. Kaeni hapa mkeshe pamoja nami." Akaenda mbele kidogo akaanguka na kuomba akisema, "Baba yangu ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke, lakini si kwa mapenzi yangu ila tu utakavyo wewe."

Yesu alipomaliza kuomba vile akarudi kwa wanafunzi wake akawakuta wamelala akawaamsha na kuwaambia, "Hamkuweza kukesha pamoja nami hata saa moja?" Wakaona haya sana. Akaenda tena mara ya pili kuomba akisema, "Baba yangu niepushe kikombe hiki, lakini si kulingana na mapenzi yangu bali mapenzi yako yatimizwe." Akaja tena mara ya pili akakuta wamelala kwa sababu macho yao yalikuwa mazito. Kisha akarudi kuomba mara ya tatu na akaja akawaambia wanafunzi wake, "Amkeni! Saa imekaribia na yule msaliti yu karibu."

Alipokuwa katika kusema, Yuda akaja na kundi kubwa la jeshi akamsalimu Yesu kwa busu na askari wakamshika Yesu wakaenda naye. Wanafunzi wote wa Yesu wakatoroka kwa uoga.

Kwanza, maaskari na viongozi wa Wayahudi walimpeleka Yesu kwa nyumba ya Kuhani Mkuu. Mashahidi walimnenea mambo mengi ya uwongo lakini alikuwa kimya. Kuhani Mkuu akamwuuliza Yesu. "Hujibu neno, mwanaume? Kwa nini husemi kitu kujitetea? Tuambie, wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu?" Yesu akajibu, "Naam, mimi ndiye. Nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa Mungu." Kuhani Mkuu aliposikia hayo, akararua mavazi yake akisema "Amekufuru! Tuna haja gani tena na mashahidi?" Na watu wote wakasema, "Ana hatia na anastahili kufa!"

Kulipokuwa asubuhi, viongozi wa Wayahudi walikuwa wamemaliza kuuliza Yesu maswali, wakamchukua wakamleta mbele ya Pilato, aliyekuwa kiongozi wa Kirumi katika pahali hapo. Pilato akawauliza, "Ni kosa gani mtu huyu amefanya? Viongozi wa Wayahudi wakasema, "Yeye anasema ni mfalme." Pilato akamwuuliza Yesu, "Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi?" Yesu akasema, "Ndiyo, lakini ufalme wangu si wa ulimwengu huu."

Ndipo Pilato akamtwaa Yesu kwa askari wakampiga mijeledi. Baada ya kumpiga Yesu sana, Pilato akarudi kuongea na Wayahudi akisema, "Mtu huyu namleta kwenu tena, mpate kujua ya kuwa mimi sioni hatia yoyote kwake."

Wakapiga kelele wakisema, “Hapana! Msulubishe, msulubishe!” Pilato akawaambia, “Mimi sioni hatia kwake.” Basi Wayahudi wakapaza sauti wakisema, “Ukimfungua huyu, wewe si rafiki yake Kaisari katika Rumi!” Hatimaye Pilato aliwapa Yesu mikononi mwao ili asulubishwe.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, umekataliwa au kushtakiwa kwa uwongo vipi? Umehisije hakuna mtu upande wako?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?) Vipi?**
    - Mungu alikuwa uongozini. Yesu alinyenyekea katika mapenzi ya Baba wake. Alijua mpango wa Mungu kupeana wokovu kwa wenye dhambi lazima utimizwe.
    - Yesu alisema, “Wakati umefika. Msaliti yuko karibu.” Alijua Mungu alikuwa anafanya mpango wake wa enzi.
    - Yesu hakujaribu kupigana dhidi ya mipango ya Mungu hata aliposhtakiwa kwa njia ya uwongo.
- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu anajua kila kitu? Vipi?**
    - Yesu alijua kuhusu mateso ambayo yalikuwa mbele yake. Alijua jinsi yatakavyokuwa magumu.
    - Alijua “saa ilikuwa imefika.”
    - Alijua kusudi lake la kuja duniani.
    - Alijua kile ambacho Yuda na viongozi wa Kiyahudi walikuwa wakifanya.
- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi? Vipi?**
    - Mungu ni mtakatifu. Dhambi za mwanadamu zingelipwa tu kwa kifo cha Mwanawe.
    - Gadhabu ya Mungu juu ya dhambi lazima ingetoshelezwa.
- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?) vipi?**
    - Mungu hakumhurumia mwanawe, bali alimtoa kulipia dhambi zetu. Alijua jinsi ilikuwa mbaya kwa Yesu, angesikiliza ombi lake lakini akakusudia kwamba bado lazima afe kwa ajili ya dhambi zetu.
    - Alimruhusu mwanadamu mwenye dhambi kumsaliti, kumshitaki kwa madai ya uwongo, kumpiga na mwishowe kumsulubisha Yesu.
    - Mungu alimpa Yesu neema ya kuvumilia katika mateso yake, na kwa uvumilivu kuruhusu mambo hayo yafanyike.
    - Yesu alikuwa mwenye uvumilivu kwa udhaifu na hofu ya wanafunzi wake. Hakuwakataa hata walipomkosea.
    - Yesu alikuwa mtu mkamilifu. Kwa neema alinyenyekea kwa mateso makuu ya kibinadamu kwa niaba yetu.
    - Unyenyekevu wa Kristo - Hata ingawa alikuwa Mungu wa mbingu na ardhi, aliteseka kwa dhihaka kuu kwa sababu ya upendo kwa mwanadamu.
- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**

- Ahadi ya Mungu katika bustani ya Edeni kumleta mwokozi ambaye angemshinda Shetani ilitimizwa. Ilikuwa ni ahadi sawa ambayo alipewa Abrahamu kwamba atabariki mataifa yote kupitia kwa uzao wake. Ilikuwa ni ahadi iliyorudiwa katika historia yote ya Israeli. Hakubadili mipango yake hata ngawa ilimaanishwa kusema "HAPANA" kwa mwana wake mwenyewe na hata kutomsikiliza kwa muda mfupi.
- Yesu alijua mpango wa Mungu na akakataa kwenda kinyume na mpango huo, hata ingawa ilimaanisha uchungu mkubwa kwa yeye mwenyewe.
- Inatukumbusha unabii wa Isaya kuhusu Mwokozi ambaye atateseka, kuongozwa kifoni kama mwanakondoo atakayechinjwa bila kujitetea.
- Unabii uliyotimizwa
- Zaburi 41:9 – kusalitiwa na rafiki.
- Isaya 53:3 – kukataliwa na Israeli.
- Zekaria 11:12-13 – kusalitiwa kwa vipande thelathini vya fedha.
- Zaburi 27:12 – kushtakiwa kwa madai ya uwongo.
- Isaya 53:7 – alibaki kimya mbele ya washtaki wake.

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- Mwanadamu ni mwasi dhidi ya Mungu. Yeye mwenyewe hataki mapenzi ya Mungu juu yake. Anataka kutawala maisha yake. Watu wote wa kidini walikataa kuziangalia dhambi zao wenyewe na kuziungama na kushindwa kwao na kunyenyekea kwa mpango wa Mungu.
- Mwanadamu hawezi kujiokoa. Hata wanafunzi, wale waliokuwa karibu sana na Yesu, wale ambao walikuwa wamesikia maneno yake na kuona miujiza yake, walikuwa wadhaifu mno kusimama naye.
- Dhambi za mwanadamu ndizo sababu ya Yesu kunyenyekea kwa dhihaka na uchungu huo.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**
**Jinsi mtu anavyohusiana na Mungu?**

- Yesu aliomba kwa Baba wake. Hata Mwana wa Mungu alimsihi. Mungu lakini pia alikuwa na imani kamilifu katika kusudi la Mungu kwake.
- Kuendelea katika maombi. Yesu alirudia ombi lake mara tatu.
- Mwanadamu anaweza kuokolewa tu kwa mpango wa Mungu hawezi kujiokoa.
- Tunawezaje kujifunza katiaka hadithi hii kutoka kwa Yesu jinsi ya kukabiliana na majaribu?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Je, ni hali gani kama waumini tunaweza kumbana nazo leo ambazo zinazofanya tuhisi kwamba tumeachwa au kushtakiwa kwa uwongo? Tunahimizikaje kujua ya kwamba Yesu mwenyewe alipitia haya pia?
- Je, kukumba matukio ya kuteswa kwa Yesu kutatusaidiaje kukuza imani yetu?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>** (chagua moja au mbili)

- **Je, ni wakati gani umewahi achwa au kushtakiwa kwa uwongo, na ikaonekana kwamba hakuna aliyekutetea? Je mfano wa yale Yesu alipitia utakuhimiza vipi? Dhabihu Yake msalabani inawezaje kupa nguvu za kustahimili?**

- Je, umefikiria jinsi Mungu anavyokupenda sana na yale ametenda kukuokoa? Chukua muda utafakari yale Yesu alipitia kule Gethsemane na mbele ya watawala. Kumbuka kuhusu gharama Yesu alilipa kwa ajili ya wokovu wako. Je, haya yatakuathiri vipi kama mtu binafsi?

## 39. KUSULUBISHWA KWA YESU
## Jn. 19:16b-42; Mat. 27:27-61; Mk. 15:16-47; Lk. 23:26-56

Baada ya kusimama mbele ya Pilato, Yesu alikuwa amepigwa sana, na askari wa Kirumi walikuwa wamemvika taji ya miiba kichwani ili kumdhihaki. Damu ilitiririka kwenye uso wake na kwenye mgongo wake alipokuwa amepigwa. Baada ya Pilato kuwapa maaskari Yesu kusulubishwa, Maaskari wa Kirumi walimfanya Yesu kuubeba msalaba wake mwenyewe. Yesu alipoubeba mpaka pahali alipoweza, maaskari wakamlazimisha mtu kutoka kwenye kusanyiko, kumbebea Yesu msalaba. Jina lake lilikuwa Simoni Mkurene. Wakatembea kupitia barabara za Yerusalemu na nje ya mji na hadi juu ya mlima ulioitwa Golgotha.

Walipofika Golgotha, walimsulubisha Yesu pamoja na wezi wawili. Kwanza maaskari waliweka mbao chini kama msalaba na wakamweka Yesu juu ya hizo mbao. Kisha wakaifungia mikono yake kwa mbao kwa kutumia kamba na wakagonga misumari mikubwa kupitia mikono na miguu yake hadi kwenye mbao. Hivi ndivyo walivyoweka Yesu msalabani. Basi, kwa kutumia kamba, waliuinua msalaba hewani wakausimamisha. Pia wakawasulubisha wezi wawili vivyo hivyo, mmoja kwa kila upande wa Yesu. Baadaye, waliketi chini ya msalaba wakaanza kuipigia kura nguo yake.

Kulikuwa na watu wengi karibu wakitazama kuona ni nini kingefanyika. Kulikuwa na wanawake waliomfuata katika huduma yake yote. Walikuwa wanasimama wakitazama kila kitu kwa karibu. Makuhani wakuu na walimu wa sheria walikuweko pia. Walikuwa wakimdhihaki na kumtusi na kumchekelea. “Aliwaokoa wengine. Kwa nini hawezi kujiokoa?”

Mmoja wa wezi pia alimdhihaki na kumtukana Yesu. Lakini mwingine alimkemea akisema, “Hapana! Nyamaza! Sisi tuna hatia. Tunastahili kusulubishwa, bali mtu huyu hana hatia.” Kisha akamwambia Yesu, “Nikumbuke utakapofika katika ufalme wako.” Yesu akamjibu, “Nakuambia ukweli, leo hii utakuwa nami katika Paradiso.”

Ilipokuwa karibu na adhuhuri kulikuwa na giza kuu katika nchi yote mpaka saa tisa. Wakati huo kulikuwa na tetemeko la ardhi kubwa sana na watu wote waliogopa. Wakati huo, Yesu alilia kwa sauti kuu, “Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?” Pia akasema, “Imeisha!” Kisha akatoa roho kwa Mungu akafa. Hata pazia ndani ya hekalu iliraruka katika vipande viwili toka juu hadi chini. Kulikuwa na amrijeshi wa Kirumi chini ya msalaba, alipoona mambo haya yote, akasema, “Hakika, huyu alikuwa Mwana wa Mungu.”

Ilikuwa mila ya Wayahudi kutoacha maiti zikining’inia usiku wote hata siku ya Sabato. Kwa hivyo, wakawaomba maaskari kumaliza kazi yao. Maaskari walivunja miguu ya wezi wawili nao walikufa haraka. Lakini walipomwendea Yesu, walipata kwamba

alikuwa ameshakufa. Kwa hiyo hawakuivunja miguu yake kama ilivyotabiriwa. Mmoja wa maaskari alidunga mkuki kwenye upande wa Yesu. Alipotoa mkuki, damu na maji yalimwagika kutoka mwili wa Yesu.

Mwanamume mmoja aliyeitwa Yusufu wa Arimathea aliomba ruhusa ili kuchukua mwili wa Yesu. Akauchukua mwili na kuuzika katika kaburi lililokuwa karibu ambalo halikuwa limetumika kamwe. Kisha akabingirisha jiwe juu ya kaburi na akaenda zake. Lakini wanawake waliomfuata Yesu katika huduma yake yote, walitazama mambo yote kwa uangalifu na kuona pahali ambapo Yusufu alimzika Yesu.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, kuelewa au kukumbuka kifo cha Yesu msalabani kunaathirije maisha yako ya kila siku?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Tunajifunza nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
  - Anga ilibadilika kukawa giza mchana.
  - Mungu alituma tetemeko la ardhi.
  - Mungu alirarua pazia ya hekalu katika vipande viwili Yesu alipokufa.
  - Mungu alitetemesha mioyo ya watu kama mkuu wa jeshi la kirumi.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu / Yesu anajua kila kitu? Vipi?**
  - Yesu alikuwa ametabiri kufa kwake na mateso yake mara nyingi.
  - Yesu alijua kile alikuwa anakumbana nacho na hakupinga.
  - Yesu alijua kwamba mwizi angekuwa naye katika paradiso.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi?) Vipi?**
  - Yesu alikuwa dhabihu kamilifu. Alikuwa bila dhambi au waa lolote. Ni yeye tu ambaye angekuwa dhabihu inayofaa kwa dhambi zetu ili kutosheleza gadhabu ya Mungu. Alichukua adhabu yetu.
  - Kama mwanakondoo wa pasaka, mifupa yake haikuvunjwa.
  - "Imekwisha!" Yale yote ambayo Kristo alipaswa kufanya kutosheleza ghadhabu ya Mungu kumwezesha kuwapa wenye dhambi upendo yalikuwa yametimizwa.
  - Pahali patakatifu zaidi palikuwa pamewezeshwa kufikiwa kwa kifo cha Kristo. Inatukumbusha kwamba Mungu ni mtakatifu sana na tunaweza tu kwenda kwaye ikiwa yeye mwenyewe atatengeneza njia. Alifanya hivyo katika Kristo.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?) vipi?**
  - Yesu alijinyenyekesha kwa kila aina ya dhihaka na mateso ili kutuokoa sisi wenye dhambi.
  - Alitemewa mate, dhihakiwa, tusiwa na kuchekelewa.

- Alipigwa, pigwa mateke, kufanywa kubeba msalaba wake, kusulubishwa, kuwa msalabani kwa uchungu, kisha akafa.
- Aliteseka uchungu wa babake kutomsikia. Alijitoa kwa hiari. Mungu alimtoa kwa sababu alitupenda sana.
- Yesu alikufa ili wale wanaomwamini waweze kuishi.
- Mungu aliupenda ulimwengu kwamba alimtoa mwanawe mmoja na wa pekee ili yeyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.
- Kristo alimwaga damu yake na kuuvunja mwili wake kwa wenye dhambi sisi.
- Pazia ya hekalu ilipasuka. Wenye dhambi sasa wanaweza kuingia pahali patakatifu zaidi kwa imani katika damu ya mwanakondoo, Yesu Kristo.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
    - Alitimiza ahadi ya Mungu katika bustani ya Edeni na kila pahali katika maandiko kwamba Mungu angemtuma Mwokozi kwa ulimwengu ili atoe uhai wake kwa wenye dhambi.
    - Yesu kwa kweli ndiye aliyekuwa Mwanadondoo halisi wa Mungu aziondoaye dhambi za ulimwengu.
    - Yesu alikuwa mwanakondoo kamilifu, bila dhambi. Mifupa yake haikuvunjwa.
    - Yesu alitimiza kazi ya maskani. Kupasuka kwa pazia kunaonyesha kwamba mwanadamu mwenye dhambi hahitaji tena kuhani au dhabihu ya dhambi. Yesu alimaliza kazi ya dhabihu.
    - Mahitaji yote ya dhabihu ya damu yalitimizwa milele katika Kristo. Kila dhabihu ya Agano la Kale ilikuwa inaelekezwa kwa wakati huu.
    - Unabii mwingi ulitimia. Kwa mfano:
    - Isaya 53:4-6 – dungwa, pondwa, teseka kwa dhambi zetu.
    - Isaya 50:6 – pigwa na kutemewa mate.
    - Isaya 53:12 – kusulubishwa na wenye dhambi.
    - Zaburi 22:16; Zakaria 12:10 – Mikono na miguu ilidungwa.
    - Zaburi 22:6-8 – dhihakiwa, tusiwa.
    - Zabur 22:18 – pigia kura mavazi yake.

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- Mwenye dhambi, mwovu, mwasi, mwenye moyo mgumu. Wayahudi walimchukia Yesu, wakafanya auwawe. Walikataa kuamini hitaji lao kwa Mwokozi. Walikataa kuona dhambi yao. Walijaa kiburi.
- Dhaifu, wasioweza kujiokoa wenyewe. Wanafunzi walijificha na kumtoroka Yesu.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u>**
**Jinsi mtu anavyohusiana na Mungu?**

- Ni kwa kumwamini Yesu na kile alichofanya msalabani ndipo watu wanaweza kuokolewa.
- Kama mwanakondoo wa Pasaka, sasa watu wanaokolewa kwa kuweka tumaini lao katika njia ya wokovu ambayo Mungu amepeana. Ni wale wenye dhambi ambao wanajificha nyuma ya damu ya mwanakondoo ambao wanaokolewa kutoka kwa kifo.
- Mwizi alizikubali dhambi zake, akatubu, akmwamini Yesu naye akaokolewa.
- Imekwisha! Yale yote ambayo yalihitajika kutosheleza ghadhabu ya Mungu kwa wenye dhambi yamefanyika.

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Yote yamekwisha! Imekamilika! Yesu amefanya yote ambayo ni muhimu kwako ili ukombolewe kutoka katika dhambi na kifo. Anakuita utubu dhambi zako na kuamini kwa kile alichoteseka kwa ajili yako. Anaendelea kukuita hata baada ya kuokoka. Toba na imani ndicho kiini cha jinsi ya kuendelea kumkaribia Yesu. **Je, kuna nini kinachokuzuia kuchukua hatua hiyo ya toba na imani?**

- Hujafanya lolote kupata wokovu wako kwa hivyo huna sababu ya kuwa na kiburi. Yesu mwenyewe alifanya yote! Mwitikio wako unafaa kuwa wa shukrani na unyenyekevu. Je, kuishi maisha ya unyenyekevu wa kina yanawezaje kukusaidiaje kuwavuta wengine kwa Mwokozi wetu?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- **Je, ni kitu gani maishani mwako kinachokuzuia kuishi maisha ya toba nakuamini injili?**

- Muumini, ikiwa ungeishi kikamilifu zaidi siku baada ya siku kwa kuamini kweli kwamba umeokoka na kutakaswa na kusamehewa, maisha yako yangekuwaje tofauti? **Je, ni juhudi gani za kujiokoa unaweza sasa kuweka kando ili kupata uhuru, ukijua Yesu alimaliza kazi ya kukupa wokovu?**

## 40. UFUFUO
## Mathayo 28:1-15, Marko 16:1-8, Luka 24:1-12, Yohanna 20:1-18

Yesu alizikwa kabla ya jua kutua siku ya Ijumaa, naye Pilato akawaweka maaskari wanne wa Kirumi kulinda kaburi. Sabato ilimalizika jioni ya Jumamosi. Kabla ya jua kuchomoza jumapili asubuhi, wanawake walienda kwenye kaburi wakiwa na manukato na mafuta ili kuutayarisha mwili wa Yesu. Wakiwa njiani waliulizana, "Ni nani atakayetuondolea jiwe?" Kisha kukawa na mtetemeko mwingine mkubwa. Malaika wa Bwana alilimbingirisha jiwe na kulikalia! Maasakari wa Kirumi waliogopa sana wakaanguka chini kama waliokufa.

Malaika akawaambia wale wanawake, "Msiogope. Ninajua mnamtafuta Yesu, lakini hayuko hapa. Amefufuka kama vile alivyosema. Je, hamkumbuki aliyosema – 'Mwana wa Adamu atapeanwa katika mikono ya wenye dhambi, asulubishwe na baada ya siku tatu atafufuka'"? Kisha malaika akasema, "Njooni mtazame alipolazwa. Basi, nendeni upesi mkawaambie wanafunzi wake kwamba anaenda Galilaya mbele yenu na mtamwona huko. Msisahau yale niliyowaambia." Nao wanawake hao wakakimbia kwenda kutafuta wanafunzi wa Yesu.

Wanawake walipoondoka, baadhi ya maaskari walinzi kwenye kaburi walienda kwa makuhani wakuu na kuwaambia kilichotendeka. Hao viongozi wa dini wakawapa hao maaskari pesa nyingi wakisema, "Lazima mseme kwamba wanafunzi wake walikuja na kuiba mwili tulipokuwa tumelala."

Wanawake walipowapata wanafunzi waliwaambia kila kitu kilichofanyika. Lakini wengi wa wanafunzi hawakuwaamini ila Petero na Yohana walikimbia kwenye kaburi. Yohana akafika kaburini kwanza kwa kuwa alikimbia haraka akaangalia ndani lakini hakuingia. Petero alipofika aliingia moja kwa moja ndani ya kaburi. Aliona sanda ambazo Yesu alikuwa amefungwa. Lakini hapakuwa na mwili ndani ya sanda! Kisha Yohana akaingia ndani pia. Wote wakaona kwamba kaburi lilikuwa tupu bila mwili.

Walirudia wanafunzi wengine mahali walipokuwa na wakawaambia walivyoona. Wote walistaajabu kwamba Yesu alikuwa amefufuka. Jioni ya siku hiyo Yesu alitokea katikati ya wanafunzi walipokuwa wamejificha, lakini Tomaso hakuwepo. Baadaye walipomwambia Tomaso kuhusu kujitokeza kwa Yesu, alijibu, "Sitaamini hadi nione alama za misumari na kuweka kidole ubavuni."

Baadaye wanafunzi walipokuwa katika chumba cha juu na mlango umefungwa, Yesu aliwatokea. Akasema, "Amani iwe kwenu. Tomaso, njoo, uone mikono yangu na uweke kidole ubavuni mwangu. Acha shaka na amini!" Tomaso akasema, "Bwana wangu na Mungu wangu!" Yesu akajibu, "Umeona ukaamini lakini wamebarikiwa wale wanaoamini bila kuona."

## MPANGILIO wa SOMO

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Kwa nini ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu ni muhimu?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
    - Alimfufua Yesu kutoka kwa wafu!
    - Alikuwa na mamlaka juu ya uumbaji alisababisha tetemeko la ardhi.
    - Alikuwa na mamlaka juu ya malaika. Malaika alimbingirisha jiwe kisha akaongea na wanawake.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu / Yesu anajua kila kitu? Vipi?**
    - Alikuwa amesema atakufa na kufufuka tena baada ya siku tatu, Halafu yalifanyika!
    - Alijua pahali ambapo wanafunzi wangekutana naye Yesu.
    - Alijua ni lipi lingefanyika kupata ushindi dhidi ya kifo na kujenga imani ya wanafunzi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?) vipi?**
    - Mungu aliwapa wote ambao wanamwamini Yesu ushindi dhidi ya mauti.
    - Alionyesha rehema kwa maskari Wakirumi na viongozi wa dini licha ya dhambi zao dhidi yake kwa sababu aliwapa nafasi ya kuendelea kuishi na kutubu.
    - Mungu aliwasiliana na wanawake kupitia kwa malaika.
    - Yesu alijiruhusu kupeanwa mikononi mwa watu wenye dhambi - kwa ajili ya watu wenye dhambi!

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
    - Yesu alisema tena na tena kwamba angefufuka kutoka kwa wafu – na hilo lilifanyika!
    - Mungu aliahidi katika bustani ya Edeni kwamba angemtuma Mwokozi siku moja, Uzao wa mwanamke ambaye angemshinda Shetani na kushinda kifo ambacho kililetwa ulimwenguni na dhambi ya mwanadamu.
    - Zaburi ilisema Mwokozi atafufuka kutoka kwa wafu naye alifufuka!

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**
- Mwanadamu hung’ang’ana na kutoamini kama vile wanafunzi walivyofanya.
- Mwanadamu hudanganya ili kuficha ukweli, kama vile viongozi wa kidini walivyolipa walinzi kusema uwongo.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU? Jinsi mtu anavyohusiana na Mungu?**
- Mungu alipaswa kufanya njia ya mwanadamu kuokolewa. Ni yeye mwenyewe tu aliyemfufua Yesu.
- Wanawake walimwamini malaika. Mwanadamu anaokolewa kwa imani katika Mwokozi.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Mungu alifanya haya yote kwa ajili yako! Yesu alijitoa mwenyewe kwa watu wenye dhambi ili asulubiwe ili dhambi zako zilipwe. Na akamfufua kutoka kwenye wafu ili kuthibitisha kwamba alikuwa ametushindia kifo. Je, kila mmoja wetu anapaswa kuitikiaje kwa habari hii ya ajabu ya upendo wake?

- Ikiwa Mungu ana uwezo wa kumfufua Yesu kutoka kifoni, yeye ana uwezo wa kutatua shida zetu. Je, ni hali gani ambazo waumini hupitia leo ambapo tunastahili kukumbuka nguvu za Mungu?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):**

- Kufufuka kwa Yesu kunathibitisha ufufuo wetu katika siku ya mwisho kuingia kwa uzima wa milele. Mkristo, kuamini katika ufufuo wako wa siku ya mwisho kunaweza kubadilisha kwa njia gani jinsi unavyoishi maisha yako sasa? **Ni wapi kuna mashaka katika maisha yako? Je, itakuwaje kumwamini Mungu kwa hoja hii au wasiwasi hii leo?**

## 41. BARABARA ya EMAU
## Luka 24:13-35

Siku hiyo hiyo, wawili kati ya wafuasi wa Yesu wakawa wanaenda katika kijiji kimoja kiitwacho Emau umbali wa kilomita saba au kumi kutoka Yerusalem. Wakawa wakizungumza juu ya yale yaliyotukia wakati huo. Walipokuwa wakizungumza na kujadiliana, Yesu mwenyewe akatokea akatembea pamoja nao. Walimwona kwa macho lakini hawakumtambua.

Akawauliza, "Ni mambo gani haya mnayozungumza mnapotembea??" Nao wakisimama kimya, nyuzo zao zikiwa zimejikunja kwa huzuni. Mmoja wao aitwaye Kleopa, akamjibu, "Je, wewe ni mgeni peke yako Yerusalemu ambaye hujui yaliotukia huko siku hizi?"

Naye akawauliza "Mambo gani?"

Nao wakamjibu, "Mambo yaliyompata Yesu wa Nazareti. Yeye alikuwa nabii mwenye uwezo wa kutenda na kufundisha mbele ya Mungu na mbele ya watu wote, makuhani na watawala wetu walimtoa ahukumiwe kufa wakamsulubisha. Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli."

"Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu mambo haya yalipotendeka tena wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushtua walipokwenda kaburini mapema asubuhi wasikute mwili wake. Wakarudi wakasema ya kwamba walitokewa na malaika waliowaambia kwamba yu hai. Wengine wetu walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo, kama wale wanawake walivyosema, ila yeye hawakumwona."

Kisha msafiri (yaani Yesu) akawaambia, "Enyi msiofahamu wenye mioyo mizito kuamini yote yaliyosemwa na manabii. Je, haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake"? Na kuanzia Musa na manabii wote, alieleza kila kitu ambacho maandiko yalisema juu yake mwenyewe.

Walipokaribia kile kijiji walichokuwa wakienda, Yesu akajifanya kama anazidi kuenda mbele lakini wao wakamsihi wakisema, "Kaa pamoja nasi kwa kuwa kumekuchwa na usiku unakaribia." Basi akaingia kijijini akakaa pamoja nao.

Walipokaa kula Yesu akachukua mkate akaubariki, akaumega, kisha akawapa. Mara macho yao yakafumbuliwa wakamtambua. Kisha akatoweka mbele yao. Basi wakaulizana, "Je, mioyo yetu haikuwa inawaka ndani yetu wakati alipokuwa akitufafanulia maandiko matakatifu kule njiani?"

Wakaondoka saa ile ile wakarudi Yerusalemu, wakawakuta wale mitume kumi na mmoja na wale wengine waliokuwa pamoja nao wamekusanyika, wakasema, "Hakika Bwana amefufuka kweli kweli, naye amemtokea Simioni." Basi nao wale wafuasi wawili wakawajulisha yale yaliyowapata njiani na jinsi walivyomtambua katika kumega mkate.

**MPANGILIO wa SOMO**

**UTANGULIZI:** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Je, kuna wakati katika maisha yako ambapo mambo hayakuwa kama ulivyotarajia? Je, Mungu alikusaidiaje kuvuka wakati huo?**

**HADITHI:** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**MJADALA baada ya HADITHI:** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
  - Uwezo wa kufufua Yesu kutoka kwa wafu.
  - Uwezo wa kutokea na kutoweka mara moja.
  - Uwezo wa kutambulika alipotaka.
  - Uwezo wa kubadilisha mioyo ya watu, na kuwahimiza.
  - Malaika waliwatokea wanawake na Petro.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu / Yesu anajua kila kitu? Inaonyesha kwamba Mungu yupo kila pahali? Vipi?**
  - Alijua wanafunzi na mawazo yao na hali yao.
  - Alijua maandiko kikamilifu na jinsi ya kuyaweka wazi kwa wafuasi wake.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?) vipi?**
  - Yesu kwa uvumilivu aliwasiliana na watu hawa wawili, akiwaelezea maandiko.
  - Yesu alionyesha kwamba maandiko ni hadithi ya Mungu ya neema kwa wenye dhambi.
  - Yesu alivumilia mashaka na kutoamini.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
  - Yesu alionyesha kwamba maandiko yote yalikuwa yanaelekeza kwa wakati huu. Wakati amabo masihi angeteseka na kufa kwa dhambi za ulimwengu na kisha kufufuliwa baada ya siku tatu ilikuwa utimizo wa ahadi kuu za Mungu.
  - Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu, akitimiza ahadi yake ya kutuma uzao wa mwanamke ambaye angemshinda Shetani na kifo.

**Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?**

- Mwanadamu ni dhaifu na anaelewa vitu polepole, ana mashaka na hofu nyingi.
- Mwanadamu alikuwa anatafuta aina ya Mwokozi ambaye alitaka. Watu walitaka uhuru wa kitaifa kuliko uhuru kutoka kwa dhambi. Mwanadamu ni kipofu kiasi cha dhambi zake.

- Mwanadamu anaweza tu kuelewa Mungu na kazi yake jinsi Mungu anavyoielezea katika neno lake.

**Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU? Jinsi mtu anavyohusiana na Mungu?**

- Yesu aliwaita hawa wanaume ili kuelewa ahadi na imani ya Mungu katika Kristo.
- Ni kupitia tu kutimizwa kwa mpango wa Mungu wa Mkombozi ndipo mwanadamu anaweza kuokolewa kutoka kwa dhambi.
- Wokovu ungekamilika tu iwapo Kristo angeteseka kama ilivyoelezwa katika Biblia.
- Yesu alifanyia imani katika mioyo ya watu. Ni kwa njia ya imani tu ndipo wangemjua kwa kweli. Aliwapa changamoto kuhusiana na kutoamini kwao.

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :**

- Je,mambo gani maishani mwetu hutushusha moyo na kufanya tukate tamaa? Ni mambo gani hufanya kuwa vigumu kuamini Mungu anatenda kazi maishani mwetu? Je hadithi hii inaweza kutuhimiza vipi?

**MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):** (chagua moja au mbili)

- Je, umeshushwa moyo leo? Ni kwa njia gani unaona Mungu hajakuja kukusaidia? Hadithi hii inaweza kukutia moyo vipi?

- Yesu alikuwa na subira na wale wanafunzi wawili alipokuwa akiwaelezea yote ambayo maandiko yalisema kumhusu yeye. Je, ni eneo gani la maisha yako unahitaji kukumba subira yake kwako?

## 42. YESU AKIWATOKEA WANAFUNZI WAKE / KUPAA KWAKE
## Luka 24:36-53

Walipokuwa wangali wanaongea kuhusu taarifa kutoka ndugu wa Emau, Yesu mwenyewe alisimama katikati yao akawaambia, "Amani iwe kwenu." Walishangaa na kuogopa sana, wakidhani wameona mzimu. Yesu akawaambia, "Mbona mnafadhaika, na kwa nini mna shaka mioyoni mwenu? Ebu tazameni mikono na miguu yangu. Ni mimi mwenyewe! Niguzeni mwone; pepo hana mwili na mifupa jinsi nilivyo." Baada ya kusema haya, akawaonyesha mikono na miguu yake. Na wakiwa wangali hawawezi kusadiki kwa sababu ya furaha na mshangao, Yesu akawauliza, "Je, mna chochote cha kula? Wakampa kipande cha samaki aliyepikwa, akachukua akala mbele yao.

Akawaambia, "Hili ndilo nililowaambia nilipokuwa ningali nanyi. Kila jambo lililoandikwa kuhusu mimi katika sheria ya Musa, manabii, na zaburi lazima litimie." Kisha akafungua akili zao ili wayafahamu maandiko. Akawaambia, "Haya ndiyo yaliyoandikwa: Kristo atateswa na kufa kisha atafufuka kutoka kwa wafu siku ya tatu, na toba na msamaha wa dhambi utahubiriwa katika jina lake kwa mataifa yote kuanzia Yerusalemu. Ninyi ni mashahidi wa mambo haya. Ninaenda kuwatumia kile Baba ameahidi; lakini kaeni mjini hadi mtakapovalisha nguvu mpya kutoka juu."

Alipokuwa amewaongoza hadi eneo la Bethania, aliinua mikono yake akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwa sababu hii, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, nanyi wafundisheni kuyashika mambo yote niliyowaamuru ninyi. Hakika mimi niko pamoja nanyi siku zote, hadi mwisho wa nyakati." Alipokuwa akiwabariki, aliwaacha akachukuliwa juu hadi mbinguni. Kisha wakamwabudu na kurudi Yerusalemu na furaha kuu wakakaa kwa muda katika Hekalu wakimsifu Mungu.

**<u>MPANGILIO wa SOMO</u>**

**<u>UTANGULIZI:</u>** Kabla ya kusimulia hadithi uliza swali kama hili kwa kikundi kizima kujadili au kujadiliwa wawili wawili.

- **Inamaanisha nini kufanya wanafunzi?**

**<u>HADITHI:</u>** Simulia hadithi na mjifunze pamoja kama kikundi kupitia marudio mengi.

**<u>MJADALA baada ya HADITHI:</u>** Ongoza mjadala unaoongozwa na maswali haya:

**Maswali ya Kujadiliana**

**<u>Hadithi hii inatufundisha nini kuhusu MUNGU?</u>**

- **Je, hadithi hii inaonyesha vipi, kwamba Mungu ni mwenye UWEZO wote? (ana mamlaka yote, anaongoza vitu vyote?)**
  - Aliwatokea katika chumba kilichofungwa.
  - Kwa kweli alifufuliwa kimwili kutoka kwenye wafu na kulithibitisha jambo hilo.
  - Aliweza kuwapa amani katika mioyo yao iliyokuwa imefadhaika.
  - Yesu alikuwa anabadilisha mioyo ya wanafunzi. Walikuwa wenye furaha baada ya kuwaacha mara ya pili badala ya kufedheheka.

- Aliahidi kuwapa uwezo mkuu kutoka juu ili wawe mashahidi wake.

- **Je, hadithi hii inatuonyesha kwamba Mungu / Yesu anajua kila kitu?Vipi?**
  - Alijua mashaka yao na jinsi ya kuwapa hakikisho.
  - Alijua kwamba atawaacha na yale ambayo yatawatokea baadaye.
  - Alijua Roho atawapa mamlaka.
  - Alijua maandiko yote, na aliweza kuyaelezea yale yote ambayo yalitendeka.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu? (mwenye haki, anayepeana sheria, anachukia dhambi, anaamuru kifo kama adhabu ya dhambi? Vipi?**
  - Mungu anachukia dhambi. Njia ya pekee ya dhambi kusamehewa ni kwa Yesu kuutoa uhai wake mwenyewe kwetu sisi. Yesu aliyaelezea haya yote tena kwa wanafunzi.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwenye neema? (Anayependa, mwenye fadhili (huruma) kwa wenye dhambi, mkarimu na anawasiliana na wanadamu?) vipi?**
  - Yesu aliutoa uhai wake kwa ajili ya dhambi zetu.
  - Aliwatokea wanafunzi wake dhaifu waliokuwa wameogopa, na waliokuwa na mashaka kuwapa nguvu. Alivumilia mashaka yao. Aliwapa amani.
  - Yesu kwa uvumilivu aliwasiliana nao na kuelezea yote yaliyotendeka na yale yatakayotokea katika siku zijazo.
  - Aliwabariki wanafunzi wake kabla ya kupaa mbinguni.

- **Je, hadithi hii inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu? (Habadiliki. Anatimiza ahadi zake. Anafanya kile anasema?)**
  - Yesu alifufuka kutoka kwa wafu kama alivyokuwa ameahidi.
  - Aliwakumbusha jinsi maneno ya Musa, Zaburi, na Manabii yalikuwa yametimizwa ndani yake. Hii ilionyesha uaminifu wa Mungu kwa mpango wake wa wokovu kwa wenye dhambi.

**<u>Tunajifunza nini kuhusu MWANADAMU?</u>**

- Mwanadamu ni mwenye dhambi. Hii ndiyo sababu Yesu alitufilia.
- Hata wanafunzi wake, wao waliomjua bora zaidi, walikuwa wadhaifu na waliojaa mashaka. Hawangejiokoa au kujisaidia, nao walimhitaji Yesu ili awahimize.
- Baada ya Yesu kuwatokea na kutia nguvu imani yao, wanafunzi walijaa furaha na shukrani kwa Mungu, tayari kumtumikia.

**<u>Hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu jinsi ya wanadamu kumwendea Mungu, yaani kuhusu WOKOVU?</u> Jinsi mtu anavyohusiana na Mungu?**

- Wokovu unawezekana kupitia tu kwa kifo na kufufuka kwa Yesu. Lakini lazima watu wanatubu dhambi zao na kupokea msamaha kwa kumtumaini Yesu.
- Yesu hutumia wanafunzi wake kama mashahidi kuhubiri toba na msamaha wa dhambi kwa mataifa.

**<u>** JE, INAMAANISHA NINI KUSEMA, "KUFANYA WANAFUNZI"</u>?**

- **Fikiria kile Yesu anasema:** "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi." Kulingana na taarifa hii, kufanya wanafunzi kunatia ndani nini?
  - Kubatiza - hii inamaanisha nini? Je, ina maana tu kitendo halisi cha kubatiza?
    - Hapana, inamaanisha kuinjilisha, kuwaongoza watu kwenye toba na imani katika Yesu na kuwafanya wajitambulishe hadharani na Kristo na watu wake kwa njia ya ubatizo.
  - Kufundisha (kufanya uanafunzi na waumini) - Kwa hivyo ufuasi huu unahusisha nini?
- **Ufuasi:** Hebu tuangalie ufuasi ni nini na jinsi tunavyopaswa kuishi kwa kufanya wanafunzi. Hapa kuna ufafanuzi mzuri wa uanafunzi:

- Ufuasi ni ***kwa makusudi*** kuwaandaa waumini kwa **Neno la Mungu** kwa njia **ya kuwajibika mahusianokuwezeshwa na Roho Mtakatifu** ili kuzidi kuishi maisha yanayojikita katika **toba na imani inayoendelea katika Injili** ili kuiga wafuasi waaminifu wa Kristo.
- **Kwa hivyo, ukiangalia kwa makini ufafanuzi huu, ni zipi sehemu muhimu za ufuasi?**
    - Kusudi - Ni mazoezi ya makusudi ya waumini waliokomaa kuwasaidia waumini wachanga
    - Msingi wa Biblia - Yaliyomo katika Neno la Mungu, na njia zake zinaongozwa na Neno la Mungu.
    - Kuwajibika - inahusisha kujitolea kutoka kwa mfuasi na yule anayefunzwa.
    - Uhusiano - inafanywa vyema zaidi katika muktadha wa uhusiano wa maana, wa kujitolea kati ya waumini na wale wanaowafundisha. Inatimizwa vyema katika uhusiano wa mtu mmoja-mmoja au wa kikundi kidogo.
    - Kuwezeshwa na Roho - Mwanafunzi na mfuasi wote kwa maombi wanamtegemea Roho Mtakatifu ili kuwaongoza na kuwaimarisha kwa ajili ya safari.
    - Kuongozwa na Injili - mtindo wa maisha wa kujichunguza kwa Roho, kuongezeka kwa toba, na kuamini zaidi katika yote ambayo Kristo alitufanyia msalabani ni ufunguo wa kuzalisha wanafunzi ambao ni wanyenyekevu na wenye furaha na wanaopenda kutii Neno la Mungu zaidi na zaidi.
- **Kusudi la haya yote ni nini?**
    - Kusaidia kukua wafuasi wa Kristo waliokomaa na waaminifu, waliojawa na unyenyekevu na upendo, wanaoishi katika kutubu na kutumainia Injili inayoongezeka, inayofurika na upendo wa Kristo kwa waliopotea, kwa waumini wengine, na kwa ulimwengu.

- **Hebu tuangalie nyuma katika hadithi ambazo tumekuwa tukijifunza kuhusu Yesu Kristo na tuangalie jinsi Yesu alivyofanya uanafunzi.**
    - **Ni katika hadithi zipi tunamwona Yesu akiwa amekusudia kuwafundisha wanafunzi wake?**
    - **Je, ni katika hadithi zipi tunamwona Yesu akiwafanya wanafunzi kwa msingi wa Neno la Mungu?**
    - **Ni katika hadithi zipi tunaona Yesu akiwawajibisha wanafunzi wake?**
    - **Ni katika hadithi zipi tunaona ufuasi wa Yesu ukiegemezwa kwenye uhusiano wa karibu?**

**Je, katika hadithi zipi tunamwona Yesu akitegemea nguvu za Roho Mtakatifu katika ufuasi wake?**

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa JUMLA (jadili na kikundi kizima) :</u>**

- Je,  ni baadhi ya mambo gani ambayo hutuzuia kusaidia wale wanaookoka kukua zaidi na zaidi hadi wawe wanafunzi wa Yesu? Je ni mambo gani tofauti tunaweza kufanya katika makanisa yetu ya kutusaidia kazi nzuri ya 1) Kuongoza watu kwa kuamini Kristo. 2)Kuwasaidia kuwa wanafunzi waliokomaa wakimfuata Kristo katika kila eneo la maisha yao.
- Je, kujua kwamba Kristo yu pamoja nawe na yuko mkono wa kuume wa Mungu sasa akikuombea kunakuhimiza  vipi kuwa shahidi Wake  na kuwafanya wanafunzi?

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI wa KIBINAFSI (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):</u>**  (chagua moja au mbili)

- Ikiwa umepitia toba na msamaha wa dhambi kupitia Kristo, je, uko tayari sasa kuwa shahidi wake popote akuwekapo? **Je, unadhani ni nani Mungu anakuita  kushiriki naye Habari Njema juma hili?**

- **Ni mtu gani mmoja ambaye unaweza kuendelea kumfundisha au unaweza kuanza kumfundisha kuwa mwanafunzi? (Mtaje kwa jina hasa).** Unawezaje kuanza kutumia mbinu hii ya kusimulia Hadithi za Biblia na maelezo sahihi kuhusu kufanya wanafunzi kukusaidia kukuza mfuasi mwaminifu wa Yesu?

- Ni nani unaweza kumwomba akusaidie kukua kama mfuasi wa Kristo? Omba Mungu akusaidie kumpata huyo mtu.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO #1
## MUHTASARI wa CBS: Kufuatilia Ahadi ya Mwokozi

*Hapo mwanzo Mungu aliumba kila kitu kizuri. Hakukuwa na kitu kibaya, cha dhambi, au kilichovunjika. Hakuna ugonjwa, hakuna vita, hakuna migogoro, hakuna njaa. Aliwaumba malaika wamwabudu na kumtumikia. Walikuwa sehemu ya uumbaji wake mzuri. Lusifa, malaika mwenye nguvu kuliko wote, alitaka kufanana na Mungu na kuchukua nafasi yake, kwa hiyo alimwasi Mungu pamoja na baadhi ya malaika wengine. Walifukuzwa kutoka kwa uwepo wa Mungu kwa sababu Mungu ni Mungu anayejua yote, mwenye nguvu zote, na Mtakatifu. Mungu huyu Mtakatifu hawezi kukaa na wenye dhambi na dhambi lazima iadhibiwe, hivyo mwanamume na mwanamke walifukuzwa nje ya bustani mbali na uwepo wa Mungu. Malaika hao waasi sasa ni roho waovu duniani leo, na hata Lusifa, ambaye sasa anaitwa Shetani, bado anajaribu kuwadanganya watu ili wasimsikilize Mungu.*

*Kwa hivyo tena, Mungu aliumba ulimwengu mzuri kabisa na akamuumba mwanadamu maalum zaidi. Mwanadamu ndiye kilele cha uumbaji kwa sababu tuliumbwa kwa mfano wa Mungu. Mwanadamu alipewa kuitawala nchi na kuambiwa zaeni mkaongezeke na kuijaza nchi. Mungu alipumzika na kuwa mfano wa mapumziko ya Sabato kwa ajili yetu. Hadithi inayofuata inaonyesha kwamba mwanadamu aliumbwa kwa njia ya pekee kutoka kwa mavumbi ya ardhi. Kazi yake katika bustani ilikuwa kulima na kutunza uumbaji wa Mungu. Mungu alikuwa ameumba miti miwili maalum katikati ya bustani; mti wa uzima na mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Mtu huyo aliamuru kwamba angeweza kula matunda ya miti yote isipokuwa mti wa ujuzi wa mema na mabaya kwa sababu siku atakapokula matunda ya mti huo atakufa. Hakukuwa na msaidizi wa kufaa kwa huyo mwanamume hivyo Mungu akamletea usingizi mzito na kutoka katika ubavu wake akamfanya mwanamke. Wawili hao waliunganishwa pamoja wakawa mwili mmoja. Wote wawili walikuwa katika bustani ya Edeni bila dhambi na bila aibu.*

*Katika hadithi inayofuata nyoka anakuja kwa mwanamke na kumdanganya kwa kumwambia kwamba kama akila tunda, atakuwa na hekima kama Mungu, akijua mema na mabaya. Alipoona kwamba tunda hilo lilikuwa jema kwa chakula, lapendeza macho, na linafaa kwa kupata hekima, anaamua kwenda kinyume na amri ya Mungu na kula tunda hilo. Kisha anampa mume wake ambaye pia alikuwa pamoja naye. Tunajifunza kwamba mume alikuwepo na alikuwa kimya na hakuzungumza na kumzuia mke wake asitende dhambi bali alishiriki dhambi kimakusudi. Mara tu Mungu anapokabiliana nao, mwanamume na mwanamke huanza kujifunika ili kuficha aibu yao, na kisha kulaumu dhambi yao kwa wengine. Kisha Mungu akaleta laana juu ya nyoka, mwanamke, na mwanamume. Tulijifunza kwamba katika laana juu ya nyoka, ambaye alikuwa Shetani kwa kujificha, Mungu aliahidi kwa siri Mwokozi katika Mwa 3:15 alipomwambia nyoka,*

*“Nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, kati ya uzao wako na uzao wake. , uzao wa mwanamke utakuponda kichwa, na wewe utampiga kisigino.” Mungu pia alitoa mfano wa dhabihu ya damu katika hadithi hii ambapo alitoa ngozi za wanyama kwa mwanamume na mwanamke. Hawangeweza kuficha, kuficha, au kulaumu dhambi zao. Hawangeweza kukubaliwa na Mungu bila damu kumwagwa na mbadala asiye na hatia ambaye alikufa mahali pao Baada ya haya wanafukuzwa kutoka kwa uwepo wa Mungu. Walitenganishwa kimwili na kiroho na Mungu, na uhusiano ukavunjika. Sehemu iliyobaki ya Agano la Kale inaonyesha Mungu kuwa mwaminifu kutimiza ahadi ya Mwa 3:15 kwamba siku moja atamleta kupitia ukoo wa mwanamke, mtu ambaye atamponda Shetani na kazi zote za uharibifu na uozo ambazo alituongoza. ndani., Mwokozi huyu angeondoa uchungu wa dhambi na kifo na kuwarudisha wanadamu katika uhusiano ufaao pamoja naye.*

*Hadithi inayofuata, Kaini na Abeli, inaonyesha kwamba mwanadamu lazima aje kwa Mungu jinsi Mungu ameagiza. Kama Mungu alivyomwambia Kaini, dhambi inatuotea mlangoni na inataka kutumeza. Hata baada ya Kaini kumuua kaka yake Abeli, Mungu alikuwa na neema na kutoa mwana badala katika Sethi ambaye kupitia kwake ahadi ya Mwokozi ingekuja.*

*Kisha, katika hadithi ya Nuhu na gharika, dhambi ya wanadamu ilikuwa imeongezeka duniani, na "Mungu akaona kwamba kila kusudi la fikira za moyo wa mwanadamu ni mbaya siku zote." Mungu aliahidi kuokoa Nuhu na familia yake na kuwaokoa kutoka kwa gharika kuu. Ingawa Nuhu alikuwa mwenye dhambi kama wanadamu wote, alikuwa mtu mwadilifu ambaye alitembea na Mungu. Alifanya kile ambacho Mungu alimwamuru kutayarisha gharika, kujenga safina na kukusanya wanyama wote. Baada ya kumwokoa Nuhu, Mungu aliweka upinde wa mvua angani kama ahadi ya agano lake na wanadamu kwamba hatagharikі tena dunia yote kwa gharika. Hadithi hii ni picha ya wokovu. Kwa kumweka Nuhu na familia yake wakiwa hai, Mungu alikuwa akiweka hai ahadi yake ya Mwokozi ambaye siku moja angekuja kupitia Mbegu ya mwanamke. Safina pia ilikuwa picha ya wokovu. Njia pekee ya Nuhu na familia yake kuokolewa kutokana na kuzama ni kuwa ndani ya safina gharika ilipokuja. Kulikuwa na mlango mmoja tu au njia moja ya wokovu kutoka kwa gharika. Yesu ndiye mlango wetu mmoja wa wokovu. Alisema, "Mimi ndimi njia, ukweli na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi." ( Yohana 14:6 ) Yesu pia alisema, "Mimi ndimi mlango. Mtu akiingia kwa mimi ataokoka." ( Yohana 10:8,9 ).*

*Vizazi vingi baada ya Nuhu Mungu alimtokea mtu aliyeitwa Abramu ambaye, pamoja na mke wake, walikuwa mzee sana na hawakuwa na mtoto. Aliambiwa aache kila kitu na aende na mke wake na mpwa wake kwenye nchi ambayo Mungu angemuonyesha. Mungu aliahidi kwamba angemfanya Abramu kuwa taifa kubwa, kwamba atalikuza jina lake, kwamba atawabariki wale wanaombariki na kuwalaani wale wanaomlaani, na kwamba mataifa yote ya dunia yangebarikiwa kupitia yeye. Mungu alikuwa akimwambia*

*Abramu kwamba ahadi ya Mwokozi kutoka kwa Uzao wa mwanamke atakuja kupitia uzao wake. Abramu alitii na kwenda Kanaani, nchi ya ahadi. Ingawa Abramu alitenda dhambi na kusema uwongo kuhusu mke wake huko Misri kwa sababu ya woga, bado Mungu alichagua kumbariki. Baadaye, baada ya yeye na Lutu kurudi Kanaani wakiwa watu matajiri sana, mzozo ulitokea kati ya wachungaji wao kuhusu nyasi na maji kwa ajili ya wanyama wao. Ingawa Abramu alikuwa na haki ya kuchagua mahali pa kuweka mifugo yake, badala yake alimruhusu Lutu kuchagua nchi ya kuishi. Baadaye Abramu alipohitaji uhakikisho, Mungu alimtokea na kumwambia asiogope. Abramu alipotilia shaka na kuuliza ingemfaa nini ikiwa angekuwa na nchi hii na wanyama wote lakini hana mwana wa kurithi, Mungu akamtoa nje, akamwonyesha anga la usiku, na kumwambia ikiwa angeweza kuhesabu nyota basi angejua wazao wake wangekuwa wangapi. Na "Abramu alimwamini Mungu na Mungu akamhesabia kuwa ni haki". Imani ya Abramu ndiyo iliyomwokoa, si matendo yake.*

*Katika hadithi inayofuata, Abramu anaonyesha imani yake kwa kuwa mtiifu kwa mwito wa Mungu wa kwenda kumtoa dhabihu mwanawe wa pekee, Isaka, ambaye alikuwa amemngoja miaka ishirini na mitano mlimani. Hadithi ni picha au mfano wa Kristo kama Isaka alikuwa mwana pekee wa Abramu kama vile Kristo alivyokuwa mwana pekee wa Mungu. Pia, Isaka alijisalimisha kwa mapenzi ya baba yake ya kutolewa dhabihu kama vile Yesu Kristo alijisalimisha kwa mapenzi ya baba yake na kufa msalabani. Isaka pia alibeba kuni juu ya mlima hadi mahali ambapo angetolewa dhabihu kama vile Kristo alivyobeba msalaba juu ya mlima ambapo angesulubishwa hadi asingeweza kuubeba tena na kupokea msaada. Tofauti pekee ni kwamba mwana-kondoo mkamilifu alionekana kuwa mwana-kondoo badala ya Isaka lakini Yesu Kristo mwenyewe alikuwa mwana-kondoo mkamilifu aliyesimama kwa ajili ya wenye dhambi wote ambao wangeweka imani yao kwake.*

*Kisha, Mungu anarudia ahadi zilezile kwa Isaka na mwanawe, Yakobo, ambazo alikuwa amempa Abrahamu. Alirudia haya katika ndoto aliyompa Yakobo alipokuwa akimkimbia kaka yake baada ya kumlaghai haki yake ya mzaliwa wa kwanza na baraka za baba yake.*

*Baada ya miaka kadhaa, Mungu anahifadhi ahadi yake ya kuleta ainabinadamu mwokozi kwa kuruhusu Yusufu, mwana kipenzi wa Yakobo auzwe na ndugu zake utumwani. Yusufu alikumbana na majaribu mengi lakini Mungu alikuwa pamoja naye na kumsaidia. Hata mwishoni kabisa baada ya Yakobo kufa na ndugu zake Yusufu waliogopa kulipiza kisasi chake, Yusufu aliweza kuwaambia, "Je, mimi ni badala ya Mungu? Mlikusudia kunidhuru, lakini Mungu alikusudia kuwa mema ili kutimiza yale yanayofanyika sasa, kuokoa maisha ya watu wengi." Mungu alimtumia Yusufu kuokoa familia yake. Mkoo wa Mwokozi aliyeahidiwa ungeendelea kupitia ndugu yake Yuda.*

*Baada ya Yusufu kufa, Farao mwingine akatokea ambaye hakumjua Yusufu, akawafanya Waisraeli kuwa watumwa wao. Baada ya takriban miaka 400 Musa alizaliwa na ikabidi kuwekwa mtoni kama Farao alivyotoa amri kwamba kila mwanamume Mwisraeli alipaswa kuuawa. Musa alinusurika na kuokolewa na binti ya Farao na kukulia katika jumba la kifalme. Baadaye aliona mateso ya Waisraeli na kumuua Mmisri aliyekuwa akimpiga mtumwa Mwisraeli. Kisha akakimbilia jangwani na kuishi huko kwa miaka arobaini iliyofuata. Akiwa huko, alioa na kuanza kuchunga kundi la baba-mkwe wake. Siku moja katika Mlima Sinai malaika wa Bwana alimtokea katika kichaka kilichokuwa kinawaka moto. Mungu aliahidi kuwaokoa watu wake kupitia Musa na kuwatoa ili kumwabudu kwenye mlima uleule aliokuwa juu ya Musa. Musa alitilia shaka lakini Mungu alimvumilia na kumpa ishara nyingi na hata akakubali ndugu yake Harun aende pamoja naye ili amsaidie.*

*Musa na Haruni walikwenda kwa Farao kumwambia Mungu alisema, "Waruhusu watu wangu waende zao!" Farao alipokataa na kuifanya kazi yao kuwa ngumu zaidi, Mungu alituma mapigo tisa tofauti. Kila mara Farao alikubali kuwaachilia watu ikiwa tauni ingeondoka, lakini baada ya tauni kuondolewa, alibadili mawazo yake na kukataa kuwaruhusu Waisraeli waende zao. Kisha Mungu akaahidi pigo moja la mwisho, ambalo kisha Farao angewafukuza kabisa. Hii ilikuwa ni Pasaka ambayo ilipaswa kuadhimishwa kila mwaka ili kuwakumbusha watu wa Israeli kwamba Mungu alikuwa amewakomboa kutoka utumwani Misri. Kila familia ilipaswa kuchukua mbuzi dume au kondoo mkamilifu wa mwaka mmoja na kumchinja. Kisha walipaswa kuipaka damu kwenye miimo ya milango na kukaa ndani nyuma ya damu ya dhabihu ya mwana-kondoo mkamilifu hadi asubuhi. Hawakuweza kuvunja mifupa na iliwabidi kufanya kila kitu ambacho Mungu aliwaamuru. Watu wa Israeli waliokolewa lakini wazaliwa wa kwanza wa Misri walikufa wote. Mambo ambayo Mungu alikuwa amemwahidi Abrahamu na muda mrefu uliopita yalikuwa yametimia. Watu walikuwa watumwa katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka 400 na kisha wakatoka na mali nyingi.*

*Waisraeli waliwekwa huru na kuelekea nchi ya ahadi wakiongozwa na nguzo ya wingu mchana na nguzo ya moto usiku. Walipofika Bahari ya Shamu, walinaswa kati ya bahari na jeshi la Farao. Waisraeli waliogopa na kumwambia Musa kwamba amefanya kosa. Musa akasema, "Msiogope. Simameni imara na mtaona ukombozi ambao Bwana atakuletea leo. Wamisri unaowaona leo hutawaona tena. Bwana atakupigania; unahitaji kunyamaza tu." Mungu alitenganisha bahari na Waisraeli wakapita moja kwa moja. Mungu aliwaokoa watu kupitia Musa mtumishi wake, na Wamisri wakashindwa. Kama vile njia pekee ya wokovu kwa Waisraeli ilikuwa kupitia Bahari ya Shamu, njia pekee ya sisi kuja kwa Mungu na kukombolewa kutoka kwa dhambi na kifo chetu ni njia ya Mungu.*

*Waisraeli wanakuja kwenye Mlima Sinai ambapo Mungu anatoa sheria yake kamilifu Mungu ni Mungu Mtakatifu ambaye alitaka kuwatenganisha watu wake na tamaduni nyingine zinazowazunguka ili wawe taifa takatifu na ufalme wa makuhani.*

*Amri kumi zilitolewa kwa Musa, na watu wakasema watazitii kabisa, Lakini kwa muda mfupi sana, Musa alipokuwa amepanda mlimani kupokea nakala iliyoandikwa ya zile amri kumi, watu wakakosa subira kwa ajili ya kurudi na kujenga. akasujudu ndama wa dhahabu. Baada ya kuwaadhibu wengi wa wale walioasi, Mungu aliwasamehe Waisraeli na kuendelea kuwa pamoja nao walipotubu. .*

*Baada ya hayo ulikuwa wakati wa kujenga makao ya Mungu pamoja na watu wake, Hema. Waisraeli walitoa vitu vyote vya thamani ili kujenga Maskani, ambayo ilikuwa hema iliyogawanywa kwa pazia katika vyumba viwili, Mahali Patakatifu na Patakatifu Zaidi. Ilikuwa imezungukwa nje na kuta za ngozi za wanyama. Kulikuwa na dhabihu maalum kila mchana na usiku na njia tofauti ambazo kuhani alipaswa kujiendesha. Haruni aliwekwa rasmi kuwa Kuhani Mkuu akielekeza kwa kuhani mkuu na wa mwisho, Yesu Kristo. Kila mwaka katika siku ya Upatanisho Kuhani Mkuu angepata fahali mmoja na mbuzi wawili. Kwanza angechinja ng'ombe dume na kuchukua damu katika Patakatifu pa Patakatifu na kuinyunyiza juu ya sanduku la agano kwa ajili ya msamaha wa dhambi zake mwenyewe kwanza. Kisha angetoa dhabihu ya mbuzi mmoja na kurudi kwenye Patakatifu pa Patakatifu na kunyunyiza damu juu ya sanduku la agano kwa ajili ya msamaha wa dhambi za watu wa Israeli. Kisha angemchukua mbuzi wa tatu na kuungama dhambi za watu juu ya kichwa cha mbuzi huyo. Kisha ingepelekwa mbali jangwani ili isirudi tena kuashiria dhambi za watu wanaobebwa. Wakati makuhani waliingia Patakatifu kila asubuhi na jioni, Kuhani Mkuu pekee ndiye angeweza kuingia Patakatifu pa Patakatifu na kisha mara moja tu kwa mwaka katika Siku ya Upatanisho kama mpatanishi wa watu wa Mungu. Hilo latuelekeza kwa mpatanishi wa kweli, Yesu Kristo, anayeketi mkono wa kuume wa Baba, akiwa mpatanishi kwa ajili ya Wakristo wote.*

*Baada ya kutoka kwenye Mlima Sinai, Mungu aliwaongoza Waisraeli hadi kwenye mpaka wa Nchi ya Ahadi ambapo Musa aliwatuma wapelelezi kumi na wawili kwenda Kanaani kuangalia nchi. Kwa kusikitisha watu waliposikia taarifa za wapelelezi, waliogopa na hawakumwamini Mungu kuwapa ushindi juu ya Wakanaani hivyo Mungu aliwaadhibu kwa kuwarudisha jangwani kwa miaka arobaini zaidi. Hatimaye baada ya wakati huu, watu wazima wote isipokuwa Kalebu na Yoshua walipokwisha kufa, Mungu alimsaidia Yoshua kuwaongoza kuingia katika Nchi ya Ahadi. Baada ya Yoshua kufa, Waisraeli hawakuwaangamiza au kuwafukuza Wakanaani wote kama Mungu alivyoagiza bali walichanganyika nao na kuongozwa katika ibada ya sanamu. Zaidi ya miaka mia nne, Waisraeli walipitia mizunguko ya kurudia-rudia ya kumwasi Mungu, kisha kuadhibiwa na Mungu kupitia mataifa adui, kisha kutubu dhambi zao, na hatimaye kukombolewa na mwamuzi ambaye Mungu alimtuma. Baada ya kipindi cha amani na mafanikio wangegeukia sanamu za majirani zao tena ili kuanzisha upya mzunguko huo. Fadhili ya Mungu katika kutuma waamuzi kama Gideoni, Debora, Samsoni, na Samweli wakati Waisraeli walipotubu ilionyesha uaminifu wake ili kutimiza ahadi ya Mwanzo 3:15 ya*

*kuleta Mwokozi kwa ajili ya mwanamume mwenye dhambi kupitia Mbegu ya mwanamke licha ya kwamba Waisraeli waliendelea kufanya yale. ilikuwa sawa machoni pao wenyewe.*

*Waisraeli walipomkataa Mungu kuwa mfalme na kuomba wapewe mfalme wa kibinadamu, Sauli aliwekwa rasmi kuwa mfalme. Alianza ufalme wake akimtumaini Mungu na kumtumikia kwa uaminifu, lakini baadaye akawa na kiburi, akakengeuka, na kutomtii Mungu mara kwa mara. Baada ya Sauli, akiwa bado mwaminifu kutimiza ahadi yake ya Mwokozi anayekuja kupitia Uzao wa mwanamke, Mungu alimteua Daudi kuwa mfalme, na kumwahidi kwamba sikuzote angekuwa na mzao anayeketi kwenye kiti cha enzi. Daudi alikuwa mtu anayeupendeza moyo wa Mungu mwenyewe, ingawa alianguka katika dhambi mara kadhaa, ikiwa ni pamoja na uzinzi wake na Bathsheba na mauaji ya mumewe. Alipotubu, Mungu alimwonyesha rehema, na hatimaye akampa mwana, Sulemani, ambaye angeendeleza kazi ambayo Mfalme Daudi alikuwa ameanzisha.*

*Baada ya Sulemani, kwa sababu ya dhambi yake, ufalme uligawanywa katika ufalme wa kaskazini, Israeli, na ufalme wa kusini, Yuda. Zaidi ya mamia ya miaka kulikuwa na wafalme wengi katika falme zote mbili. Isipokuwa baadhi ya wafalme wa Yuda, wengi wao walimwasi Mungu. Katika miaka hii Mungu alituma manabii wengi kwa falme hizi, wakionya juu ya dhambi na hukumu, akiahidi rehema wakati watu wangetubu, na kutoa tumaini la ufalme wa milele. Walitoa unabii mwingi kuhusu Mwokozi aliyeahidiwa - hali ya kuzaliwa kwake, jinsi angekuwa, angefanya nini, na jinsi angekufa na kufufuliwa tena. Baada ya watu wa Yuda kuwa uhamishoni Babiloni na kurudishwa, unabii wa mwisho ulitukia. Kisha kwa miaka 400 kukawa kimya - hakuna neno kutoka kwa Bwana. Watu wa Mungu walisubiri tu.*

*Hatimaye, baada ya miaka mia nne, ukimya ulivunjika, na Mariamu alitembelewa na malaika Gabrieli na kumwambia mtoto ambaye angemzaa ingawa alikuwa bikira, mtoto ambaye angekuwa Mwokozi wa ulimwengu. Malaika alikuwa tayari amemtokea Zekaria, na mke wake akamzaa Yohana Mbatizaji. Yesu alizaliwa na bikira Mariamu huko Bethlehemu kama ilivyotabiriwa. Baada ya Yesu kufikia utu uzima, wakati ulifika wa yeye kuingia katika huduma yake, hivyo akaja kubatizwa na Yohana. Yohana alipombatiza Yesu, mbingu zilifunguka, na roho ikashuka kama njiwa, na sauti kutoka Mbinguni ikasema, Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye. Siku iliyofuata, Yohana alimwona tena Yesu na kuwatangazia wafuasi wake, "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu!*

*Baada ya Yesu kuwachagua wanafunzi wake kumi na wawili, alifanya na kusema mambo mengi ambayo yalionyesha kwamba yeye ndiye Mwokozi aliyeahidiwa, mkataa laana. Yeye ndiye mwenye uwezo wa kumponda Nyoka/Shetani na kubadili laana zote zilizokuja juu ya wanadamu na ulimwengu katika bustani ya Edeni kwa sababu ya dhambi ya mwanadamu. Yesu alionyesha katika hadithi ya mtu aliyepooza kwamba ana uwezo wa kusamehe dhambi, kwamba yeye ni Mwana wa Adamu ambaye alitabiriwa katika Danieli.*

*Inaonyesha pia kwamba ana uwezo wa kuponya na kutia nguvu ugonjwa uliokuja ulimwenguni baada ya kuanguka kwa wanadamu. Katika hadithi ya Mwanamke Msamaria, anaonyesha kwamba ana uwezo wa kutoa maji ya uzima katika hadithi ya Mwanamke Msamaria. Kwa hakika yeye ndiye Mwokozi anayeweza kutosheleza sehemu ya ndani kabisa ya nafsi zetu. Tunapotafuta utoshelevu katika kila aina ya sanamu, Yesu ndiye pekee anayeweza kutupa maji haya ya uzima. Pia tunaona hapa kwamba Yesu akitimiza ahadi aliyopewa Abramu kwamba mataifa yote yatabarikiwa kupitia uzao wake. Yesu analeta habari njema kwa wale walio nje ya Wayahudi, katika kisa hiki Wasamaria.*

*Hadithi inayofuata inaonyesha kwamba Yesu ana uwezo wa kuvunja laana juu ya mtu huyo ambapo angelazimika kupigana ili kulisha familia yake kwa jasho la uso wake. Yesu ana uwezo wa kutoa chakula alipowalisha wale 5000. Yesu e ni mkate wa uzima.. Katika hadithi ya kumponya mvulana mwenye pepo, Yesu anaonyesha uwezo wake juu ya pepo waliokuja ulimwenguni kwa anguko la Lusifa. Hatimaye, anapomfufua Lazaro kutoka kwa wafu tunaona kwamba Yesu ana uwezo juu ya Mauti yenyewe!.*

*Hadithi mbili zinazofuata zinafundisha jinsi tunapaswa kuja kwa Yesu. Hadithi ya yule Mtawala Kijana Tajiri inaonyesha kwamba sheria haina uwezo wa kuokoa na kwamba hatuwezi kujenga uadilifu wetu juu ya matendo yetu mema bali tunahitaji njia tofauti kabisa ya kuifikiria. Chochote tunachokiamini badala ya Yesu kutupa uzima, yaani chochote kinachotuzuia kumkaribia Yesu kwa toba na imani pekee, tunatakiwa kukiuza, ili tuondokane nacho!. Msingi wetu lazima uwe Yesu Kristo na chochote tunachoweka juu yake lazima kishushwe ili kumfuata. Hadithi ya mwanamke mwenye dhambi inaonyesha kwamba tunda la kupata msamaha wa Mungu kupitia imani katika Kristo ni upendo. Wale wanaomfuata wataonyesha imani yao kwa jinsi wanavyompenda Yesu na wengine pia.*

*Sasa kwa kuwa tumeona kupitia maneno na matendo yake kwamba Yesu kwa hakika ndiye Mwokozi aliyeahidiwa katika bustani ya Edeni, Mpinduzi wa Laana, hapa katika mstari huu wa mwisho wa hadithi kwenye kitambaa chetu cha hadithi za Biblia, tunamwona Yesu AKIFANYA kile alichohitaji kufanya katika ili kutuokoa! Kwanza, katika wakati wake wa mwisho wa ushirika na wanafunzi wake kabla ya kifo chake, anashiriki Meza ya Bwana pamoja nao. Anawaagiza kwamba kwenda mbele wafuasi wake wanapaswa kula Meza ya Bwana mara kwa mara ili kutukumbusha juu ya damu yake iliyomwagika kwa ajili yetu na mwili wake uliovunjwa kwa ajili yetu. Kisha Yesu anawapeleka wanafunzi wake kwenye bustani ya Gethsemane ambako anasali. Wanafunzi wake hawawezi kukaa macho hata ingawa anawaonya na kuwasihi. Yesu anaomba sala hiyo hiyo tena na tena, "Baba, nakuomba uniondolee kikombe hiki cha mateso. Lakini, si kama nitakavyo mimi, bali vile utakavyotendewa wewe."*

*Hatimaye, Yuda anakuja kumsaliti Yesu, naye anakamatwa na kupelekwa mbele ya Kuhani Mkuu ambako ananyamaza na hajitetei dhidi ya mashtaka yote ya uwongo.*

*Hatimaye Yesu asema na kumwambia Kuhani Mkuu kwamba atamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu, dai la uungu ambalo kitabu cha Danieli kilitabiri juu yake. Kuhani Mkuu anatambua dai hili na analia, "Kukufuru" huku akirarua nguo zake na kumpeleka kwa Pilato kuhukumiwa. Pilato haoni hatia kwa Yesu, lakini anaamuru apigwe viboko. Kisha hatimaye anaamua kuruhusu umati uamue, nao wanachagua Baraba aachiliwe na Yesu asulubishwe.*

*Kisha Yesu analazimika kubeba msalaba wake katikati ya mji, ishara ya aibu kubwa. Wakati hawezi kuubeba tena mtu mmoja aitwaye Simoni analazimishwa kubeba msalaba kwa ajili yake. Anasulubishwa kule Golgotha, na askari wakapiga kura kwa ajili ya nguo zake kama vile ilivyokuwa imetabiriwa. Baada ya saa tatu, giza lote likaingia Yesu alipolia, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Ndipo akasema, "Imekwisha," na akasema, "Mikononi mwako naiweka Roho yangu." Nchi ikatikisika, kukawa giza, na pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu mpaka chini. Hata akida wa Kirumi alisema, "Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu!" Kisha Yesu akazikwa katika kaburi la tajiri, kama vile Agano la Kale lilivyotabiri.*

*Kisha, siku ya tatu, wanawake walipokuwa njiani kuelekea kaburini asubuhi na mapema, tetemeko lingine la ardhi likatokea, na malaika akaliviringisha lile jiwe. Wanawake walipofika walimkuta malaika pale na askari wa Kirumi wamelala chini kama watu waliokufa, lakini Yesu hakuwepo tena. Malaika aliwapa ripoti hiyo, na walikutana na Yesu tofauti kabla ya kuwafikia wanafunzi. Ni jambo la kushangaza kwamba ni wanawake ambao walikuwa wa kwanza kumuona Bwana mfufuka na si wanaume. Wanawake wakati huo hawakuwa na msimamo wa kisheria na ushuhuda wao haungekuwa na uzito katika mahakama ya sheria, lakini bado Mungu aliwachagua wanawake kuwa wa kwanza kushuhudia ufufuo wake.*

*Wanafunzi pia wana mwingiliano na Yesu katika kipindi kijacho cha wakati Yesu akiwatokea mara nyingi. Tomaso alikuwa mmoja wa wanafunzi waliokuwa na shaka, lakini Mungu alimtokea baadaye, na Tomaso aliamini kwa kutangaza, "Bwana wangu na Mungu wangu." Kisha Yesu akasema, "Umeona na kuamini, lakini wamebarikiwa wale ambao hawaoni na bado wanaamini. Kisha Yesu anawatokea wafuasi wake wawili kwenye barabara ya kwenda Emau. Anafungua akili zao kuelewa Maandiko na kuwafunulia jinsi Agano zima la Kale linavyomhusu yeye mwenyewe. Baadaye atokea tena kwa wanafunzi na kuwaongoza hadi karibu na Bethania na kuwabariki. Pia anafungua akili zao kuelewa Maandiko na jinsi sheria ya Musa, Manabii, na Zaburi zote zinavyojielekeza kwake yeye mwenyewe. Alipofika mahali pazuri, Yesu aliwabariki na kuwapa Agizo Kuu. Kisha akapaa mbinguni na kuwaacha wangojee kupokea Roho Mtakatifu aliyeahidiwa ambaye angewapa baada ya kupaa kwake.*

*Wakati wa hadithi hizi zote tunaona umuhimu wa dhabihu ya damu katika Agano la Kale. Hii inaonyesha kwamba lazima kuwe na umwagaji wa damu kwa ajili ya ondoleo la*

*dhambi. ( Waebrania 9:22 ) Tunaona dhabihu nyingi sana katika Agano la Kale ambapo damu ilimwagwa. Tunaona baadaye kwamba damu ya mafahali na kondoo dume haiwezi kamwe kuchukua dhambi zetu. Yote yalikuwa yakielekeza kwa mwana-kondoo mkamilifu wa Mungu, Mwana wake mwenyewe ambaye angekuja na kukaa kati yetu na kuishi maisha yasiyo na dhambi, kufa kifo msalabani ambacho sisi kama wenye dhambi tunastahili, na kisha kufufuliwa siku tatu baadaye akionyesha kwamba ana nguvu. juu ya dhambi na mauti. Shetani ameshindwa. Bado anazunguka-zunguka duniani akijaribu kuwadanganya watu, kuwazuia wasimsikilize Mungu, lakini uchungu wa sumu ambao nyoka alikuwa nao haupo tena. Yesu aliweza kuponda uchungu na sumu ya nyoka. Dhambi na kifo havina nguvu tena juu yetu. Kwa sababu ya Kristo, tunaweza kurejeshwa katika uhusiano ufaao na Mungu, na anatupa nguvu za Roho Mtakatifu wake ili kutukumbusha utambulisho wetu, kutuhukumu kuhusu dhambi, na kutuvuta karibu naye.*

# KIAMBATISHO #2

# MAPENDEKEZO KUHUSU RATIBA ZA CBS

Kwa kufundisha  masomo kimpangilio kwa kanisa lako, ambamo una wakati mwingi, tuuansisistiza sana, ufundishe, au uhubiri kufuatia hadithi zote arobaini na mbili (42) moja  baada ya nyingine , ukifanyia hadithi nyengine kwa kila wiki au kwa wiki nyengine kwa kila wiki au kwa wiki mbili, kwa kozi yote; kwa makadirio ya mwaka mmoja. Hii itaweza msingi dhabiti kwa kanisa kwa kuelewa ukamilifu wa injili na ukomavu. Ni muhimu watu waipate ufahamu Mungu akitekeleza mpango wake kimpangilio. Hii ndio maana unatakiwa ufanye kimpangilio sio kuruka hadithi muhimu.

Kwa kufundisha wachungaji au viongozi, wawe wanafunzi Ili waweze kufahamu na kwenda kufundisha hadithi katika huduma zao, pendekeza ufundishe kupitia hizo hadithi thelathini (30). Zilizowekwa alama kama hii (*) katika jedwali iliyomo. Hao viongozi unaowafundisha yapasa waweze kukariri hizo hadithi zingine katika kitabu cha mwongozo na wafundishe kufuatia ule mwongozo uliowapatia. Tena hakikisha wamefahamu ule mwenendo wake Mungu kudhihirisha mpango wake wa kuleta mwokozi. Kuna aina nyingi za mpangilio wa kufundisha hadithi hizo thelatini ili kuweza kuelimisha viongozi wengine wa kanisa. Unatakiwa kuchagua moja ambayo inafaa kwa hali yako na hali ya wanafunzi wako.Hapa kuna aina tofauti tofauti;

**Mipango ya Jumla inayowezekana kuandaa mafunzo ya wiki thelathini ndani ya mwaka moja.**

